

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini na Tatu - Tarehe 19 Mei, 2016

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli za leo na Mkutano wetu wa Tatu Kikao cha Ishirini na Tatu. Katibu.

NDG. JOHN N. JOEL - KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Naomba kuweka mezani hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Naibu Waziri. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Catherine Magige.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Catherine Magige kwa niaba ya Kamati, sasa naomba nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Nishati na Madini.

MHE. JOHN W. HECHE - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Nishati na Madini kuhusu Makadario ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Maswali kwa Waziri Mkuu, tunakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu usoge hapa mbele. Waheshimiwa Wabunge ninawakumbusha kuhusu maswali kuwa mafupi, yaliyonyooka, yasiyohitaji takwimu, ya kisera ili watu wengi zaidi waweze kupata nafasi ya kuuliza maswali.

Leo Kiongozi wa Upinzani Bungeni yupo. Karibu sana Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa swali la kwanza. (Makofi)

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu maswali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu unatambua kwamba sasa hivi nchi ina uhaba mkubwa wa sukari. uhaba huu wa sukari umesababishwa na amri iliyotolewa na Mheshimiwa Rais mwezi Februari mwaka huu ya kuzuia uagizaji wa sukari bila kufuata utaratibu ama kufanya utafiti wa kutosha kuhusiana na tatizo zima ama biashara nzima ya uagizaji na usambazaji wa sukari katika Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunatambua kwamba nchi yetu inazalisha takribani wastani wa tani milioni 300 na zaidi ya tani 180 hivi zinaagizwa kutoka nchi za nje na sasa hivi wewe mwenyewe umetoa kauli kwamba Serikali imeagiza sukari.

Sasa swali langu ni hili; maadam sukari ina utaratibu maalum wa uagizaji ambao unasimamiwa na Sheria ya Sukari ya mwaka nafikiri *Sugar Industry Act* ya mwaka 2001 na kwamba Bodi ya Sukari inatoa utaratibu maalum wa uagizaji wa sukari hii na biashara ya uagizaji sukari sio tu uagizaji kwa sababu ya fedha ni pamoja na muda maalum, circle maalum wakati gani agizo hili isingane na uzalishaji katika viwanda vya ndani ambavyo Mheshimiwa Rais alidai alikuwa na nia ya kuvilinda ambalo ni jambo jema.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa unaweza ukatuambia hiyo sukari uliyoagiza umeiagiza kwa utaratibu gani? Anaiagiza nani? Inategemewa kufika lini? Ni kiasi gani? Na itakapofika haitagongana na uzalishaji katika viwanda vyetu *local* baada ya kuisha kwa msimu wa mvua na hivyo kusababisha tatizo la sukari kwa mwaka mzima ujao? *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbowe, Mbunge wa Hai na Kiongozi wetu wa Kambi ya Upinzani kwa kuuliza swali hili kwa sababu tulitaka tutumie nafasi hii kuwaondoa mashaka Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wakati wote anapotoa tamko ni kutokana na mwelekeo na mpango wa Serikali ambao umepangwa kwa lengo maalum. Sukari nchini ni kweli kwamba inaratibiwa na Bodi ya Sukari ambayo pia imewekwa kisheria na moja kati ya majukumu yao kufanya utafiti, lakini pia kusimamia viwanda vinavyozalisha kwa lengo la kusambaza sukari nchini na iweze kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu, minne ya nyuma, sukari imekuwa ikiletwa kwa utaratibu ambao baadaye tuligundua kwamba unavuruga mwenendo wa viwanda vya ndani na viwanda vya ndani havipati tija. Kwa hiyo, Serikali hii ilipoingia madarakani moja kati ya mikakati yake ni kuhahakikisha kwamba viwanda vya ndani vinalindwa, unavilindaje? Ni pale ambako sasa sukari inayoingia ndani lazima idhibitiwe lakini pia kuhamasisha viwanda hivyo kuzalisha zaidi sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya sukari nchini ni tani 420,000. Sukari ambayo inazalishwa nchini ni tani 320,000 na upungufu ni kama 100,000 hivi. Tani 100,000 hii kama hatuwezi kuiagiza kwa utaratibu na udhibiti mzuri kunaweza kuingia kwa sukari nyingi sana kwa sababu kwenye sukari tuna sukari za aina mbili, sukari ya mezani ile ambayo tunaitumia kwenye chai na sukari ya viwandani na haina utofauti mkubwa sana kwa kuingalia na sukari ya viwandani na ya mezani ni rahisi sana kwa mwagizaji kama hatuwezi kudhibiti vizuri unaweza kuleta sukari nyingi ya mezani halafu kukajaa sokoni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kauli ya Mheshimiwa Rais ni katika mpango wa kulinda viwanda vya ndani kama ambavyo umekiri, lakini jukumu la Bodi sasa ya Sukari baada ya kauli ile inatakiwa sasa iratibu vizuri. Kwa hiyo, sukari imeratibiwa vizuri na bodi ya sukari na mahitaji ya sukari ile ya tani 100,000 na mahitaji ya sukari ambayo inatakiwa kuingia ili isivuruge uzalishaji ujao ni kazi ambayo inafanywa Bodi ya Sukari.

Kwa hiyo, basi hata sukari ambayo imeagizwa sasa tunauhakika wa waagizaji na aliyeagiza ni Bodi ya Sukari na vibali vimetolewa na Bodi ya Sukari. Lakini pia kiwango ambacho tumekitaka kingie nchini cha tani zisizopungua 70,000 ambazo tungetaka ziingie kutoka sasa chini ya udhibiti wa Bodi na TRA kwa pamoja pale bandarini na hasa baada ya kuwa tumeweka vizuri mazingira ya bandari, tunaamini sukari itakayoingia haitavuruga uzalishaji kwa sababu viwanda vitaaza kazi mwezi Julai. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunao Mfungo wa Ramadhani ambao mahitaji ya sukari ni mengi kidogo. Kwa hiyo, mahitaji hasa tungeweza kuagiza tani 50,000 lakini tumeongeza 20,000 kwa sababu ulaji wa sukari utaongezeka sana hasa kipindi cha Ramadhani ambacho ni mwezi wa sita. Uzalishaji utakapoanza mwezi wa saba sukari haianzi kupatikana tu pale inapopatikana lazima kutachukua tu nusu mwezi mpaka mwezi mzima ili waweke kwenye stock waanze kuisambaza iwafikie walaji. Tunaamini kiwango ambacho tumekiagiza kitaendelea kulinda viwanda vya ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia nataka Watanzania waelewe tu kwamba sasa hivi ni wakati mzuri wa kuweka mkakati wa namna ambavyo sukari hii inaweza kuzalishwa na ikatosheleza mahitaji ya ndani. Mwenyewe Nimekaa na wamiliki wa viwanda vya sukari tumekubaliana kwa miaka minne wanaweza kuongeza uzalishaji kufikia tani 420,000 ambazo zinahitajika nchini. Lakini bado tuna maeneo mengi ya uwekezaji wa sukari, tunayo mashamba matatu sasa hivi, tuna Bagamoyo, tuna Morogoro Kidunda, lakini tuna Kigoma. Liko eneo lingine pale Kilombero yanafaa kabisa kuwekwa viwanda na tayari tumepata wawekezaji ambao wameonyesha nia kwa hivi sasa tunafanya mazungumzo yao ya mwisho tuamue kuongeza viwanda ili viweze kuzalisha sukari, iweze kufikia mahitaji, tunajua idadi ya watu inaongezeka na mahitaji makubwa lakini hiyo Bodi ya Sukari inaendelea kufanya utafiti na inaendelea kuratibu, asante sana. (Makofi)

SPIKA: Swali la nyongeza Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru kwa majibu yako na ninaomba nikuulize maswali mengine machache ya ziada.

SPIKA: Swali moja tu la nyongeza.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, ni moja tu lenye vipengele.

Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na nia njema sana ya kulinda viwanda vya ndani ni dhahiri kwamba maamuzi yote ya kiutawala lazima yafanyiwe kwanza utafiti. Na tunapozungumza ninahakika Serikali yako inatambua kwamba kuna mradi mkubwa wa uwekezaji wa kiwanda cha sukari uliokuwa umependekezwa katika eneo la Bagamoyo uliouzungumza ambao umeanza kuratibiwa tangu mwaka 2006 wenye *capacity* ya kuzalisha sukari tani 125,000 kwa mwaka, lakini Serikali mpaka dakika hii tunapozungumza urasimu unasababisha mradi huu haujapewa kibali cha kuanza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu, pamoja na kwamba ulisema kuna bei ya elekezi sukari ambayo ingehitaji soko la sukari liweze kuwa *controlled* na Serikali, jambo ambalo linaonekana kushindikana. Unatupa kauli gani Watanzania kuhusiana sasa na hatima ya hayo mambo niliyokuuliza? (Makofi)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali pana la Mheshimiwa Mbowe, Mbunge wa Hai na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kama ifuatavyo:-

Kwanza tuna hilo shamba la Bagamoyo ambalo umelisema ambalo umesema kumekuwa na urasimu wa muda mrefu. Nataka nijibu hili vizuri kwa sababu pia Wabunge tumeshirikiana nao sana katika kufanya maamuzi ya shamba lile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, shamba la Bagamoyo kwa ukubwa wake na mategemeo yake kwa mipango ya kuzalisha sukari inategemea sana Mto Wami. Mpakani mwa Mto Wami tumepakana na Mbuga ya Saadani, Mbuga ya Saadani uwepo wake na sifa iliyonayo inategemea sana wanyama wale kunywa maji Mto Wami. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa shamba la sukari unahitaji maji mengi nayo yanatakiwa yatoke Mto Wami. Bado kuna mgongano kidogo wa mpaka kati ya shamba letu hilo la sukari linalotegemewa kulima miwa na Mbuga ya Saadani. Kamati ya Kudumu ya Bunge imefanya ziara na imeishauri Serikali kuangalia vinginevyo na mimi nimepokea ushauri wao vizuri kwa sababu una mantiki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge imeishauri Serikali kwamba ni vyema tukahifadhi mbuga, tukatafuta maeneo mengine ya kilimo cha sukari ili kulinda Mto Wami ambao unatumiwa na wanyama wetu kwenye Mbuga ya Saadani kuliko kupeleka shamba tukatumia maji yale tukafukuza wanyama hakutakuwa na mbuga tena. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sisi bado tuna nafasi kubwa ya maeneo mengi ambayo yamefanyiwa utafiti ya kulima sukari, mbali ya eneo la Morogoro na kule Kigoma, lakini tuna eneo la shamba lililokuwa linamilikiwa na Bodi ya Sukari kule Kilombero, nalo pia lina nafasi nzuri tu tunaweza kuzungumza na wakulima wanaolima mashamba ya kawaida watuachie tuweze kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna Mto Rufiji tuna bonde kubwa sana uliokuwa unamilikiwa na watu wa Bonde la Rubada, wana eneo kubwa sana. Kwa hiyo, tuna maeneo hayo mengi, tutakapopata wawekezaji wengi tutaanza kupima viwanda vilivyopo na uzalishaji wake. Makubaliano ya kiwanda kipya na uzalishaji wake tukigundua kwamba, uzalishaji wake unatosha mahitaji ya nchi. Tutaanza kuwakabidha Kigoma, tutawepeleka Morogoro kule Kilosa, tutawapeleka hapa Ngerengere na Bagamoyo iwe sehemu ya mwisho baada ya kuwa Kamati ya Bunge imetushauri vizuri juu ya kulinda Mbuga yetu ya Saadani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ambalo umelitaja ni hili la bei elekezi, kwa nini tunatoa bei elekezi.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tunakaa sana na wazalishaji wa viwanda wa sukari na kufanya mapitio na kwa mara ya mwisho tumekutana hata wale waagizaji wa muda mrefu na sasa tunajua kupitia mitandao tunajua bei wanayonunulia sukari huko ughaibuni. Brazil na kule Uarabuni tumeshafanya *calculation* za pamoja mpaka sukari inaingia nchini na kulipa kodi zake.

Mheshimiwa Spika, usafirishaji kutoka Dar es Salaam na kuipeleka mpaka mkoa wa mwisho Kagera, Lindi, Ngara, tunajua kule Ngara itauzwa bei gani. Kwa hiyo, wajibu wa Serikali kutoa bei dira ni kumlinda sasa mwananchi wa kawaida asije auziwe kwa gharama kubwa kwa kisingizio cha usafirishaji huku tukiwa tunajua usafirishaji kutoka Brazil mpaka Dar es Salaam, Dar es Salaam mpaka Ngara na mwananchi wa Ngara atanunua sukari kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala la bei elekezi litategemea linaweza likabadilika kutegemea na gharama ya usafirishaji ambayo na sisi pia tunafuatilia kwa karibu kupitia Bodi yetu ya Sukari. Kwa hiyo, suala bei dira linaweza kubadilika na sisi tunatoa kauli kutegemea na uagizaji lakini lazima wananchi waamini kwamba Serikali hii inawalinda walaji wadogo ili wasinunue sukari kwa bei ya juu. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge mkiangalia saa yetu maswali haya ya Kiongozi wa Upinzani ya sukari yameshachukua robo saa kwa hiyo tunaendelea na robo saa liliyobaki. Swali la kwanza atapewa Mheshimiwa Saumu Heri Sakala, Mbunge wa CUF Viti Maalum.

MHE. SAUMU H. SAKALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, katika nchi yetu kumekuwa na baadhi ya wafanyabiashara wa mazao kuwalazimisha wakulima kufunga mazao yao kwa mtindo wa lumbesa jambo ambalo licha tu ya kumdidimiza mkulima huyu na kumnyanyasa lakini pia linaifanya Serikali inakosa mapato.

Mheshimiwa Spika, sasa ni nini kauli ya Serikali juu ya suala hili ambalo limekuwa likiendelea kwa muda mrefu sasa licha ya makemeo mbalimbali yaliyokuwa yanatokea?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saumu, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wako wafanyabiashara hasa wa mazao wamekuwa na tabia ya kuwalazimisha wakulima kununua kwa gunia lililofungwa kwa mtindo wa kuwekwa kile kichuguu maarufu lumbesa, kwanza hilo ni kosa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshatoa maelekezo kupitia Wakala wa Vipimo ambao ni wasimamizi wakuu wa kuhakikisha kwamba biashara yote ya mazao ya kilimo nchini yanauzwa kwa vipimo vya kilo na siyo kwa kufunga gunia likawa lumbesa. Lakini pia kwa mazingira ya vijijini ambako hakuna mizani imejitokeza sana hilo Mheshimiwa Mbunge la kwamba watu wanafunga gunia mpaka lumbesa ndiyo inakuwa kama gunia moja. Lakini gunia letu sisi limepimwa limeshonwa viwandani kwa vipimo sahihi na lazima lishonwe kwa uzi juu ndiyo linakuwa gunia na wala siyo ile lumbesa.

Mheshimiwa Spika, sasa jukumu la Serikali ni kuendelea kusimamia na mimi nataka nitoe wito tena kwa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Halmashauri zao za Wilaya na Maafisa Biashara walioko kwenye Halmashauri hizo kusimamia kwamba biashara hii haiwanyonyi wakulima wadogo wanaouza mazao ya mahindi, vitunguu, viazi na kitu kingine kwa kufunga magunia kwa njia ya lumbesa. Jambo hili wala siwaachii Wakuu wa Wilaya peke yao nawaagiza pia Wakuu wa Mikoa kupitia Kamati zao za Ulinzi na Usalama kwenye Mikoa, zisimamie agizo ambalo lilishatolewa na Serikali na leo Mheshimiwa Mbunge umeliuliza inawezekana mambo hayo bado yanafanyika huko na Serikali isingependa ione mnunuzi anakwenda kununua kwa mkulima na kumlazimisha amfungashie kwa lumbesa halafu anunue kwa bei ndogo ya gunia na lumbesa siyo gunia kwa sababu gunia ni lile limeshonwa kiwandani, lina vipimo na linahitaji kushonwa pale juu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikiri kwamba wako Wafanyabiashara wajanja wajanja na sisi Serikali tuko macho na sasa kupitia agizo hili kwa wafanyabiashara kwenye Halmashauri za Wilaya na maeneo yote lakini pia lishuke mpaka chini kwa Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata pale ambapo kuna biashara ya mazao kwenye maeneo yao, waendeleo kudhibiti kwamba ufungashaji wa mizigo hiyo na ununuzi haununuzi kwa kigezo cha lumbesa badala yake ununuzi kwa vigezo vya *kilogram* au kwa gunia ambalo ni rasmi kutoka viwandani. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Saumu ameridhika nashukuru. Mheshimiwa Selemani Kaunje, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini swali lako.

MHE. HASSAN S. KAUNJE: Mheshimiwa Spika, nishukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la moja kwa moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza tunafahamu kwamba maji ni uhai na Sera ya Taifa ya Maji inahitaji kila mwananchi kuweza kuyafikia maji ndani ya umbali wa mita 25. Je, Serikali ya Awamu ya Tano imejipangaje kuhakikisha maji haya yanawafikia wananchi *especially* wananchi wa Mkoa wa Lindi ambao wanatatizo kubwa sana la maji?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kaunje, amekuwa anafuatilia sana mwenendo wa maji na hasa alipoweka kule mwishoni hasa wananchi wa Mkoa wa Lindi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Sera ya Maji nchini imetamka wazi kwamba Serikali itasambaza maji kwa wananchi wake kote nchini mpaka ngazi za vijiji tena kwa umbali usiozidi mita 400 hiyo ndiyo sera na wakati wowote Wizara ya Maji inapofanya kazi yake inafanya kazi kuhakikisha kwamba sera hiyo inakamilika. Iko mipango mbalimbali na nadhani Wizara ya Maji itakuja na bajeti hapa ikiomba ridhaa yenu muipitishe Waheshimiwa Wabunge ili tukaendeleo kutekeleza hiyo sera ya kusambaza maji, na mikakati yetu sisi, maji lazima yawe yamefika kwenye ngazi za vijiji kwa asilimia mia moja ifikapo mwaka 2025 na ikiwezekana kufikia mwaka 2020 hapa kwa zaidi ya asilimia tisini huo ndiyo mkakati wetu. Mkakati huu utatokana tu kama tukaendeleo kupata fedha nyingi Serikalini na kuzipeleka Wizara ya Maji ili Wizara ya Maji waendeleo na mkakati ambao wanao.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa malengo haya tunakusudia kusambaza maji kwenye maeneo yote ya vijiji na maeneo ya miji ili wananchi wetu waweze kupata tija ya maji kwenye maeneo haya. Kwa miradi ambayo ipo, ambayo imeelezwa kwamba ipo inaendelea kutekelezwa, tunaamini miradi hiyo kwa watu wote ambao tumewapa kazi hiyo wataendelea kutekeleza kadri ambavyo tunawalipa fedha zao ili waweze kukamilisha. Waliokamilisha wakamilishe miradi ambao hawajakamilisha tunaendelea kuwapelekea fedha ili waweze kukamilisha ili maji yaweze kutolewa na kila mwananchi aweze kunufaika na sera hiyo ya Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Kaunje kama una swali la nyongeza.

MHE. HASSAN S. KAUNJE: Mheshimiwa spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, sababu zinazosababisha muda mwingine kutokupatikana maji ni pamoja na wakandarasi ambao wanakuwa wamelipwa lakini wanashindwa kukamilisha miradi ya maji kwa wakati na sababu hizo ni pamoja na mradi wa Ng'apa ambao uko Lindi. Je, ni hatua gani zinachukuliwa na Serikali dhidi ya wakandarasi wa aina hii ili maji yaweze kuwafikia wananchi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu langu la msingi, suala la wakandarasi wetu kwa sababu malengo ya Serikali tunawapa hizi kazi ili waweze kuzimaliza katika kipindi kifupi sasa kama inatokea mkandarasi hawezi kamaliza kazi kwa kipindi kifupi, ziko sababu mbalimbali ambazo pia tumezizoea maeneo mengine, malipo kutoka kwa kuchelewa nako kutokana na tatizo la fedha inawezekana mkandarasi hajamaliza. Lakini malengo yetu kama mkandarasi analipwa vizuri na kwahiyo basi anatakiwa akamilishe mradi huo kwa wakati uliokubalika. Lakini ikitokea mkandarasi hajamaliza kama kuna tatizo la fedha hilo ni juu ya Serikali kupitia Wizara ya Fedha kukamilisha kulipa madeni ili mradi ukamilike. Kama mkandarasi amelipwa fedha zote au zaidi ya asilimia 90 na hajakamilisha kwa kipindi kinachotakiwa, zipo taratibu za kisheria za kufanya kwa sababu ameingia zabuni kisheria na kwa hiyo, tunaweza tukatumia utaratibu wa kisheria pia kwa kuadhibu mkandarasi ambaye hajamaliza kazi lakini pia amelipwa fedha.

Sasa sina uhakika na mradi wa Lindi uko katika sura gani na kama ingekuwa session hii inaweza kumpa Waziri Mkuu nafasi ya kupata majibu sahihi ningweza kukupa jibu sahihi la mradi huo wa Ng'apa.

SPIKA: Tunakwenda CHADEMA Mheshimiwa Lucy Simon Magereli.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la moja kwa moja kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano ni kuipeleka Tanzania kuwa Tanzania ya viwanda na ziko changamoto zinazokabli mpango huo na moja ni namna ya kuwawezesha wazalishaji na wafungashaji wadogo katika *level* za Halmashauri kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa. Tunafahamu uwepo wa *GS1* ambayo inalengo la kuwasaidia wazalishaji na wafungashaji hao kupata *barcodes* ili waweze kuuza bidhaa zao. Mwaka jana Waziri Mheshimiwa Mizengo Pinda alitoa maelekezo ya maandishi akielekeza TAMISEMI iagize halmashauri zote zitoa ushirikiano kwa *GS1* ili waweze kuwasaidia hao wazalishaji na wafungashaji wadogo kupata *barcodes* kitu ambacho kinge-*stimulate* uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo...

SPIKA: Mheshimiwa Lucy sasa swali.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Spika ahsante, ningetamani nimalizie, *anyway*.

Nini sasa Kauli ya Serikali hasa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika kusimamia na kutekeleza maelekezo haya ambayo tayari yalishatolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu aliyepita ili kuwasaidia wazalishaji na wafungashaji wadogo hawa?

SPIKA: Mheshimiwa waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Serikali inayo mkakati, tunaendelea kuhamasisha wajasiriamali wadogo kujiendeleza kupitia viwanda vidogo vidogo na msisitizo huu wa Serikali wa viwanda unajumuisha viwanda vikubwa, vya kati na vidogo kwa lengo lile lile la kumtaka Mtanzania aweze kunufaika na hasa katika kuongeza thamani ya mazao ambayo tunayazalisha nchini.

Tumeendelea kuwa na mipango mbalimbali ambayo Serikali inaunga mkono jitihada za wazalishaji wadogo ikiwemo na uwekaji wa *barcodes* ambayo pia inamsaidia kupata bei na thamani nzuri ya mazao ambayo mjasiriamali anajihusisha katika kuchakata kwenye michakato ya awali kwa maana *processing* hii ya wali.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu bado unaendelea na tumeagiza utaratibu huu wa *barcodes* uendeleo lakini pia tumehusisha *TBS*, *TFDA* kuhakikisha kwamba chakula tunachokizalisha kinakuwa na ubora ili tukikipa

barcode, Taifa liweze kuuza bidhaa hiyo nje ya nchi na ndani ya nchi ambako tunaweza kupata fedha nyingi na wajasiriamali waweze kunufaika zaidi.

Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie tu kwamba utaratibu huo bado unaendelea ili kuweza kuipa thamani mazo yetu lakini kuwapa uwezo mkubwa wa kusafirisha bidhaa zao nje na kuzipa soko ili ziweze kuwaletwa tija Watanzania na tutaendelea pia kusimamia jambo hilo kuwa linaendelea kukamilika. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Lucy nimekuona umesimama.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilichotamani kusikia kutoka kwako ni tamko lako kama Serikali kuziagiza Halmashauri kutoa ushirikiano kwa *GS1* lakini *TFDA*, *TBS* na washirika wengine ikiwemo Wasajili wa Viwanda wa Makampuni kwa sababu hiyo ni timu inayofanya kazi pamoja. Changamoto hiyo imekuwa kubwa kwa sababu ya kupata *resistance* kutoka kwa Halmashauri, lengo mlilolianzisha lilikuwa jema lakini Halmashauri hazitoi ushirikiano na kutotoa ushirikiano zinawanyima fursa wazalishaji na wafungashaji wadogo kupata fursa hiyo.

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimekusikia kwa namna ambavyo ume-experience huko ambako umeona kwamba Halmashauri zetu hazitekelezi maagizo yetu ambayo tunayatoa na inawezekana siyo Halmashauri tu ziko pia nyingine ambazo pia zinafanya jambo hilo hilo. Kwa hiyo, nilichukue jambo lako baada ya kikao hiki nitawasiliana na Waziri wa TAMISEMI kuhakikisha kwamba maagizo yetu ya Serikali yanatekelezwa na wazalishaji wetu wadogo wanapata nafasi.

Lakini pia Wizara ya Kilimo nayo pia ilichukue hili kwa sababu tunayo Maonesho ya Kilimo ambayo sasa tumeyaanzisha katika kanda mbalimbali, hawa wajasiriamali wadogo wapate nafasi za kwenda kuonyesha bidhaa zao kwenye maonyesho yale ili pia waweze kutangaza soko lao, waonyeshe ubora wao na sasa Halmashauri zisimamie wajasiriamali wadogo hao kwenda kwenye maonyesho hayo ili kuonyesha kazi zao ziweze kuleta tija zaidi huo ndiyo msisitizo wa Serikali. (Makofi)

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo CCM, nimpe mwanamama ambaye hajawahi kuuliza, Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sera ya elimu ya nchi yetu sasa inasema ni kupata elimu bure lakini hii bure ina maana inalipiwa na Serikali. Lakini kumekuwa na kundi dogo la wazazi wengine ambao kwa kuchangia kupitia kodi zao ndizo ambazo zinatumika kusomesha watoto wao ama kugharamia elimu lakini kundi hili limekuwa likilipa kodi zote zinazotakiwa kulipwa lakini wamekuwa wakichajiwa mara mbili (*double taxation*) kupitia watoa huduma wa elimu katika taasisi binafsi.

Je, nini kauli ya Serikali ili kwamba na hawa wananchi amba tayari walikwisha kulipa kodi na kuchangia elimu bure na wenyewe waweze kufurahia keki hii ya elimu bure? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Ester swali lako hili lingesubiri Mheshimiwa Profesa Ndalichako muda mfupi ujao? Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo umesema, kwamba swali limechanganywa sana haliko wazi mno na haya ni maswali ya papo kwa papo inatakiwa liwe-clear ili na mimi niweze kujibu kitu halisi ili pia naye aweze kunufaika na majibu lakini pia Watanzania ambao wanasikia kipindi hiki waweze kujua jambo gani limeulizwa na jambo gani ambalo linatakiwa kujibiwa.

Lakini pia, amezungumzia suala la elimu bure na ni jambo ambalo watu wengi limekuwa likiwachanganya na wengine kupotosha, naomba nitoe ufafanuzi huu ufuatao ili Watanzania wajue kwamba elimu bure ni mkakati unaolenga Kurugenzi ya Msingi na Sekondari na hasa katika kuwapunguzia mzigo wazazi wa kuchangia changia michango mbalimbali shuleni.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumeanza na maeneo ambayo tumeona wazazi walikuwa wanakwazwa sana. Tumezungumza mara kadhaa lakini narudia kwamba moja kati ya maeneo hayo tumeondoa yake malipo yaliyokuwa yanaitwa ada kwa sekondari, shilingi 20,000 na shilingi 70,000. Pia kulikuwa na michango ya ulinzi, maji, umeme pale shuleni michango ile yote ile sasa Serikali imetenga fungu kwa ajili ya kuipa shule ili iweze kulipia gharama hizo, lakini suala la mitihani mbalimbali nayo pia ni eneo Serikali imeamua kulichukua kwa sababu gharama za mitihani zitafanywa na Serikali ili wazazi wasiingie kwenye michango hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunaendelea kuona ni maeneo gani mengine ambayo wazazi yanawakwaza zaidi katika kuchangia, sasa kama kuna mzazi anachangia huku nje hata kama analipa kodi maeneo mengine, ni jukumu tu la kuona kwamba kuna umuhimu wa kuchangia sekta ya elimu na kwamba yeye kama Mtanzania anayo nafasi ya kuchangia mahali popote bila kujali kama mchango huo pia unagusa kodi ambazo alikuwa anazilipa kule awali.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, tutoe wito kwa Watanzania, kwanza tupe subira Serikali kuona maeneo mengine zaidi ambayo tunaweza tukaboresha ili kumpunguzia mzazi mzigo wa kuweza kusomesha watoto hawa.

Sasa lawama inakuja pale ambako tumetoa nafasi hizi tumegundua kwamba kuna watoto wengi wa Kitanzania walikuwa hawapelekwi shuleni na kwa kuondoa hizi gharama, gharama watoto wengi wanapelekwa shule na sasa tumeanza kuona uzoefu wa kwamba watoto wengi wameendelea kusajiliwa shuleni, idadi imekuwa kubwa na kumekuwa na changamoto nyingine kama madawati na vyumba vya madarasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Watanzania, kwamba Serikali inaendelea kuweka utaratibu wake kwa ajili ya kuongeza madawati lakini pia miundombinu ya vyumba vya madarasa ili watoto wetu ambao sasa tumebaini kuwa wamekuwa wengi waweze kupata mahali pa kukaa na chumba ambacho wanaweza kupata taaluma yao. Lakini hatuzuii mlipakodi yeyote wa sekta nyingine kuchangia kujenga madarasa kwa haraka ili watoto wetu waingie ndani, kutoa madawati kama ambavyo tumeona Watanzania wengi wamejitokeza, makampuni mengi yanachangia lakini pia hata baadhi ya Wabunge tumeona mkitoa mchango wenu, na mimi nataka nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wabunge ambao pia mmeanza kuunga mkono jitihada za Serikali kuchangia madawati. Jambo hili ni letu sote, watoto ni wetu sote hebu twende pamoja, tutoe elimu hiyo ya kuchangia kwa namna mtu anavyoweza kwenye madawati, kama una uwezo wa kujenga chumba cha darasa ili watoto wetu waweze kusoma ndani, lakini Serikali inaendelea na mkakati pia wa ujenzi wa maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa nitamke hili ili wale wote wanaodhani kulundikana kwa watoto sasa ni jambo la makusudi, hapana, ni jambo ambalo tuliona ni muhimu tupunguze michango, lakini Wazazi ambao walikuwa wanashindwa kuleta watoto nao wapate kupeleka watoto, wamepeleka watoto wengi ni jukumu letu sasa kujenga vyumba na kupeleka madawati. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana, sana. Tunakushukuru sana kwa majibu ya ufasaha. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge mliokuwa mmeomba mlikuwa 17 kwa muda wetu isingewezekana na ninyi mnaona jinsi ambavyo nimejaribu kuvuta vuta hivi lakini bado muda haukuruhusu kabisa kwamba wote 17 mpate nafasi. Swali la mwisho la Mheshimiwa Ester Mahawe, baadae kabisa nilipata picha ambayo sina uhakika kama ni kweli, kwamba anamiliki shule.

Nilitaka tu kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge katika mambo ambayo tuna-*conflict of interest*, unachofanya una-*declare* tu kwanza kama Kanuni zetu zinavyotaka kusudi tusije tukawa tunauliza maswali ambayo tuna maslahi nayo ya moja kwa moja. Katibu.

NDG. JOHN N. JOEL -KATIBU MEZANI: Maswali ya kawaida.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali, swali la kwanza tunaelekeza Ofisi ya Mheshimiwa Rais, TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

Na. 194

Halmashauri Kutekeleza Maagizo ya Serikali Kuu

MHE. HAWA M. CHAKOMA aliuliza:-

Utekelezaji wa maagizo ya Serikali Kuu kwa Halmashauri imekuwa ni changamoto na mzigo mkubwa kwa Halmashauri hizo hususan Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ambapo maagizo mengi hayamo kwenye Mpango wa Bajeti na hivyo utekelezaji unakuwa mgumu.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha maagizo hayo yanatengewa bajeti?

SPIKA: Majibu ta swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Said Jaffo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kwa nyakati tofauti Serikali imekuwa ikitoa maagizo ya kiutendaji katika Halmashauri zetu nchini na si kwa Halmashauri ya Kibaha pekee ikiwa na lengo la kuhakikisha kuwa inatatua changamoto ambazo Halmashauri zinaikabili kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maagizo hayo ya hutolewa na Serikali huhitaji fedha. Maagizo hayo huingizwa kwenye mipango na bajeti ya Halmashauri yanapotolewa kabla ya bajeti kupitishwa, hata hivyo baadhi ya maagizo na maelekezo hutolewa na Serikali katikati ya mwaka wa bajeti, maagizo na maelekezo ya Serikali ambayo hukosa kabisa fedha katika mwaka husika huingizwa katika bajeti za Halmashauri ya mwaka wa fedha unaofuata kwa ajili ya utekelezaji au Halmashauri hufuata utaratibu wa kurekebisha bajeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuzihimiza Halmashauri zote nchini, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kuendelea kutenga fedha katika mpango na bajeti yao ili ziweze kutatua changamoto zinazowakabili.

SPIKA: Mheshimiwa Chakoma, swali la nyongeza.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri Jafo mpaka sasa tunavyoongea baadhi ya shule za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ikiwemo Shule ya Sekondari Magindu, Shule ya *Ruvu Station* na Shule ya Dosa Aziz katika kutii agizo la Serikali Kuu la kujenga maabara katika shule zetu za sekondari inakabiliwa na madeni makubwa ya wazabuni pamoja na mafundi. Swali langu la kwanza, ninaomba kauli ya Serikali, je, itakuwa tayari ku-clear madeni hayo ili kutua mzigo Halmashauri zetu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ni lini sasa Serikali Kuu itaacha kubebesha mizigo Halmashauri kwa kutoa maagizo nje kabisa ya bajeti ya Halmashauri ya kuzitaka zitekeleza maagizo ya Serikali kuu ikiwemo hili agizo jipya la kila mtoto kukalia dawati pasipo kuwatengea fungu maalum. Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Majibu ya swali hilo lililopigiwa makofi mengi Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ni kweli Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa agizo la ujenzi wa maabara na agizo lile lilikuwa ni agizo la kimkakati. Kwa sababu shule nyingi sana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa hizi shule za kata zilikuwa zina upungufu wa maabara. Sambamba na hiyo watoto walikuwa wakienda shuleni wanakosa fursa ya kupata masomo ya sayansi, kwa mtazamo ulio makini ndiyo maana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

alitoa agizo hilo. Lakini naomba niseme wazi kwamba agizo lile limeleta manufaa makubwa sana kwa watoto wetu wanaosoma shule za kata. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hili niwapongeze Watanzania wote kwa ujumla wamejitahidi katika kila eneo moja kufanya fursa, hata Halmashauri ya Kibaha najua walikuwa na mchakato wa kujenga takribani maabara nane, changamoto iliyokuwepo ni upatikanaji wa fedha ilikuwa ni changamoto kubwa kwa sababu Kibaha peke yake walichanga shilingi milioni 218. 6 lakini bahati mbaya upelekaji wa fedha haukuwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie suala la upelekaji wa fedha lilikuwa sio suala la sekta ya elimu peke yake, mnakumbuka hata miradi ya maji ilisimama ndiyo maana ajenda kubwa ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliposhika madaraka aliazimia kuhakikisha kwamba kodi inakusanywa ili mradi kulipa madeni ya wakandarasi wa aina mbalimbali. Hili naomba niseme pale kuna wakandarasi wanadai na niseme Serikali inalitambua hilo na juhudi ya Serikali itaendelea kukusanya kodi ili mradi kulipa madeni ya wakandarasi kwa kadri iwezekanavyo kuweza kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni lini Serikali sasa itaacha kutoa maelekezo haya. Naomba niwaambie ndugu zangu, Serikali inapima nini kifanyike katika muda gani na hivi sasa mnakumbuka kuna maagizo mbalimbali yametoka lakini lengo lake kubwa ni kuisaidia jamii.

Kwa hiyo, naamini maagizo yote yaliyotolewa na Serikali ni maagizo na kuona ni uhitaji wa kiasi gani uweze kufanyika kwa ajili ya kutatua matatizo ya Watanzania. Lakini hili nililosikia kwamba kila mtoto achangie dawati, hili nadhani ngoja tutalifanyia kazi kwa sababu maagizo yetu ya Serikali kama watu watachangia ni wadau wenyewe katika maeneo husika wanajihamasisha kama tunavyoona hivi sasa, na juzi nishukuru nilikabidhi madawati hapa Dodoma. Watu/wadau waliamua kuchangia madawati lakini siamini kama kuna watu wanalazimishwa kuchangia madawati kwa sababu hizo ndiyo miongoni mwa kero tuliamua kuzitatua katika Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ili mradi mwananchi wa kawaida aweze ku-access elimu ya mtoto wake. Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Jamani leo ndiyo siku ya elimu kwa nini hatumpi nafasi Profesa aje, nimemuona Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

MHE. FREEMAN H. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri.

Maadam Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba maelekezo ambayo Serikali Kuu inatoa kwa Serikali za Mitaa yanasimamiwa ama yanasimamia msingi wa nia njema na kwa sababu tunakubaliana katika utawala wa nchi, nia njema haiwezi ikazidi utaratibu uliowekwa kwa sheria, kanuni na taratibu za kiutawala na kwa sababu kumekuwepo na tatizo kubwa sana la muingiliano wa maelekezo hususan kwenye zile Hamlashauri za Wilaya ama Manispaa ambazo zinaongozwa na vyama tofauti na Chama cha Mapinduzi.

Je, ili kuweka utawala wa sheria, unaoheshimu mifumo yetu ya kiutawala iliyowekwa na sheria, Waziri haoni kwamba ni muhimu na busara sana Serikali ikatoa tamko katika Bunge hili kwamba viongozi katika ngazi ya Wilaya kwa maana ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa waache kuingilia majukumu ya Halmashauri za Wilaya na Manispaa ili kuruhusu maamuzi ya vikao vya Madiwani na wengine kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu za sheria?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba tuweke kumbukumbu sawa sawa, lengo letu Serikali za Mitaa zimeyekwa kwa mujibu wa Katiba Ibara 145 na utekelezaji wake unaelezewa katika Ibara 146; kwa hiyo, maana yake ni chombo halali ambacho kiko kwa mujibu wa sheria. Nimesema pale awali maelekezo hasa ya kutoka Serikali Kuu, maana yake kikubwa zaidi yanania njema kama Mheshimiwa Mbowe ulivyorejea hapa. Lakini anasema jinsi gani Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wasiingilie maamuzi, kinachofanyika ni kwamba Wakuu wa Mikoa na Wilaya sio wanaingilia, wanachokifanya ni nini? Kinachotakiwa hasa cha msingi ni kuona kama utaratibu unakiukwa pale Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya ana haki ya kuweza kulingilia hilo jambo lisiharibike kwa ajili ya maslahi ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani haiwezekani kikao halali cha baadhi ya Madiwani kimefanya ambayo hakuna utaratibu wowote uliokiukwa Mkuu wa Mkoa au Wilaya atakuwa ameingilia. Lakini kama kuna jambo linaenda kinyume na Mkuu wa Mkoa yupo, naye anaona jambo linaharibika kwa makusudi mbele yake ni lazima aingilie hapo ilimradi kuweka mambo sawasawa. Kwa sababu mwisho wa siku ni kwamba watu wanatarajia kwamba Serikali hiyo iliyowekwa kwa mujibu wa sheria basi itatimiza majukumu yake kama wananchi walivyoipa ridhaa itawaongoza katika kipindi hicho mambo yanayohitajika yaweze kufikiwa na yaweze kufahanikiwa. Kwa sababu sasa hivi Tanzania tunaongozwa kwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa ni kwamba kuanglia kama Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya aharibu utaratibu wa Baraza la Madiwani lakini wanahakikisha kwamba utekelezaji wa Ilani unakamilika kama ilivyokusudiwa na wananchi walioichagua Serikali hiyo. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Tunaenda na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na kwa Wizara zilizobaki kutakuwa hakuna swali la nyongeza hata moja. Swali la Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali. Kwa niaba ya Mheshimiwa.

Na. 195

Tatizo la Barabara Wilaya ya Kilombero

MHE. SUSAN L. KIWANGA (K.n.y. MHE PETER A. LIJUALIKALI) aliuliza:-

Wilaya ya Kilombero ni moja kati ya Wilaya zinazozalisha kwa wingi mazao ya chakula lakini barabara zake nyingi ni mbovu na hivyo kushindwa kusafirisha mazao kwa urahisi.

(a) Je, ni lini barabara ya Kidatu - Ifakara na Ifakara - Mlimba zitajengwa kwa kiwango cha lami?

(b) Je, ni lini daraja la Mto Kilombero linalounganisha Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga litamalizika?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Lijualikali, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Kidatu hadi Ifakara kwa kiwango cha lami umekuwa ukitekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika awamu ya kwanza Serikali ilijenga kilometa 10 kutoka Kijiji cha Kiberege hadi Ziginali ambapo kazi hii ilikamilika mwaka 2006. Katika awamu ya pili, Serikali ilijenga kilometa 6.17 kutoka Kibaoni hadi Ifakara Mjini ambapo kazi ilikamilika mwaka 2008.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali ilipata msaada kutoka Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa la *USAID* kwa ajili ya kugharamia kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara yote. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Kazi ya kuandaa nyaraka za zabuni na kutafuta Mhandisi Mshauri atakayesimamia ujenzi wa barabara inaendelea. Kazi ya ujenzi wa barabara ya Mikumi - Kidatu -

Ifakara itaanza mara baada ya kukamilika taratibu za ununuzi ili kumpata mkandarasi wa kujenga barabara hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ifakara - Mlimba kwa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya barabara kutoka Ifakara hadi Kihansi kilometa 126 ili kuunganisha na sehemu ya barabara ya lami yenye urefu wa kilometa 24 iliyojengwa hapo awali kati ya Kihansi na Mlimba. Kazi ya upembuzi yakinifu ipo katika hatua za mwisho na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016. Kazi ya usanifu wa kina inatarajiwa kuanza mara baada ya upembuzi yakinifu kukamilika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja la Kilombero ulianza tarehe 21 Januari, 2013 ambapo gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 55.97. Utekelezaji wa kazi ya ujenzi wa daraja la Kilombero umefikia 50% ambapo kazi inaendelea vizuri na inategemewa kukamilika mwezi Disemba, 2016.

SPIKA: Mheshimiwa Susan Kiwanga swali fupi la nyongeza.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante nimepokea majibu bahati nzuri naifahamu sana hii yote.

Kwa kuwa kwenye kikao cha RCC Mkoa tulipewa taarifa hiyo kwamba fedha hizo kweli za barabara ya Kidatu - Ifakara ina ufadhili wa *USAID*; nilitaka kujua sasa, mkandarasi huyu inachukua muda gani kwa sababu hela ipo tayari. Kwa hiyo, ili kumpata mkandarasi wa kuanza ujenzi barabara hiyo ningependa kupata majibu ya Serikali inachukua muda gani ili wananchi wa Kilombero wajue hii barabara inaanza kujengwa lini kwa kuwa hela ipo na upembuzi umeshafanyika? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mbili; kwa kuwa ujenzi wa daraja la Kilombero ulianza tarehe 21 Januari, 2013 na mimi nilienda kwenye uzinduzi wa ujenzi wa daraja hilo na ahadi ya Waziri wakati huo kwa wananchi waliambiwa ujenzi wa daraja utamalizika mwaka 2015. Leo mnasema Disemba, 2016. Kwa kuwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika lile daraja walitoa taarifa kwangu na kwa Peter Lijualikali kwamba kule chini kuna crack jamani, je, kwa taarifa hizi ambazo wafanyakazi wapo na unasema daraja linaendelea vizuri ingawa si kweli sio asilimia 50, je, Serikali iko tayari sasa kwenda kufanya utafiti lile daraja kabla halijaenda mbali zaidi tuangalie...

SPIKA: Mheshimiwa Susan Kiwanga swali!

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Madhara yanayoweza kujitokeza katika daraja hilo kabla ya kuendelea?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Mbunge wa Mlimba, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano *Engineer* Edwin Ngonyani

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, tulieleza tarehe 27 Januari, wakati Mheshimiwa Peter Lijualikali alipouliza swali la nyongeza kuhusiana na hilo hilo kwamba tulilazimika kubadilisha muda kutokana na upatikanaji wa fedha. Hatuna namna, fedha hazikupatikana, kwa hiyo, hilo suala tunalikamilisha kadiri fedha zitakapokuwa zinapatikana. Kwa hiyo, kwa upande wa *USAID* ni kweli fedha zipo utaratibu wa kumpata mkandarasi ni lazima tuufuate kwa sababu tukiwaharakisha hata *USAID* wenyewe hawatatoa hizo fedha. Kwa hiyo, naomba tuvumiliane taratibu za *ki-procurement* zikamilike kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa suala la pili mimi naomba tu nimjulishe kwamba katika Wizara ambayo ina wataalam ni pamoja na sekta ya ujenzi. Naomba aamini suala hilo analoliongelea la *crack* ni la kitaalam, naomba tuwaachie wataalam na kwa mujibu wa wataalam wanaosimamia pale kazi ya ujenzi wa daraja hili itakamilika mwezi Disemba, 2016.

SPIKA: Ahsante sana tunaendelea na Wizara hiyo hiyo swali la Mbunge wa Itilima, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga.

Na. 196

Ujenzi wa Barabara ya Maswa – Itilima

MHE. NJALU D. SILANGA aliuliza:-

Mkandarasi katika barabara ya kutoka Mwegusi - Maswa tayari ameshapatikana na yuko eneo la kazi.

Je, ni lini barabara ya kutoka Maswa - Itilima - Bariadi itapatiwa mkandarasi kwa ajili ya kuunganisha kipande hicho cha barabara?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Maswa – Itilima hadi Bariadi ni sehemu ya mradi wa barabara kuu ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi hadi Lamadi yenye urefu wa kilometa 171. Mradi huu umegawanywa katika sehemu kuu tatu; sehemu ya Mwigumbi hadi Maswa - kilometa 50.3, sehemu ya Maswa hadi

Bariadi - kilometa 48.9; na sehemu ya Bariadi hadi Lamadi - kilometa 71.8. Mradi huu wa barabara ya kutoka Mwigumbi - Maswa - Bariadi hadi Lamadi unatekelezwa kwa awamu kwa kugharamiwa na Serikali kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Bariadi hadi Lamadi - kilometa 71.8 umekamilika. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Mwigumbi hadi Maswa - kilometa 50.3 unaendelea kutekelezwa. Aidha, kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Maswa hadi Bariadi yenye urefu kilometa 48.9 ambapo ujenzi utaanza baada ya fedha kupatikana.

SPIKA: Mheshimiwa Silanga, swali la nyongeza.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lini sasa kauli ya Serikali hiyo barabara kipande cha kilometa 48 kitakamilika?

SPIKA: Majibu ya swali hilo zuri fupi sana Mheshimiwa Naibu Waziri, lini?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la awali kwamba tunatafuta fedha ili kuanza kujenga barabara hii na mara tutakapopata fedha tutaanza kujenga barabara hii. Kutaka *commitment* ya Serikali kuhusu lini tutamaliza nadhani ni mapema mno. Naomba wananchi watuvumilie na Mheshimiwa Mbunge mtuvumilie tukipata fedha tutaanza kujenga na tutawajulisha wakati huo lini tutaweza kukamilisha.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma.

Na. 197

Ujenzi wa Bomba la Maji Toka Mto Ruvuma

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA aliuliza:-

Miundombinu ya maji Mtwara na mikoa yote ya Kusini mwa Tanzania ni hafifu na wakazi wengi wa miji ya Kusini na vijijini hawapati maji safi na salama.

Je, Serikali iko tayari kujenga bomba la kuvuta maji toka Mto Ruvuma ambalo limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu bila mafanikio?

SPIKA: Hivi Mtwara Mjini ilipotea eeh? Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer Isack Kamwelwe*.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara pamoja na vijiji 25 vitakavyopitiwa na bomba kuu ndani ya kilometa 12 kila upande, kazi hiyo imekamilika mwezi Julai, 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na majadilinao na Serikali ya China kwa ajili ya kupata mkopo nafuu wa utekelezaji wa mradi huo. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa chanzo, mtambo wa kutibu maji, bomba kuu la kupeleka maji Mtwara Mikindani, matanaki pamoja na mabomba ya kusambazia maji.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa swali langu lilikuwa na sehemu mbili hivi, lakini limejibiwa swali moja tu.

Nilikuwa nimezungumza kwamba tatizo la maji kwa Mikoa hii ya Kusini na hasa miundombinu yake ambayo imejengwa tangu ukoloni ni miundombinu hafifu sana. Kwa mfano, mradi ule wa maji wa Makonde umejengwa mwaka 1953 na mpaka hivi sasa navyozungumza unatoa maji kwa asilimia 30 tu kwa sababu ya miundombinu yake ni hafifu. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa katika majibu yake ya msingi Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala zima la mradi wa maji wa Mto Ruvuma na akasema kwamba upembuzi yakinifu umekamilika na wananchi watapata maji na vijiji takribani 25 vinavyopitia lile bomba ambalo linatarajiwa kujengwa wataweza kunufaika na mradi huu wa maji.

Mheshimiwa Spika, swali tangu mwaka 2015 mpaka hivi sasa navyozungumza wale wananchi wameambiwa maeneo yale ambayo maji yatapita au ule mradi utapita wasiendeleze yale maeneo na hawajalipwa fidia hata senti moja mpaka hivi sasa, je, ni lini wale wananchi watapewa fidia ili waweze kutumia zile fedha kwenda kununua maeneo mengine waweze kuendeleza kilimo?

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kilio kikubwa sana Mtwara Mjini na maeneo mengine ya Kusini, kwamba watendaji wa Idara za Maji wanavyokuja kusoma mita hawasomi zile mita na wamekuwa wakikadiria malipo ya mita kila mwezi, wanaona usumbufu kwenda kuzipitia mita wakati mwingine na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi na kuwabambikia fedha nyingi za kodi ya maji kinyume na taratibu na kanuni. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka huu mwezi wa pili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji alitembelea kule Mtwara na wananchi waliandamana kwa ajili ya tatizo hili, naomba atoe majibu ya uhakika kwamba ni lini sasa Serikali itakoma kukadiria mita za maji...

SPIKA: Mheshimiwa Nachuma yaani umehutubia.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: ...na badala yake waende kusoma mita?
(Makofi)

SPIKA: Yaani mkutano wa hadhara hasa Mheshimiwa Nachuma.
(Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana muda haupo upande wetu kabisa, Mheshimiwa Waziri wa Maji amesimama, Mheshimiwa Naibu mwachie boshi wako.

MBUNGE FULANI: Murji, Murji.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nitoe majibu ya nyongeza kwa maswali mawili aliyouliza Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma mpaka Mtwara ni kweli tumezungumza kwa muda lakini Serikali imedhamiria kuujega mradi huu kwa kutumia utaratibu wa PPP, imeshapata mbia ambaye atatafuta fedha kwa maana *building and finance*, Serikali yenyewe itachangia kwa kuweka msimamizi atakayesimia. Kazi ambazo tunafanya sasa ni kufanya *due diligence* ya ile kampuni kama ina uwezo wa kufanya kazi hii na tuko kwenye hatua ya mwisho na ndio maana tumesema kuanzia mwaka wa fedha huu unaoanza mwezi wa saba tunaweza kuanza kujenga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa tutakapokuwa tumekamilisha hatua zote hizi ndio tutakapolipa fidia ya wale wananchi ambao mradi utapita hatutaweza kulipa fidia kabla hatujakamilisha majadiliano na ile kampuni ambayo itajenga ili kusudi tuwe na uhakika kwamba wale wanaohusika wote na watakaoathirika na mradi huu wataweza kulipwa. Lakini katika swali lake la pili la kwamba ni lini Serikali itaacha kukadiria, ninafikiri suala la kukadiria mita siyo utaratibu

tunasema kila mtu atalipa maji kulingana na namna anavyoyatumia. Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo bado yana utata kuhusu ukadiriaji hili mtuachie tutalifanyia kazi ili tuhakikishe kwamba kila mmoja alipe maji kwa kadri anavyokuwa ameyatumia, ahsante.

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

Na.198

Magari Yanayojaza Abiria Kutozwa Faini

MHE.FAKHARIA SHOMAR KHAMIS aliuliza:-

Magari yanayobeba abiria nchini yamekuwa yakitozwa faini pindi yanapokamatwa kwa kosa la kujaza abiria zaidi ya uwezo wake badala ya kutakiwa kupunguza abiria waliozidi.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kutoza faini na kuacha gari liendelee na safari huku likiwa limejaza ni sawa na kuhalalisha kosa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ikiwashusha abira waliozidi itakuwa imetoa fundisho na kupunguza ajali kwa abiria ambao hupanda gari huku wakijua limejaa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabani Sura ya 168, kifungu cha 58 ni kosa kwa abiria au mtu yeyote kutokuwa na kiti cha kukaa ndani ya gari la abiria na hivyo mtu huyo atahesabika kwamba amening'inia ndani ya gari hilo. Mabasi yanatozwa faini kwa kuzidisha abiria yakiwa kituoni na maeneo salama abiria wote waliozidi huteremshwa na kurudishiwa nauli zao na utaratibu wa kuwatafutia mabasi mengine ambayo yana nafasi. Aidha, pale ambapo mabasi haya yalizidisha abiria yakikamatwa katika maeneo ambayo si salama huachwa na kuendelea na safari kisha mawasiliano hufanyika katika vituo vya polisi vilivyopo mbele ili abiria washushwe kwenye maeneo ambayo ni salama kwa abiria.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani imekuwa ikiwashusha abiria waliozidi ndani ya basi hasa pale inapokuwa imeonekana maeneo wanayoshushwa ni salama kwa maisha na mali za abiria hao na kutafutiwa usafiri mwingine.

SPIKA: Mheshimiwa Fakharia swali la nyongeza.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Ahsante Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa ajali zinazotokea huacha athari nyingi mfano vifo, ulemavu, uharibifu wa mali na hata ya mayatima, je, kwa nini Serikali sasa isianzishe Mfuko wa Ajali yaani *Accident Fund* kwa ajili ya wahanga wanaofikwa na matatizo hayo? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili kwa nini wale abiria wanaopanda ndani ya gari ambao umetuambia kwamba mnawashusha na kuwarejeshea fedha zao. Ningeona kwa nini na wao wasingetozwa faini ikawa kama ni sehemu ya wengine kuogopa kupanda magari ambayo watu wamezidi? Wakiona wanatozwa faini najua na wale watakuwa kama kigezo kwamba nikiingia kwenye gari hii na mimi nitatozwa faini wakati gari imejaa? Naomba Mheshimiwa unijibu.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ametoa ushauri kwamba tuanzishe mfuko kwa ajili ya wahanga wa ajali hizi lakini pia ametoa ushauri kwamba abiria ambao wamezidi kwenye mabasi nao washitakiwe kwa maana ya kulipishwa faini. Naomba tu nishauri kwamba mapendekezo yake haya mawili niyachukue kwa ajili ya kuyafanyia kazi.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa kwa sababu ya muda naomba mniwie radhi, mkiangalia saa yetu wenyewe mtakuwa mashahidi kwamba muda hauko upande wetu.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusiana na wageni walioko katika jukwaa la Spika, ninao wageni sita wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, ambao ni viongozi wa taasisi ya *Islamic Help UK* ambayo ni NGO kutoka Birmingham, Uingereza wakiongozwa na Ijazi Ahmed Shami Imamu Mkuu wa Birmingham, UK. Asanteni sana, karibuni sana wageni wetu kutoka Uingereza. (Makofi)

Pia wako wageni wa Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, Waziri wa Nishati Na Madini, ambao ni Profesa Justin Ntalikwa, Katibu Mkuu wa Wizara, ahsante, Profesa James Mdoe, Naibu Katibu Mkuu - Madini na Dkt. Juliana Pallangyo, Naibu Katibu Mkuu - Nishati. Pia tuna Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Nishati na Madini, Wakuu wa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hiyo, Makamishina, Wakurugenzi, Mameneja Wakuu wa Miradi na Maafisa wengine kutoka Wizara ya Nishati na Madini, karibuni wote. (Makofi)

Wageni na Waheshimiwa Wabunge; wageni 20 wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu ambao ni wanafunzi wanaotokea Muheza, wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana Wanamuheza karibuni sana. Pia kuna wageni 42 wa Mheshimiwa Antony Mavunde ambao ni wachezaji wa timu ya mpira ya *Muungano Sports Club* ya Dodoma. Karibuni sana Muungano ninyi wanyakaya, kwa hiyo karibuni sana nyumbani. (Makofi)

Wageni watano wa Mheshimiwa Ally Ungando ambao ni ndugu zake kutoka Rufiji, Mkoa wa Pwani. Ahsante sana wageni kutoka Rufiji natumaini mmetuletea samaki huko. Kuna wageni 11 wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Ushindi ya Mbunge wao. Ninyi wageni kutoka Urambo wapi Profesa Kapuya? Mambo haya mazito haya. (Makofi/Kicheko)

Wageni wa Mheshimiwa Ally Ungando ambao ni ndugu wa Mheshimiwa kutoka Kibiti wakiongozwa na Mheshimiwa Kusa Kisoma ambao ni Diwani wa Ngorongo, pamoja na Ndugu Kassim..., no, hapana, ahsante. (Makofi)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji ambao ni Diwani wa Kata ya Ngorongo, ndugu Mussa Bakari Kisomo na Kassimu Mussa Matea - Mwenyekiti wa Kijiji cha Ngorongo. Kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga, ambao ni wawakilishi wa wachimba madini wadogo kutoka Ulanga, Mkoa wa Morogoro wakiongozwa na ndugu Christom Msakamba - Mwenyekiti wa wachimba madini. (Makofi)

Wageni 12 ambao ni waalimu kutoka vyuo vya ufundi vya VETA kutoka mikoa mbalimbali wakiongozwa na ndugu Dominic Safari - Mratibu wa Mafunzo, wageni kutoka VETA, karibuni sana. Kuna wageni watatu wa Waheshimiwa Wabunge wote wa Geita ambao ni ndugu Leonard Kiganga - Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Mheshimiwa Adam Mbaraka - Mwenyekiti wa Wazazi CCM Geita na Mheshimiwa Malimi Saguda - Diwani wa Kata ya Nyawayeye. (Makofi)

Mgeni wa Mheshimiwa Halima Bulembo ambaye ni ndugu Fadili Hezekia, Mfamasia kutoka kampuni ya *Novorodisc Phramacetical Company* karibu sana.

Pia kuna wageni watatu kutoka chuo kikuu cha UDOM ambao ni wahadhiri Dkt. Remigius Andrew, Dkt. Amani Sagula Hilla na Dkt. Lugano Wilson. (Makofi)

Wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Tiba cha Afya Muhimbili Dar es Salaam, karibuni sana mjifunze Bunge linavyofanya kazi. (Makofi)

Mwisho wanafunzi 19 kutoka Taasisi ya Vijana inayoitwa DOYODO ya Mjini Dodoma. Wanafunzi kutoka DOYODO karibuni sana, karibuni ninyi wa kutoka hapa Dodoma. Sikumbuki kama niliwataja wageni wa Mheshimiwa Shangazi, ndugu Ejazi Ahmedi Shami, ndugu Ahmed Salim, ndugu Farouq Shahazad, ndugu Sultani Niaz na ndugu Shukuru Mohamed, karibuni sana hawa wageni wametoka Mlalo. (Makofi)

Matangazo ya kazi ni la Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu anaomba Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, saa saba mkutane Msekwa C. Pia Kamati ya Mheshimiwa Andrew Chenge anaomba Wajumbe wa Kamati yake mkutane saa 7.30 mchana Msekwa D. Katibu tuendeleo.

HOJA ZA SERIKALI

NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI: Kwamba Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mwongozo Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Wenye miongozo tutaje majina.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Bobali.

SPIKA: Mwingine yeyote, Mheshimiwa Bobali Peke yako.

MBUNGE FULANI: Susan Lyimo yule kule.

SUSAN A. J. LYIMO: Suzan Lyimo.

SPIKA: Aaah Susan samahani haya, Mheshimiwa Bobali.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuomba Mwongozo wako, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na nitaishoma pamoja na Kanuni ya 47, lakini kutokana na muda sitasoma.

Mheshimiwa Spika, jana usiku nje kidogo ya Jiji la Mwanza, kwenye eneo linaloitwa Mkolani katika msikiti maarufu kwa jina la Abuu Ismail kuna watu watatu waliokuwa wamevalia kininja, waliingia msikitini wakati waumini wa msikiti huo walikuwa wanaswali sala ya *Inshah* na kuwakatakata kwa mapanga watu watatu akiwepo Imamu wa msikiti huo na watu wote watatu waliokatwa mapanga wamefariki.

Naomba Mwongozo wako na kama utaona inafaa kwa Kanuni ya 47 naomba jambo hili lijadiliwe ili tuone inawezekana Serikali ikatupatia majibu ya kina juu ya suala hili kwa sababu ni suala ambalo lime-*create tension* kubwa hususani kwa waumini wa kiislamu wanaokwenda kuswali muda wa usiku, naomba mwongozo wako. (Makofi)

SPIKA: Kabla sijasema chochote Mbunge wa Jimbo husika wa Mwanza yupo atuambie chochote kuhusu hilo.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana Mbunge wa Jimbo la Nyamagana ambako ndiko anakotaarifu Mbunge yuko kwenye ziara kikazi kwa maana ya yuko kwenye ile Tume ya Bunge na taarifa alizozitoa bahati mbaya pia hata mimi sijazipata.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Bobali na Waheshimiwa Wabunge, habari ambazo Mheshimiwa Bobali ametupatia ni za ghafla lakini za kusikitisha sana natumaini kwa niaba ya Bunge zima lazima tutoe salamu za rambirambi kwa wote waliopatwa na tukio hili, tuombe Mwenyezi Mungu azipokee roho zao mahali pema peponi linavyosimuliwa kama vile siyo la Tanzania hapa.

Waheshimiwa Wabunge, hatuwezi kufanya mjadala kwa sababu hata tukiruhusu mjadala tutajadili nini sasa kwa sasa hivi kwa hiyo, tuchukulie kama ni taarifa kwa Serikali acha Serikali iijipange iangalie ni jambo gani linaloendelea kwa kuwa limetokea kama unavyosema usiku wa kuakia leo, naamini kabisa vyombo vya ulinzi na usalama viko *on* watakapokuwa tayari watatutaarifu kuhusiana na jambo hili kadri inavyoendelea. Lakini kabla sijamaliza huenda Mheshimiwa Waziri wa Nchi ana sentensi mbili, tatu za kusema.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa taarifa hiyo na wakati mwingine ni jambo jema kama Bunge hili linaweza kuwa linapokea taarifa mbalimbali za matukio mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, umetoa maelekezo basi sisi kama Serikali tutafuatilia tuweze kujua nini ambacho kimejiri kule na chanzo chake ni nini na kwa

mwongozo wa kiti chako basi tutaona ni namna gani tunaweza tukapeana habari na kujua kabisa kwa dhati ni jambo gani lilitokea na hatua zilizochukuliwa.

SPIKA: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Bobali tuwe na uvumilivu, tutafika mahali tutaelewa. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nasimama kwa Kanuni hiyo ya 68(7). Wiki iliyopita niliomba mwongozo katika Kiti chako kuhusiana na jinsi ambavyo tumekaa sasa ni Mkutano wa Tatu bado hatujapata vitabu vile ambavyo vina anuani za Wabunge wote hasa ukizingatia zaidi ya 70% ya Wabunge ni wapya lakini hata tuliokuwepo bado wale watatuona ni wapya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako ni kwa nini mpaka leo hatujapata hivi vitabu pamoja na kwamba najua kuna kubana matumizi lakini ni muhimu sana tujuane humu ndani lakini vilevile tunapata shida tunapoombwa namba ya fulani au unaulizwa namba ya fulani unakuwa hujui. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako ni lini basi tutapatiwa vitabu hivi kwa sababu *last time* niliuliza Ofisi ya Katibu nikaambiwa kwamba ni kwa sababu Baraza Kivuli lilikuwa bado halijajulikana lakini sasa hivi tayari Baraza Kivuli lipo kwa hiyo, naomba mwongozo wako.

SPIKA: Ahsante Sana. Baadaye kidogo nitatoa mwongozo wa jambo hilo, ngoja nilifanyie kazi kidogo kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na kwa vile Katibu alishasoma shughuli inayofuata moja kwa moja nimwite Mheshimiwa Profesa Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini ili aweze kutoa hotuba yake. (Makofi)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2015/2016 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, hicho kitabu cha bajeti kina kurasa 92, naomba zote ziingie kwenye *Hansard* kwa sababu siwezi nikaeleza kila kitu hapa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano kwa kupitia Chama cha Mapinduzi. Nampongeza kwa ushindi huo uliodhihirisha kukubalika kwake kwa Watanzania hususan kutokana na uchapakazi wake na ufuatiliaji wake wa masuala ya maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini chini ya Uongozi wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko kwa kuipitia, kuichambua na kuitolea ushauri bajeti ya Wizara yangu. Aidha, natumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu kwa kuniteua kuongoza Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuongelea kuhusu mpango na bajeti. Kwa mwaka huu tunaoumaliza, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 642.12 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, bajeti hiyo iliongezeka kutoka shilingi bilioni 642.12 hadi shilingi bilioni 762.12 ili kutekeleza miradi mikubwa ya kufua umeme ikiwemo Kinyerezi II wa megawatt 240. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 565.51 sawa na 74% ya bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 215.98 sawa na 75% ya lengo la shilingi bilioni 286.66. Kwa mwaka wa fedha ujao, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 370.68 ikiwa ni ongezeko la 29% ikilinganishwa na lengo la mwaka tunaoumaliza na hii ni kwa sababu ya mauzo ya gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati (umeme). Uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini (*total installed capacity*) kwenye gridi ya Taifa umeongezeka kutoka MW 1,222.24 mwezi Aprili mwaka jana hadi MW 1,461.69 mwezi Aprili mwaka huu, hili ni sawa na ongezeko la 19%. Ukijumlisha *on grid* na *off grid* unapata jumla ya uwezo wetu wa kuzalisha umeme nchini ni MW 1,540.98. Kati ya uwezo huo 49% ni kutokana na gesi asilia, 39% ni maji, 12% ni mafuta na tungamotaka (*biomass*). Aidha, mahitaji ya juu ya umeme yameongezeka kutoka MW 988.27 mwezi Disemba mwaka jana hadi kufika MW 1,026.02 kwa mwezi Machi mwaka huu, ni sawa na ongezeko la 4% lakini kwa wiki mbili zilizopita tumefikisha MW 1,100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania waliofikiwa na huduma ya umeme (access level) wameongezeka kutoka 36% mwezi Machi mwaka jana hadi kufikia 40% Aprili mwaka huu. Ongezeko hili limetokana na juhudi za Serikali za kusambaza umeme nchini kupitia REA na TANESCO. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, miradi ya umeme. Nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mradi wa Kinyerezi I wenye uwezo wa kuzalisha MW 150 kwa kutumia gesi asilia umekamilika. Mradi huu ulizinduliwa rasmi na Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Oktoba mwaka jana. Mradi uligharimu dola za Marekani milioni 183 na unamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imepanga kuongeza mitambo mingine ya kuzalisha umeme Kinyerezi I (Extension) yenye uwezo wa kuzalisha MW 185 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 188. Fedha zilizotengwa kwa mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya mradi huu ni shilingi bilioni 119.04 na mradi utakamilika mwaka 2019. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa Kinyerezi II wa MW 240 wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia umeanza. Jiwe la msingi la utekelezaji wa mradi huu liliwekwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, mwezi Machi mwaka huu. Gharama ya mradi huu ni Dola za Marekani milioni 344 ambapo Dola za Marekani milioni 292 sawa na 85% ni kutoka Japan. Aidha, Serikali imetoa shilingi bilioni 110 ikiwa ni 15% ya gharama ya mradi wote. Katika mwaka wa fedha ujao Serikali itaendelea kutekeleza mradi huu utakaokamilika Disemba, 2019. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya uzalishaji umeme iliyopo kwenye hatua za mwisho za kuanza kutekelezwa ni pamoja na Kinyerezi III, tunaanza na MW 300 baadaye tunaenda MW 600; Rusumo MW 80; Malagarasi MW 45 na Kakono MW 87. Miradi hii itakamilika kabla ya Mwaka 2020. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme inayoanzia Iringa hadi Shinyanga ya msongo wa kV 400 ulifikia wastani wa 89% mwezi Aprili mwaka huu. Gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 224. Mradi utakamilika Septemba 2016. Naomba nirudie hapo, mradi wa umeme mwingi kutoka Iringa hadi Shinyanga utakamilika mwezi Septemba mwaka huu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa kwa mwaka ujao wa fedha ni shilingi bilioni 20. Vilevile, mwezi Agosti mwaka jana TANESCO ilisaini mikataba na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 kutoka Makambako kwenda Songea na vituo vya kupozea umeme vya

Madaba na Songea vilivyopo Mkoani Ruvuma. Aidha, kazi ya kusambaza nguzo za umeme wa msongo wa kV 33 katika Mikoa ya Njombe na Ruvuma imeanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha ujao, kazi zilizopangwa kufanywa ni kukamilisha ujenzi wa njia ya kusambaza umeme katika Wilaya za Ludewa, Mbinga, Namtumbo, Njombe, Songea Mjini na Songea Vijijini na kuanza ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa vituo vya kupozea umeme. Gharama za mradi huu ni Krona za Sweden milioni 500 sawa na shilingi bilioni 112 na mradi huu utakamilika Disemba mwaka kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya ujenzi wa njia za kusafirisha umeme zenye uwezo mkubwa ni Singida – Arusha – Namanga kV 400, narudia. Miradi mingine ya ujenzi ya kusafirisha umeme mwingi ni Singida – Arusha – Namanga kV 400; Bulyankulu – Geita kV 220; Geita – Nyakanazi kV 220; kutoka Dar-es-Salaam – Pwani – Tanga – Arusha kV 400 na Somangafungu – Kinyerezi kV 400. Utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha wa 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini (REA II) inaendelea kutekelezwa katika mikoa yote Tanzania Bara kupitia REA ambapo umefikia 85%. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa vituo sita vya kupozea umeme katika Miji ya Kasulu, Kibondo, Kigoma, Mbinga, Ngara na Tunduru; ujenzi wa njia za kusambaza umeme wenye urefu wa takribani kilometa 15,000 wa msongo wa kV 33; ujenzi wa vituo vidogo 3,100 vya kupozea na kusambaza umeme na ujenzi wa njia ndogo za usambazaji wa umeme wenye urefu wa kilometa 7,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia REA imekamilisha kazi ya kuunganisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya nne za Buhigwe, Kakonko na Uvinza zilizopo katika Mkoa wa Kigoma na Nyasa iliyopo katika Mkoa wa Ruvuma. Kuanzia Julai mwaka jana hadi Aprili mwaka huu idadi ya wateja waliunganishiwa umeme kwenye REA II ukiunganisha na wale wa TANESCO ni 220,128 sawa na 88% ya lengo la kuunganisha wateja robo milioni ifikapo Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016/2017 Serikali itanza utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya REA baada ya kukamilisha tathmini ya utekelezaji wa Awamu ya Pili. Utekelezaji wa miradi ya REA Phase III utakamilika mwaka wa fedha 2018/2019, tusikilizane kwa makini hapo. Serikali imeongeza bajeti ya maendeleo ya fedha za ndani kwa REA kutoka shilingi bilioni 357.12 mwaka unaokwisha kwenda shilingi bilioni 534 kwa mwaka wa fedha ujao sawa na ongezeko la 50%. Tumeongeza 50% hakuna MCC hapa. Ongezeko hilo ni katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM hasa Ibara ya 43(c)(1). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatangazia ndugu zetu wa vijijini kwamba gharama ya kuunganisha umeme majumbani wa REA Awamu ya Tatu ni ileile ya Sh. 27,000/= ambayo kawaida ni majogoo matatu tu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mipango ya kuboresha sekta ndogo ya umeme, Serikali ilikamilisha kazi mbalimbali zikiwemo utayarishaji wa Mikataba Kifani ya Kuuziana Umeme (*Model Power Purchasing Agreement*) mwezi Agosti mwaka jana na Mwongozo wa Tozo kwa kampuni moja kutumia miundombinu ya kampuni nyingine kusafirishia umeme (*Transmission Willing Charging Rules*). Katika mwaka wa fedha unaokuja Serikali itaendelea kutekeleza mpango huo ikiwa ni pamoja na zoezi la kutathmini mali za TANESCO, rasilimali watu ambao wanaweza kuingia kwenye sekta ya umeme, mafuta na gesi asilia na ukaguzi wa mifumo ya computer za TANESCO.

Mheshimiwa Spika, punguzo la viwango vya bei za umeme. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imetekeleza ahadi yake ya kupunguza bei za umeme. Kuanzia tarehe 1 Aprili, Serikali imepunguza bei ya umeme kwa kati ya 1.5% na 2.4%. Serikali vilevile imeondoa gharama za maombi ya kuunganishia umeme (*application fee*) ya Sh. 5,000/= haipo tena! Tozo ya huduma za mwezi (*service charge*) ya Sh. 5,520/= haipo tena kwa wateja wa umeme wa daraja la T1 na D1 ambao wengi ni wa umeme wa majumbani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia watumiaji wadogo wa umeme mijini na vijijini kumudu gharama za matumizi ya umeme hivyo kuboresha shughuli za kijamii na kiuchumi. Ndugu zangu wa Lindi na Mtwara punguzo lile la umeme mnaunganisha kwa Sh. 99,000/= badala ya Sh. 177,000/= bado liko palepale. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nishati jadidifu. Serikali imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia maporomoko ya maji (*mini hydros*). Katika mwaka huu tunaoumaliza miradi iliyokamilika ni Adoya – Mbinga, Darakuta – Manyara, Tulila – Songea, Iyovi – Kilosa, yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya MW 6.6 na mwaka ujao wa fedha tutaendeleza miradi hii ambayo jumla yake ni MW 10.24.

Serikali imeandaa ramani zinazoonesha maeneo yanayofaa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya upepo na jua kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji kwenye aina hizo za nishati. Katika kutekeleza Ibara ya 45(a) ya Ilani ya Uchaguzi ya tutapeleka umeme wa jua kwenye visiwa ndani ya Ziwa Viktoria na Bahari ya Hindi ikiwemo kisiwa cha Mafia na fedha tulizotenga ni shilingi bilioni 6.5. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mafuta na gesi asilia. Kampuni ya *Dodsal* imekamilisha tathmini ya kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa katika kisima cha Mambakofi – I kwenye Kitalu cha Ruvu Mkoani Pwani. Tathmini hiyo inaonesha uwepo wa gesi asilia kiasi cha futi za ujazo trilioni 2.17, huu ni mwanzo tu, wana gesi nyingi pale, hivyo kufanya gesi asilia iliyogundulika nchini kufikia mwezi Mei, 2016 tunafikia futi za ujazo trilioni 57.25. Ni zaidi ya mwaka jana iliyokuwa trilioni 55.08, ni gesi nyingi sana hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Mtwara kupitia Lindi hadi Dar es Salaam kilomita 542 pamoja na mitambo ya kusafisha gesi asilia katika maeneo ya Madimba (Mtwara) na Songosongo (Lindi). Kukamilika kwa mradi huu kumeongeza mchango wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia kufikia asilimia 49 na kupunguza gharama za uzalishaji wa umeme nchini kutoka wastani wa shilingi 262 hadi 229 kwa *unit* moja ya umeme, hii ndiyo maana ya nchi yenye viwanda, umeme chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na taratibu za kuanzisha Mamlaka ya Udhidhi wa Mkondo wa Juu wa Masuala ya Petroli (*Petroleum Upstream Regulatory Authority*). Mwezi Februari, 2016, Serikali imeunda Kamati ya Mpito ya kutekeleza majukumu ya *PURA* katika kipindi hiki na kufanya maandalizi ya kuwezesha mamlaka hii ianze kazi Julai, 2016.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengine, *PURA* itakagua mikataba na kuchambua masuala ya kiuchumi katika kuingia mikataba ya utafutaji na ugawanaji wa mapato yatokanayo na shughuli za mafuta na gesi asilia; itasimamia masuala ya ushiriki wa Watanzania katika shughuli za utafutaji na uvunaji wa mafuta na gesi asilia na itakagua au itaagiza kufanyika ukaguzi wa vyanzo vya mapato ya Serikali katika sekta ya mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi kwenye shughuli za uagizaji wa mafuta na petroli nchini mwezi Februari, 2016, Serikali ilikamilisha uanzishwaji wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (*Petroleum Bulk Procurement Agency*). Wakala huo pamoja na kazi nyingine utatekeleza majukumu yaliyokuwa ya kampuni binafsi ya kuratibu uagizaji wa mafuta ya petroli kwa pamoja yaani *PICL*. Katika mwaka wa fedha ujao, wakala huu utaanza vilevile kuratibu uagizaji wa *Liquefied Petroleum Gas (LPG)* pamoja na mafuta mazito (*HFO*) kwa kupitia mfumo wa *BPS*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2015, bei ya mafuta katika soko la dunia ziliendelea kushuka kufikia wastani wa dola za Marekani 38 kwa pipa la mafuta ghafi kwa Desemba 2015. Kwa kuzingatia bei hiyo ya soko la dunia kupungua pamoja na thamani ya shilingi, bei za mafuta zimeendelea kupungua nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania. Mwezi Aprili, 2016, Serikali ya Tanzania ilisaini makubaliano ya awali na Serikali ya Uganda kwa ajili ya ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima Uganda hadi bandari ya Tanga. Bomba hilo litakuwa na urefu wa kilomita 1,443 ambapo kati ya hizo kilomita 1,115 zitakuwa upande wa Tanzania. Bomba hilo litakuwa na uwezo wa kusafirisha mapipa 200,000 ya mafuta ghafi kwa siku. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania utekelezaji wa mradi huu utakuwa na manufaa mbalimbali yakiwemo kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato kupitia bandari ya Tanga; tozo ya kupitisha mafuta ghafi kwenye bomba, mapipa 200,000 kwa siku; kuongezeka kwa uwekezaji wa fedha za kigeni; fursa za ajira kwa kazi za awamu nafasi 10,000 na kazi za kudumu 1,000. Majadiliano ya utekelezaji wa mradi huu kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda, Kampuni ya TPDC na Uganda *Nationa Oil Company* na Kampuni za TOTAL (Ufaransa), CNOOC (China) na Tullow (UK) yameanza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushirikiano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali ya Uganda imealika nchi za Burundi, Kenya, Rwanda na Tanzania kushiriki katika uwekezaji kwenye mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kusafisha mafuta ghafi (*oil refinery*) nchini Uganda. Kila nchi imepewa fursa ya kushiriki kwa kununua asilimia nane ya hisa zote za mradi ambazo makisio ya awali ni dola za Marekani milioni 150.4 sawa na shilingi bilioni 335.08. Katika mradi huu sekta binafsi pia imekaribishwa kushiriki. Waheshimiwa Wabunge tuna 8% tutafute hizo dola milioni 150.4 na sekta binafsi inakaribishwa.

Mheshimiwa Spika, sera na sheria katika sekta ya nishati. Katika mwaka huu tunaoumaliza, Serikali imekamilisha Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015 na Sheria ya Petroli ya mwaka 2015. Lengo la kupitisha sera na sheria hizo ni kuimarisha usimamizi wa sekta za nishati nchini. Katika mwaka huu wa fedha tutakaouanza kanuni na miongozo mbalimbali itatayarishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia EWURA imeandaa miongozo ya uanzishwaji wa miradi ya umeme kwa mujibu wa kifungu cha tano (5) cha Sheria ya Umeme ya mwaka 2008, *The Electricity (Initiation of Power Procurement) Rules 2014*. Lengo la mwongozo huu ni kuhakikisha kuwa uwekezaji katika miradi ya umeme unafanyika kwa tija na kuleta faida kwa wananchi na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, biashara ya madini imeathiriwa kwa kushuka kwa bei za madini katika soko la dunia na kusababisha kushuka kwa mapato ya Serikali na uwekezaji katika sekta ya madini. Kwa mwaka 2015, jumla ya wakia milioni 1.37 za dhahabu, wakia 497,152 za fedha, ratili milioni 13.76 za shaba zilizalishwa

na kusafirishwa nchi za nje kutoka migodi mikubwa ya dhahabu ya Geita, Bulyanhulu, Buzwagi, North Mara, *Stamigold* na New Luika ya Chunya. Jumla ya thamani ya madini hayo ni dola za marekani bilioni 1.63 na mrabaha uliolipwa Serikalini kutokana na madini hayo ni dola za Marekani milioni 63.2.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali katika mwaka huu tunaoumaliza ilipata mrabaha wa dola za Marekani 223,979 kutokana na mauzo ya *Tanzanite*. Kwa upande wa madini ya Almasi kutoka Mgodi wa Mwadui, Serikali ilipata mrabaha wa Dola za Marekani milioni 2.30.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na *Tanzania Mineral Dealers Association* imeendesha maonesho ya Kimataifa ya vito yaliyofanyika Mjini Arusha kuanzia tarehe 19 hadi 22 Aprili, 2016. Katika maonesho hayo, madini yenye thamani ya dola za Marekani milioni 4.04 yaliuzwa. Serikali ilikusanya mrabaha wa dola za Marekani 158,597.6 ambazo ni sawa na shilingi milioni 353.34. Vilevile shilingi bilioni 1.36 zilipatikana kutokana na mauzo ya sehemu ya madini yaliyokamatwa yakitoroshwa nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha tutakaouanza Serikali itaboresha usimamizi na biashara hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka uliopita, Kampuni ya *Acacia, El- Hillal, Geita Gold Mining Limited, Shanta Gold, Wiliamson Diamonds Limited*, zimelipa ushuru wa huduma (*service levy*) kwa jumla ya shilingi bilioni 10.34 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.1 kwa mwaka 2014. Malipo hayo yameongezeka kwa asilimia 152. Mapato hayo yamelipwa kwenye Halmashauri zifuatazo:-

Kahama shilingi milioni 866.25; Msalala shilingi bilioni 1.59; Tarime shilingi bilioni 2.01; Chunya shilingi bilioni 831.41; Kishapu shilingi milioni 362.42 na Geita shilingi bilioni 400.67. Naomba kutoa wito kwa viongozi wa Halmashauri na Wabunge wahusika kuhakikisha kuwa, fedha hizo zinatumika kwenye shughuli za maendeleo kwa manufaa ya wananchi wa maeneo husika na Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 shilingi bilioni 2.9 zilikusanywa ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.2 zilizopatikana kutokana na uchenjuaji wa marudio ya udongo wenye dhahabu kama inavyoonekana kwenye picha. Katika mwaka wa fedha ujao, Wizara itaendelea kuboresha uvunaji wa dhahabu kwa kutumia njia hii.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo. Katika kutekeleza Ilani ya CCM ya uchaguzi hasa Ibara ya 35(m), kipengele cha kwanza na cha pili zinazoelekeza kuwapatia wachimbaji wadogo maeneo ya uchimbaji na ruzuku, mwaka huu tunaoumaliza Serikali ilitenga maeneo ya Nyamongo (Tarime) na Muhintiri (Singida) yenye ukubwa wa hekta 7,731 kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Aidha, Serikali ilitoa ruzuku ya shilingi bilioni 700.24 kwa miradi 111 ya

wachimbaji wadogo. Katika mwaka wa fedha huu tunaouanza hivi karibuni, Serikali itatenga maeneo sita yenye ukubwa wa takribani hekta 12,000 na kutoa ruzuku za dola za Marekani milioni tatu kupitia Mfuko wa Benki ya Dunia kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa ya madini. Serikali imeendelea kuhamasisha uendelezaji wa miradi mikubwa ya madini ikiwemo miradi ya *graphite* ya kule Ruangwa na Epanko Wilaya ya Ulanga. Miradi mingine ni urani ya Mto Mkuju na Wilaya ya Namtumbo na *niobium* kwenye Wilaya ya Songea. Dunia ya sasa madini yenye thamani ni *graphite, rare earth elements* pamoja na hizi *niobium*, achana na dhahabu na chuma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Sheria katika Sekta ya Madini. Rasimu za Sheria ya Baruti na Uongezaji Thamani Madini zimekamilika. Lengo la sheria hizi ni kuimarisha usimamizi katika matumizi ya baruti na fataki pamoja na shughuli za uongezaji thamani madini. Hata hivyo, Wizara inaendelea kukusanya maoni zaidi kutoka kwa wadau muhimu ili kuboresha rasimu hizo. Katika mwaka wa fedha tutakaouanza, Wizara itazikamilisha na kuziwakilisha katika mamlaka husika ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania. Mwaka huu wa fedha tunaomaliza Wakala ulikusanya taarifa zitakazowezesha kuchorwa kwa ramani kwa ajili ya uhamasishaji uwekezaji (*Mineral Promotion Block Map*) katika Wilaya za Masasi, Nachingwea na Tunduru. Katika mwaka wa fedha tutakaouanza, Wakala utachapisha ramani kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji katika Wilaya hizo baada ya kupata *data* kutoka kwenye maabara. Kazi hizo zinagharamiwa na Serikali ya Finland kwa jumla ya Euro 700,000 sawasawa na shilingi bilioni 1.74.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA). Kati ya mwezi Julai, 2015 na Machi, 2016, TMAA ilifanya ukaguzi wa hesabu za fedha za migodi na kuwezesha kodi ya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 107.7 kukusanywa. Fedha hizo zililipwa na Kampuni za *Geita Gold Mine, North Mara Gold Mining Limited* na *Resolute*. Serikali ilikusanya mrabaha wa shilingi bilioni 5.5 kutokana na uzalishaji huo. Mwaka wa fedha tutakaouanza TMAA itaendelea kwa kasi kubwa kusimamia mapato kutoka kwenye migodi yetu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini STAMICO. Katika kipindi kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016, STAMICO kupitia Kampuni tanzu yake ya *Stamigold* ya Biharamulo ilizalisha na kuuza wakia 17,346 za dhahabu, madini yaliyokuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 19.80. STAMICO ilipata shilingi milioni 426.49 kutoka *Stamigold* ikiwa ni ada ya usimamizi. Kwa mwaka ujao, STAMICO itafufua Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira na kuanza kuzalisha MW 200 na shilingi bilioni mbili zimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini (*Mineral Resources Institute*). Mwezi Desemba, 2015, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) lilitoa kibali cha kuiwezesha taasisi hii kujitegemea kitaaluma na kiutawala. Chuo hicho kitaitwa *Dodoma Polytechnic of Energy and Earth Resources Management*. Katika mwaka wa fedha unaokuja, chuo kitaendelea kuimarisha utendaji wake wa kuandaa fani mpya; kuwaendeleza watumishi wake na miundombinu yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Asasi ya Uwazi katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (*TEITI*). Kama ilivyoahidiwa na Serikali, Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania ya mwaka 2015 ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 455 la tarehe 16 Oktoba, 2016. Pamoja na mambo mengine, sheria hiyo inaipa nguvu kisheria Kamati ya *TEITI* kuzitaka kampuni kuweka wazi taarifa za malipo, mauzo na gharama za uwekezaji na Serikali kutakiwa kuweka wazi taarifa zake za mapato yanayotokana na rasilimali za madini, mafuta, gesi asilia na matumizi ya mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha tutakaouanza, Wizara itakamilisha maandalizi ya kanuni za sheria hiyo. Aidha, rejista ya majina ya wamiliki hisa kwenye leseni na mikataba katika makampuni ya madini, mafuta na gesi asilia itaanzishwa ili kuwatambua kwa majina wanaomiliki hisa katika kampuni hizi, rejista itatoa ubishi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ajira na maendeleo ya rasilimali watu. Wizara imeendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo kutoa ufadhili wa mafunzo kwa Watanzania. Katika mwaka 2015/2016, Watanzania 18 walipata ufadhili wa mafunzo katika Serikali ya Jamhuri ya watu wa China. Aidha, jumla ya Watanzania 321 walipata ufadhili wa mafunzo ambapo kati ya hao 112 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi; 178 stashahada na 31 walihudhuria mafunzo ya shahada za uzamili katika fani mbalimbali zikiwemo za mafuta na gesi asilia. Fedha zilizotumika ni jumla ya dola 506,000 na kwa mwaka unaokuja Serikali itaendelea kuwapatia uwezo wataalam wetu.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa Kimataifa. Washirika wa Maendeleo wameendelea kushirikiana na Wizara katika shughuli mbalimbali hususani kwenye miradi ya maendeleo na kuwajengea watumishi wetu uwezo. Kwa kutambua mchango huo, kwa niaba ya Serikali, natumia fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya BADEA, Benki ya Dunia, Benki ya Exim ya China, Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile, natoa shukurani kwa Taasisi na Mashirika ya AFD (Ufaransa), CIDA (Canada), DFID (Uingereza), ECDF (Korea Kusini), ICEIDA (Iceland), FINIDA (Finland), JICA (Japan), KfW (German), NORAD (Norway), OFID

(Saudi Arabia), ORIO (The Netherlands), SIDA (Sweden), UNDP, USAID (Marekani) na Umoja wa Ulaya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, shukrani. Natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mbunge wa Jimbo la Chato kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini. Natoa pia shukrani kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Profesa Justin William Ntalikwa pamoja na Naibu Makatibu Wakuu, Profesa Joseph Epifani Mdoe na Dkt. Juliana Leonard Pallangyo, kwa umahiri wao wa kuchapa kazi kwa bidii na kwa ufanisi mkubwa na kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipatia. Hawa wasomi hawawezi kushindwa kazi. Vilevile natumia fursa hii kuwashukuru kwa kazi nzuri Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi wote Wizarani. Vilevile nawashukuru Wenyevitwa wa Bodi pamoja na Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara yetu kwa ushirikiano mzuri wanaonipa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa shukrani kwa wananchi wa Jimbo langu la Musoma Vijijini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na imani kubwa kwelikweli waliyonayo kwangu kwa kuleta maendeleo Jimboni mwetu na kwa Tanzania nzima. Kwa namna ya pekee naishukuru familia yangu kwa kunitia moyo na kunifariji katika kutekeleza majukumu yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee kabisa nawashukuru Wabunge na wananchi wanaonipatia taarifa mbalimbali za Sekta za Nishati na Madini. Naomba waendeleo kufanya hivyo kwani taarifa hizo zinaboresha utendaji wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2016/2017 ni jumla ya shilingi trilioni 1.22. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.06 ni fedha za miradi ya maendeleo sawa na asilimia 94. Naomba nirudie, bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, asilimia 94 ni miradi na asilimia sita tu ndiyo OC na mambo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ibara ya 43(a) ya CCM, Serikali imeongeza fedha na kati ya fedha hizo asilimia 98 zinaenda kwenye nishati. Fedha za matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 66.23 sawa na asilimia sita ya bajeti yote. Katika fedha hizo, shilingi bilioni 38.87 ni kwa ajili ya OC ambayo ni sawa na asilimia 90 ya mengineyo na shilingi bilioni 27.4 sawa na asilimia 41 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tukushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Muhongo kwa kusoma hotuba yako vizuri kabisa na Wabunge wamekusikiliza. Kama mlivyosikia, hela zinazoombwa asilimia 94 ni miradi ya maendeleo, haijapata kutokea. Leo Wabunge hapa ni kuunga mkono tu basi. (Makofi/Kicheko)

HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI NA MADINI MHE. PROF. SOSPETER MWIJARUBI MUHONGO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZIKWA MWAKA 2016/17 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2015/16 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka 2016/17.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwasilisha Hotuba hii kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015. Uchaguzi huo uliwezesha Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM). **Nampongeza kwa ushindi huo uliodhihirisha kukubalika kwake kwa Watanzania, hususan kutokana na uchapakazi na ufuatiliaji wake wa masuala ya maendeleo.** Ni ukweli usioplingika kwamba maamuzi anayoyachukua na mbinu anazozitumia katika kuongoza Taifa letu ni za kipekee na zinatakiwa kuungwa mkono na kila Mtanzania bila kujali tofauti ya itikadi zetu.

3. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuandika historia mpya ya nchi yetu ya kuwa Mwanamke wa Kwanza kushika wadhifa huo. Hii ni ishara njema kwa nchi yetu katika kuongeza nafasi za juu za wanawake katika Uongozi wa Taifa letu.

4. Mheshimiwa Spika, vilevile, natumia nafasi hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania. Pia, nimpongeze Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu.

6. Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kumshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu kwa kuiteua kuongoza Wizara ya Nishati na Madini. Niwahakikishie Watanzania kwamba nitatumia weledi na uzoefu wangu wote katika kuhakikisha kuwa Sekta za Nishati na Madini zinaleta manufaa makubwa ya kiuchumi kwa Taifa letu.

7. Mheshimiwa Spika, nampongeza Mhe. Doto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mhe. Deogratias Francis Ngalawa (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Vilevile, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri na maoni yao katika kuendeleza na kusimamia Sekta za Nishati na Madini. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuteuliwa kwao kuwawakilisha wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

8. Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo yafuatayo ni maelezo ya Mapitio ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2015/16 pamoja na Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2016/17.

A. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2015/16 NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17

9. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Wizara ya Nishati na Madini iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopangwa. Katika kutekeleza majukumu hayo, Wizara iliidhinishiwa na Bunge Jumla ya **Shilingi bilioni 642.12**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 502.30** sawa na **asilimia 78** ya Bajeti yote zilikuwa ni Bajeti ya Maendeleo. Aidha, **Shilingi 139.82**, sawa na **asilimia 22** ya Bajeti yote zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara na Taasisi zake.

10. Mheshimiwa Spika, hata hivyo Bajeti hiyo iliongezeka kutoka **Shilingi bilioni 642.12** hadi **Shilingi bilioni 762.12**. Lengo la ongezeko ni kutekeleza miradi mikubwa ya kufua umeme ukiwemo Mradi wa Kinyerezi II - MW 240 ili kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

11. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2016, Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi bilioni 565.51**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 506.28** sawa na **asilimia 90** zilikuwa ni za Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani zilikuwa **Shilingi bilioni 472.93** sawa na **asilimia 93** ya fedha za Maendeleo zilizopokelewa na **Shilingi bilioni 33.35** sawa

na **asilimia 7** ni fedha za nje. Kiasi kilichobaki cha **Shilingi bilioni 59.23** sawa na **asilimia 10** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

12. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 Wizara ilikuwa imekusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 215.98** sawa na **asilimia 75** ya lengo la **Shilingi bilioni 286.66**. Kasi ya makusanyo ya mapato imepungua kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupungua kwa shughuli za utafiti na uzalishaji wa madini kutokana na kushuka kwa bei za madini kwenye Soko la Dunia.

13. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Wizara inatarajia kukusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 370.68** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 29** ikilinganishwa na lengo la Mwaka 2015/16. Ongezeko hilo litatokana na mauzo ya Gesi Asilia. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha usimamizi wa ukusanyaji wa maduhuli kwa kuziba mianya ya utoroshaji madini, kuimarisha ukaguzi wa uzalishaji na usafirishaji madini pamoja na kuboresha mazingira ya Wachimbaji Wadogo wa madini. Vilevile, Serikali itaboresha mfumo wa masoko ya madini ndani ya nchi kwa ajili ya kuongeza ushindani wa bei ili kuongeza mapato ya Serikali.

SEKTA YA NISHATI SEKTA NDOGO YA UMEME

(i) Hali ya Uzalishaji Umeme

14. Mheshimiwa Spika, uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini (*total installed capacity*) umeongezeka kutoka **MW 1,226.24** mwezi Aprili, 2015 hadi **MW 1,461.69** mwezi Aprili, 2016 sawa na ongezeko la **asilimia 19**. Ongezeko hilo limechangiwa na mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia baada ya kukamilika kwa Bomba la kusafirisha Gesi Asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam. Kati ya uwezo huo, MW 711.00 (**asilimia 49**) ni Gesi Asilia, MW 566.79 (**asilimia 39**) zinatokana na umeme wa nguvu za maji na MW 183.90 (**asilimia 12**) ni mafuta na tungamotaka. Aidha, mahitaji ya juu ya umeme yameongezeka kutoka **MW 988.27** mwezi Desemba, 2015 hadi kufikia **MW 1,026.02** mwezi Machi, 2016 sawa na ongezeko la **asilimia 4**.

15. Mheshimiwa Spika, kiasi cha umeme kilichoingizwa kwenye Gridi ya Taifa kiliongezeka kutoka **GWh 6,033.98** Mwaka 2014 na kufikia **GWh 6,227** Mwaka 2015, sawa na ongezeko la takriban **asilimia 3**. Uzalishaji katika vituo vilivyoko nje ya Gridi ya Taifa uliongezeka kutoka **GWh 191.8** Mwaka 2014 hadi kufikia **GWh 201.44** Mwaka 2015, ikiwa ni ongezeko la **asilimia 5**.

(ii) Upatikanaji wa Huduma ya Umeme Nchini

16. Mheshimiwa Spika, kiwango cha upatikanaji wa huduma ya umeme (*access level*) kimekuwa kikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Watanzania waliofikiwa na huduma hiyo wameongezeka kutoka **asilimia 36** mwezi Machi, 2015 hadi kufikia takriban **asilimia 40** mwezi Aprili, 2016. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za Serikali za kusambaza umeme nchini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

(iii) **Miradi ya Kuzalisha Umeme**

17. Mheshimiwa Spika, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mradi wa Kinyerezi – I wenye uwezo wa kuzalisha MW 150 kwa kutumia Gesi Asilia umekamilika. Mradi huu ulizinduliwa rasmi na Rais wa Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Oktoba, 2015. Mradi uligharimu **Dola za Marekani milioni 183** sawa na takriban **Shilingi bilioni 315.47** na unamilikiwa na Serikali kwa **asilimia 100** kupitia TANESCO.

18. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuongeza uzalishaji umeme, Serikali pia imepanga kuongeza mitambo mingine ya kuzalisha umeme ya **Kinyerezi – I Extension MW 185**. Mwezi Aprili, 2016 TANESCO na Mkandarasi Kampuni ya Jacobsen Elektro AS wamesaini Mkataba wa utekelezaji wa Mradi huu. Gharama za Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 188** sawa na takriban **Shilingi bilioni 418.85**. Fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2016/17 kwa ajili ya Mradi huu ni **Shilingi bilioni 119.04** na umepangwa kukamilika mwishoni mwa Mwaka 2019.

19. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa **Mradi wa Kinyerezi - II MW 240** wa kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia umeanza. Jiwe la msingi la utekelezaji wa Mradi huu liliwekwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwezi Machi, 2016. Gharama za Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 344**, sawa na **Shilingi bilioni 564**, ambapo **Dola za Marekani milioni 292** sawa na **asilimia 85** ni Mkopo kutoka Japan Bank for International Corporation (JBIC) na Sumitomo Mitsui Banking Corporation (SMBC) za Japan. Aidha, Serikali imetoa **Shilingi bilioni 110** ikiwa ni **asilimia 15** ya gharama za Mradi wote.

20. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mradi huo ikiwa ni pamoja na taratibu za ununuzi na usafirishaji wa mitambo na vifaa kutoka Japan. Mradi umepangwa kukamilika Mwezi Desemba, 2019.

Miradi ya Uzalishaji Umeme Iliyo katika Hatua za Mwisho Kuanza Utekelezaji

21. Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya miradi mbalimbali ya uzalishaji umeme. Miradi hiyo ni pamoja na

Kinyerezi III - MW 300, Rusumo Falls - MW 80, Malagarasi - MW 45 na Kakono - MW 87 na imepangwa kukamilika kabla ya Mwaka 2020.

22. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kinyerezi - III MW 300 utatekelezwa katika eneo la Kinyerezi Mkoa wa Dar es Salaam. Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika. Mradi utatekelezwa kupitia Kampuni ya SHANGTAN ambayo ni Kampuni ya ubia kati ya TANESCO (**asilimia 10**) na Shangai Electric Power Company ya China (**asilimia 60**). Aidha, **asilimia 30** ya Hisa zitauzwa kwa Wawekezaji wengine wa Ndani. Gharama ya Mradi ni **Dola za Marekani milioni 389.7** sawa na takriban **Shilingi bilioni 868.2**. Katika Mwaka 2016/17, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha majadiliano ya Mkataba wa kuuziana umeme, kuza **asilimia 30** ya Hisa kwa Wawekezaji wa Ndani na kuajiri Mkandarasi wa utekelezaji wa Mradi. Mradi utakamilika katika muda wa miezi 36 baada ya kuanza utekelezaji wake.

23. Mheshimiwa Spika, maandalizi ya ujenzi wa Mradi wa Rusumo Falls wa kuzalisha umeme wa MW 80 kwa kutumia nguvu za maji kwa ushirikiano wa nchi yetu na nchi za Rwanda na Burundi yamekamilika. Kazi zilizofanyika katika Mwaka 2015/16 ni: kupatikana kwa Wataalamu Washauri Kampuni ya AECOM ya Canada na Kampuni ya ARTELIA ya Ufaransa kwa ajili ya kazi ya kusimamia ujenzi wa mtambo wa kufua umeme na njia ya kusafirisha umeme; na kupatikana kwa Mkuza kwa ajili ya kujenga njia ya kusafirisha umeme.

24. Mheshimiwa Spika, fedha za kutekeleza Mradi huu zimepatikana kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Gharama za ujenzi wa Mtambo zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 340** sawa na takriban **Shilingi bilioni 757.52**. Katika Mradi huu, mchango wa Tanzania ni mkopo wa **asilimia 100 (Dola za Marekani milioni 113.33)**. Aidha, Rwanda imepata mkopo wa **asilimia 50 (Dola za Marekani milioni 56.67)** na ruzuku ya **asilimia 50 (Dola za Marekani milioni 56.67)** na Burundi imepata ruzuku ya **asilimia 100 (Dola za Marekani milioni 113.33)**.

25. Mheshimiwa Spika, Mradi pia utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Msongo wa kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 98. Gharama ya njia hiyo ya kusafirisha umeme ni **Dola za Marekani milioni 35** sawa na takriban **Shilingi bilioni 77.98**. Kazi zitakazofanyika Mwaka 2016/17 ni kukamilisha taratibu za kupata Wakandarasi wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. Fedha za nje zilizotengwa kwa Mwaka 2016/17 ni **Shilingi bilioni 5**. Mradi huu utanza Mwaka 2016/17 na utakamilika Mwaka 2019/20.

26. Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya Mradi wa Malagarasi wa MW 44.8 Mkoa wa Kigoma imekamilika. Gharama za

Mradi ni **Dola za Marekani milioni 149.5** sawa na **Shilingi bilioni 333.08**. Katika Mwaka 2016/17, kazi zitakazofanyika ni kukamilisha shughuli za usanifu na kutengeneza nyaraka za zabuni ambapo **Shilingi bilioni 5** zimetengwa. Mradi huu unatarajia kukamilika Mwaka 2019/20.

27. Mheshimiwa Spika, Serikali pia kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD) imekamilisha upembuzi yakinifu wa **Mradi wa Kakono wa MW 87** Mkoa wa Kagera. Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Msongo wa kV 132 yenye urefu wa kilomita 38.8 kutoka Kakono hadi Kyaka (Uganda). Miongoni mwa kazi zitakazofanyika ni kumpata Mtaalamu Mshauri wa Mradi, kutayarisha usanifu wa mitambo na kuandaa hati za zabuni. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 379.4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 845.27**. Fedha zilizotengwa katika Mwaka 2016/17 kwa ajili ya Mradi wa Kakono ni **Shilingi bilioni 3**. Mradi huu utakamilika Mwaka 2019/20.

28. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2015 Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ilitisha Mkutano na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kutafuta fedha za utekelezaji wa Miradi ya Malagarasi na Kakono. Kufuatia Mkutano huo, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) zimeonesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Kakono na Malagarasi.

Miradi ya Uzalishaji Umeme ya NDC

29. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uzalishaji umeme kutokana na Makaa ya Mawe, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) linaendelea kusimamia utekelezaji wa **Mradi wa Mchuchuma wa MW 600 na Ngaka MW 400**. Miradi hiyo inasimamiwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

(iv) Miradi ya Usafirishaji Umeme

30. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme inayoanzia **Iringa hadi Shinyanga ya Msongo wa kV 400 (Backbone)** unaendelea vizuri. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 utekelezaji wa Mradi huo ulifikia wastani wa **asilimia 89**. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 224** sawa na takriban **Shilingi bilioni 387.5**. Mradi utakamilika mwezi Septemba, 2016. Mradi huo utaboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Arusha, Mwanza, Singida, Shinyanga na Tabora. Aidha, utasaidia kuunganisha Gridi za Taifa za Tanzania, Kenya na Zambia na kuiwezesha Tanzania kushiriki kikamilifu katika biashara ya umeme kupitia *Eastern African Power Pool (EAPP)* na *Southern African Power Pool (SAPP)*. Fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2016/17 ni **Shilingi bilioni 20**.

31. Mheshimiwa Spika, Mwezi Agosti, 2015 TANESCO ilisaini Mikataba na Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa **Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa kV 220 kutoka Makambako hadi Songea** na vituo vya kupoeza umeme vya Madaba na Songea vilivyopo Mkoa wa Ruvuma. Aidha, kazi ya kusambaza nguzo za umeme wa Msongo wa kV 33 katika Mikoa ya Njombe na Ruvuma imeanza.

32. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17 kazi zilizopangwa ni: kukamilisha ujenzi wa njia za usambazaji wa umeme kwa kiwango cha kV 33 na 0.4 katika Wilaya za Ludewa, Mbinga, Namtumbo, Njombe, Songea Mjini na Songea Vijijini; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoeza umeme. Gharama za Mradi huu ni **Krona za Sweden milioni 500** sawa na **Shilingi bilioni 112**. Fedha zilizotengwa na Serikali kwa Mwaka 2016/17 ni **Shilingi bilioni 42**. Mradi umepangwa kukamilika mwezi Desemba, 2017.

Miradi ya Usafirishaji Umeme Iliyo Katika Hatua za Mwisho Kuanza Utekelezaji

33. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha umeme unaozalishwa unafika katika maeneo unakohitajika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa njia za kusafirisha umeme zenye uwezo mkubwa, hususan kV 400. Miradi ambayo utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika ifikapo Mwaka 2019/20 ni pamoja na Singida – Arusha – Namanga kV 400, Bulyanhulu – Geita kV 220, Geita – Nyakanazi kV 220, North – East Grid kV 400 na Somanga – Kinyerezi kV 400.

34. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa **Mradi wa Singida – Arusha - Namanga kV 400** ambao ni sehemu ya Mradi unaunganisha Gridi za Taifa za Zambia, Tanzania na Kenya (ZTK Interconnector) umeanza. Mwezi Aprili, 2015 Serikali ilisaini Mkataba wa Mkopo wa **Dola za Marekani milioni 116.7** sawa na **Shilingi bilioni 259.99** na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu. Serikali pia ilisaini Mkataba mwingine wa Mkopo wa Mradi huu wa **Dola za Marekani milioni 98.23** sawa na **Shilingi bilioni 218.85** na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) mwezi Januari, 2016.

35. Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika ni: kukamilisha tathmini ya mali za watu watakaopisha Mradi katika Mikoa ya Arusha na Manyara; na kutangazwa kwa zabuni za Wakandarasi wa kujenga vituo vya kupoeza umeme pamoja na njia ya kusafirisha umeme. Utekelezaji wa Mradi kwa sehemu ya kutoka Singida hadi Namanga unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 258.82** sawa na **Shilingi bilioni 576.63**. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2016/17 ni **Shilingi bilioni 23**. Mradi unatarajiwa kukamilika Mwaka 2018/19.

36. Mheshimiwa Spika, Serikali iliajiri Kampuni ya Shaker Consulting Group ya Misri kuwa Mshauri Mwelekezi wa kusimamia utekelezaji wa **Mradi wa Bulyanhulu – Geita kV 220** wenye urefu wa kilomita 55. Mshauri huyo pia atasimamia usambazaji umeme katika vijiji 10 Wilayani Geita pamoja na kujenga Kituo cha kupozea umeme Wilayani humo. Kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka 2016/17 ni kumpata Mkandarasi na kuanza kwa utekelezaji wa Mradi. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 23** sawa na takriban **Shilingi bilioni 41**. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mradi huu ni **Shilingi bilioni 6** na unatarajiwa kukamilika Mwaka 2017/18.

37. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2015 Kampuni ya Lahmeyer International ya Ujerumani iliajiriwa kuwa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kusimamia **Mradi wa Geita – Nyakanazi kV 220** wenye urefu wa kilomita 133. Mshauri huyo pia atasimamia ujenzi wa Kituo cha kupozea umeme cha Nyakanazi pamoja na usambazaji wa umeme kwenye vijiji 23 vinavyopitiwa na Mradi. Kazi nyingine zilizokamilika ni Tathmini ya Athari za Kijamii na Mazingira na upimaji wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme. Mradi unatarajiwa kukamilika Mwaka 2018/19.

38. Mheshimiwa Spika, Gharama za utekelezaji wa Mradi huo ni **Euro milioni 45** sawa na takriban **Shilingi bilioni 81.48**. Mradi huo unafadhiliwa na KfW (Germany), AFD (France), EU na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo ni **Shilingi bilioni 7**. Utekelezaji wa Mradi utanza mwezi Oktoba, 2016 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2018.

39. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16 kazi zilizokamilika katika **Mradi wa North – East Grid kV 400** ni pamoja na Tathmini ya Athari za Kijamii na Mazingira; na tathmini ya mali kwa watu watakaopisha Mradi katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Aidha, majadiliano kati ya Serikali yetu na Benki ya Exim ya China kwa ajili ya Mkopo wa **Dola za Marekani milioni 588** sawa na **Shilingi bilioni 1,310** yamekamilika. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 85** ya gharama za Mradi wote na **asilimia 15** itatolewa na Serikali.

40. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, kazi zitakazofanyika ni kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi kwa sehemu ya Kinyerezi hadi Chalinze na kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mradi. Gharama ya Mradi ni **Dola za Marekani milioni 693** sawa na **Shilingi bilioni 1,543.9** ambapo Serikali inachangia **asilimia 15**. Jumla ya fedha zilizotengwa katika Mwaka 2016/17 kwa ajili ya Mradi huo ni **Shilingi bilioni 16** na utakamilika Mwaka 2019/20.

41. Mheshimiwa Spika, TANESCO imesaini Mkataba wa Mkopo wa **Dola za Marekani milioni 150** sawa na **Shilingi bilioni 334.19** na Benki ya

Maendeleo ya TIB mwezi Novemba, 2015. Mkopo huo ni kwa ajili ya utekelezaji wa **Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa kV 400 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi**. Njia hiyo itakuwa na urefu wa kilomita 198 na pia itahusisha Kituo cha kupozea umeme katika eneo la Somanga Fungu. Mradi huu utaunganisha na kusafirisha hadi Dar es Salaam umeme unaotarajiwa kuzalishwa kutoka Somanga Fungu (MW 350) na Kilwa Energy (MW 320) Mkoani Lindi.

42. Mheshimiwa Spika, TANESCO imekamilisha tathmini ya ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi huu. Hadi mwezi Aprili, 2016 **Shilingi bilioni 26.06** tayari zimelipwa na TANESCO kwa watu 947 katika Wilaya za Ilala na Temeke. Kazi zitakazofanyika kwa Mwaka 2016/17 ni kumpata Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa Mradi. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2019. Gharama ya Mradi huo ni **Dola za Marekani milioni 150** sawa na **Shilingi bilioni 334.19**. Fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2016/17 kwa ajili ya Mradi huo ni **Shilingi bilioni 5**. Mradi unatarajiwa kukamilika Mwaka 2019/20.

(v) Miradi ya Usambazaji Umeme

43. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa **Mradi wa Electricity V** ulikamilika mwezi Desemba, 2015. Mradi huo ulihusu ujenzi wa njia ya kusambaza umeme wa Msongo wa kV 33, kufunga transfoma na kuwaunganishia umeme wateja 8,600 katika Wilaya za Bukombe, Kwimba, Magu, Mbogwe, Misungwi na Sengerema. Wateja waliunganishiwa umeme hadi mwezi Aprili, 2016 ni 4,001. Pamoja na kuwa Mradi umekamilika kulingana na Mkataba wa Mkopo kutoka AfDB, TANESCO itaendelea na kazi ya kuwaunganishia umeme wateja waliobaki.

44. Mheshimiwa Spika, Mradi huu pia ulihusu ukarabati wa Vituo vya kupozea umeme vya Ilala na Sokoine katika Jiji la Dar es Salaam na upanuzi wa Kituo cha kupozea umeme cha Njiro Mkoani Arusha. Mradi ulitekelezwa na Serikali kupitia Mkopo uliotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mradi uligharimu Jumla ya **Unit of Account (UA) milioni 32.25** sawa na takriban **Shilingi bilioni 101.31**. Kati ya fedha hizo **UA milioni 28.68** sawa na **asilimia 89** ni Mkopo kutoka AfDB na **UA milioni 3.57** sawa na **asilimia 11** zilitolewa na Serikali yetu.

45. Mheshimiwa Spika, Awamu ya Pili ya **Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini (REA Turnkey Phase II)** inaendelea kutekelezwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa Vituo sita (6) vya umeme wa kV 11/33 katika Miji ya Kasulu, Kibondo, Kigoma, Mbinga, Ngara na Tunduru; ujenzi wa njia za kusambaza umeme zenye urefu wa takriban kilomita 15,000 za Msongo wa kV 33; ujenzi wa Vituo vidogo 3,100 vya kupozea na kusambaza umeme vyenye uwezo wa kV 33/0.4/0.23; na ujenzi wa njia ndogo ya usambazaji umeme

wenye urefu wa kilomita 7,000. Kwa ujumla hadi kufikia Aprili, 2016 utekelezaji wa Mradi wa REA Turnkey Phase II umefikia **asilimia 85**.

46. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia REA imekamilisha kazi ya kuunganisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya 4 za Buhingwe, Kakonko na Uvinza zilizopo katika Mkoa wa Kigoma na Nyasa iliyopo katika Mkoa wa Ruvuma. Kuanzia Julai, 2015 hadi Aprili, 2016 idadi ya wateja waliounganishiwa umeme na REA pamoja na TANESCO ni 220,128 sawa na **asilimia 88** ya lengo la kuunganisha wateja 250,000 ifikapo Juni, 2016.

47. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17 Serikali itafanya tathmini ya kina ya Awamu ya Kwanza na ya Pili ya utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini. Lengo la tathmini hiyo ni kuboresha maandalizi na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini (REA Turnkey Phase III). Pamoja na tathmini hiyo, masuala yatakayozingatiwa katika Awamu ya Tatu ni kupeleka umeme: kwenye vijiji ambavyo havikupata umeme katika awamu ya kwanza na ya pili; kwenye viwanda vidogo vya uzalishaji mali; na katika shule za sekondari, hospitali, zahanati, vituo vya afya, pampu za maji na maeneo mengine muhimu ya huduma za jamii. Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini itaanza Mwaka 2016/17 na kukamilika Mwaka 2018/19.

48. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza wigo wa upatikanaji umeme vijijini, Serikali imeongeza Bajeti ya Maendeleo ya fedha za ndani kwa REA kutoka **Shilingi bilioni 357.12** kwa Mwaka 2015/16 hadi **Shilingi bilioni 534.4** kwa Mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la **asilimia 50**. Ongezeko hilo ni katika kutekeleza **Ibara ya 43 C(i) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 – 2020**. Aidha, fedha za nje zilizotengwa kwa ajili ya Mradi huo ni **Shilingi bilioni 53.21** sawa na **asilimia 9** na hivyo kufanya Jumla ya Bajeti yote ya REA kwa Mwaka 2016/17 kuwa **Shilingi bilioni 587.61**. Vilevile, REA ipo katika taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi atakayetekeleza Mradi wa kusambaza umeme kwenye vijiji 121 inakopita njia kuu ya umeme ya Iringa hadi Shinyanga (Backbone). Taratibu hizo za ununuzi zitakamilika ifikapo Mwezi Desemba, 2016.

49. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya kusambaza umeme vijijini, REA imeanza miradi ya kusambaza umeme kwenye vijiji vinavyopitiwa na miundombinu ya umeme ya Msongo wa kV 11 na 33 (*Underline Distribution Transformers*). Mradi huu unahusisha kufunga transfoma na kusambaza umeme kupitia miundombinu ya kusambaza umeme ya Msongo wa kV 0.4/0.23. Tathmini ya Awamu ya Kwanza ya Mradi imekamilika katika Mikoa ya Arusha, Iringa, Mara, Mbeya, Pwani na Tanga. Katika Mwaka 2016/17, REA inatarajia kuanza kutekeleza Mradi huu baada ya taratibu za kuwapata Wakandarasi kukamilika Mwezi Desemba, 2016. Mradi huu utagharimu Jumla ya **Shilingi bilioni**

58.4. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 28.7** sawa **asilimia 49** ni fedha za Mfuko wa Nishati Vijijini na **Shilingi bilioni 29.7** sawa na **asilimia 51** ni fedha kutoka Serikali ya Sweden na Norway. Mradi utanza kutekelezwa Mwezi Januari, 2017 na utakamilika baada ya miezi 18.

50. Mheshimiwa Spika, TANESCO imeendelea kutekeleza **Mradi wa kupeleka umeme katika Wilaya za Biharamulo, Mpanda na Ngara kupitia Programu ya ORIO.** Kwa upande wa Wilaya za Biharamulo na Ngara utekelezaji umefikia **asilimia 65.** Ufungaji wa jenereta zenye uwezo wa Jumla ya MW 2.5 kwa kila Wilaya umeanza mwezi Aprili, 2016. Vilevile, ujenzi wa njia za kusambaza umeme umeanza mwezi Februari, 2016.

51. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha mchango wake wa **Shilingi bilioni 22** kwa ajili ya Mradi huu baada ya kutolewa kwa **Shilingi bilioni 11.5** mwezi Machi, 2016 ili kupeleka umeme Wilaya ya Mpanda. Kufuatia kutolewa kwa fedha hizo, utekelezaji wa Mradi ulianza mwezi Aprili, 2016 kwa Mkandarasi ZWART Teknik B.V kutoka Uholanzi kuagiza majenereta. Gharama za Mradi ni **Euro milioni 33.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 81.5.** Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ufalme wa Uholanzi. Upelekaji umeme katika Wilaya za Biharamulo na Ngara unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2016 na Wilaya ya Mpanda utakamilika mwezi Juni, 2017.

52. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa **Mradi wa Tanzania Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP)** unaendelea katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Kilimanjaro. Jumla ya Vituo 19 vya kusambaza umeme wa Msongo wa kV 33/11 vitakarabatiwa. Aidha, ujenzi wa njia za usambazaji umeme za Msongo wa kV 33 zenye urefu wa kilomita 107 zinajengwa. Vilevile, njia za usambazaji umeme wa Msongo wa kV 11 zenye urefu wa kilomita 50 zitajengwa. Jumla ya transfoma 65 za kV 33/0.4 zitafungwa. Katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi huu ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2016.

53. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Programu ya Awamu ya Pili ya **Mradi wa Sustainable Solar Market Package (SSMP – II)** ulianza mwezi Oktoba, 2015. Mradi huu unahusu ujenzi wa mifumo ya Umeme wa Jua katika Wilaya nane (8) za Biharamulo (Kagera), Bukombe na Chato (Geita), Kasulu na Kibondo (Kigoma), Namtumbo na Tunduru (Ruvuma) na Sikonge (Tabora). Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 18** sawa na **Shilingi bilioni 40.1** ambazo ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika Wilaya hizo kupitia REA katika Mwaka 2016/17 na utakamilika Mwaka 2017/18.

(vi) Kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme

54. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati na Mwelekeo wa Kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme (*Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap*). Katika Mwaka 2015/16 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha utayarishaji wa Mikataba Kifani ya Kuuziana Umeme (*Model Power Purchase Agreement -MPPA*) mwezi Agosti, 2015; kukamilisha uandaaji wa *Grid Codes*; na mwongozo wa tozo kwa kampuni moja kutumia miundombinu ya kampuni nyingine kusafirisha umeme (*transmission wheeling charges rules*).

55. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango huo ikiwa ni pamoja na zoezi la tathmini ya mali za TANESCO; tathmini ya rasilimali watu inayohitajika katika Sekta Ndogo ya Umeme, Mafuta na Gesi Asilia; na ukaguzi wa mifumo ya kompyuta ya TANESCO.

(vii) Punguzo la Viwango vya Bei za Umeme

56. Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imetekeleza ahadi yake ya kupunguza bei za umeme. Kuanzia tarehe 01 Aprili, 2016 Serikali imepunguza bei ya umeme kwa kati ya **asilimia 1.5** na **2.4**. Serikali pia imeondoa tozo ya kuwasilisha maombi ya kuunganishiwa umeme (*application fees*) ya **Shilingi 5,000** na tozo ya huduma ya mwezi (*service charge*) ya **Shilingi 5,520** kwa Wateja wa Umeme kwa Daraja la T1 na D1, ambao wengi wao ni wa majumbani. Hatua hii itawasaidia watumiaji wadogo wa umeme mijini na vijijini kumudu gharama hizo, hivyo kuboresha shughuli za kijamii na kiuchumi.

(viii) Kuboresha Huduma za Wateja kwa Kuanzisha Ofisi Ndogo za TANESCO

57. Mheshimiwa Spika, kufuatia kuongezeka kwa utekelezaji wa miradi ya usambazaji umeme vijijini, Serikali kupitia TANESCO ina mpango wa kufungua Ofisi mpya 20 zenye hadhi ya Wilaya na Ofisi Ndogo (*sub-offices*) 46 katika maeneo mbalimbali nchini ili kuboresha huduma za TANESCO kwa wateja. Ujenzi wa Ofisi hizo unakadiriwa kugharimu **Shilingi bilioni 43.2** kwa kutumia vyanzo vya ndani vya Shirika. Aidha, endapo TANESCO itatumia majengo ya kupanga, gharama zinakadiriwa kuwa **Shilingi milioni 948** kwa Mwaka. Vigezo vitakavyotumika kuanzisha Ofisi mpya ni: urefu wa njia za umeme katika eneo husika; idadi ya transfoma na wateja waliopo; mahitaji ya juu ya umeme; na umbali kutoka Ofisi ya TANESCO ya Mkoa au Wilaya.

58. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini, Mwaka 2014 TANESCO ilianzisha Kampuni Tanzu ya Tanzania Concrete Poles Manufacturing Company Limited (TCPCO). Kampuni hiyo imeainisha Kanda nne kwa ajili ya kujenga viwanda vya kutengeneza nguzo za zege nchini. Kanda hizo ni Mashariki, Kaskazini, Ziwa na Nyanda za Juu Kusini Magharibi. Baada ya kukamilisha maandalizi na ujenzi wa viwanda hivyo, TCPCO inatarajia kuanza uzalishaji wa nguzo za zege Mwaka 2016/17.

Kuboresha Miundombinu ya Umeme Jijini Dar es Salaam

59. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha kupoeza umeme cha kV 132/33/MVA 2x45 City Centre umekamilika. Kituo kipo katika hatua za majaribio na kinatarajiwa kufunguliwa rasmi Mwezi Juni, 2016. Aidha, ujenzi wa Kituo cha kuongoza mifumo ya usambazaji umeme katika msongo wa kV 33 na kV 11 (*Distribution SCADA*) umekamilika na Kituo kipo kwenye majaribio. Vilevile, ujenzi wa njia ya umeme chini ya ardhi kwa msongo wa kV 132 kutoka Makumbusho kwenda City Centre umekamilika. Miongoni mwa manufaa ya Mradi huu ni kuwezesha wateja kupata huduma bora za umeme. Mradi huu unatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Finland na Japan kwa gharama za **Shilingi bilioni 123** sawa na **Dola za Marekani milioni 55.21**.

60. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi huu utaendelea katika Mwaka 2016/17 kwa kukamilisha ujenzi wa njia ya umeme chini ya ardhi kwa msongo wa kV 132 kutoka City Centre hadi Shule ya Sekondari Jangwani na ujenzi wa njia ya kV 132 kutoka Ilala hadi Shule ya Sekondari Jangwani.

(ix) Uendelezaji wa Nishati Jadidifu

61. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia **maporomoko madogo ya maji (mini – hydro)**. Katika Mwaka 2015/16 Miradi iliyokamilika ni Andoya (Mbinga), Darakuta (Manyara), Tulila (Songea) na Yovi (Kilosa) na ina uwezo wa kuzalisha Jumla ya MW 6.6. Aidha, katika Mwaka 2016/17 Serikali itasimamia Miradi inayoendelea yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 10.24 na mingine yenye Jumla ya MW 58.6 ambayo ipo katika hatua za mwisho za kuanza utekelezaji.

Bayogesi (Biogas)

62. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Uendelezaji wa Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) iliendelea kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Kujenga Mitambo ya Bayogesi nchini. Hadi mwezi Mei, 2016 Jumla ya Mitambo 14,000 ilijengwa katika

ngazi ya kaya ikilinganishwa na Mitambo 12,000 kwa Mwaka 2014/15. Programu hiyo imewezesha wananchi 84,000 kutumia nishati hiyo kwa ajili ya kupikia na kupata mwanga. Hadi kufikia mwishoni mwa Mwaka 2017 CAMARTEC itakuwa imejenga Jumla ya Mitambo 21,000.

63. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2016 Serikali pia imeanza kutekeleza Mradi wa matumizi ya Bayogesi majumbani kupitia REA. Mradi unahusisha ujenzi wa mifumo 10,000 ya Bayogesi kwenye Mikoa yote ya Tanzania Bara katika kipindi cha miaka miwili kuanzia Mwaka huu. Mradi unafadhiliwa na Serikali ya Norway kwa gharama ya **Shilingi bilioni 3.2**. Lengo la Serikali ni kuhamasisha matumizi ya Bayogesi majumbani ili kupunguza matumizi ya kuni, mkaa na aina nyingine za tungamotaka zinazosababisha uharibifu wa mazingira.

64. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme kwa kutumia bayogesi ni moja ya vyanzo vinavyotarajiwa kuchangia ongezeko la umeme katika Gridi ya Taifa. Kampuni ya Mkonge Energy Systems inatarajia kutumia majitaka ya mkonge (*sisal waste water*) kuzalisha Jumla ya MW 1.5 katika mashamba ya mkonge yaliyoko kwenye vijiji vya Magoma (kW 500), Mwelya (kW 500) na Usambara (kW 500) vilivyopo Wilaya ya Korogwe.

Jotoardhi (Geothermal)

65. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Serikali kupitia Kampuni Tanzu ya TANESCO ya Uendelezaji wa Jotoardhi (*Tanzania Geothermal Development Company Limited - TGDC*), imekamilisha utafiti na kuthibitisha sehemu tatu katika eneo la Ziwa Ngozi, Mbeya zitakazochorongwa visima virefu ili kutathmini kiasi cha mvuke kinachoweza kuzalisha umeme. Vilevile, mwezi Desemba, 2015 Serikali ilisaini Mkataba wa Ushirikiano (*Partnership Agreement*) na Serikali ya Iceland kupitia Shirika la Maendeleo la Iceland (ICEIDA) kwa lengo la kuzalisha umeme kutokana na jotoardhi.

66. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Serikali kupitia TGDC itachoronga visima virefu vitatu katika eneo la Ziwa Ngozi, Mbeya kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 38** sawa na **Shilingi bilioni 84.66**. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali, *Global Risk Mitigation Fund (GRMF)* na *Investment Climate Fund (CIF)* kupitia *Scaling-Up Renewable Energy Programme (SREP)*. TGDC pia itaendeleza utafiti katika maeneo ya Kisaki (Morogoro), Luhoi (Pwani), Mbaka (Mbeya), Mlima Meru na Ziwa Natron (Manyara) kwa kushirikiana na *Federal Institute for Geosciences and Natural Resources (BGR)*, *Global Risk Mitigation Fund (GRMF)*, *Icelandic International Development Agency (ICEIDA)* na *United Nations Environment Programme (UNEP)*.

67. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha Miongozo, Mipango na Sheria ya kuendeleza Jotoardhi nchini. Katika Mwaka 2016/17, Jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mradi wa Jotoardhi ni **Shilingi bilioni 28**. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 2** sawa na **asilimia 7** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 26** sawa na **asilimia 93** ni fedha za nje.

Nishati ya Upepo na Jua (*Wind and Solar Energy*)

68. Mheshimiwa Spika, kazi ya kubainisha maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa umeme kwa kutumia nishati ya jua na upepo zimekamiliwa. Taarifa za utafiti zilikusanywa na kutumika kuandaa Ramani zinazoonisha maeneo yanayofaa kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo hivyo. Lengo la kuwa na Ramani hizo ni kuhamasisha uwekezaji kwenye vyanzo vya kufua umeme kutokana na nishati mbadala au jadidifu.

69. Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya utekelezaji wa **Ibara ya 45(a) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2015 – 2020)** Serikali imepanga kupeleka umeme maeneo yasiyofikiwa kwa urahisi na Umeme wa Gridi kwa kutumia mifumo midogo ya Umeme wa Jua. Katika Mwaka 2016/17, Serikali inapanga kupeleka umeme katika maeneo ya visiwa vidogo katika Ziwa Victoria na eneo la Kisiwa cha Mafia kwa kutumia mifumo midogo ya Umeme wa Jua. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hizo ni **Shilingi bilioni 6.5**.

Tungamotaka (*Biomass*)

70. Mheshimiwa Spika, Mwezi Januari, 2016 Wizara ilifanya majadiliano na Kampuni za kuzalisha sukari za Kagera, Kilombero, Mtibwa na TPC kwa lengo la kuongeza uzalishaji umeme kwa kutumia mabaki ya miwa (*bagasse*). Endapo umeme mwingi utazalishwa na viwanda hivyo, ziada itaweza kuuzwa kwa TANESCO. Aidha, viwanda hivyo vimeshauriwa kupunguza matumizi ya mvuke katika uzalishaji wa sukari ambapo wataweza kuokoa kiasi cha MW 2 zinazoweza kuuzwa TANESCO.

(x) Matumizi Bora ya Nishati (*Energy Efficiency*)

71. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*) imekusanya takwimu za matumizi ya nishati kwenye viwanda vikubwa (*baseline information*). Takwimu hizi zitasaidia kuandaa Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati Nchini (*Energy Efficiency Action Plan*). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *GIZ* ilifanya *Energy Audit* ili kuhamasisha matumizi bora ya nishati katika Mamlaka za Maji za Morogoro na Singida kwa lengo la kupunguza matumizi ya umeme yasiyo ya lazima. Matokeo ya ukaguzi uliofanyika yalionyesha kuwa uniti 1,031,570 na uniti 786,458

za umeme zinaweza kuokolewa kwa mwaka kwenye Mamlaka za Maji za Morogoro na Singida, sawia kwa kutekeleza mipango ya matumizi bora ya nishati.

72. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Serikali kwa kushirikiana na GIZ itakamilisha na kuanza utekelezaji wa Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati. Vilevile, Serikali itafanya utafiti wa kiasi cha nishati kinachoweza kuokolewa katika Ofisi za Serikali na Viwandani ikiwa matumizi bora ya nishati yatazingatiwa.

SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

(i) Shughuli za Utafutaji Mafuta na Gesi Asilia

73. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Dodsai imekamilisha tathmini ya kiasi cha Gesi Asilia kilichogunduliwa katika Kisima cha Mambakofi – I kwenye Kitalu cha Ruvu Mkoa wa Pwani. Tathmini hiyo inaonesha uwepo wa Gesi Asilia kiasi cha futi za ujazo trilioni (TCF) 2.17, hivyo kufanya Gesi Asilia iliyogunduliwa nchini hadi mwezi Mei, 2016 kufikia **TCF 57.25** ikilinganishwa na **TCF 55.08** zilizokuwepo mwezi Aprili, 2015. Kati ya kiasi hicho **TCF 47.13** zipo kwenye kina kirefu baharini na **TCF 10.12** zipo nchi kavu.

74. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba, 2015 Kampuni ya Pan African Energy (PAET) ilikarabati Visima vya SS – 5, SS – 7 na SS – 9 pamoja na kuchoronga Kisima kipya cha SS – 12 mwezi Januari, 2016. Shughuli hizo zimeongeza uzalishaji wa Gesi Asilia kutoka Songo Songo kutoka futi za ujazo milioni (mmscfd) 105 kwa siku hadi futi za ujazo milioni (mmscfd) 190 kwa siku.

75. Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limeendelea kusimamia kazi ya utafutaji Mafuta na Gesi Asilia katika maeneo mbalimbali nchini. Katika Mwaka 2015/16, Shirika lilikusanya takwimu za kijiolojia kwa kutumia ndege - *Airborne Gravity Gradiometer (AGG)* na *Full Tensor Gradiometry (FTG)* katika maeneo ya Eyasi-Wembere (Manyara), Ziwa Tanganyika Kaskazini (Kigoma), Songo Songo Magharibi na Mandawa (Lindi) kwa lengo la kuongeza thamani ya maeneo hayo. Katika Vitalu 4-1B na 4-1C vilivyopo katika kina kirefu baharini, TPDC ilikamilisha tathmini ya awali ya kijiolojia na kijiofizikia kwa kukusanya takwimu za Mitetemo ya 2D katika maeneo hayo. TPDC inaendelea kufanya uchambuzi wa takwimu hizo ili kujiridhisha kama maeneo husika yana dalili za kuwa na Mafuta au Gesi Asilia. Kazi hiyo itakamilika mwishoni mwa Mwezi Juni, 2016.

76. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti, 2015 Kampuni ya Maurel & Prom pamoja na Wabia wake walifanikiwa kuchoronga Kisima MB – 4 katika Kitalu cha Mnazi Bay (Mtwara). Aidha, Kisima hicho kipya pamoja na Visima vya

MB – 2, MB – 3 na MSX – 1 viliunganishwa kwenye Mtambo wa kusafisha Gesi Asilia katika eneo la Madimba (Mtwara). Hadi sasa Gesi Asilia iliyopo katika Kitalu hicho inakadiriwa kufikia futi za ujazo trilioni (TCF) 5 na uzalishaji wake ni wastani wa futi za ujazo milioni 59 kwa siku.

(ii) Miundombinu ya Kusafisha na Kusafirisha Gesi Asilia

77. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara kupitia Lindi hadi Dar es Salaam (kilomita 542) pamoja na Mitambo ya kusafisha Gesi Asilia katika maeneo ya Madimba (Mtwara) na Songo Songo (Lindi). Mradi huo ulizinduliwa rasmi na Rais wa Awamu ya Nne Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Oktoba, 2015. Kukamilika kwa Mradi huo kumeongeza mchango wa uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia kufikia **asilimia 49**. Uzalishaji wa umeme kwa kutumia Gesi Asilia umewezesha gharama za uzalishaji umeme nchini kupungua kutoka wastani wa **Shilingi 262 hadi 229** kwa uniti moja ya umeme.

Mradi wa Miundombinu ya Liquefied Natural Gas (LNG)

78. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2015 TPDC ilikamilisha taratibu za kupata ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Mitambo ya kusindika Gesi Asilia (LNG) katika Kijiji cha Likong'o (Lindi). TPDC ilipewa Hati Miliki na Serikali kwenye eneo la ukubwa wa Hekta 2,071 kwa ajili ya kujenga Mitambo hiyo. Washirika wakubwa katika Mradi huu ni pamoja na TPDC, Kampuni za BG/Shell, Statoil, ExxonMobil, Pavillion na Ophir. Katika Mwaka 2016/17, kazi zitakazofanyika ni pamoja na upimaji wa eneo la kujenga Mitambo ya Mradi wa LNG, kupata vibali vya kuingiza kwenye Ramani za Mipango Miji michoro ya LNG, maeneo ya viwanda (*Industrial Parks*) na uwanja wa ndege. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo ni **Shilingi milioni 800**.

Mradi wa Usambazaji Gesi Asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara

79. Mheshimiwa Spika, TPDC ilikamilisha upembuzi yakinifu wa awali, Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza Gesi Asilia katika Miji ya Kilwa, Lindi na Mtwara. TPDC pia imeajiri Kampuni ya KIMPHIL Konsult (T) Limited kuwa Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi wa kina kuhusu Mradi huu. Mradi utahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza Gesi Asilia kwa njia ya Bomba (*Piped Natural Gas – PNG*) na iliyoshindiliwa (*Compressed Natural Gas - CNG*). Lengo la Mradi huu ni kusambaza Gesi Asilia kwa ajili ya mitambo ya kuzalisha umeme, matumizi majumbani, viwandani, kwenye magari na taasisi mbalimbali. Gharama za awali za Mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 10** sawa na takriban **Shilingi bilioni 22.3**. Katika Mwaka 2016/17 fedha zilizotengwa ni **Shilingi milioni 700**.

Usambazaji wa Gesi Asilia Jijini Dar es Salaam

80. Mheshimiwa Spika, lengo la Mradi huu ni kujenga Mtandao wa kusambaza Gesi Asilia kwa njia ya Mabomba na CNG. Kwa hatua za awali Mradi utaunganisha wateja 30,000 wa majumbani na kujenga vituo 15 vya kujazia Gesi Asilia kwenye magari. Kazi za upembuzi yakinifu na uandaaji wa michoro kwa ajili ya Mradi zimekamiliika. Gharama za Mradi ni takriban **Dola za Marekani milioni 150** sawa na **Shilingi bilioni 334.19**. Serikali kupitia Wizara ya Fedha, inafanya majadiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kupata fedha za kutekeleza Mradi huu. Katika Mwaka 2016/17 fedha zilizotengwa ni **Shilingi bilioni 5**.

(iii) Mradi wa Uzalishaji Mbolea kwa kutumia Gesi Asilia

81. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TPDC imesaini Mkataba wa Ubia na Kampuni ya Ferrostaal ya Ujerumani mwezi Septemba, 2015 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea. Mradi huu utagharimu **Dola za Marekani bilioni 1.98** sawa na **Shilingi bilioni 4,411.24** na ujenzi unatarajiwa kuchukua takriban miaka mitatu na nusu. Kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha Mbolea ya Urea tani 3,850 kwa siku na kitatumia Gesi Asilia kiasi cha futi za ujazo Trilioni 1 kwa miaka 20. Vilevile, mchango wa TPDC katika Mradi huu ni ardhi yenye eneo la ukubwa wa Hekari 425 lililopo Kilwa Masoko (Lindi) ambapo kiwanda kitajengwa. Kwa mujibu wa Mkataba wa utekelezaji wa Mradi huu, TPDC itaruhusiwa kumiliki hadi **asilimia 40** ya Hisa za Kampuni itakayojenga kiwanda hiki.

(iv) Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Masuala ya Petroli

82. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria ya Petroli ya Mwaka, 2015 Wizara inaendelea na taratibu za kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Masuala ya Petroli (*Petroleum Upstream Regulatory Authority - PURA*). Mwezi Februari, 2016 Serikali imeunda Kamati Maalum (*Interim Committee*) ya kutekeleza majukumu ya PURA katika kipindi cha mpito pamoja na kuratibu shughuli mbalimbali zinazolenga kuifanya PURA kuwa chombo kamili cha udhibiti ifikapo mwezi Julai, 2016.

83. Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuandaa Mpango Kazi wa Uanzishwaji wa PURA; kuandaa Muundo na Kazi za Mamlaka (*Organisational Structure and Scheme of Service*); kuandaa Rasimu ya Mpango Mkakati (*Draft Strategic Plan*); kuandaa Bajeti pamoja na Mpango wa upatikanaji wa rasilimali fedha; na kuandaa Rasimu za Miongozo na Kanuni (*Rules and Regulations*) mbalimbali zitakazowezesha PURA kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Bodi ya Wakurugenzi ya PURA itateuliwa Mwezi Julai, 2016.

84. Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengine PURA itakagua Mikataba na kuchambua masuala ya kiuchumi katika kuingia Mikataba ya utafutaji na ugawanaji mapato yatokanayo na shughuli za Mafuta na Gesi Asilia; itasimamia masuala ya ushiriki wa Watanzania katika shughuli za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia; na kufuatilia na kutathmini shughuli za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, Sheria ya Usimamizi wa Mapato yatokanayo na Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2015 inaipa PURA mamlaka ya kukagua au kuagiza kufanyika ukaguzi wa vyanzo vya mapato ya Serikali katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

(v) Wakala wa Uagizaji wa Mafuta ya Petroli kwa Pamoja

85. Mheshimiwa Spika, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekamilisha uanzishwaji wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (*Petroleum Bulk Procurement Agency – PBPA*) mwezi Januari, 2016. Wakala huo pamoja na kazi nyingine unatekeleza majukumu ya iliyokuwa Kampuni Binafsi ya kuratibu Uagizaji wa Mafuta ya Petroli kwa Pamoja (*Petroleum Importation Coordinator Limited - PICL*). Kampuni hiyo ilikuwa inamilikiwa na Kampuni binafsi za uagizaji na usambazaji wa mafuta ya petroli nchini. Lengo la kuanzisha Wakala huu ni kuongeza ufanisi katika shughuli za uagizaji mafuta ya petroli nchini.

86. Mheshimiwa Spika, miongoni mwa majukumu ya Wakala huu ni kusimamia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta ya Petroli kwa Pamoja (*Petroleum Bulk Procurement System - BPS*) na kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya petroli ya kutosha wakati wote nchini. Katika Mwaka 2016/17, Wakala utaanza pia kuratibu uagizaji wa *Liquefied Petroleum Gas - LPG* pamoja na mafuta mazito (*Heavy Fuel Oil - HFO*) kupitia mfumo wa BPS.

Uagizaji wa Mafuta ya Petroli

87. Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Serikali iliahidi katika Bunge lako la Bajeti ya Mwaka 2015/16, Bandari ya Tanga ilianza kupokea mafuta kupitia Mfumo wa Uagizaji Mafuta ya Petroli kwa Pamoja (*BPS*) kuanzia mwezi Julai, 2015. Katika kipindi cha Januari na Desemba, 2015 Jumla ya lita **bilioni 5.16** za mafuta ya petroli ziliingizwa nchini kupitia Bandari za Dar es Salaam (lita bilioni 4.25) na Tanga (lita milioni 91.27). Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 12** ikilinganishwa na **lita bilioni 4.63** zilizoingizwa Mwaka 2014. Kati ya mafuta hayo, **lita bilioni 3.1** sawa na **asilimia 60** yalikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na **lita bilioni 2.06** sawa na **asilimia 40** yalikuwa kwa ajili ya nchi jirani.

88. Mheshimiwa Spika, mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani yameongezeka kwa **asilimia 9** kutoka **lita bilioni 2.84** Mwaka 2014 hadi **lita bilioni 3.10** Mwaka 2015. Aidha, mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya nchi jirani

yameongezeka kwa **asilimia 15** kutoka **lita bilioni 1.79** Mwaka 2014 hadi **lita bilioni 2.06** Mwaka 2015. Ongezeko hilo linatokana na kukua kwa mahitaji ya Mafuta ndani ya nchi pamoja na nchi jirani kuongeza uagizaji wa Mafuta kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

(vi) Mwenendo wa Bei za Mafuta katika Soka la Dunia

89. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2015 bei ya Mafuta katika Soko la Dunia ziliendelea kushuka na kufikia wastani wa **Dola za Marekani 38** kwa pipa la Mafuta Ghafi kwa Mwezi Desemba, 2015. Aidha, wastani wa bei ya Mafuta yaliyosafishwa kwa kipindi cha kati ya Mwezi Januari na Desemba, 2015 ulikuwa kama ifuatavyo: Petroli kutoka **Dola za Marekani 669** hadi **Dola za Marekani 437** kwa tani; Dizeli kutoka **Dola za Marekani 570** hadi **Dola za Marekani 335** kwa tani; na Mafuta ya Taa/Ndege kutoka **Dola za Marekani 570** hadi **Dola za Marekani 363** kwa tani ambayo ni sawa na punguzo la **asilimia 35** kwa Petroli, **asilimia 41** kwa dizeli na **asilimia 39** kwa Mafuta ya Taa/Ndege, sawia.

90. Mheshimiwa Spika, Bei ya Mafuta katika Soko la Ndani hutegemea bei ya mafuta ya petroli katika Soko la Dunia pamoja na Thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na Dola ya Marekani. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2015 wastani wa bei za mafuta katika Soko la Ndani kwa lita ilikuwa: Petroli **Shilingi 1,973**, Dizeli **Shilingi 1,808** na Mafuta ya Taa **Shilingi 1,739** ikilinganishwa na wastani **Shilingi 2,186** kwa Petroli, **Shilingi 2,082** kwa Dizeli na **Shilingi 2,030** kwa Mafuta ya Taa kwa kipindi kama hicho katika Mwaka 2014.

91. Mheshimiwa Spika, EWURA iliendelea kusimamia shughuli za uagizaji wa LPG nchini. Kati ya Januari na Desemba, 2015 Jumla ya tani 70,061 ziliagizwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali nchini ikilinganishwa na tani 65,611 Mwaka 2014, sawa na ongezeko la **asilimia 7**. Ongezeko hilo linatokana kuongezeka kwa uelewa kuhusu manufaa ya matumizi ya LPG, kuboreshwa kwa miundombinu ya kuhifadhi, kujaza mitungi na kusambaza LPG. Katika Mwaka 2016/17 EWURA itaendelea kuisimamia Sekta Ndogo ya Mafuta Nchini.

(vii) Hisa za Serikali katika Kampuni za PUMA, TAZAMA na TIPER

92. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia Hisa zake katika Kampuni za PUMA Energy Tanzania Limited – **asilimia 50**; Tanzania - Zambia Pipeline Limited (TAZAMA – **asilimia 30**); na Tanzania International Petroleum Reserve (TIPER – **asilimia 50**). Kampuni hizo zimekamilisha hesabu za Mwaka 2014, ambapo Serikali imepata Gawio la **Shilingi bilioni 3** kutoka PUMA. Kampuni ya TIPER ilipata faida ya **Dola za Marekani milioni 11.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 25.6**, ambapo wanahisa walikubaliana badala ya

kutoa Gawio waziwekeze katika kuboresha miundombinu ya hifadhi ya mafuta kutoka lita za ujazo 71,000 hadi lita za ujazo 212,000. Aidha, Kampuni ya TAZAMA haikutoa Gawio kwa kuwa haikupata faida katika kipindi husika. Katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kuzisimamia Kampuni hizo ili kuongeza ufanisi na kupata Gawio kubwa zaidi.

(viii) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania

93. Mheshimiwa Spika, Mwezi Aprili, 2016 Serikali ya Tanzania ilisaini Makubaliano ya Awali (MoU) na Serikali ya Uganda kwa ajili ya ujenzi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Bandari ya Tanga, Tanzania. Bomba hilo litakuwa na urefu wa kilomita 1,443 ambapo kati ya hizo kilomita 1,115 zitakuwa upande wa Tanzania. Bomba hilo litakuwa na uwezo wa kusafirisha mapipa 200,000 ya Mafuta Ghafi kwa siku.

94. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania, utekelezaji wa Mradi huu utakuwa na manufaa mbalimbali yakiwemo: kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato kupitia Bandari ya Tanga na tozo ya kupitisha Mafuta Ghafi kwenye Bomba; kuongezeka kwa uwekezaji wa fedha za kigeni; na fursa za ajira za kudumu kwa Watanzania takriban 1,000 na 10,000 za muda wakati wa ujenzi. Majadiliano ya utekelezaji wa Mradi huu kati ya Serikali za Tanzania, Uganda, TPDC pamoja na Kampuni za TOTAL (France), CNOOC (China) na Tullow (UK) yameanza.

95. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushirikiano wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali ya Uganda imealika nchi za Burundi, Kenya, Rwanda na Tanzania kushiriki katika uwekezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kusafisha Mafuta Ghafi (*Oil Refinery*) nchini Uganda. Kila nchi imepewa fursa ya kushiriki kwa kununua **asilimia 8** ya Hisa za Mradi ambazo makisio yake ya awali ni **Dola za Marekani milioni 150.4** sawa na **Shilingi bilioni 335.08**. Katika Mradi huo, Sekta Binafsi pia imekaribishwa kushiriki. Serikali ya Tanzania imeridhia ushiriki katika uwekezaji kwenye Kiwanda hicho cha Kusafisha Mafuta Ghafi.

(ix) Sera na Sheria katika Sekta ya Nishati

96. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Serikali imekamiliha Sera ya Taifa ya Nishati, 2015 na Sheria ya Petroli, 2015. Lengo la kupitisha Sera na Sheria hizo ni kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Nishati nchini. Katika Mwaka 2016/17, Kanuni na Miongozo mbalimbali itaandaliwa kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa Sera na Sheria hizo.

97. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia EWURA imeandaa Miongozo ya Uanzishwaji wa Miradi ya Umeme kwa mujibu wa Kifungu cha 5

cha Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008 - *The Electricity (Initiation of Power Procurement) Rules 2014*. Lengo la Mwongozo ni kuhakikisha kuwa uwekezaji katika Miradi ya Umeme unafanyika kwa tija na kuleta unafuu kwa wananchi na uchumi wa nchi yetu.

SEKTA YA MADINI

Uzalishaji na Biashara ya Madini

98. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015 Jumla ya wakia milioni 1.37 za dhahabu, wakia 497,152 za fedha na ratili milioni 13.76 za shaba zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka Migodi Mikubwa ya dhahabu ya Geita, Bulyanhulu, Buzwagi, North Mara, Stamigold Biharamulo na New Luika. Jumla ya thamani ya madini hayo ni **Dola za Marekani bilioni 1.63** ikilinganishwa na **Dola za Marekani bilioni 1.66** kwa Mwaka 2014, sawa na pungufu kwa takriban **asilimia 2**. Mrabaha uliolipwa Serikalini kutokana na madini hayo ni **Dola za Marekani milioni 63.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 140.8**.

99. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini ya Tanzanite, Jumla ya gramu milioni 2.4 za Tanzanite ghafi zenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 4.48** zilizalishwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi na Kampuni ya TanzaniteOne. Mrabaha uliolipwa Serikalini kutokana na mauzo ya Tanzanite ni Jumla ya **Dola za Marekani 223,979**. Vilevile, Jumla ya karati 191,407 za madini ya almasi zenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 53.34** zilizalishwa na kuuzwa na Mgodhi wa Mwadui ambapo Mrabaha wa **Dola za Marekani milioni 2.30** ulilipwa Serikalini.

100. Mheshimiwa Spika, biashara ya madini Duniani imeendelea kukumbwa na mtikisiko kutokana na kushuka kwa bei kulikoathiri uwekezaji kwenye Sekta hiyo. Bei ya wakia moja ya dhahabu imeshuka kutoka **Dola za Marekani 1,266.19** Mwaka 2014 hadi kufikia wastani wa **Dola za Marekani 1,160.12** Mwaka 2015, sawa na upungufu wa **asilimia 8**. Bei ya shaba ilishuka kwa **asilimia 20** kutoka wastani wa **Dola za Marekani 3.11** kwa ratili Mwaka 2014 hadi **Dola za Marekani 2.50** Mwaka 2015, huku bei ya fedha ikishuka kwa **asilimia 18** kutoka **Dola za Marekani 19.08** Mwaka 2014 hadi **Dola za Marekani 15.70** kwa wakia Mwaka 2015. Hali hiyo imesababisha kushuka kwa Mrabaha na mapato mengine yanayokusanywa kutokana na madini hayo.

101. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali imeendelea kuongeza uwezo wa kusimamia madini yanayouzwa nje ya nchi kwa kudhibiti utoroshwaji wake. Udhibiti huo kwa Mwaka 2015 umewezesha kukamata na kutaifisha madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya Jumla ya **Dola za Marekani milioni 1.5** sawa na **Shilingi bilioni 3.34**. Madini hayo yalikamatwa katika matukio 25 kwenye viwanja vya ndege vya Kimataifa vya Julius Nyerere (Dar es Salaam) na KIA (Kilimanjaro).

102. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeongeza usimamizi katika eneo la Merelani kwa kuunda Kikosi Kazi cha kufuatilia uchimbaji na biashara ya Tanzanite. Kikosi Kazi hicho kimefanikisha: kukamatwa madini ya Tanzanite yenye uzito wa kilogramu 2.02 yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 1.21** sawa na **Shilingi bilioni 2.70** kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KIA); kukamata madini ya Tanzanite gramu 13,314.6 yenye thamani ya **Shilingi milioni 54.69** kutoka kwa wafanyabiasha wa ndani wasio na leseni; kuondolewa nchini kwa wafanyakazi 15 wa kutoka nje ya nchi waliokuwa wanafanya kazi katika Mgodi wa TanzaniteOne kinyume cha Sheria; na kujitokeza kwa Wafanyabiasha 361 kuomba leseni za udalali katika Ofisi za Arusha (194) na Merelani (167).

103. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa biashara ya vito, Wizara kwa kushirikiana na *Tanzania Mineral Dealers Association (TAMIDA)* imeendesha Maonesho ya Kimataifa ya vito yaliyofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 19 hadi 21 Aprili, 2016. Katika Maonesho hayo madini yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 4.04** sawa na **Shilingi bilioni 9** yaliuzwa. Katika hatua za awali, Serikali ilikusanya Mrabaha wa **Dola za Marekani 158,597.46** sawa na **Shilingi milioni 353.34** na **Shilingi bilioni 1.36** zilipatikana kutokana na mauzo ya sehemu ya madini yaliyokamatwa yakitoroshwa nje ya nchi.

104. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Serikali itaboresha usimamizi wa uzalishaji na biashara ya madini ili kuongeza mchango wa Sekta hiyo katika maendeleo ya Taifa. Aidha, mpango mwingine ni kuendelea kuendesha minada ya ndani ya madini ya vito ikiwemo Tanzanite sambamba na kuimarisha udhibiti wa utoroshaji madini katika maeneo ya migodi na kwenye mipaka ya nchi.

Malipo ya Ushuru wa Huduma

105. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015, Migodi ya Geita, Bulyanhulu, Buzwagi, North Mara, New Luika na Williamson Diamonds Limited imelipa ushuru wa huduma (*service levy*) wa Jumla ya **Shilingi bilioni 10.34** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 4.1** Mwaka 2014. Malipo hayo yameongezeka kwa **asilimia 152**. Ongezeko hili limechangiwa na Kampuni zenye *Mining Development Agreements (MDAs)* kulipa ushuru wa huduma wa **asilimia 0.3** ya mapato ghafi badala ya **Dola za Marekani 200,000** kwa Mwaka.

106. Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo: Kampuni ya Acacia imelipa **Shilingi milioni 866.25** kwenye Halmashauri ya Kahama, **Shilingi bilioni 1.59** kwa Halmashauri ya Msalala na **Shilingi bilioni 2.01** kwa Halmashauri ya Tarime. Vilevile, Kampuni ya Shanta Gold Mining Limited imelipa **Shilingi milioni 831.41** kwa Halmashauri ya Chunya, Kampuni ya Williamson Diamonds Limited imelipa **Shilingi milioni 334.85** kwa Halmashauri ya Kishapu na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited imelipa

Shilingi bilioni 4.67 kwa Halmashauri ya Geita. Kampuni ya Almasi ya El-Hillal pia imelipa ushuru wa huduma wa **Shilingi milioni 27.57** Mwaka 2015 kwa Halmashauri ya Kishapu.

107. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa Viongozi wa Halmashauri husika **kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa na Kampuni za uchimbaji madini ikiwemo malipo ya ushuru wa huduma zinatumiwa katika shughuli za maendeleo kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.**

Kuendeleza Uchimbaji Mdogo wa Madini

108. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza **Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020, Ibara ya 35(m)(i) inayoelekeza kuwapatia maeneo Wachimbaji Wadogo**, kwa Mwaka 2015/16, Serikali ilitenga maeneo mawili (2) yenye ukubwa wa Hekta 7,731. Maeneo hayo yapo Nyamongo (Tarime) na Muhintiri (Singida) na yalipatikana kwa utaratibu wa ushirikiano kati ya Serikali na Kampuni za Acacia Mining Plc na Shanta Gold Mining Limited.

109. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Serikali itatenga maeneo sita (6) yenye ukubwa wa takriban Hekta 12,000 kwa ajili ya uchimbaji mdogo. Taratibu za kupatikana maeneo hayo zitazingatia taarifa za kijiolojia kutoka kwa Kampuni mbalimbali za utafutaji madini kwa kushirikisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST).

110. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza ahadi yake ya kuwapatia Ruzuku Wachimbaji Wadogo. Katika Mwaka 2015/16 Serikali imetoa Ruzuku ya **Shilingi bilioni 7.24** kwa Miradi 111 ya uchimbaji mdogo wa madini. Katika Mwaka 2016/17, **Dola za Marekani milioni tatu (3)** sawa na **Shilingi bilioni 6.68** zimetengwa kupitia Mradi wa SMMRP kwa ajili ya kutoa Ruzuku. Wizara itaendelea kutathmini maendeleo ya miradi iliyopata Ruzuku ili kuhakikisha inaleta manufaa.

111. Mheshimiwa Spika, pamoja na kutenga maeneo kwa Wachimbaji Wadogo wa madini, Serikali ilitoa mafunzo kwa Wachimbaji Wadogo 181. Mafunzo hayo yalifanyika Mkoani Dodoma mwezi Oktoba, 2015 na yalihusu namna bora ya matumizi ya Ruzuku na utunzaji wa kumbukumbu. Aidha, mwezi Februari, 2016 Wafanyabiashara 23 wa madini walipewa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa utoaji taarifa za biashara ya madini. Mafunzo hayo yalifanyika Jijini Mwanza.

112. Mheshimiwa Spika, mafunzo mengine yalifanyika mwezi Machi, 2016 Jijini Dar es Salaam kwa viongozi 38 wa Vyama vya Wachimbaji Wadogo ambavyo ni FEMATA, TAWOMA, WIMA, TASPA na REMAS. Mafunzo hayo yalihusu mfumo wa utoaji wa taarifa za uchimbaji mdogo na kanzidata ya vifaa vya

uchimbaji na uchenjuaji madini. Katika Mwaka 2016/17, Wizara kupitia STAMICO na GST itaendelea kutoa huduma za ugani na mafunzo ya nadharia na vitendo kwa Wachimbaji Wadogo pamoja na Viongozi wa Wilaya na Halmashauri.

Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini

113. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16 Wizara ilianzisha Mfumo wa malipo ya leseni kwa njia ya mtandao (*online payments system*). Mfumo huo ulianza rasmi tarehe 10 Desemba, 2015 kwa lengo la kuimarisha utoaji na usimamizi wa leseni za madini. Sambamba na hatua hiyo, Wizara imeendelea kusajili wateja zaidi kwenye Mfumo wa kupokea maombi ya leseni kwa njia ya mtandao (*Online Mining Cadastre Transactional Portal - OMCTP*), hatua ambayo imeboresha utendaji na kupunguza mianya ya rushwa.

114. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Jumla ya leseni 4,803 za utafutaji na uchimbaji wa madini zilisajiliwa kwenye Mfumo huo (OMCTP) kati ya leseni 38,695 zilizopo. Kati ya leseni hizo zilizosajiliwa: leseni 1,628 ni za utafutaji mkubwa wa madini; leseni 65 ni za uchimbaji mkubwa na wa kati; na leseni 3,110 ni za uchimbaji mdogo. Kwa upande wa umiliki wa leseni za utafutaji na uchimbaji mkubwa wa madini, Watanzania wanamiliki **asilimia 68** ya leseni zote, Wageni **asilimia 28** na **asilimia 4** ya leseni zinamilikiwa kwa ubia kati ya Watanzania na Wageni. Leseni za uchimbaji mdogo ambazo ni 35,273 zinamilikiwa kwa **asilimia 100** na Watanzania.

115. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kati ya mwezi Julai, 2015 na Machi, 2016 Jumla ya maombi ya leseni 8,025 ya utafutaji na uchimbaji madini yalipokelewa. Jumla ya leseni 4,782 zilitolewa ambapo kati ya hizo, leseni 112 ni za utafutaji mkubwa wa madini, leseni 12 za uchimbaji wa kati, leseni moja (1) ya uchimbaji mkubwa na leseni 4,657 ni za uchimbaji mdogo wa madini. Aidha, maombi 2,716 ya leseni yalikataliwa kwa kushindwa kukidhi masharti. Maombi 527 yanaendelea kuchambuliwa kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

116. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya ukaguzi wa maeneo ya leseni na uchambuzi wa taarifa za utendaji kwenye leseni za madini. Uchambuzi wa taarifa za leseni umewezesha kubaini wamiliki wasiozingatia masharti ya leseni zao. Hatua za kisheria zimeendelea kuchukuliwa kwa wamiliki wasiotimiza masharti ya leseni.

117. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kati ya mwezi Julai, 2015 na Machi, 2016, Jumla ya leseni 1,330 zilifutwa. Kati ya leseni hizo, 151 zilikuwa ni za utafutaji madini na 1,179 ni za uchimbaji mdogo wa madini. Aidha, hati za makosa (*default notice*) 117 zilitolewa kwa leseni 111 za utafutaji madini na 6 za uchimbaji wa kati. **Napenda kutoa wito kwa wamiliki wa leseni za madini**

kutimiza masharti yaliyowekwa kwenye leseni hizo ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kufuta leseni zao.

118. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuboresha huduma kwa wateja ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za leseni za madini kwa njia ya Mtandao. Aidha, usimamizi wa leseni utaimarishwa ili kuhakikisha kuwa wamiliki wote wa leseni wanatimiza masharti ya kisheria. Hatua nyingine zitakazochukuliwa ni pamoja na kushughulikia malalamiko na migogoro katika Sekta ya Madini kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali, zikiwemo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

119. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha utunzaji wa taarifa na takwimu katika Sekta ya Madini. **Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imejenga na kuanzisha Kituo Maalum cha Kuhifadhi Takwimu za Madini (Data Recovery Centre).** Kituo hicho ambacho kimejengwa Mjini Morogoro kilianza kazi rasmi mwezi Februari, 2016. Kituo hicho kitawezesha Serikali kuwa na uhakika wa upatikanaji wa taarifa zinazohusu Sekta ya Madini kwa nchi nzima endapo litatokea tatizo katika Ofisi yoyote ya Madini huko Mikoani.

Kuimarisha Usimamizi wa Masuala ya Baruti Nchini

120. Mheshimiwa Spika, kazi za uagizaji, uzalishaji, usafirishaji, uhifadhi na matumizi ya Baruti ziliendelea. Jumla ya tani 22,229 za Baruti ziliingizwa nchini kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikilinganishwa na tani 24,308 za Baruti zilizoingizwa Mwaka 2014/15 sawa na upungufu wa **asilimia 9**. Upungufu huo unatokana na shughuli za utafiti wa madini kupungua kwa kipindi husika kwa sababu ya kushuka kwa bei za madini, hususan dhahabu, shaba na fedha kwenye Soko la Dunia.

121. Mheshimiwa Spika, Wizara pia iliendelea kusimamia uingizaji wa fataki ambapo kwa kipindi cha kati ya mwezi Julai, 2015 na Januari, 2016 vipande 4,189,337 viliagizwa. Fataki hizo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo uchimbaji madini, utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na miradi ya ujenzi wa miundombinu. Aidha, Wizara ilitoa vibali 86 vya kuingiza Baruti nchini, vibali 75 vya kulipulia Baruti na leseni 9 za maghala ya kuhifadhi Baruti.

122. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa masuala ya Baruti nchini. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu na mafunzo ya matumizi bora na salama ya Baruti kwa Wachimbaji Wadogo na wadau wengine wa Baruti ambao wanafikia takriban 800 nchi nzima.

Usimamizi wa Migodi Nchini

123. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2015/16, Jumla ya Migodi 1,241 ilifanyiwa ukaguzi wa masuala ya afya, usalama na utunzaji wa mazingira. Ukaguzi huo ulifanyika katika Migodi Mikubwa minne ya dhahabu ambayo ni North Mara, Bulyanhulu, Buzwagi, Geita na Migodi wa almasi wa Mwadui; Migodi ya Kati 75; na Migodi Midogo 1,161. Ukaguzi huo ulilenga kuboresha afya, usalama na utunzaji mazingira migodini kwa kuzingatia Taratibu na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

124. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha uwezo wa Wakaguzi wa Migodi, mwezi Novemba, 2015 Wizara iliendesha mafunzo yanayohusu usalama katika Migodi ya Makaa ya Mawe. Mafunzo hayo yalifanyika Mjini Bagamoyo Mkoa wa Pwani na yalikusisha Wakaguzi 75. Mafunzo hayo yalitolewa na Wakufunzi wa *Centre for Science and Environment* kutoka nchini India. Aidha, Wizara imeanzisha Timu ya Uokoaji (*Mine Rescue Team*) itakayofanya kazi ya uokoaji katika matukio ya ajali yanayotokea migodini. Timu hiyo iliyoundwa mwezi Oktoba, 2015 ina Wakaguzi wa Migodi 17 kutoka Ofisi za Madini na imeanza kupatiwa mafunzo kuhusu masuala ya uokoaji.

125. Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kusimamia na kuboresha afya, usalama na utunzaji wa mazingira migodini, katika Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi wa migodi ya Wachimbaji Wadogo, wa kati na wakubwa na imepanga kufanya ukaguzi kwa Jumla ya Migodi 1,500 nchini. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Utunzaji Mazingira (*Environmental Protection Plan - EPP*) kwa Wachimbaji Wadogo wa madini. Pia, Wizara itakamilisha Mikataba kati yake na migodi inayomilikiwa na Kampuni ya Acacia (Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara) kwa ajili ya kuweka Hati Fungani (*rehabilitation bond*) ifikapo Mwezi Juni, 2016.

Kuimarisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini Nchini

126. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Wizara iliendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini ambapo Jumla ya Leseni 20 za uchenjuaji madini ya dhahabu zilitolewa na kufikia Jumla ya Leseni 162. Kutolewa kwa leseni hizo kumeongeza chachu ya wananchi kuendelea kushiriki zaidi katika shughuli za kuongeza thamani madini, hususan uchenjuaji wa marudio ya dhahabu. Aidha, ongezeko la leseni hizo limewezesha Serikali kuongeza mapato yatoakanayo na shughuli za uchenjuaji dhahabu. Katika kipindi cha kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 **Shilingi bilioni 2.9** zilikusanywa ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 2.2** zilizopatikana kipindi kama hicho katika Mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la **asilimia 32**.

127. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuhamasisha na kusimamia shughuli za uongezaji thamani madini. Kipaumbele kitawekwa katika kuhamasisha uwekezaji wa viwanda ili kuwezesha Watanzania wengi kushiriki katika shughuli hizo.

128. Mheshimiwa Spika, Kituo cha Jemolojia Tanzania (*Tanzania Gemological Centre – TGC*) cha Arusha kiliandaa mitaala ya kufundishia fani za *gemology, jewelry design & manufacturing* na *stone carving*. Aidha, taratibu za kukisajili Kituo hicho NACTE zinaendelea. Katika Mwaka 2015/16, Kituo kimetoa mafunzo ya kukata na kusanifu madini ya vito kwa Wanawake 14 na hivyo kuongeza idadi ya wahitimu wa mafunzo hayo kufikia Wanawake 29.

129. Mheshimiwa Spika, Kituo kimeendelea kujiimarisha kwa kununua vifaa vya kufundishia mafunzo ya Jemolojia vikiwemo *gemological microscopes 25, refractometer 25, spectroscope 25, diamond tester 10, digital refractometer* na *hydrostatic balance*. Vifaa vingine vilivyounuliwa ni kwa ajili ya kufundishia usanifu na usonara ambavyo ni pamoja na *computer 8, GEMCAD software 5, 3-D wax printer 3, card printer 3, wire wrapping, forming, soldering* na *cutting tools*. Vilevile, mashine 21 za kukata na kung'arisha madini ya vito (*faceting machines*) zilinunuliwa. Jumla ya **Dola za Marekani milioni 1.3** sawa na takriban **Shilingi bilioni 2.9** zimetumika katika ununuzi wa vifaa hivyo kupitia Mkopo kutoka Benki ya Dunia chini ya Mradi wa SMMRP.

130. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Kituo kitaanzisha maabara ya utambuzi wa madini ya vito pamoja na kutoa vyeti vya uthibitisho (*Certificate of Authenticity*). Aidha, shughuli za utafiti (*research and design*), huduma za ushauri na ugani zitatolewa kwenye madini ya vito na usonara. Vilevile, huduma nyingine itakayotolewa ni ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito kwa Wajasiriamali na Wachimbaji Wadogo.

Uchambuzi na Uthaminishaji wa Madini ya Vito

131. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Wizara iliendelea na usimamizi wa tasnia ya almasi na vito. Katika kipindi cha kati ya Julai, 2015 na Februari, 2016 karati 129,329 za almasi zenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 40.90** zilithaminishwa. Kutokana na mauzo hayo, Serikali ilipata Mrabaha wa **Dola za Marekani milioni 2.04** sawa na **Shilingi bilioni 4.42**.

132. Mheshimiwa Spika, madini ya vito yalithaminishwa kama ifuatavyo: tani 1,299.48 za madini ya mapambo, gramu milioni 2.02 za vito ghafi na karati 66,849.24 za madini ya vito yaliyochongwa. Madini hayo yalithaminishwa kwa Jumla ya **Dola za Marekani milioni 15.32** na yaliipatia Serikali Mrabaha wa **Dola za Marekani 608,580.79** sawa na **Shilingi bilioni 1.36**. Katika Mwaka 2016/17,

Serikali itaendelea kuimarisha shughuli za uchambuzi na uthaminishaji wa madini ya almasi na vito ili kuongeza mapato kwa Serikali.

Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP)

133. Mheshimiwa Spika, Mradi wa SMMRP upo katika awamu ya pili ya utekelezaji ambayo ilianza rasmi Septemba, 2015 na itaisha Desemba, 2018. Katika Mwaka 2015/16, Mradi umewezesha ukarabati wa Ofisi za Madini za Mtwara, Moshi, Nachingwea na Tunduru. Aidha, ununuzi wa vifaa vya mafunzo kwa ajili ya Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) na vitendea kazi kwa Ofisi za Madini za Bariadi, Moshi, Nachingwea, Njombe na Songea umefanyika. Fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na ukarabati wa Ofisi hizo ni **Shilingi bilioni 1.35** ambazo zimetolewa na Benki ya Dunia.

134. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, kupitia Mradi wa SMMRP kazi zifuatazo zitatekelezwa: ukarabati na upanuzi wa Ofisi za Madini za Bariadi, Bukoba, Chunya, Kigoma, Mpanda, Musoma na Songea; Ofisi za STAMICO (Dar es Salaam) na Chuo cha Madini (Dodoma). Kupitia Mradi huu, vifaa mbalimbali vya ugani vitanunuliwa ili kusaidia Wachimbaji Wadogo wa madini kupitia STAMICO, GST na Ofisi za Madini za Kanda. Aidha, Mradi utawezesha GST kufanya utafiti katika maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za uchimbaji mdogo na yale yanayopendekezwa kuwa vituo vya mafunzo. Lengo ni kutathmini mashapo yaliyopo na hivyo kuwawezesha Wachimbaji Wadogo kufanya shughuli zao kwa uhakika zaidi.

135. Mheshimiwa Spika, Wizara pia itaanzisha Vituo saba (7) vya mfano vya kuchenjua madini kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo katika Mikoa ya Kagera, Katavi, Lindi, Mara, Mbeya, Ruvuma na Shinyanga. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuendeleza Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) na kuwezesha usimikaji wa Mtandao wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika Ofisi za Madini za Bariadi, Mbeya, Moshi, Mtwara, Nachingwea na Njombe. Makadirio ya ujenzi wa vituo hivyo ni **Dola za Marekani milioni 6** sawa na **Shilingi bilioni 13.4**.

Miradi Mikubwa ya Madini

136. Mheshimiwa Spika, pamoja na bei ya madini ya dhahabu na nikeli kushuka katika Soko la Dunia, Serikali imeendelea kuhamasisha uendelezaji wa miradi mikubwa ya madini. Uhamasishaji huo unahusisha pia madini ya *graphite* ambayo bei zake hazijaathirika katika Soko la Dunia. Miongoni mwa miradi ya madini ambayo ipo katika hatua za uendelezaji ni pamoja na Mradi wa *graphite* uliopo Nachu Wilaya ya Ruangwa na Mradi wa *graphite* uliopo Epanko Wilaya ya Ulanga.

137. Mheshimiwa Spika, Miradi mingine iliyopo katika hatua za uendelezaji ni Mradi wa Urani uliopo eneo la Mto Mkuju Wilaya ya Namtumbo na Mradi wa Niobium uliopo Wilaya ya Songwe. Madini ya Niobium hutumika katika utengenezaji wa vifaa vya kieletroniki. Upembuzi yakinifu wa Miradi hii miwili umekamilika.

Utatuzi wa Migogoro katika Uchimbaji Madini

138. Mheshimiwa Spika, kero na migogoro mbalimbali ya madini imeendelea kutatuliwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inaendeshwa kwa amani. Mojawapo ya mgogoro ni leseni 15 za utafutaji madini ya dhahabu zilizotolewa karibu na eneo la Kambi ya Jeshi lililopo Kiabakari, Wilaya ya Butiama. Aidha, kuna maombi mengine ya leseni za utafiti ambayo yamo ndani ya eneo la Kambi hii. Katika utatuzi wa mgogoro huu, Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kutafuta ufumbuzi wa suala hilo.

139. Mheshimiwa Spika, upo mgogoro unaohusu eneo la Nyarugusu, hususan Kitongoji cha Buziba, Mkoa wa Geita ambalo wananchi wamekuwa wakiliomba kwa muda mrefu ili kuchimba madini ya dhahabu. Eneo hilo lina leseni hai ya utafiti wa madini inayomilikiwa kwa ubia kati ya STAMICO na Kampuni ya Mineral Royalty ya Canada. Pamoja na kuwepo kwa leseni hiyo, Serikali inakamilisha taratibu za kisheria za kuchukua sehemu ya eneo hilo kwa ajili ya kuligawa kwa wananchi. Katika Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kutatua migogoro iliyopo katika maeneo mbalimbali ya uchimbaji madini nchini.

Sheria katika Sekta ya Madini

140. Mheshimiwa Spika, Rasimu za Sheria za Baruti na Uongezaji Thamani Madini zimekamilika. Lengo la Sheria hizo ni kuimarisha usimamizi katika matumizi ya Baruti na Fataki pamoja na shughuli za uongezaji thamani madini. Hata hivyo, Wizara inaendelea kukusanya maoni zaidi kutoka kwa wadau muhimu ili kuziboresha Rasimu hizo. Katika Mwaka 2016/17, Wizara itakamilisha Rasimu hizo na kuziwasilisha katika Mamlaka husika ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ajili ya maamuzi.

Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST)

141. Mheshimiwa Spika, Wakala ulikusanya taarifa zitakazoweza kuchorwa kwa Ramani kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji (*Mineral Promotion Block Map*) katika Wilaya za Masasi, Nachingwea na Tunduru. Wakala pia kwa kushirikiana na *Geological Survey of Finland* (GTK) na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) unaendelea na kazi ya uchunguzi wa maabara wa sampuli za

udongo zilizokusanywa katika Wilaya hizo. Matokeo ya uchunguzi wa udongo yatawezesha Wakala kuchora Ramani za Jiokemia (*Multi-Element Geochemical Atlas*) kwa Wilaya hizo tatu.

142. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Wakala utachapisha Ramani kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji katika Wilaya hizo na taarifa zake baada ya kupata matokeo ya utafiti kutoka maabara. Kazi hizo zinagharimu Jumla ya **Euro 700,000** sawa na takriban **Shilingi bilioni 1.74** na zinafadhiliwa na Serikali ya Finland.

143. Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha Wachimbaji Wadogo, Wakala ulifanya utafiti wa kina wa Jiokemia na Jiofizikia katika maeneo ya Kyerwa Mkoa wa Kagera. Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kubaini kiasi na mwelekeo wa mbale ya madini (*ore*) ya bati (*tin*). Matokeo ya utafiti yatasaidia Wachimbaji Wadogo kuchimba kwa kufuata mwelekeo wa mbale na hivyo kuwa na uchimbaji salama na wenye tija kwa lengo la kuongeza kipato chao. Kazi ya utafiti itakamilika Mwezi Juni, 2018 na itagharimu **Shilingi milioni 640** na fedha hizo zitatoka Mradi wa SMMRP.

144. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, GST itafanya utafiti wa jiokemia, jiolojia, jiofizikia na tabia za mbale (*ore characteristics*) katika maeneo ya Endabash (Manyara), Handeni (Tanga), Ibindi (Katavi), Itumbi (Mbeya), Kapanda (Katavi), Katente (Geita), Kilindi (Tanga), Kyerwa (Kagera), Merelani (Manyara), Mgusu (Geita), Mvomero (Morogoro), Nyamongo (Mara) na maeneo ya Mkoa wa Singida ya Kilondata, Londoni Sambaru, Mpambaa na Muhintiri. Lengo ni kusaidia Wachimbaji Wadogo namna ya kutafuta mwelekeo wa mbale pamoja na kuwaelimisha kuhusu uchimbaji na uchenjuaji salama na wenye tija.

145. Mheshimiwa Spika, vilevile GST itafanya kazi maalum (*field checks*) ya jiolojia na jiokemia ili kuboresha Ramani za QDS 49, 64 na 65. Kazi hiyo itasaidia kukusanya na kuhakiki taarifa za uwepo wa madini nchini na kuboresha kanzidata yake. Wakala utaendelea kuratibu majanga ya asili ya jiolojia ikiwa ni pamoja na matetemeko ya ardhi na milipuko ya volkeno. Wakala pia utabaini maeneo yenye hatari ya kupata maporomoko ya ardhi ikiwemo Safu za Milima ya Usambara na kutoa ushauri kwa wananchi waishio katika maeneo hayo.

Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA)

146. Mheshimiwa Spika, TMAA imeendelea na kazi ya ukaguzi wa Hesabu za Fedha za Migodi na kuwezesha Kodi ya Mapato ya Jumla ya **Shilingi bilioni 107.7** kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Fedha hizo zimekusanywa kutoka Kampuni za Geita Gold Mining Limited (**Shilingi bilioni**

76.03), North Mara Gold Mining Limited (**Shilingi bilioni 31.2**) na Resolute Tanzania Limited (**Shilingi milioni 472**) katika kipindi kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016. Pia, ukaguzi huo umewezesha Serikali kukusanya Kodi na Tozo nyingine zenye Jumla ya **Shilingi bilioni 2.79** kutoka Migodi Mikubwa na ya Kati iliyokaguliwa katika kipindi hicho.

147. Mheshimiwa Spika, ukaguzi uliofanywa na Wakala kwa kushirikiana na Ofisi za Madini za Kanda umewezesha Serikali kukusanya Mrabaha wa **Shilingi bilioni 5.1** kutokana na shughuli za uzalishaji na biashara ya madini ya ujenzi na viwandani. Fedha hizo zilizokusanywa katika kipindi kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 ni ongezeko la **asilimia 16** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 4.4** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka 2014/15.

148. Mheshimiwa Spika, katika kipindi kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 Wakala ulifanya ukaguzi na uhakiki wa madini katika Migodi Mikubwa na ya Kati. Ukaguzi huo uliwezesha mrabaha wa Jumla ya **Dola za Marekani milioni 52** sawa na takribani **Shilingi bilioni 115.85** kulipwa Serikalini. Malipo hayo yalikuwa kama ifuatavyo: Bulyanhulu **Dola za Marekani milioni 10.53**; Buzwagi **Dola za Marekani milioni 5.88**; Geita **Dola za Marekani milioni 17.88**; North Mara **Dola za Marekani milioni 9.95**; Mwadui **Dola za Marekani milioni 3.37**; New Luika **Dola za Marekani milioni 3.36**; STAMIGOLD Biharamulo **Dola za Marekani milioni 0.75**; TanzaniteOne **Dola za Marekani milioni 0.05**; na Ngaka **Dola za Marekani milioni 0.25**.

149. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kuimarisha ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini katika migodi kupitia TMAA. Lengo ni kuhakikisha kuwa Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali ya madini na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa.

Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

150. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 STAMICO kupitia Kampuni yake Tanzu ya STAMIGOLD imezalisha na kuuza wakia 17,346 za dhahabu. Madini hayo yalikuwa na thamani ya **Dola za Marekani milioni 19.80**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 44.11**. STAMICO ilipata **Shilingi milioni 426.49** kutoka STAMIGOLD ikiwa ni ada ya usimamizi (management fee).

151. Mheshimiwa Spika, kati ya Mwezi Julai, 2015 na Machi, 2016 Mgodi wa TanzaniteOne unaomilikiwa kwa ubia wa asilimia 50 kwa 50 kati ya STAMICO na Kampuni ya Sky Associates ulizalisha karati 10,927,080 za Tanzanite. Madini hayo ya Tanzanite yalikuwa na thamani ya **Dola za Marekani milioni 1.4**, sawa

na takriban **Shilingi bilioni 3.12**. STAMICO imepata **Shilingi milioni 30.43** kutoka TanzaniteOne ikiwa ni ada ya usimamizi.

152. Mheshimiwa Spika, Shirika limekamilisha utafiti wa awali wa kijiolojia katika leseni yake ya madini adimu (*Rare Earth Elements*) iliyopo eneo la Sengeri Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe. Matokeo ya utafiti huo wa awali yameonesha uwepo wa madini hayo ambayo hutumika kutengeneza vifaa vya kisasa vya kielektroniki. Shirika pia limekamilisha utafiti wa awali wa madini ya chuma (*iron ore*) na *feldspar* katika leseni yake iliyopo Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro ambapo matokeo ya maabara yameonesha uwepo wa madini ya chuma katika eneo hilo.

153. Mheshimiwa Spika, STAMICO imeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Wachimbaji Wadogo ili kuboresha shughuli zao za uchimbaji. Mwezi Februari, 2016 Shirika lilikamilisha na kuzindua tovuti ya uchimbaji mdogo (*Small Scale Mining Portal*). Jumla ya Wachimbaji Wadogo na Wafanyabiashara wa madini 35 walipatiwa mafunzo ya jinsi ya kuunganishwa na kutumia tovuti hiyo.

154. Mheshimiwa Spika, Shirika kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani limefanikiwa kununua mashine ya uchorongaji (*Drilling Rig*) moja yenye thamani ya **Dola za Marekani 350,000** sawa na takriban **Shilingi milioni 780**. Kununuliwa kwa mashine hiyo kutaongeza uwezo katika kazi za uchorongaji na utafiti kwenye maeneo yanayomilikiwa na Shirika, Wachimbaji Wadogo na kukodisha kwa wadau wengine wanaohitaji huduma hiyo.

155. Mheshimiwa Spika, STAMICO ilifanya uchambuzi yakinifu kuona uwezekano wa kujenga kiwanda cha kuchenjua mabaki ya dhahabu katika Mgodi wa Buhemba. Ilibainika kuwa, katika mabaki ya mchanga wa dhahabu ambayo ni tani 796,400 kuna dhahabu gramu 1.07 kwa kila tani ambazo kwa mabaki yote ya dhahabu wastani wa kilo 682 za dhahabu zitapatikana (ikichukuliwa kuwa asilimia 80 ya mabaki ya mchanga utakaochenjuliwa yatatoa dhahabu). Katika Mwaka 2016/17, **Shilingi bilioni 10.58** kutoka vyanzo vya ndani vya STAMICO zitatumika kununua mashine ya kuchenjua mabaki ya dhahabu.

156. Mheshimiwa Spika, STAMICO imetekeleza kazi mbalimbali za kuendeleza Mradi wa kuzalisha umeme wa MW 200 wa Makaa ya Mawe wa Kiwira, Mbeya zikiwemo: kukamilisha tathmini ya awali ya maeneo yatakayoathiriwa na njia ya kupitisha umeme yenye urefu wa kilomita 100 kutoka Kiwira hadi Mwakibete Jijini Mbeya; kupitia upya taarifa za mashimo ya kijiolojia (*drill hole data*) kwa ajili ya kutathmini kiasi cha mashapo ya makaa ya mawe kilichopo kwenye leseni za Ivogo na Kabulo; na kuandaa *Concept Note* ya Mradi kwa ajili ya kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali.

157. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, STAMICO itaendelea kufufua Mradi wa Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira kwa nia ya kuzalisha umeme wa MW 200, ambapo **Shilingi bilioni 2** zimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu.

Chuo cha Madini - MRI

158. Mheshimiwa Spika, hatua za kukipandisha hadhi Chuo cha Madini Dodoma ziliendelea ambapo mwezi Desemba, 2015 Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) lilikipa mamlaka kamili ya kujitegemea kitaaluma na kiutawala (*Autonomous Status*). Chuo hicho kilipata idhini ya kuwa *Dodoma Polytechnic of Energy and Earth Resources Management*. Kutokana na hadhi hiyo, Chuo hicho kitajiendesha kwa kufuata taratibu za NACTE na kuboresha taaluma zinazotolewa. Kwa sasa taratibu za mwisho za kufikia hadhi hiyo zinaendelea ikiwemo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya elimu kuwasilisha Bungeni tamko husika kabla ya mwisho wa Mwaka 2016.

159. Mheshimiwa Spika, Chuo pia kimekamilisha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 88 kwa wakati mmoja. Vilevile, Chuo kimekamilisha ukarabati na upanuzi wa Jengo la Bwalo la chakula na sasa lina uwezo wa kuchukua wanafunzi 120 kwa pamoja tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo uwezo wake ulikuwa wanafunzi 50. Aidha, katika Mwaka 2015/16 Chuo kimedahili wanafunzi 586 katika fani mbalimbali. Jumla ya wanafunzi 182 wanatarajiwa kuhitimu mwezi Mei, 2016 katika ngazi ya stahabada ambapo kati yao wanawake ni 14 na wanaume ni 168. Wizara ya Nishati na Madini imetoa ufadhili wa **Shilingi milioni 539.34** kwa wanafunzi 178 waliojiunga katika fani za Mafuta na Gesi Asilia. Katika Mwaka 2016/17, Chuo kitaendelea kuimarisha utendaji wake kwa kuandaa fani mpya za masomo na kuendeleza watumishi na miundombinu.

Asasi ya Uwazi katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative – TEITI)

160. Mheshimiwa Spika, kama ilivyoahidiwa na Serikali, Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania (*Tanzania Extractive Industries Transparency and Accountability Act, 2015*) ilipitishwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 455 la tarehe 16 Oktoba, 2015. Pamoja na mambo mengine, lengo la Sheria hiyo ni kuipa nguvu ya kisheria Kamati ya TEITI ya kuzitaka Kampuni kuweka wazi taarifa za malipo, mauzo na gharama za uwekezaji; na Serikali kutakiwa kuweka wazi taarifa zake za mapato yanayotokana na rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na matumizi ya mapato hayo.

161. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Wizara itakamilisha maandalizi ya Kanuni za Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania ya Mwaka 2015. Aidha, Rejista ya Majina ya Wamiliki Hisa kwenye Leseni na Mikataba katika Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia itaanzishwa ili kuwatambua kwa majina wanaomiliki Hisa katika Kampuni Binafsi.

162. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2015 Kamati ya TEITI ilikamilisha na kutoa kwa umma taarifa za ulinganisho kwa Mwaka 2012/13 na 2013/14. Taarifa ni za malipo ya kodi yaliyofanywa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa Serikali Kuu na katika Halmashauri ambazo zinapokea Tozo kwa mujibu wa Sheria. Taarifa hizo zilibainisha baadhi ya Kampuni kubwa za uchimbaji wa madini ya dhahabu na vito ambazo hazijaanza kulipa Kodi ya Mapato (*Corporate Tax*). Kampuni hizo ni Acacia Mining (inayomiliki Migodi ya Bulyanhulu, North Mara na Buzwagi), Shanta Mining na TanzaniteOne Mining Limited.

163. Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa hizo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzielekeza Kampuni hizo kulipa Kodi ya Mapato na malimbikizo yote. Kufuatia hatua hizo, Kampuni ya Acacia imelipa Kodi ya Mapato ya **Dola za Marekani milioni 14** sawa na takriban **Shilingi bilioni 31.2** kwa Mgori wake wa North Mara Mwezi Machi, 2016.

AJIRA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

164. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza tija na motisha kwa watumishi, kwa Mwaka 2015/16 Wizara iliwapandisha vyeo Jumla ya watumishi 38 katika fani mbalimbali, kuwathibitisha kazini watumishi 108 na kuwabadilisha watumishi 11 kutoka kwenye kada moja kwenda nyingine (*re-categorization*).

165. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuajiri na kuendeleza watumishi wake ili waweze kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi. Katika Mwaka 2015/16, Jumla ya watumishi walioajiriwa na Wizara na Taasisi zake katika kada mbalimbali ni 179. Kati ya hao, Wizara iliajiri watumishi 68, TMAA 22, REA 6, TPDC 36, GST 44 na STAMICO 3.

166. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kutoa ufadhili wa masomo kwa Watanzania katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia. Mafunzo hayo hutolewa katika shahada za uzamili na uzamivu ili kuiwezesha nchi kuwa na Wataalamu wa Kitanzania katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia. Katika Mwaka 2015/16, Watanzania 18 walipata ufadhili wa mafunzo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

167. Mheshimiwa Spika, vilevile, kupitia *Energy Sector Capacity Building Program* inayoratibiwa na Wizara, Jumla ya Watanzania 321 walipata ufadhili wa mafunzo ambapo kati ya hao, 112 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi; 178 stashahada; na 31 walihudhuria mafunzo ya shahada za uzamili katika fani mbambali zikiwemo za Mafuta na Gesi Asilia. Fedha zilizotumika kwa ajili ya mafunzo hayo ni **Dola za Marekani 506,000** sawa na **Shilingi bilioni 1.13**. Fedha hizo zimetolewa kupitia Mkopo wa Benki ya Dunia na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Canada (CIDA). Katika Mwaka 2016/17 Serikali itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

168. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwapatia lishe na madawa maalumu watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) na wenye UKIMWI kulingana na miongozo iliyopo. Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi kujiepusha na tabia ambazo zinaweza kusababisha maambukizi ya UKIMWI na kupima afya zao mara kwa mara. Katika kipindi cha kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 Jumla ya **Shilingi milioni 12.6** zimetolewa kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI.

USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

169. Mheshimiwa Spika, Washirika wa Maendeleo wameendelea kushirikiana na Wizara katika shughuli mbalimbali, hususan kwenye miradi ya maendeleo na kuwajengea watumishi uwezo. Kwa kutambua mchango huo, na kwa niaba ya Serikali natumia fursa hii kutoa shukurani kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya BADEA, Benki ya Dunia (WB), Benki ya Exim ya China, Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan (JBIC) na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB). Vilevile, natoa shukurani kwa Taasisi na Mashirika ya AFD (Ufaransa), CIDA (Canada), ECDF (Korea Kusini), ICEIDA (Iceland), FINIDA (Finland), JICA (Japan), KfW (German), NORAD (Norway), OFID (Saudi Arabia), ORIO (Uholanzi), Sida (Sweden), UNDP, USAID (Marekani) na Umoja wa Ulaya (EU).

B. SHUKURANI

170. Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mbunge wa Jimbo la Chato, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini. Natambua uzoefu wake katika Sekta za Nishati na Madini na ninamshukuru kwa dhati kwa jinsi anavyoshirikiana nami katika kusimamia Wizara hii. Natoa shukurani pia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Prof. Justin William Ntalikwa, pamoja na Naibu Makatibu Wakuu Prof. James Epifani Mdoe na Dkt. Juliana Leonard Pallangyo kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipa katika kusimamia majukumu ya Wizara.

171. Mheshimiwa Spika, ufanisi wa Sekta za Nishati na Madini kwa kiasi kikubwa unategemea Wataalam wa fani mbalimbali. Hivyo, natumia fursa hii kuwashukuru watumishi wa Wizara wakiongozwa na Kamishna wa Nishati na Masuala ya Petrol; Kamishna wa Madini; na Wakuu wa Idara na Vitengo kwa kutekeleza majukumu yao ya kazi ipasavyo. Vilevile, nawashukuru Wenyevitwa Bodi pamoja na Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mzuri wanaonipa.

172. Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wananchi wa Tanzania kwa ujumla kwa kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ikiwemo kunipatia taarifa muhimu katika Sekta ninazosimamia. Aidha, natoa shukurani kwa wananchi wa Jimbo langu la Musoma Vijijini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na imani waliyonayo kwangu katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu. Kwa namna ya pekee naishukuru familia yangu kwa kunitia moyo na kunifariji katika kutekeleza majukumu yangu.

C. HITIMISHO

173. Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2016/17 ni Jumla ya **Shilingi 1,122,583,517,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,056,354,669,000** ni fedha za Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 94**. Kwa kuzingatia **Ibara ya 43(a) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020** inayoelekeza Serikali kuongeza kiwango kikubwa cha uzalishaji wa nishati ili kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa, **asilimia 98** ya Bajeti ya Maendeleo imetengwa kwa ajili ya Sekta ya Nishati.

174. Mheshimiwa Spika, fedha za Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 66,228,848,000** sawa na **asilimia 6** ya Bajeti yote. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 38,871,230,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) sawa na **asilimia 59** na **Shilingi 27,357,618,000** sawa na **asilimia 41** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

175. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja la Mheshimiwa Rashid Shangazi, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Waislamu wote, wakati wa kuahirisha Bunge saa saba mchana mkutane katika ukumbi wa Gairo kule *Morena Hotel*. Atakuwepo mgeni wenu Imam Ijaz Ahmad Shami wa kutoka *Islamic Help* Uingereza. (Makofi)

Mheshimiwa Susan Lyimo aliniomba Mwongozo lakini mwongozo huo ulikwishajiwa na Mheshimiwa Naibu Spika siku aliyomwomba. Kwa hiyo, nitasoma tena tu kwa mara nyingine kama alivyojibiwa na Mheshimiwa Naibu Spika ilivyokuwa kwenye *Hansard* ili jibu hilo litoshe pia kwa leo kama hakuwa

amesikia na leo pia hayupo, kwa hiyo siku nyingine atauliza tena mwongozo wake.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya mwongozo ule wa kwa nini vitabu vyenye picha na majina ya Waheshimiwa Wabunge havijatawanywa Bungeni, Mheshimiwa Naibu Spika alisema yafuatayo na mimi nanukuu:-

"Waheshimiwa Wabunge, asubuhi niliombwa mwongozo na Mheshimiwa Susan Lyimo kuhusu vitabu vyenye anuani za Wabunge na nilisema nitatoa maelezo kabla hatujasitisha shughuli za Bunge. Taarifa iliyopo vitabu hivi vitapatikana mwishoni mwa mwezi huu baada ya kupata Wajumbe watano kutoka Baraza la Wawakilishi ambao ni sehemu ya Bunge hili. Kwa hiyo, wakishaleta wale majina yao na wao wakaja hapa basi kitabu kitakuwa kimekamilika. Kwa jinsi hiyo, mwishoni mwa mwezi huu kitabu kitakuwa tayari na kitasambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni."

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo maneno ambayo nimeyanakuu moja kwa moja kama jibu, mwisho wa kunakuu. Kwa hiyo, jibu la Mheshimiwa Susan ni kwamba kuweni na subira, Mheshimiwa Naibu Spika alishasema, mpaka tupate wale watano kutoka Baraza la Wawakilishi waliotokana na ule uchaguzi wa marudio. (Makofi/Kicheko)

Tunaendelea na sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, karibu sana Mheshimiwa. (Makofi)

MHE. DOTO M. BITEKO - MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana kwa lengo la kupokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016 na kupitia makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Katika kufanikisha jukumu hili Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa kwa mujibu wa kanuni ya 98(1) cha Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

(ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

(iii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato ya matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/ 2017.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inaonesha matokeo ya shughuli hizo pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kutembelea Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Manyara, Njombe, Mbeya kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Nishati na Madini iliyotengewa fedha na kupelekewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu miradi iliyotembelewa na Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Kinyerezi I wa MW 150; bomba la gesi la Mtwara;

(ii) Mgodini wa Tanzanite One;

(iii) Makambako/Songea *transmission line* wenye msongo wa kilovoti 220;

(iv) REA katika vijiji vya Mkoa wa Njombe; na

(v) Mgodini wa makaa ya mawe ya Kiwira.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu maendeleo ya miradi iliyokaguliwa. Miradi iliyokaguliwa na Kamati kwa ujumla wake inahusu mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Uzalishaji wa umeme wa Kinyerezi I MW 150;

(ii) Bomba la kusafirisha gesi kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam pamoja na mitambo ya kuchakata na kusafirisha gesi ya Mnazi Bay na Songosongo;

(iii) Mradi wa Makambako wa kusambaza umeme katika Mikoa ya Ruvuma na Njombe. Kamati ilikagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini katika Vijiji vya Lyamkena, Itipingi, Igongolo na Tagamenda. Hiyo ndiyo miradi ambayo Kamati ilitembelea kuhusiana na miradi ya umeme vijijini.

(iv) Mgodini wa Tanzanite One pia ulitembelewa na Kamati yako; na

(v) Mgodi wa Makaa ya mawe ya Kiwira.

Mheshimiwa Spika, mradi wa REA. Miradi ya REA inagharamiwa na fedha za Mfuko wa Nishati Vijijini ambao vyanzo vyake ni mapato pamoja na tozo ya sh. 100 katika kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli na sh. 150 katika kila lita moja ya mafuta ya taa. Kamati inasikitishwa na hali ya kusuasua kwa upelekaji wa fedha za miradi ya REA licha ya fedha hizo kuwekewa wigo wa kisheria (*ring-fenced*). Takwimu zinaonesha kwamba tangu tozo zilipoanza kukusanywa Julai, 2013 hadi kufikia Machi, 2016 shilingi bilioni 493.8 zimekusanywa kutoka kwenye tozo ya petroli na dizeli, shilingi bilioni 448.5 kutoka kwenye mafuta ya taa na shilingi bilioni 45.4 kutoka kwenye *custom processing fee*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, licha ya makusanyo hayo, kiasi cha fedha kilichopelekwa kwenye Mfuko wa Nishati ya Umeme Vijijini hadi Aprili, 2016 ni shilingi bilioni 366.95 sawa na asilimia 37.5 tu ya makusanyo yote kutoka kwenye tozo hizo. Aidha, Kamati hairidhishwi na mwenendo wa utolewaji wa fedha za bajeti zinazoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya REA.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kwamba katika miaka mitatu ya fedha iliyopita yaani mwaka wa 2013/2014 hadi mwaka wa 2015/2016 mwezi Aprili, upatikanaji wa fedha za REA ulikuwa ni kwa asilimia 60 peke yake. Ufafanuzi huu kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha hii umeelezwa kwenye kiambatisho kilichoambatanishwa pamoja na taarifa hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati inahoji juu ya wapi ziliko shilingi bilioni 73.5 ambazo ni tofauti ya tozo ya fedha zilizokusanywa kwa ajili ya Mradi wa Umeme Vijijini katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako hili Tukufu. Kutokujulikana fedha hizi ziliko, kunaleta hisia kwa Kamati kwamba fedha hizi zina matumizi mengine tofauti na yale yaliyokusudiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu liitake Serikali itoe ufafanuzi wa kina ni kwa nini fedha hizi ambazo ukusanyaji wake ni wa uhakika na zimewekewa wigo wa kisheria (*ring-fenced*) hazipelekwi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya REA? Vinginevyo Kamati haioni mantiki ya kuweka tozo hii ya mafuta maana ni kuendelea kuwaumiza wananchi wakati fedha hizi haziendi kwenye miradi iliyokusudiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kutotolewa kwa fedha za REA kikamilifu kumekuwa na athari mbalimbali katika usambazaji wa umeme vijijini ikiwa ni pamoja na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA kutokulipwa kwa wakati jambo linaloongeza gharama za miradi. Aidha, utaratibu umedhihirisha kuwa Wizara haitaweza kufikia malengo yaliyowekwa ya usimamizi na uendeshaji wa sekta

ya nishati kwa sababu fedha zinazotengwa hazipelekwi kwa kiwango kinachoridhisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni TANESCO kushindwa kusimamia kikamilifu wakandarasi wanaotekeleza miradi na hivyo kusababisha miradi inayotekelezwa kuwa chini ya kiwango. Kwa mfano, katika Mkoa wa Njombe wakandarasi walifunga mashine humba yaani *transformers* 60 zilizokuwa chini ya kiwango. Hadi Kamati inakwenda kukagua mradi huo na kufanya ziara kwenye mkoa huo jumla ya mashine 35 kati ya hizo 60 zilikuwa zimekwishaharibika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira. Iwapo Mgodi wa Makaa ya Mawe ya Kiwira utaanza uzalishaji utaongeza MW 400 kwenye *grid* yetu ya Taifa. Uzalishaji huu utaboresha upatikanaji wa umeme na kuchangia kufikiwa kwa azma yetu ya kuingia kwenye uchumi wa viwanda. Hata hivyo, Kamati inasikitishwa na haioni dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza mgodi huu kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Kiasi cha fedha ambacho kimekuwa kikitengwa kwa ajili ya mgodi huu ni kidogo sana na kisichozingatia mahitaji ya mgodi. Kwa mfano, kiasi cha fedha kinachohitajika kwa ajili ya kuendesha mgodi huu ni shilingi bilioni 145 lakini katika mwaka wa fedha 2015/2016 mgodi huo uliidhinishwa shilingi bilioni mbili tu. Aidha, katika mwaka 2016/2017, mgodi huu umetengewa kiasi kile kile cha shilingi bilioni mbili.

(ii) Kutokupelekwa kwa fedha zilizoidhinishwa. Kamati imebaini kwamba licha ya fedha zinazoidhinishwa kwenye bajeti kwa ajili ya mgodi huu kuwa kidogo bado hazipelekwi. Kati ya shilingi bilioni mbili zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hakuna fedha yoyote iliyokwishaapelekwa hadi mwisho wa mwezi Aprili, 2016.

(iii) Serikali kutokuwa na mkakati wa kupata matumizi mengine ya madini haya, kunalipunguzia Taifa pato kubwa ambalo lingeweza kupatikana kupitia makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya mazungumzo na viwanda vya simenti ili vitumie makaa ya mawe yanayozalishwa hapa nchini. Kwa mfano, kiwanda cha Dangote kinatumia makaa ya mawe kutoka Afrika Kusini. Kamati inashauri Serikali vilevile, kama haijawa na dhamira ya dhati ya kuanzisha au kuendeleza mgodi huu, ni vyema bajeti hii kidogo ikaelekezwa sehemu nyingine kuliko kupelekwa kwenye mradi huu wakati hauleti tija ya aina yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 Makambako/Songea. Mradi huu unatekelezwa na ufadhili wa pamoja baina ya Serikali ya Sweden na Tanzania, unahusisha ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 250 kutoka Makambako hadi Songea ambako inatarajiwa kuwa na uwezo wa kusafirisha (*carrying capacity*) ya MW 150 ya nishati ya umeme. Aidha, mradi huu muhimu kwa Mikoa ya Njombe na Ruvuma umeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kulipa wakandarasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati yako baada ya kufanya ziara ya ukaguzi imesaidia mradi huo kupelekewa fedha hizo zilizokuwa zimekwama kutoka Hazina. Hali hii inadhihirisha kwamba fedha ya miradi zilikuwepo lakini hakukuwa na dhamira ya dhati ya kuzipeleka kwa wakati fedha hizi. Utaratibu huu wa kuchelewesha fedha za miradi umekuwa ukiingizia Serikali hasara kwa kuwa imekuwa ikilazimika kulipa fidia kwa wakandarasi kutokana na kuchelewesha malipo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini, madini ya *Tanzanite*. *Tanzanite* ni madini yanayopatikana Tanzania peke yake. Hata hivyo, kama Taifa tumekuwa hatunufaiki na mapato yanayotokana na uchimbaji wake kutokana na Serikali kukosa mfumo madhubuti wa usimamizi. Vilevile, kukosekana kwa miundombinu ya ukataji wa *Tanzanite* hapa nchini kumesababisha wawekezaji pamoja na wachimbaji wadogo wadogo kutorosha madini hayo nje kwa kigezo cha kwenda kuyasafisha.

Mheshimiwa Spika, jambo hili siyo tu kwamba linatukosesha mapato stahiki, bali linatufedhehesha kama Taifa pekee linalozalisha madini haya duniani kwa kutufanya tushike nafasi ya nne nyuma ya nchi za India, Afrika Kusini na Kenya katika uuzaji wa *Tanzanite*. Kwa kuwa hakuna dhamira ya dhati ya Serikali ya kudhibiti utoroshaji wa *Tanzanite* ghafi, Kamati inashauri kuwa usimamizi wa mgodi huu uangaliwe upya ili kulinda rasilimali hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na jitihada finyu za kuutafutia ufumbuzi mgogoro wa muda mrefu kati ya wachimbaji wadogo na mwekezaji. Mgogoro huu unatokana na mwingiliano wa maeneo ya uchimbaji chini ya ardhi maarufu kama mitobozano. Pia Sheria ya Madini inachangia ukuaji wa mgogoro huu kwa kukosa vifungu vinavyoelezea uchimbaji wa *Tanzanite* ambao ni tofauti ikilinganishwa na uchimbaji wa madini mengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeunda Tume zaidi ya sita (6) kuanzia mwaka 2001 - 2008 kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa mgogoro baina ya wawekezaji na wachimbaji wadogo wadogo. Hata hivyo, maoni na ushauri wa Tume hizi haujafanyiwa kazi kwa muda mrefu na kufanya tatizo hili kuendelea kuwepo. Kwa kuwa juhudi za Serikali katika kushughulikia mgogoro huu

zimeonekana kushindwa, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu lifuatilie kwa kina mgogoro huu kwa maslahi ya Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, madini ya almasi. Pamoja na uchimbaji wa muda mrefu wa almasi hapa nchini, Taifa limekuwa linanufaika kwa kiwango kidogo na rasilimali hii. Mgodi pekee unaochimba madini hayo wa Mwadui umekuwa haulipi *corporate tax* (kodi ya mapato) kama inavyotakiwa kisheria kwa kisingizio cha kuzalisha kwa hasara. Kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Mapato Tanzania, mgodi huu umelipa kodi ya mapato (*corporate tax*) kwa miaka minne tu ambayo ni kuanzia mwaka 2008/2009 hadi 2013/2014. Kamati haiamini kwamba mgodi huu kama kweli umekuwa ukijiendesha kwa hasara kwa miaka yote hii. Kama ungekuwa ukifanya shughuli za uchimbaji huu kwa hasara basi mgodi huu ungekuwa umeshafunga shughuli zake kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, madini ya dhahabu. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa migodi mikubwa ya dhahabu nchini hailipi kodi ya mapato kwa kisingizio cha kupata hasara endelevu katika uzalishaji. Hata hivyo, Kamati haikubaliani na sababu hii kwani taarifa zinaonesha kwamba makampuni yanayomiliki migodi hii yamekuwa yakipata faida katika masoko ya hisa ambako makampuni haya yamesajiliwa. Aidha, taarifa ya TMAA ya mwaka 2015 inaonesha kwamba makampuni ya madini ya dhahabu hayakulipa jumla ya shilingi bilioni 10.27 kwa ajili ya ushuru wa huduma (*service levy*) na mrabaha (*royalty*) kwenye Halmashauri husika. Kamati inaitaka Serikali ifuatilie tozo hizo ili Halmashauri hizo ziweze kunufaika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na ulipaji mbovu wa kodi ya mapato kwa mgodi wa ACACIA zamani *Barrick Gold Mine* kwa kutolipa kodi ya zuio (*withholding tax*) pamoja na (*corporate tax*) kwa miaka minne hata baada ya kuamuriwa na Mahakama ya Usuluhishi kulipa kodi inayofikia shilingi bilioni 89. Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua madhubuti juu ya mwenendo huu ili kudhibiti ukosefu wa mapato kama ilivyotokea kwenye migodi ya *Resolute* na Tulawaka ambayo ilifunga shughuli zake za uchimbaji bila kulipa kodi stahiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua jitihada ambazo zimekuwa zikifanywa na Serikali katika kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo katika shughuli zao za uchimbaji kwa kuwatengea maeneo ya kuchimba, kuwapa ruzuku na kuwajengea uwezo kupitia mafunzo mbalimbali. Hata hivyo, jitihada hizi bado hazijakidhi mahitaji kwani kumekuwa na malalamiko ya wachimbaji wadogo wadogo kukosa maeneo ya kuchimba pamoja na mitaji.

Mheshimiwa Spika, pia wananchi wa maeneo yanayozunguka migodi waliochukuliwa maeneo yao wamekuwa wakilalamika juu ya ucheleweshaji wa

kulipwa fidia. Mfano mzuri ni wananchi wa maeneo ya Nyamongo na Nyamichele yanayozunguka mgodi wa *North Mara* ambao maeneo yao yamechukuliwa na mgodi zaidi ya miaka mitatu iliyopita lakini hawajalipwa fidia, jambo linalowafanya wananchi hawa kuishi maisha ya shida na kushindwa kuendeleza shughuli zao kama walivyo wananchi wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, miradi ya gesi. Sekta ya gesi asilia ina fursa kubwa kuchangia katika ukuaji wa nchi yetu. Hata hivyo, ugunduzi wa rasilimali hii umeendelea kubainika katika nchi mbalimbali zikiwemo nchi jirani. Masoko tunayotegemea kuuza gesi yetu ndiyo hayo hayo yanayotegemewa pia na nchi nyingine zinazogundua gesi. Katika mazingira ya aina hii, ni wazi kwamba tutegemee ushindani mkubwa wa biashara ya gesi kwa kuzingatia nguvu ya soko ambayo zinaonesha kwamba kuna uwezekano uzalishaji wa gesi ukawa mkubwa kuliko mahitaji (*global oversupply of gas against low demand*).

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, malengo ya Serikali ya kuanza kuuza gesi nje ya nchi ifikapo mwaka 2023 yanaweza yasifikwiwe kutokana na kasi ndogo ya Serikali katika kukamilisha ujenzi wa mtambo wa kusindika gesi wa *LNG plant* huko Lindi. Sambamba na hilo kuwe na mkakati madhubuti kuhusu matumizi ya ndani ya gesi asilia kwa lengo la kutumia kikamilifu soko la ndani kabla ya kutafuta soko la nje. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutumia soko la ndani kwa kuwezesha gesi hiyo kutumika katika mitambo ya Kinyerezi I ambayo ina uwezo wa kuzalisha MW 150.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi kwa mwaka 2015/2016. Kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Serikali iandae mpango mkakati utakaowezesha usimamizi na matumizi ya gesi asilia. Kamati inashangazwa na Kiwanda cha Dangote kutotumia gesi inayozalishwa Mtwara;

(ii) Serikali iharakishe ukamilishaji wa ujenzi wa mtambo wa usindikaji gesi utakaowezesha gesi hiyo kusafirishwa kwa urahisi;

(iii) Kuwe na usimamizi mzuri na wa karibu kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hususani ile ya REA;

(iv) Serikali itenge fedha za kutosha na kuzipeleka kwa wakati kwenye miradi ya kimkakati kama vile Mgodi wa Makaa ya Mawe huko Kiwira;

(v) Serikali iwekeze katika miundombinu na utaalum wa madini ya vito ili kuwezesha ukataji na uuzaji wa *Tanzanite* kufanyika hapa nchini;

(vi) Madeni ya wakandarasi yalipwe kwa wakati ili kuepusha ongezeko la gharama linalotokana na Serikali kulipa fidia; na

(vii) Serikali itatafute namna bora ya kumaliza migogoro ya muda mrefu baina ya wawekezaji na wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa na utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka 2015/2016. Kamati ilifanya uchambuzi wa bajeti kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2015/2016, hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini wakati huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi huo. Wizara ilipanga kukusanya maduhuli jumla ya shilingi bilioni 291.98 sawa na asilimia 45.5 ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016. Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa hadi kufikia Machi, 2016, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 157.64 sawa na asilimia 54.99 ya lengo lililokusudiwa. Mwenendo huu ni ishara ya kutofanikiwa kwa lengo la makusanyo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Ni maoni ya Kamati kwamba, Wizara iweke makadirio ya makusanyo ambayo ni halisi badala ya kuweka makadirio makubwa yasiyotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa mchango wa Idara ya Madini kwa mwaka fedha 2016 umeshuka kwa asilimia 19.4 ikilinganishwa na mwaka 2015/2016 wakati mchango wa Idara ya Nishati umeongezeka kwa asilimia 25.5 ikilinganishwa na mwaka 2015/2016. Ufafanuzi zaidi umeambatanishwa pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilielezwa sababu zilizosababisha kushuka kwa makusanyo ya mapato kutoka kwenye madini kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kama ifuatavyo:-

(i) Kushuka kwa bei ya dhahabu katika Soko la Dunia;

(ii) Kupungua kwa uzalishaji wa migodi; na

(iii) Kupungua kwa shughuli za utafiti katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Nishati na Madini iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 642.12 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Taarifa ya Wizara inaonesha kuwa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 iliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 762.12 sawa na asilimia 18 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Ongezeko hilo limetokana na uhamisho wa fedha za ndani wa shilingi bilioni

120 ili kuongeza bajeti ya utekelezaji wa mradi wa Kinyerezi II wa MW 240 na ulipaji wa sehemu ya madeni ya ankara za umeme yanayodaiwa na TANESCO na Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa jitihada zake na nia yake ya dhati ya kuanza kutekeleza mradi huu muhimu ambao utaweza kuzalisha umeme wa MW 240. Ongezeko hili la MW 240 kwenye Gridi ya Taifa utapunguza tatizo la upatikanaji wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini na kuwaletea wananchi maendeleo yanayokusudiwa hasa maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2016, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 625.34 sawa na asilimia 82. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 579.54 zilikuwa ni fedha za maendeleo sawa na asilimia 93 ya fedha zilizopatikana hadi kufikia Machi, 2016. Katika fedha hizo, shilingi bilioni 546.18 sawa na asilimia 94.2 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 33.36 sawa na asilimia 5.8 ni fedha za nje. Ili kutoa picha halisi, jedwali limeambatanishwa pamoja na taarifa hii kwa ajili ya ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya upembuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha na unaonesha kuwa Wizara ilipata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo kwa kiasi kinachozidi bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2015/2016, kama inavyofafanuliwa kwenye jedwali hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko hilo, Kamati ilitaka kupata maelezo ya kina ili kulinganisha upatikanaji wa fedha pamoja na bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa ili kuwe na utekelezaji bora wa bajeti, Wizara inapaswa kuzingatia mahitaji halisi, vipaumbele na uwezekano wa upatikanaji wa fedha. Kwa kufanya hivyo, itakuwa si rahisi upatikanaji wa fedha kuzidi kiasi cha bajeti inayoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati. Wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo katika maeneo ya umeme, gesi asilia, biashara ya mafuta, utendaji wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa lakini yapo mambo kadhaa pia ambayo hayakuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo la kukaimisha watendaji na wasaidizi kwa muda mrefu bila kuwapatia mamlaka kamili ya kiutendaji. Tatizo hili lipo STAMICO na Chuo cha Madini. Hali hii inaendelea kukwamisha utekelezaji bora

wa mipango ya maendeleo. Aidha, jitihada za Serikali za kutafutia ufumbuzi suala hili siyo za kuridhisha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali kuhusu utekelezaji wa miradi ya umeme wa jua, umeme wa upepo, umeme wa joto ardhi na tungamotaka haioneshi nia ya dhati ya Serikali ya kutekeleza miradi hiyo muhimu hasa kwa kutengewa bajeti kidogo mwaka 2016/2017. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu mzuri wa fedha za REA uliowekwa kisheria kuhusu fedha zake kuwekewa wigo wa kisheria (*ring fenced*) bado upatikanaji wake hauridhishi kama nilivyoeleza. Miradi ya REA kwa mwaka 2015/2016 ilitengewa shilingi 357.1 na hadi sasa zimepelekwa shilingi bilioni 168 sawa na asilimia 47 ya bajeti yote iliyokuwa imetengwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulipa madeni ya TANESCO kupitia Hazina na kwa mwaka 2015/2016 zimelipwa jumla ya shilingi bilioni 184 sawa na asilimia 59.74 ikiwa ni madeni ya Serikali na taasisi zake. Utaratibu huu wa malipo unakwamisha utekelezaji shughuli mbalimbali za TANESCO. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza maoni na ushauri wa Kamati kwa kuingiza kwenye bajeti ya Wizara ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi (Fungu 58) kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara imejiwekea malengo makuu matano yafuatayo:-

(i) Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa sekta ya nishati kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

(ii) Kuboresha uendelezaji na usimamizi endelevu wa rasilimali za madini kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

(iii) Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wadau katika sekta za nishati na madini.

(iv) Kuboresha utoaji wa huduma kwa watumishi waathirika wa VVU na UKIMWI ili kupunguza maambukizi.

(v) Kuondoa vitendo vya rushwa katika sekta ya nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini imekuwa na malengo haya haya kwa muda mrefu toka mwaka wa fedha 2011/2012 hadi mwaka 2016/2017. Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu kujirudiarudia kwa malengo haya na kufanya rejeo katika Hati Idhini (*Government Instrument*) iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali Na.144 la tarehe 22 Aprili, 2016. Kamati ilibaini kuwa malengo hayo yanaendana na Mpango wa Taifa. Aidha, Kamati katika uchambuzi wake

imeridhia malengo hayo kutokana na umuhimu wake. Malengo haya yamezingatia majukumu yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara, Sura 299. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato. Makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017 yanakadiriwa kuwa jumla ya shilingi bilioni 370.68 ikilinganishwa na shilingi bilioni 286.66 kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Kati ya makusanyo hayo, shilingi bilioni 215.96 sawa na asilimia 58.3 zitakusanywa na Idara ya Madini na shilingi bilioni 154.378 sawa na asilimia 41.6 zitakusanywa na Idara ya Nishati na Sh.344,003,000 sawa na asilimia 0.1 zitakusanywa na idara na vitengo vilivyo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya makusanyo ya mapato yameongezeka kwa asilimia 29.3 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo ya mwaka 2015/2016. Aidha, ongezeko hili la makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017 linalotokana na sababu zifuatazo:-

- (i) Kuendelea kutumia gesi asilia;
- (ii) Kuendelea kuhamasisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi;
- (iii) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa wachimbaji wadogo wadogo;
- (iv) Wizara kutoa malengo ya ukusanyaji kwa kila Kamishna Msaidizi na Mkazi katika ofisi za mikoa;
- (v) Kuimarisha ushirikiano wa taasisi nyingine za Serikali katika kuzuia utoroshaji madini; na
- (vi) Kukusanya matumizi ya ndani ya gesi asilia ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa matumizi. Makadirio ya matumizi ya bajeti ya mwaka huu 2016/2017 ni jumla ya shilingi trilioni 1.122 kilinganishwa na Shilingi bilioni 642.123 zilizoidhinishwa na Bunge, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 74. Kamati ilielezwa kuwa ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa fedha za miradi. Aidha, bajeti ya fedha za ndani za REA imeongezeka pia.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 inakadiriwa kuwa jumla ya Sh. 1,056,354,669,000 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 502.303 kwa mwaka 2015/2016, ongezeko hilo ni sawa na asilimia 110.3. Ongezeko la bajeti ya maendeleo ni sawa na asilimia 94 ya bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Fungu 58 kwa mwaka 2016/2017, fedha za ndani za maendeleo zimeongezeka vilevile kutoka shilingi bilioni 280 hadi kufikia shilingi bilioni 724. Aidha, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imetengwa jumla ya Shilingi bilioni 66 sawa na asilimia sita tu ya bajeti yote ya Wizara na kati ya fedha hizo shilingi bilioni 38.654 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

Mheshimiwa Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida imepungua kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na bajeti ya mwaka uliopita na hili ni jambo jema kwa sababu fedha nyingi kwa mwaka huu wa fedha zitaelekea kwenye miradi ya maendeleo. Mwaka wa fedha 2016/2017, bajeti ya miradi ya maendeleo imeongeza kwa asilimia 110. Ongezeko hilo litasaidia kukamilisha miradi kipaumbele iliyokuwa imesimama.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati. Kamati katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ya ukaguzi na uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara inatoa ushauri na maoni yafuatayo:-

(i) Serikali iandae mpango mkakati utakaowezesha usimamizi mzuri wa gesi asilia nchini ikiwa ni pamoja na kutafuta masoko.

(ii) Serikali iharakishe ukamilishwaji wa mradi wa usindikaji gesi.

(iii) Kuwe na usimamizi mzuri na wa karibu kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maendeleo hususan ile ya REA.

(iv) Serikali itenge fedha za kutosha na kuzipeleka kwa wakati kwenye miradi ya kimkakati kama vile Mgodini wa Makaa ya Mawe.

(v) Serikali iwekeze katika miundombinu na utaalam wa madini na vito ili ukataji wa madini hayo na uuzaji wake ufanyike hapa nchini.

(vi) Madeni ya wakandarasi yalipwe kwa wakati.

(vii) Serikali itekeleze kwa dhati ushauri na mapendekezo ya Tume mbalimbali zilizoundwa kwa ajili ya kutatua mgogoro wa muda mrefu wa wachimbaji wadogo pamoja na wawekezaji huko Mererani.

(viii) Chuo cha madini kitengewe fedha za kutosha ili kuweza kuzalisha wataalam wa kutosha kwa ajili ya hii rasilimali muhimu. (Makofi)

(ix) Wakandarasi wanaotekeleza miradi mbalimbali walipwe kwa wakati ili kukwepa kulipa fidia zisizokuwa za lazima.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Naomba nichukue fursa hii nikupongeze wewe binafsi, Naibu Spika, wenyevidi wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu wenu huu muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru sana wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano walionipa wakati wote wa kujadili na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 58 mwaka 2016/2017. Naomba majina yao yaingizwe kwenye *Hansard* kama yalivyorodheshwa.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nichukue fursa hii nimshukuru sana Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein, Makatibu wa Kamati ndugu Mwanahamisi Mukunda na Felister Mgonja kwa kuratibu vizuri shughuli za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii. Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Bunge kwa ushirikiano wao walioweza Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa imani yao kubwa waliyonipatia kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao katika nyumba hii. Naomba niwahakikishie kwa moyo wa dhati, sitawaangusha katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio na mapato ya matumizi ya Fungu 58 kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambayo ni Shilingi trilioni moja bilioni mia moja ishirini na mbili, milioni mia nane arobaini na tano mia saba arobaini na moja elfu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Doto Biteko, tunakushukuru sana kwa hotuba nzuri yenye uchambuzi muhimu; itawasaidieni sana Waheshimiwa Wabunge mnaotaka kuchangia Wizara hii kwa sababu Kamati imetufanyia kazi kubwa sana.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA
MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA
WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016 /2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana kwa lengo la kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Katika kufanikisha jukumu hili, Kamati ili tekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa Fedha kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inaonesha matokeo ya shughuli hizo pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kwa kutembelea Mikoa ya Dar Es salaam, Mtwara, Manyara, Njombe na Mbeya kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya Wizara ya Nishati na

Madini iliyotengewa na kupelekewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu miradi hiyo kama ifuatavyo:-

- i) Kinyerezi I MW 150.
- ii) Bomba la Gesi Mtwara
- iii) Mgodini wa Tanzanite one,
- iv) Makambako/Songea Transimission Line wenye msongo wa kilovoti 220
- v) REA katika vijiji vya mkoa wa Njombe pamoja na
- vi) Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira.

2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

Mheshimiwa Spika, Miradi iliyokaguliwa na Kamati kwa ujumla wake inahusu mambo muhimu yafuatayo:-

- i) Uzalishaji wa Umeme wa Kinyerezi I MW 150;
- ii) Bomba la kusafirisha gesi kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam pamoja na mitambo ya kuchakata na kusafisha gesi ya Mnazi bay na Songo Songo;
- iii) Mradi wa Makambako/Songea wa kusambaza umeme katika mikoa ya Ruvuma na Njombe. Kamati ilikagua utekelezaji wa mradi katika vijiji vya Lyamkena, Itipingi, Igongolo na Tagamenda;
- iv) Mradi wa REA katika Mkoa wa Njombe. Kamati ilikagua utekelezaji wa mradi huo katika vijiji vya Itulahumba, Isindangosi, Iteni, Usuka, Mlevela pamoja na Nyumbanitu na Kichiwa;
- v) Mgodini wa Tanzanite One;
- vi) Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira;

2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

2.2.1 Miradi ya Sekta ya Nishati

2.2.1.1 Mradi wa REA

Mheshimiwa Spika, Miradi ya REA inagharamiwa na fedha za Mfuko wa Nishati Vijijini ambao vyanzo vyake vya Mapato ni pamoja na tozo ya shilingi 100 katika kila lita ya mafuta ya Petroli na Dizeli na shilingi 150 katika kila lita ya mafuta ya taa. Kamati inasikitishwa na hali ya kusua sua katika upelekaji wa fedha za miradi ya REA, licha ya fedha hizo kuwekewa wigo wa kisheria (Ring fenced).

Takwimu zinaonesha kwamba tangu Tozo hizi ilipoanza kukusanywa Julai 2013 hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya shilingi Bilioni 493.8 zimekusanywa kutoka kwenye tozo za Petroli na Dizeli, shilingi bilioni 448.5 kutoka kwenye Mafuta ya Taa na shilingi bilioni 45.4 kutoka kwenye Custom Processing Fee.

Mheshimiwa Spika, licha ya makusanyo hayo, kiasi cha fedha kilichopelekwa kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini hadi Aprili 2016 ni shilingi bilioni 366.95 s.awa na asilimia 37.15 ya makusanyo yote kutoka kwenye Tozo hizo.

Aidha, Kamati hairidhishwi na mwenendo wa utolewaji wa fedha za bajeti zinazoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya REA. Takwimu zinaonesha kwamba, katika miaka mitatu ya fedha iliyopita (2013/14 hadi Aprili 2015/16 wastani wa upatikanaji wa fedha za REA ulikuwa ni kwa asilimia 60. Ufafanuzi kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa kipindi cha miaka mitatu umeelezwa katika jendwali lifuatalo:-

Mwaka wa Fedha	Fedha iliyoidhinishwa	Fedha iliyotolewa	Asilimia ya Lengo
2013/2014	Bilioni 285.5	Bilioni 184.9	65
2014/2015	Bilioni 271.6	Bilioni 189.7	70
2015/2016	Bilioni 357.1	Bilioni 168.9 Hadi Aprili 2016	47.3

Mheshimiwa Spika, Kamati inahoji juu ya wapi zilipo shilingi bilioni 73.5 ambazo ni tofauti ya tozo zilizokusanywa na Mfuko wa Nishati Vijijini katika kipindi cha miaka mitatu ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya REA? Kutojulikana zilipo fedha hizo kuna leta hisia kwa Kamati kwamba fedha hizi zina matumizi mengine tofauti na yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inalishauri Bunge lako liitake Serikali itoe ufafanuzi wa kina ni kwanini fedha hizi ambazo ukusanyaji wake ni wa uhakika na zimewekewa wigo kisheria (Ring fenced) hazipelekwi kwenye utekelezaji wa

miradi REA? Vinginevyo Kamati haioni mantiki ya kuweka tozo kwenye mafuta nakuendelea kumuumiza wanachi ilihali fedha hizo hazitekelezi jambo lilokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kutotolewa kwa fedha za REA kikamilifu kumekuwa na athari mbalimbali katika usambazaji wa umeme vijijini, ikiwa ni pamoja na Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA kutolipwa kwa wakati jambo linaloongeza gharama za mradi. Aidha, utaratibu unaidhihirishia Kamati kuwa, Wizara haitaweza kufikia malengo ya kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Nishati kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni TANESCO kushindwa kushindwa kusimamia kikamilifu Wakandarasi wanao tekeleza miradi na hivyo kusababisha miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango. Kwa mfano katika mkoa wa Njombe Wakandarasi walifunga mashine Humba (**Transformers**) 60 zilizochini ya kiwango hadi wakati Kamati inafanya ziara mashine 35 kati ya hizo zilikuwa zimeisharibika.

2.2.1.2 Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira

Mheshimiwa Spika, iwapo Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira utanza uzalishaji, utaongeza umeme kwa MW400. uzalishaji huu utaboresha upatikanaji wa umeme na kuchangia kufikiwa kwa azma ya nchi yetu kuingia katika uchumi wa Viwanda. Hata hivyo, kamati inasikitishwa kuwa haioni dhamira ya dhati ya Serikali kuendeleza Mgodi huu kutokana na sababu zifuatazo:-

Moja, kiasi cha fedha ambacho kimekuwa kikitengwa kwa ajili ya mgodi huu ni kidogo sana na kisicho zingatia mahitaji ya Mgodi, Kwa mfano kiasi cha fedha kinachohitajika ili mgodi uweze kuanza uzalishaji wa MW 50 kwa awamu ya kwanza unahitaji jumla ya **shilingi bilioni 145** lakini katika mwaka wa fedha 2015/2016 mgodi uliidhinishwa shilingi Bilioni 2 tu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017 mgodi umetengewa kiasi kile kile.

Mbili, kutopelekwa kwa fedha zinazoidhinishwa. Kamati imebaini kwamba, licha ya fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya mgodi kuwa ni kidogo fedha hizo hazipeleki. Kati ya shilingi bilioni 2 zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 hakuna fedha yoyote iliyopelekwa hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2016.

Tatu, Serikali kutokuwa na mkakati wa kupata matumizi mengine ya madini haya, kunalipunguzia Taifa pato kubwa ambalo lingeweza kupatikana kupitia Makaa ya mawe. Kamati inaishauri Serikali kufanya mazungumzo na Viwanda vya simenti ili vitumie makaa ya Mawe yanayozalishwa hapa nchini. Mfano:- Kiwanda cha DANGOTE kinatumia Makaa ya Mawe kutoka Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuwa kama haijawa na dhamira ya dhati ya kuanzisha uzalishaji katika Mgodhi huu ni vema Bajeti kidogo inayotengwa ikaelekezwa katika Miradi mingine ya Nishati.

2.2.1.3 Mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 wa Makambako/Songea

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unaotekelezwa kwa ufadhili kwa pamoja baina ya Serikali ya Sweden na Tanzania, unahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 250 kutoka Makambako hadi Songea, ambayo inatarajiwa kuwa na uwezo wa kusafirisha (*carrying capacity*) MW 150 za nishati ya umeme. Aidha, mradi huu muhimu kwa mikoa ya Njombe na Ruvuma umeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana changamoto ya upatikanaji wa fedha za kulipa Wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hatua ya Kamati yako kufanya ziara ya ukaguzi imesaidia mradi huo kupelekwa fedha zilizokuwa zimekwamba kutoka Hazina. Hali hii inadhihirisha kwamba fedha ya mradi ilikuwepo lakini hakuwa na dhamira ya kuipeleka.

Utaratibu huu wa kuchelewesha fedha za miradi umekuwa ukiingizia Serikali hasara kwani imekuwa ikilazimika kulipa fidia kwa Wakandarasi kutokana na kuchelewesha malipo.

2.2.2 Miradi Sekta ya Madini

2.2.2.1 Madini ya Vito

2.2.2.1.1 Madini ya Tanzanite

Mheshimiwa Spika, Tanzanite ni madini yanayopatikana Tanzania peke yake, hata hivyo kama Taifa tumekuwa hatunufaiki na mapato yanayotokana na uchimbaji wake, kutokana na Serikali kukosa mfumo madhubuti wa usimamizi.

Vilevile, kukosekana kwa miundombinu ya kukata Tanzanite hapa nchini kumesababisha Wawekezaji pamoja na wachimbaji wadogo wadogo kutorosha madini nje ya nchi kwa kigezo cha kwenda kuyasafisha. **Jambo hili siyo tu kwamba lina ikosesha nchi mapato stahiki, bali linatufedhehesha kama Taifa pekee linalozalisha madini haya dunia kwa kutufanya tushike nafasi ya nne nyuma ya nchi za India, Afrika Kusini na Kenya katika uuzaji wa Tanzanite.**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hakuna dhamira ya dhati ya Serikali ya kudhibiti utoroshaji wa Tanzanite ghafi, kamati inashauri kuwa usimamizi wa Mgodhi huu uangaliwe upya ili kulinda rasilimali hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na jitihada finyu za kutafutia ufumbuzi wa mgogoro wa muda mrefu kati ya Wachimbaji wadogo na mwekezaji. Mgogoro huu unatokana na muingiliano wa maeneo ya uchimbaji chini ya ardhi (maarufu kama “mitobozano”). Pia Sheria ya madini inachangia ukuaji wa mgogoro huu kwa kukosa vifungu vinavyoelezea uchimbaji wa madini ya Tanzanite, ambao ni tofauti ikilinganishwa na uchimbaji wa madini mengine.

Serikali imeunda Tume zaidi ya 6 kati ya mwaka 2002 hadi 2008 kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa mgogoro baina ya Wawekezaji na Wachimbaji wadogo wadogo. Hata hivyo, Maoni na ushauri wa Tume hizi haujafanyiwa kazi jambo linalisababisha kuendelea kukua kwa mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa juhudi za Serikali katika kushughulikia mgogoro huu zimeonekana kushindwa, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu lifuatilie kwa kina mgogoro huu kwa maslahi ya Taifa letu.

2.2.2.1.2 Madini ya Almasi

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchimbaji wa muda mrefu wa Almasi hapa nchini, Taifa limekuwa halinufaiki na mapato yatokanayo na rasilimali hii. Mgodi pekee unaochimba madini hayo wa Mwadui umekuwa haulipi Corporate Tax kama inavyotakiwa kisheria kwa kisingizio cha kuzalisha kwa hasara.

Kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Mapato Tanzania, mgodi huu umelipa kodi ya mapato (corporate tax) kwa miaka minne tu ambayo ni kuanzia mwaka 2008/2009 hadi 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Kamati haiamini kwamba mgodi huu umekuwa ukijiendesha kwa hasara kwa miaka yote ambayo umekuwa ukifanya shughuli za uchimbaji wa madini hayo kama unavyodai. Iwapo madai hayo yangekuwa na ukweli wowote, ni wazi kwamba mgodi ungekuwa umeshafunga shughuli za uzalishaji.

2.2.2.2 Madini ya Dhahabu

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa migodi mikubwa ya dhahabu nchini hailipi kodi ya mapato (Corporate tax) kwa kisingizio cha kupata hasara endelevu katika uzalishaji. Hata hivyo kamati haikubaliani na sababu hiyo kwani taarifa zinaonesha kwamba makapuni yanayomiliki migodi hiyo yamekuwa yakipata faida kwenye masoko ya hisa ambako kampuni hizi zimesajiliwa.

Aidha, Ripoti ya TMAA ya mwaka 2015 inaonesha kwamba makapuni ya madini ya dhahabu hayakulipa jumla ya shilingi bilioni 10.27 kwaajili ya ushuru wa Huduma (Service Levy), na Mrabaha (Royalty) kwenye Halmashauri husika. Kamati inaitaka Serikali ifuatilie malipo ya tozo hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na ulipaji mbovu wa kodi kwa mgodi wa **ACACIA** (zamani Baarick gold na African Barrick Gold) kwa kutolipa kodi ya zuio (Withholding Tax) na kodi ya mapato (Corporate Tax) kwa miaka minne hata baada ya kuamriwa na mahakama ya usuluhishi kulipa kodi hiyo inayofikia jumla ya shilingi bilioni 89.

Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua madhubutu juu ya mwenendo huo. Ili iweze kudhibiti ukosefu wa mapato kama ilivyotokea kwenye migodi ya **Resoulte** na **Tulawaka** ambayo ilifunga shughuli za uchimbaji bila kulipa kodi stahiki.

Mheshimiwa Spika, kamati inatambua jitihada ambazo zimekuwa zikifanywa na Serikali katika kuwawezesha Wachimbaji wadogo wadogo katika shughuli zao za uchimbaji kwa kuwatengea maeneo ya uchimbaji, kuwapa ruzuku na kuwajengea uwezo kupita mafunzo mabalimbali. Hata hivyo, jitihada hizi bado hazijakidhi mahitaji kwani kumekuwa na malalamiko ya Wachimbaji wadogo wadogo kukosa maeneo ya uchimbaji pamoja na mitaji.

Pia Wananchi wa maeneo yanayozunguka migodi waliochukuliwa maeneo yao wamekuwa wakilalamika juu ya kucheleweshewa au kutolipwa fidia zao. Mfano mzuri ni wananchi wa maeneo ya **Nyamongo** na **Nyamichele** yanayozunguka mgodi wa North Mara ambao maeneo yamechukuliwa na Mgodi zaidi ya miaka mitatu iliyopita lakini hawajalipwa faidi hali hii inawafanya wananchi hawa kuishi maisha ya shida na kushindwa kuendeleze shughuli zao mbalimbali.

2.3 Miradi ya Gesi

Mheshimiwa Spika, Sekta ya gesi asilia ina fursa kubwa ya kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo ugunduzi wa rasilimali hiyo umeendelea kubainika katika nchi mbalimbali zikiwemo nchi jirani. Masoko tunayotegemea kuuza gesi yetu ndiyo ambayo yana tegemewa pia na nchi nyingine zenye gesi.

Katika mazingira ya aina hii ni wazi kwamba tutegemee ushindani mkubwa wa biashara ya gesi kwa kuzingatia nguvu ya soko ambayo zinaonesha kwamba kuna uwezekano uzalishaji wa gesi ukawa mkubwa kuliko mahitaji (global oversupply of gas against low demand).

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, malengo ya Serikali ya kuanza kuuza gesi nje ya nchi ifikapo mwaka 2023 yanaweza yasifikwiwe kutokana na kasi ndogo ya Serikali katika kukamilisha ujenzi wa mtambo wa kusindika gesi asilia (LNG plant). Sambamba na hilo kuwe na mkakati madhubuti kuhusu matumizi ya ndani ya gesi asilia kwa lengo la kutumia kikamilifu soko la ndani kabla ya kuatafuta soko la nje.

Hata hivyo, kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutumia soko la ndani kwa kuwezesha gesi hiyo kutumika katika mitambo ya **Kinyerezi I** ambayo inauwezo wa kuzalisha **MW 150**.

2.4 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

- i) Serikali iandae Mpango mkakati utakaowezesha usimamizi na matumizi wa Gesi asilia. Kamati inashangazwa na Kiwanda cha Dangote kutotumia Gesi inayozalishwa Mtwara.
- ii) Serikali iharakishe ukamilishwaji wa Mradi wa usindikaji gesi (Liquefied Natural Gas) utakaowezesha gesi hiyo kusafirishwa kwa urahisi.
- iii) Kuwe na usimamizi mzuri na wa karibu kwa Wakandarasi wanao tekeleza miradi ya maendeleo hususan Miradi ya REA.
- iv) Serikali itenge fedha za kutosha na kuzipeleka kwa wakati kwenye miradi ya kimkakati kama vile Mgoji wa makaa ya Mawe wa Kiwira.
- v) Serikali iwekeze katika miundombinu na utaalumu wa madini ya vito ili kuwezesha ukataji na uuzaji wa Tanzanite kufanyika hapa nchini.
- vi) Madeni ya Wakandarasi yalipwe kwa wakati ili kuepusha ongezeko la gharama linalotokana na Serikali kulipa fidia.
- vii) Serikali itatafute namna bora ya kumaliza migogoro ya mrefu ya baina ya Wawekezaji na Wachimbaji wado wadogo.

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJAI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni **Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa**

fedha 2015/2016, Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini wakati huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

3.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli jumla ya Shilingi bilioni **291.98 sawa na asilimia 45.5** ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa, hadi kufikia Machi, 2016, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **shilingi bilioni 157.64** sawa na **asilimia 54.99** ya lengo.

Mwenendo huu ni ishara ya kutofanikiwa kwa lengo la makusanyo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Ni Maoni ya Kamati kwamba, Wizara iweke makadirio ya makusanyo ambayo ni halisi badala ya kuwa na makadirio makubwa yasiyotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa mchango wa idara ya Madini kwa mwaka fedha 2016/2017 umeshuka kwa asilimia 19.4 ikilinganishwa na Mwaka 2015/16 wakati mchango wa idara ya Nishati umeongezeka kwa asilimia 25.5 ikilinganishwa na Mwaka 2015/16.

Ufafanuzi zaidi umeoneshwa kupitia Jedwali Na. 01 la Taarifa hii.

2015/2016			2016/2017	
VYANZO VYA MAPATO	KIASI	ASILIMIA	KIASI	ASILIMIA
IDARA YA MADINI	211,962,385,000	72.6	215,962,385,000	58.3
IDARA YA NISHATI	79,697,501,000	27.3	154,377,501,000	41.6
IDARA NA VITENGO VINGINE	324,000,000	0.1	344,003,000	0.1
JUMLA KUU	291,983,889,000	100	370,683,889,000	100

Aidha Kamati ilielezwa sababu zilizosababisha kushuka kwa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kama ifuatavyo:-

- Kushuka kwa bei ya dhahabu katika Soko la Dunia

- ii) Kupungua kwa uzalishaji katika Migodi; na
- iii) Kupungua kwa shughuli za utafiti katika Sekta za Nishati na Madini;

3.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Nishati na Madini iliidhinishiwa jumla ya shilingi 642.12 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Taarifa ya Wizara inaonesha kuwa, Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 imeongezeka hadi kufikia 762.12 sawa na **asilimia 18** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Ongezeko hili limetokana na uhamisho wa fedha za ndani wa **shilingi bilioni 120** ili kuongeza bajeti ya utekelezaji wa Mradi wa Kinyerezi II MW 240 na ulipaji wa sehemu ya madeni ya Ankara za umeme yanayodaiwa na TANESCO na Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kwa nia yake ya dhati ya kuanza kutekeleza Mradi huu Muhimu ambao utaweza kuzalisha umeme wa MW 240, ongezeko hili la MW 240 katika Grid ya Taifa itasaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa umeme katika maeneo mbali mbali ya nchi hii na kuwaletea wananchi maendeleo yanayokusudiwa hasa maendeleo ya Viwanda.

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi bilioni 625.34** sawa na **asilimia themanini na mbili 82**. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 579.54** zilikuwa ni fedha za Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia tisini na tatu 93** ya fedha zilizopatikana hadi kufikia Machi, 2016. Katika fedha hizo **shilingi bilioni 546.18** sawa na **asilimia tisini na nne nukta mbili 94.2** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 33.36** sawa na **asilimia tano nukta nane 5.8** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ili kutoa picha halisi ya uwiano kati ya Bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizopatikana.

Jedwali Na. 2 la tarifa hii linafafanua

BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2015/2016			FEDHA ILIYOPATIKANA HADI MACHI, 2016	
UFAFANUZI	KIASI	ASILIMIA	KIASI	ASILIMIA
JUMLA KUU	642.12	100	625.34	97.4
FEDHA ZA MAENDELEO	502.3	78.2	579.54	115.4
MATUMIZI YA KAWAIDA	139.82	21.7	45.8	33

CHANZO: Taarifa ya Wizara ya Nishati na Madini fungu 58 kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya upembuzi yakinifu wa hali ya upatikanaji wa fedha unaonesha kuwa Wizara ilipata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo kwa kiasi kinachozidi Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2015/2016, kama inavyofafanuliwa katika Jedwali namba mbili la tarifa hii.

Mheshiwa Spika, Kutokana na ongezeko hilo, Kamati ilitaka kupata maelezo ya kina ili kulinganisha upatikanaji wa fedha na bajeti iliyoidhinishwa. ***Aidha, ni maoni ya kamati kuwa ili kuwe na utekelezaji bora wa Bajeti, Wizara inapaswa kuzingatia mahitaji halisi, vipaumbele na uwezekano wa upatikanaji wa fedha kwa kufanya hivyo, itakuwa si rahisi upatikanaji wa fedha kuzidi kiasi cha Bajeti inayoidhinishwa na Bunge.***

3.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo katika maeneo ya Umeme, Gesi asilia, Biashara ya Mafuta, Utendaji wa Wizara na Taasisi chini ya Wizara. Napenda kuliifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya Ushauri uliotolewa na Kamati haukuzingatiwa na kufanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo la kukaimisha Watendaji Wasaidizi kwa muda mrefu bila kuwapatia mamlaka kamili ya kiutendaji. Tatizo hili lipo STAMICO na Chuo cha Madini. Hali hii inaendelea kukwamisha utekelezaji bora wa Mipango ya Maendeleo. Aidha, jitihada za Serikali za kutafutia ufumbuzi suala hili siyo za kuridhisha sana.

Mheshimiwa Spika, Hatua zilizochukuliwa na Serikali kuhusu utekelezaji wa miradi ya umeme wa jua (Solar Energy), umeme wa upepo (Wind Energy), umeme wa joto ardhi (Geothermal) na Tungamotaka (Renewable Energy) haioneshi nia ya dhati ya Serikali ya kutekeleza miradi hiyo muhimu hasa kwa kutengewa bajeti kidogo mwaka 2016/17.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na kasi ya EWURA katika kuwaelimisha na kuwasimamia wajenzi na wamiliki wa vituo vya mafuta hasa katika maeneo ya Vijijini, Kanuni zilizo andaliwa kuhusu Usimamizi wa Ujenzi na Uendeshaji wa Vituo maeneo ya vijijini **(The Petroleum (Rural Retail Outlets Operation) Rules, 2015,** Kanuni hizi hazifahamiki kwa watumiaji hivyo kuleta usumbufu wakati wa ukaguzi wa vituo kwa kutoza faini ya Shilingi milioni tano hata kama wana vibali vya ujenzi toka Halmashauri na NEMC.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na utaratibu mzuri wa fedha za REA uliwekwa kisheria kuhusu fedha zake kulindwa (Ring Fenced) bado upatikanaji wake hauridhishi, Miradi ya REA kwa mwaka uliopita 2015/2016 ulitengewa **Shilingi 357.1** na hadi sasa zimepelekwa **Shilingi bilioni 168** sawa na asilimia arobaini na saba (47%) ya bajeti yote iliyokuwa imetengwa katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulipa madeni ya TANESCO kupitia Hazina na kwa mwaka 2015/2016 zimelipwa jumla ya **Shilingi bilioni 184 ambayo ni sawa na asilimia 59.74** ikiwa ni madeni ya Serikali na Taasisi zake, utaratibu huu wa malipo unakwamisha utekelezaji shughuli mbali mbali za TANESCO.

Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza maoni na ushauri wa Kamati kwa kuingiza kwenye Bajeti ya Wizara ya mwaka 2016/17, hivyo utekelezaji unaendelea.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA (FUNGU 58) MWAKA WA FEDHA 2016/2017

4.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 wizara imejiwekea Malengo Makuu Matano (5) yafuatayo:-

- i) Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Nishati kwa maendeleo endelevu ya Taifa.
- ii) Kuboresha uendelezaji na usimamizi endelevu wa rasilimali za madini kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi
- iii) Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wadau katika Sekta za Nishati na Madini.
- iv) Kuboresha utoaji wa huduma kwa watumishi waathirika wa VVU na UKIMWI ili kupunguza maambukizi
- v) Kuondoa vitendo vya Rushwa katika sekta ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Wizara ya Nishati na Madini imekuwa na malengo haya ya muda mrefu kuanzia mwaka 2011/12 hadi mwaka 2016/17. Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu kujirudia kwa malengo hayo na kufanya rejea katika Hati Idhini (Government Instrument) iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 144 la tarehe 22 Aprili, 2016. Kamati ilibaini kuwa

malengo hayo yanaendana na Mpango wa Taifa, aidha Kamati katika uchambuzi wa bajeti imeridhia malengo hayo kutokana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, malengo haya yamezingatia majukumu yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara, sura 299, *The Ministers (Discharge of the Ministerial Functions) Act*.

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Makisio ya makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 yanakadiriwa kuwa jumla ya **Shilingi 370.68** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 286.66** kwa mwaka wa fedha 2015/16. Kati ya makusanyo hayo **Shilingi bilioni 215.96** sawa na **asilimia 58.3** zitakusanywa na idara ya Madini, **shilingi 154.378** sawa na **asilimia 41.6** zitakusanywa na idara ya Nishati na **shilingi 344,003,000** sawa na **asilimia 0.1** zitakusanywa na idara na vitengo vingine katika Wizara.

Makadirio ya makusanyo ya mapato yameongezeka kwa asilimia **29.3** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo ya mwaka 2015/16. Aidha ongezeko hili la Makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/17 linatokana na sababu zifuatazo:-

- i) Kuendelea kutumia Gesi Asilia badala ya mafuta mazito katika miradi mikubwa ya uzalishaji umeme;
- ii) Kuendelea kuhamasisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia ili kuongeza uzalishaji na mauzo;
- iii) Kuendeleza kuimarisha usimamizi wa wachimbaji wadogo kwa kutoa huduma za ugani na kuwapa mafunzo ili wafuate Sheria katika shughuli zao ikiwa ni pamoja na kulipa Maduhuli ya Serikali;
- iv) Wizara kutoa malengo ya ukusanyaji kwa kila Kamishna Msaidizi na Mkazi katika ofisi za Mikaoni;
- v) Kuimarisha ushirikiano na Taasisi nyingine za Serikali katika kuzuia utoroshaji na biashara isiyo rasmi ya madini ikiwa ni pamoja na kuanzisha masoko ya madini ya vito;
- vi) Kukuza matumizi ya ndani ya gesi asilia ili kuongeza mapato na kupunguza uharibufu wa mazingira unaotokana na matumizi ya kuni na mkaa.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2016/2017 ni jumla ya **Shilingi 1,122,845,741,000** ikilinganishwa na Shilingi 642,123,079,000 zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2015/2016, hii ni sawa na ongezeko la **asilimia sabini na nne nukta tisa 74.9**. Kamati ilielezwa kuwa ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa fedha za miradi ya Maendeleo.

Aidha, Bajeti ya fedha za ndani za REA imeongezeka kutoka Shilingi **357,117,000,000** mwaka 2015/16 hadi **Shilingi 534,400,000,000** kwa mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la **asilimia arobaini na tisa nukta sita 49.6** ya bajeti ya REA kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 inakadiriwa kuwa jumla ya **Shilingi 1,056,354,669,000** ikilinganishwa na **Shilingi 502,303,938,000** kwa mwaka 2015/16, ongezeko hilo ni sawa na **asilimia mia moja na kumi nukta tatu 110.3**. **Ongezeko hilo la Bajeti ya Maendeleo ni sawa na asilimia tisini na nne 94** ya Bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, fungu 58 kwa mwaka 2016/2017 fedha za ndani za maendeleo zimeongezeka kutoka **shilingi bilioni 280.00** hadi **shilingi bilioni 724.84**, fedha za nje zimeongezeka kutoka **shilingi bilioni 85.35** hadi **shilingi bilioni 331.51**.

Aidha, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2016/17 imetengwa jumla ya **Shilingi 66,481,072,000** sawa na **asilimia sita 6** ya bajeti yote ya Wizara kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 38,654,138,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **shilingi bilioni 27.83** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

Bajeti ya matumizi ya kawaida imepungua kwa kiasi kikubwa sana ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa Fedha 2015/16 ambapo ilikuwa shilingi 171,613,498,000 sawa na asilimia thelathini na mbili 32 ya Bajeti yote ya Wizara, bajeti hii ni pungufu kwa **asilimia 38.73** ya bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni sawa na **asilimia 10.04** ya Bajeti Kuu ya Maendeleo ya Taifa. Bajeti ya Matumizi mengineyo ni sawa na **asilimia 0.49** ya Bajeti ya Matumizi ya kawaida ya Taifa, bajeti hii ni pungufu ya bajeti ya mwaka 2015/2016 kwa **asilimia 1.28**.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2016/17 bajeti ya Miradi ya maendeleo imeongeza kwa **asilimaia 110.3** toka kwenye Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Ongezeko hilo litasaidia kukamilisha miradi kipumbele ya Taifa hasa kwa upande wa Nishati na miradi ya kinkakati kwa Wizara itatekelezwa kwa ufanisi.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ya ukaguzi wa miradi, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2015/16 na uchambuzi wa makadirio na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2016/17 ufuatao ni ushauri na maoni ya Kamati:-

- i) Serikali iandae Mpango mkakati utakaowezesha usimamizi mzuri wa Gesi asilia inayozalishwa nchini ikiwa ni pamoja na kutafuta masoko.
- ii) Serikali iharakishe ukamilishwaji wa Mradi wa usindikaji gesi (Liquefied Natural Gas) utakaowezesha gesi hiyo kusafirishwa kwa urahisi
- iii) Kuwe na usimamizi mzuri na wa karibu kwa Wakandarasi wanao tekeleza miradi ya maendeleo hususan Miradi ya REA.
- iv) Serikali itenge fedha za kutosha na kuzipeleka kwa wakati kwenye miradi ya kinkakati kama vile Mgodi wa makaa ya Mawe wa Kiwira.
- v) Serikali iwekeze katika miundombinu na utaalamu wa madini ya vito ili kuwezesha ukataji na uuzaji wa Tanzanite kufanyika hapa nchini.
- vi) Madeni ya Wakandarasi yalipwe kwa wakati ili kuepusha ongezeko la gharama linalotokana na Serikali kulipa fidia.
- vii) Serikali itekeleze kwa dhati ushauri na mapendekezo ya Tume mbalimbali zilizoundwa ili kutua mgogoro wa muda mrefu wa Wachimbaji wadogo wadogo wa Tanzanite.
- viii) Chuo cha Madini kitengewe fedha za kutosha ili kuweza kuzalisha wataalamu watakaoundeleza rasilimali muhimu za Taifa hili.
- ix) Wakandarasi wanaotekeleza miradi mbali mbali walipwe kwa wakati ili kukwepa kulipa fidia zisizo za lazima.
- x) Fedha za REA zinazokusanywa kutoka kwenye tozo ziwasilishwe moja kwa moja kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini .

- xi) Serikali isimamie kwa makini ukamilishwaji wa miradi ya vipaumbele ya kuzalisha umeme ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika na kwa bei nafuu.
- xii) Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua madhubuti na zakupimika katika kusimamia madini haya adimu ya Tazanite ili kuiondoa nchi katika aibu ya utorohaji wa Madini.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi.

Kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu 58 kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Naomba majina yao yaingizwe kwenye Hansard kama yalivyo:-

- | | |
|--|---------------------|
| 1. Mhe. Doto Mashaka Biteko, Mb - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Deogratius Ngalawa, Mb - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb - | “ |
| 5. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb- | “ |
| 6. Mhe. Zainabu Mussa Bakar, Mb - | “ |
| 7. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb - | “ |
| 8. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb - | “ |
| 9. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb - | “ |
| 10. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb - | “ |
| 11. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb - | “ |
| 12. Mhe. Stella Ikupa Alex, Mb - | “ |
| 13. Mhe. Joyce Bitta Sokombi, Mb - | “ |
| 14. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb - | “ |
| 15. Mhe. Maulel Said Abdallah Mtulia, Mb | “ |
| 16. Mhe. Desderius John Mipata, Mb | “ |
| 17. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb - | “ |
| 18. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb - | “ |
| 19. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb- | “ |
| 20. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb- | “ |
| 21. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb - | “ |
| 22. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb- | “ |
| 23. Mhe. Ezekiel Magolyo Maige, Mb - | “ |
| 24. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb - | “ |
| 25. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb- | “ |

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashiilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Makatibu wa Kamati Ndg. Mwanahamisi Munkunda na Ndg. Felister Mgonja, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 58** kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 ambayo ni Shilingi **1,122,845,741,000**.

Mheshimiwa Spika, Naunga mkono hoja na Naomba kuwasilisha.

Dotto Mashaka Biteko, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI
20 May, 2016

SPIKA: Sasa naomba moja kwa moja nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Wizara ya Nishati na Madini. Kwa muda mrefu nilikuwa sijamwona John John, karibu sana Mheshimiwa Mnyika. (Makofi)

MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hotuba ni ndefu na hapa nitasoma muhtasari naomba hotuba yote kama ilivyowasilishwa mezani iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kuwasilisha kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9), Toleo la mwaka 2016, Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Juu ya Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2015/2016 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wote mliokuwa pamoja na familia yetu kwa hali na mali katika kipindi kigumu cha msiba wa baba yetu John Michael Dalali. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru wananchi wa Kibamba kwa kunichagua kuwa Mbunge, lakini pia kwa kuchagua Madiwani wa Kata zote kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kwa kutoa kura nyingi zaidi kwa mgombea wa urais wa UKAWA. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Richmond na Kuhusu Account ya Escrow ya Tegeta Pamoja na Umiliki wa Kampuni ya IPTL. Kama nilivyodokeza awali naomba maelezo yote kuhusu *Richmond* yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kurejea maamuzi na maazimio ambayo Bunge hili Tukufu lilikwisha yafanya kuhusiana na mikataba ambayo Serikali inaingia na makampuni mbalimbali hasa kwenye sekta ya nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, aidha Katika maazimio ya Bunge kuhusiana na fedha ufisadi uliofanyika katika akaunti ya *Tegeta Escrow* na umiliki wa *IPTL*, maazimio yanayohusu Sekta ya Nishati na Madini bado hayajatekelezwa kwa ukamilifu wake. Maazimio hayo yaliyotolewa na Bunge la Kumi, Mkutano wa Kumi na Saba katika kikao cha Ishirini kilichofanyika tarehe 29 Novemba, 2014 katika maazimio namba mbili (2), saba (7) na nane (8).

Mheshimiwa Spika, Bunge katika azimio namba mbili (2) liliazimia kwamba, naomba kunukuu; kwa kuwa, Taarifa Maalum ya Kamati imeonesha jinsi ambavyo *TANESCO* imekuwa ikitumia mabilioni ya fedha kulipa gharama za umeme unaozalishwa na *IPTL* na hivyo kuathiri hali ya kifedha ya Shirika hilo; na kwa kuwa, Taarifa Maalum ya Kamati inaonesha kwamba *TANESCO* itaendelea kulipa fedha nyingi kwa ajili ya gharama za umeme huo wa *IPTL* hivyo basi Bunge linaazimia kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kununua mitambo ya kufua umeme ya *IPTL* na kuimilikisha kwa *TANESCO* kwa lengo la kuokoa fedha za Shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kuona kwamba, mbali ya Serikali kushindwa kununua lakini bado inaendelea kulipia gharama za *capacity charges* na hivyo kuendelea kukiukwa kwa azimio ya Bunge. Hivyo basi, tunamtaka Waziri alieleze Bunge ni kwa kiasi gani azimio hili halijatekelezwa na ni kwa nini Serikali hii ya hapa kazi tu inaendelea kulipa malipo ya kifisadi kwa kampuni ya *IPTL*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika azimio namba saba (7) lililohusu kuwajibishwa kwa Mawaziri na watendaji wakuu wa Wizara na Bodi ya *TANESCO* lilisema kwamba, nanukuu:-

Kwa kuwa, vitendo vya kijinai wanavyohusishwa navyo viongozi wa umma na maafisa wa ngazi za juu Serikalini vinakiuka pia maadili ya viongozi wa umma na kuwanyima viongozi na maafisa hao uhalali wa kuendelea kushikilia nafasi za mamlaka katika uongozi wa umma; hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Ardhi, Nyumba na

Maendeleo ya Makazi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa TANESCO wawajibishwe, kwa kuishauri mamlaka yao ya uteuzi kutengua uteuzi huo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, bila ya kujali nini Bunge lilikwishaaazimia katika kikao ambacho na yeye alikuwa sehemu ya azimio hilo, lakini bado akamteua Mheshimiwa Profesa Muhongo kuendelea kuiongoza Wizara hii. Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona jambo hili kama ni dharau sana kwa Bunge na ni fedheha binafsi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, narudia. Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, bila ya kujali nini Bunge lilikwishaaazimia katika kikao ambacho na yeye alikuwa sehemu ya azimio hilo, bado akamteua Mheshimiwa Profesa Muhongo kuendelea kuiongoza Wizara hii. Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona jambo hili kama ni dharau sana kwa Bunge na ni fedheha binafsi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Uagizaji wa Mafuta Bila Ushindani. Aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini wa Serikali ya Awamu ya Nne katika mabadiliko ya mwisho, George Simbachawene aliagiza mafuta kwa ajili ya miezi ya Septemba, Oktoba na Novemba 2015 bila ya ushindani.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Waziri huyo ambaye sasa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), ulisababisha mafuta hayo kununuliwa kwa zaidi ya Shilingi bilioni 40, ambayo ni mara mbili ya bei ambayo ingetumika kama zabuni zingeshindanishwa. Aidha, uamuzi huu ulisababisha wananchi kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kutokana na pamoja na mambo mengine kuongezeka kwa gharama za uagizaji.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri akifanya uamuzi huo, tayari EWURA ilikuwa katika mchakato wa *tender* za kuagiza mafuta hayo na *tender* hizo namba 37, 38 na 39 za Septemba, Oktoba na Novemba, tayari zilikuwa zimeshapokelewa kwa ajili ya kushindanishwa.

Mheshimiwa Spika, historia inaonesha kuwa Sekta ya mafuta ndiyo kimekuwa kichaka kikuu cha kuficha ufisadi mkubwa, kwani Waziri utetezi wake ni kuwa alifanya kwa nia njema. Hiyo nia njema ya Mheshimiwa Waziri ambayo haikuzingatia ushindani na kupuuza ushauri wa mamlaka husika inapimwa kivi? Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa, uamuzi wa Waziri kupuuza ushauri wa EWURA ambayo ni mamlaka ya udhibiti, unaonyesha ipo haja ya uchunguzi juu ya nini kilimsukuma kuchukua uamuzi huu. Hapa lipo jipu linalohitaji kutumbuliwa.

Mheshimiwa Spika, maelezo yote kuhusu ushauri katika sekta ya nishati yaingie kwenye kumbukumbu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao ni mwendelezo wa miaka mitano iliyopita unakusudia kuwa Tanzania iendeshwe na uchumi wa viwanda. Katika kufika huko umeme wa uhakika katika sekta ya uzalishaji viwandani ni muhimu sana. Hatuwezi kuanzisha na kuendesha viwanda kwa kuwa na umeme usiokuwa na uhakika, kufanya hivyo bidhaa zitakazozalishwa zitakuwa ni ghali sana kwa kulinganisha na uzalishaji wa bidhaa kama zetu toka nchi nyingine, jambo ambalo zitashindwa kushindana kwa bei sokoni.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Nishati, Mpango uliweka lengo la kuzalisha *megawatt* 2,780 za umeme kwa kipindi cha miaka mitano. Maana yake ni kwamba kila mwaka ilitakiwa kuzalisha *Megawatt* 556 ili kufikia lengo lililowekwa na Mpango.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano zimeweza kuongezeka *Megawatt* 496.24 tu katika uzalishaji wa umeme nchini. Hii maana yake ni kwamba, kila mwaka tuliongeza uzalishaji wastani wa *megawatt* 100 za umeme nchini. Kwa mwenendo huu wa konokono, ili kufikia lengo la kuzalisha *megawatt* 2,780 tunahitaji miaka 13 ili kuweza kufikia lengo la Mpango wa Miaka Mitano ya awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili ni kwanini haikutekeleza lengo la Mpango wa Maendeleo la kuzalisha *megawatt* 2,780 za umeme?

Mheshimiwa Spika, sekta ya uzalishaji wa umeme imekuwa ndiyo sekta yenye ukiritimba, jambo linalopelekea kuwa sekta yenye rushwa kubwa kubwa, jambo hilo linasababisha wawekezaji wengi wanaotaka kuzalisha umeme kushindwa kufanya hivyo. Mfano mzuri ni mvutano mkubwa uliokuwepo kati ya RUBADA na TANESCO kuhusu uzalishaji wa umeme wa maji kwenye mabonde ambayo yanamilikiwa na Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Moja katika ya rasilimali kuu za Bonde la Rufiji ni chanzo cha uzalishaji umeme wa maji. Kwa utafiti uliofanywa na RUBADA mwaka 1984 kwa kutumia Kampuni ya Norway ya *Norconsult* kwenye *Rufiji Basin Hydropower Master Plan* ilionesha kuwa bonde lina vyanzo vikuu vinane vya uzalishaji wa umeme na vyanzo hivyo ni; *Stigler's Gorge*, Mpanga, Ruhudji, Mnyera, Iringa, Lukose, Kihansi and Kilombero.

Mheshimiwa Spika, Bonde la Mto Rufiji lina uwezo wa kuzalisha umeme wa mpaka *Megawatt* 2,729 bila ya kuathiri shughuli nyingine za kiuchumi, lakini kwa

sasa Bonde la Mto Rufiji lina mabwawa matatu tu yanayotumika kwa ajili ya uzalishaji wa umeme ambayo ni Kidatu, Kihansi na Mtera ambayo yanazalisha umeme wa *Megawatt* za umeme 460 tu.

Mheshimiwa Spika, inasadikika kwamba Tanzania ina uwezo wa kuzalisha umeme wa maji wa *megawatt* 4,700 kwa kutumia mabonde yake ya mito sita, ambayo ni; Rufiji, Pangani, Kagera, Malagarasi, Ruvuma na Rumakali . Kwa Bonde la Mto Rufiji kuhusu uzalishaji wa umeme hapa nchini, mradi wa *Stigler's Gorge* pekee toka miaka ya 1980 upembuzi yakinifu ulikwishafanywa na kuonekana kuwa ndicho chanzo ambacho kingeweza kuzalisha umeme wa kutosha kwa mahitaji ya matumizi yote ya viwandani na majumbani kwa gharama nafuu. Chanzo hiki ndicho kilichokuwa chanzo cha uhakika kwa kuiweka Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa Kati.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuelezwa toka upembuzi huo ufanyike ni hatua gani imeshafanyika kuona vyanzo hivyo vinatumika kuzalisha umeme kwa matumizi ya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*). Shirika hili la mafuta ndilo lililo na jukumu la msingi la kuhakikisha kuwa rasilimali ya mafuta na gesi iliyo hapa nchini inajulikana ilipo na inajulikana kiasi cha hazina kilichopo na inavunwa na nani na Watanzania watanufaika vipi na rasilimali hizo. Katika kutekeleza hayo yote shirika kwa mwaka wa fedha 2015/2016 liliomba kiasi cha shilingi bilioni 12 kama fedha za maendeleo, lakini hadi Kamati za Bunge zinakutana hakuna hata shilingi iliyokuwa imetolewa na hazina kama fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha *TPDC* imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za maendeleo, zikiwa ni fedha za ndani, kati ya fedha hizo shilingi milioni 700 ni ujenzi mtandao wa kusambaza gesi asili kwa mikoa ya Mtwara na Lindi na shilingi milioni 800 ni mradi wa kuchakata gesi asili na kuwa kimiminika kwa ajili ya kuisafirisha nje na ndani ya nchi ikiwa imesindikwa na shilingi bilioni 9.2 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani imeeleza hapo awali kwamba kazi ya kusimamia kwa kuelewa rasilimali ya mafuta na gesi ilipo na ni kiasi gani kilichopo ni kazi inayohitaji rasilimali. Kitendo cha kukosa fedha kwa ajili ya kutekeleza jukumu hili ni dhahiri kwamba makampuni yanayojihusisha na biashara hiyo, ambayo kwayo ni lazima yawe na fedha za kutosha ni rahisi kuiweka *TPDC* mifukoni mwake na mwisho wa siku Watanzania wakakosa kunufaika na rasilimali hizo.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa fedha unaolikumba shirika hili ndiyo unaopelekea mapato ya gesi kutokusanywa kwa kadri mikataba na sheria zinavyosema. Kwa mujibu wa taarifa ya TPDC inaonesha kuwa...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI: Kwa mujibu wa taarifa ya TPDC, kumradhi, inaonesha kuwa...

SPIKA: Naomba tumvumilie msomaji amalizie, endelea tu msomaji. Nime-take note, endelea Mheshimiwa Mnyika, makatibu changamkeni.

MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa fedha unaolikumba shirika hili ndiyo unaopelekea mapato ya gesi kutokusanywa kwa kadri ya mikataba na sheria zinavyosema. Kwa mujibu wa taarifa ya TPDC inaonesha kuwa Songas inadaiwa jumla ya Sh. 50,275,344,006/= na Pan African Energy inadaiwa jumla ya sh. 60,665,839,011/-. Kampuni zote hizo zinadaiwa na TPDC jumla ya shilingi bilioni 110.94.

Mheshimiwa Spika, je, kwa mwendo huu gesi hii inaweza kuwa na manufaa kwa wananchi, kama madeni yanashindwa kudaiwa kwa kusimamia mikataba iliyopo? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge ni kwa vipi imeshindwa kukusanya madeni makubwa ya kiasi hiki ilhali kuna fedha za miradi ya maendeleo nchini zinakosekana.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini, Wachimbaji Wadogo Wadogo. Serikali inatoa ruzuku kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili kuwezesha kuimarisha mazingira ya kazi zao. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kuwa utoaji wa ruzuku hiyo hauna utaratibu unaoeleweka kwani walengwa hawanufaiki na fursa hiyo. Malalamiko haya yanatolewa na wachimbaji wadogo wanaotoka Kanda ya Ziwa (Shinyanga, Geita, Mwanza, Mara, Simiyu na Kagera) ambao ni takriban asilimia 80 ya wachimbaji wadogo nchi nzima. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza utaratibu unaotumika kupatiwa ruzuku hiyo ya Dola za Marekani 100,000 kwa kila mwaka. Bila ya kuwepo uratibu na utaratibu unaoeleweka fedha hizi zitatolewa kwa upendeleo na hivyo kutowanufaisha walengwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, huko huko Musoma Vijijini, Jimbo la Butiama kuna mgodi ambao upo katika Kijiji cha Nyamikoma, Kata ya Kyanyari kuna

Kampuni ya Madini ya *M/S HENAN AFRO ASI-GEO ENGINEERING (T) Co. LTD* ambayo sasa ni takribani miaka nane wanafanya utafiti na muda wa utafiti ulitakiwa umalizike mwaka huu mwezi wa Mei. Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya alitoa kibali bila ya utaratibu cha kuongeza muda wa utafiti kwa barua yake ya tarehe 27/4/2016 yenye Kumb. Na. AB. 128/270/01/A/66 kwenda kwa Afisa Tarafa wa Tarafa ya Makongoro. Utafiti huo umeharibu sana miundombinu ya barabara na mazingira. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo Bungeni juu ya hatua hii iliyochukuliwa na Mkuu wa Wilaya kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tarime ina mgodi wa North Mara ambao sasa uko chini ya kampuni ya *ACACIA*, ulioanza rasmi mwaka 1994 lakini ulikuta wananchi katika eneo hilo la Nyamongo wakiwa wanachimba madini eneo la Nyarugusu na Nyabirama. Baada ya wawekezaji kupewa leseni Dar es Salaam walitwaa eneo hilo bila kuwaachia wananchi wa Tarime hata eneo la mita tano kuchimba. Leo Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo ya uongo Bungeni kwamba wananchi wa Nyamuhongo wametengewa eneo, jambo ambalo si la kweli kwa taarifa zilizopo kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hivyo, baadaye utaeleza ni hatua zipi atachukuliwa Mheshimiwa Waziri iwapo anatoa taarifa za uongo kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni wananchi kuuawa kila mara kwa kisingizio cha kuingia mgodini. Tangu mwaka 1994 zaidi ya watu 400 wamekwishauawa na wengine wengi wamebaki na vilema vya maisha na bila suluhisho kupatikana. Mgodi wa Nyamongo tofauti na migodi mingine uko katikati ya makazi ya watu, hivyo wananchi walitakiwa kuhamishwa kwa kulipwa fidia ili kupisha shughuli za uchimbaji kama inavyosema Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Hata hivyo, hadi sasa wananchi wanaishi mita takriban mbili kutoka mgodini kinyume cha sheria inavyosema wawe umbali wa mita 200 kutoka eneo la mgodi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kuhusu Kamati ya Kupitia Matatizo yote yanayowakabili wananchi wa Nyamongo na Kampuni ya *ACCACIA* iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka taarifa hiyo iwasilishwe Bungeni ili kunusuru majanga yasiendelee kwani tayari mauaji yanaendelea, ambapo hivi karibuni kijana mmoja alipigwa risasi na askari na kuuawa.

Mheshimiwa Spika, Malalamiko ya Kampuni ya *Bismark Hotel and Mining Limited*; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina taarifa kuwa kumekuwana mgogoro wa muda mrefu kati ya Kampuni ya uchimbaji ya *Bismark Hotel (Mining) Limited* dhidi ya Kampuni za madini za *Pangea Minerals Limited, Barrick*

Exploration Africa Limited na Acacia Mining PLC (zamani *Barrick Gold PLC*) ambapo kampuni hizo za kigeni ziliingia kwenye makubaliano ya pamoja na kampuni ya Bismark ya kupangisha eneo la kuchimba madini la Mgusu huko Geita mwaka 1995; maelezo ya mgogoro mzima yamefafanuliwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli hapa Bungeni kutokana na sakata hilo kwa kuwa Serikali yenyewe kupitia Wizara ya Nishati na Madini imekuwa ikitoa mara kwa mara tafsiri tofauti za kifungu cha 15(2) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Aidha, Waziri atoe kauli mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu hatua gani zimechukuliwa dhidi ya *Engineer John M. Nayopa* ambaye ametuhumiwa kuhusika katika sakata hili wakati wote na taarifa zake kupelekwa TAKUKURU na kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu Taka Sumu Zinazotoka Katika Mgodi wa Geita na Tatizo la Mpaka Kakola yaingie kwenye kumbukumbu za Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA). Kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, wakala alitengewa jumla ya Sh. 420,492,701,200/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kwa mujibu wa taarifa ya utendaji ya Wakala ni kwamba hadi Desemba 2015 zilikuwa zimepokelewa jumla ya sh. 141,163,133,226/= tu ambazo ni sawa na asilimia 34. Hii ni aibu kwa Serikali inayojinasibu kuwa hapa kazi tu na ni kinyume cha utekelezaji wa Ilani ya CCM ambayo Serikali hii inajigamba. Kati ya fedha hizo hakukuwa na fedha zozote zitokanazo na tozo za mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) zinaonesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2015/2016 wakala uliingiza mafuta ya *Petrol* jumla ya tani 571,681, mafuta ya *Diesel* tani 1,052,129 na mafuta ya taa tani 12,238.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria ya fedha iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu ilitoa haki ya kwamba kila lita moja ya mafuta ya *petrol* na mafuta ya dizeli ikatwe sh. 100/= na sh. 150/= zikatwe kwa kila lita ya mafuta ya taa na zipelekwe kwa wakala wa umeme vijijini kwa ajili ya kuimarisha usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa mahesabu ya tani zilizoigizwa na wakala ni kwamba tozo za mafuta ya *petrol* na *diesel* kwa jumla ya tani 1,623,810 ni Sh. 162,381,000,000/= na kwa tani 12,238 za mafuta ya taa ni sawa na Sh. 1,885,700,000/= na hivyo kufanya jumla ya fedha za tozo zinazotokana na mafuta ni Sh. 164,216,700,000/=.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba, kwa mwelekeo huu, gharama za miradi ya umeme ambayo inatekelezwa na makandarasi mbalimbali ni dhahiri fedha hizo kama kweli zilitolewa ni uhakika kwamba madeni yanayodaiwa na wakala yasingekuwepo. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni kiasi gani hadi sasa cha fedha za tozo ya mafuta kati ya fedha tajwa hapo awali kimepelekwa REA na ni kwa nini Serikali inakiuka Sheria na inashindwa kupelekea fedha zinazokusudiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaiona hali hii, kuwa kwa vyovyote vile kama fedha hazipelekwi hata nyongeza ambayo Wizara inajisifia kuongezwa kwenye bajeti inakuwa kiini macho kwa kuwa fedha zinatengwa, lakini fedha hazipelekwi kwenye miradi ya maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uziduaji (*Extractive Industries*), maelezo yote kuhusu STAMICO yaingie kwenye kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa kawaida ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa sheria zinazopitishwa na Bunge hili zinatekelezwa kwa haraka na kwa umahiri. Kambi Rasmi ya upinzani ingependa kutaarifu Bunge lako Tukufu kuwa takribani mwaka mmoja baada ya kupitishwa kwa sheria ya Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2015 (*The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act, 2015*) haijaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na Wizara ya Nishati na Madini kuendeleleza urasimu, kung'ang'ania na kuhodhi madaraka iliyopewa Kamati tekelezi TEITI Multi Stake Holder Group kwa mujibu wa sheria hii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaomba itoe mifano kuonyesha jinsi gani kucheleweshwa kwa sheria hii inahatarisha ukuaji na usimamizi wa sekta.

Kifungu namba 4 cha sheria hii kinasema ifuatavyo:-

(1) *There shall be a Committee to be known as the Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Committee.*

(2) *The Committee shall be an independent Government entity which shall be an oversight body for promoting and enhancing transparency and accountability in the extractive industry.*

Mheshimiwa Spika, Mwezi Septemba 2015 Tanzania ilifungiwa na Bodi ya Kimataifa Inayosimamia Uwazi Katika Sekta ya Uziduaji (*Extractive Industry Transparency Initiative*) kwa barua iliyoandikwa na Mwenyekiti Mheshimiwa

Claire Short. Uamuzi huo ulichukuliwa baada ya Wizara ya Nishati na Madini kuchelewesha mchakato wa kupatikana kwa mkaguzi wa mahesabu kwa mahesabu ya 2012/2013. Hii iliitia aibu Tanzania mbele ya jumuiya ya kimataifa hasa kwa kuwa tumekuwa tukijitambulisha kuwa mfano wa uwazi na uwajibikaji na kutumbua majipu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tatizo la manunuzi litatuliwa tu kama Kamati Tekelezi (MSG) itapewa mamlaka kamili ya kusimamia manunuzi yake bila kuingiliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa Machi 2015, Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT) iliitaka *African Barrick Gold Mine* kwa sasa *Acacia* kulipa Serikali kodi ya Dola za Marekani 41.25 milioni zaidi ya Shilingi bilioni 89, baada ya kugundua udanganyifu katika ulipaji wa kodi kwa miaka minne mfululizo. Hata hivyo ripoti zilizochapishwa na Kamati Tekelezi (TEITI Multi Stakeholder Group) katika miaka yote hiyo hazikugundua upungufu huo. Hii inaonyesha udhaifu mkubwa katika uendeshaji na usimamizi wa ukaguzi wa mahesabu ya Sekta ya Madini na Mafuta. Ni maoni yetu kuwa hii ingeweza kuepukwa ikiwa kutakuwa na wafanyakazi wenye weledi pamoja na rasilimali za kutosha.

Mheshimiwa Spika, wakati taasisi nyingi za Serikali zinakosa rasilimali fedha, Kamati Tekelezi (TEITI MSG) ni chombo kinalalamikiwa na wafadhili kwa kurudisha kapuni fedha kwa kushindwa kuzitumia. Hii inatokana na kutokuwa na wataalam wa kutosha na uoga wa kufanya maamuzi ndani ya *Secretariat*. Pia inatokana na urasimu wa kuidhinisha matumizi ndani ya Wizara ya Nishati na Madini. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwa nini inakuwa king'ang'anizi na kushindwa kutekeleza ipasavyo matakwa ya Sheria iliyopitishwa na Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST). Majukumu ya msingi ya wakala huyo ni pamoja na kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kutunza takwimu na taarifa mbalimbali za jiosayansi, kutengeneza ramani mbalimbali za jiosanyansi zinazoainisha uwepo wa madini ya aina mbalimbali, kusambaza ramani, taarifa na takwimu kwa wadau ili ziweze kutumika kwa shughuli mbalimbali. Kutoa ushauri wa kitaalam kwa wachimbaji madini wakubwa na wadogo na pia kwa sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji ya Wakala kwa mwaka wa fedha unaomalizika wa 2015/2016 inaonesha kuwa katika fedha zilizotengwa za matumizi mengineyo, sh. 4,433,482,000/- lakini hadi mwezi Machi, 2016 ni jumla ya shilingi bilioni moja tu, sawa na asilimia 22.55, ndizo zilizokuwa zimetolewa. Aidha, wakala haukutengewa fedha yoyote kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa mwaka wa fedha unaotarajiwa kuanza mwezi wa Saba, wakala unaomba

kuidhinishiwa kiasi cha sh. 4,417,444,000/- lakini kama ilivyokuwa mwaka jana haikutengwa hata shilingi moja kwa ajili ya miradi ya maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kabisa kwamba Tanzania imebahatika kuwa na madini ya kila aina, hivyo basi ni jukumu la wakala huyu kufanya utafiti na kubaini kila eneo lina madini ya aina gani na kwa kiasi gani na matumizi ya madini hayo na ni njia gani inatakiwa kutumika katika uchimbaji wake. Kitendo cha Serikali kutokutoa fedha yoyote kwa ajili ya kupata vifaa vya kisasa vya kutafuta na kupimia sampuli za miamba au udongo kwa kulenga hali ya madini ya aina yanapopatikana ni kuifanya Sekta ya Madini kuendelea kuhodhiwa na wale wenye uwezo wa kifedha tu na hasa makampuni ya kigeni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, makampuni makubwa yamekuwa yanapata leseni ya kuchimba aina moja ya madini, lakini ukweli ni kuwa katika mchakato wa kuchimba madini hayo, yanakuwemo madini mengine yanayoambatana na madini yaliyooombewa leseni, hivyo nchi imekuwa inapoteza mapato na inakuwa ni faida kwa wenye leseni kwani wanachukua madini hayo bure kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba wakala huyu ili kazi yake iwe ya manufaa kwa Taifa na kwa jamii ni lazima apatiwe fedha za maendeleo ili rasilimali hizo ziweze kujulikana zilipo na kiasi kilichopo na pia thamani yake ijulikane na hivyo mfanyabiashara apate stahili yake na Serikali ipate stahili yake kwa niaba ya wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Wizara ya Nishati na Madini ina wajibu muhimu wa kusimamia maendeleo endelevu ya rasilimali za nishati na madini ili kuwezesha maendeleo ya nchi na kuboresha maisha ya wananchi. Hata hivyo, mpaka sasa haijawezesha upatikanaji wa nishati kwa bei nafuu wala haijahakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za nishati na madini. Hali hii inahitaji mabadiliko makubwa ya kimfumo na kufungua ukurasa mpya kama Taifa kuepusha laana ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, nyenzo mojawapo ya mabadiliko ya kimfumo ni Katiba ya wananchi na si Katiba inayopendekezwa. Katiba mpya itaweka misingi bora ya nchi na wananchi kunufaika na rasilimali badala ya sheria dhaifu, mikataba mibovu na mianya ya ufisadi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha! (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa John Mnyika kwa maoni hayo ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Nishati na Madini.

**HOTUBA YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WIZARA YA
NISHATI NA MADINI MHESHIMIWA JOHN JOHN MNYIKA (MB) KUHUSU
MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA MAPITIO YA
UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2015/2016 NA
MAKADIRIO YA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI
NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. UTANGULIZI

Awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kuwasilisha kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) toleo la mwaka 2016, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016 na makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini mwaka wa fedha 2016/2017.

Nitumie fursa hii pia kuwashukuru waheshimiwa wabunge na wote mliokuwa pamoja na familia yetu kwa hali na mali katika kipindi kigumu cha msiba wa baba yetu John Michael Dalali, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema.

Aidha niwashukuru wananchi wa Kibamba kwa kunichagua kuwa mbunge lakini pia kuchagua madiwani wa kata zote kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

**2. UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KUHUSU RICHMOND NA KUHUSU
AKAUNTI YA 'ESCROW' YA TEGETA PAMOJA NA UMILIKI WA KAMPUNI YA IPTL**

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kurejea maamuzi/maazimio ambayo Bunge hili Tukufu lilikwisha yafanya kuhusiana na mikataba ambayo Serikali inaingia na makampuni mbalimbali hasa kwenye sekta ya nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, Taarifa mbili za serikali kuhusu utekelezaji wa maazimio haya ziliwasilishwa Bungeni tarehe 28 Agosti, 2008 na tarehe 11 Februari, 2009. Taarifa moja ilikabidhiwa na kujadiliwa na Kamati, ambazo zililitaarifu Bunge kuwa utekelezaji wa Maazimio 10 kati ya 23 yaliyotolewa na Bunge, yalifanyiwa kazi hadi mwezi Februari, 2009 na Maazimio 13 bado yalikuwa hayajakamilika.

Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kwamba taarifa za utekelezaji wa maazimio yaliyobaki ziwasilishwe kwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo hata hivyo kuanzia mwaka 2011 mpaka mwaka huu wa 2016 kamati hiyo haikuwasilisha taarifa yoyote bungeni ya kueleza kukamilika kwa

utekelezaji wa maazimio husika hali ambayo inahitaji bunge kuingilia kati kuweza kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Nchi Ibara ya 63 (2) na (3).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Wizara ya Nishati na Madini na Serikali kwa ujumla kutoa majibu bungeni juu ya hatma ya maazimio 10 yaliyobaki: Azimio Namba 3,5,7,8,9,10,11,13,14 na 18 ili bunge liweze kuishauri na kuisimamia serikali kuhakikisha maazimio husika yanatekelezwa kwa ukamilifu na kwa haraka. Lakini hadi sasa tunaposoma hotuba hii maazimio hayo ya Bunge bado hayajatekelezwa na Bunge kupata mrejesho rasmi.

Mheshimiwa Spika, aidha Katika maazimio ya Bunge kuhusiana na fedha ufisadi uliofanyika katika akaunti ya **“Tegeta escrow”** na umiliki wa IPTL, maazimio yanayohusu sekta ya nishati na madini bado hayajatekelezwa kwa ukamilifu wake, maazimio hayo yaliyotolewa na Bunge la Kumi, Mkutano wa Kumi na Saba katika kikao cha Ishirini kilichofanyika tarehe 29 Novemba, 2014 katika azimio namba 2,7 na 8.

Mheshimiwa Spika, Bunge katika azimio namba 2 liliazimia kwamba naomba kunukuu;

KWA KUWA, Taarifa Maalum ya Kamati imeonesha jinsi ambavyo TANESCO imekuwa ikitumia mabilioni ya fedha kulipa gharama za umeme unaozalishwa na IPTL na hivyo kuathiri hali ya kifedha ya Shirika hilo;

NA KWA KUWA, Taarifa Maalum ya Kamati inaonesha kwamba TANESCO itaendelea kulipa fedha nyingi kwa ajili ya gharama za umeme huo wa IPTL;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kununua mitambo ya kufua umeme ya IPTL na kuimilikisha kwa TANESCO kwa lengo la kuokoa fedha za Shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kuona kwamba, mbali ya Serikali kushindwa kununua lakini bado inaendelea kulipia gharama za “capacity charges” na hivyo kuendelea kukiukwa kwa azimio ya Bunge. Hivyo basi tunamtaka Waziri alieleze Bunge ni kwa kiasi gani azimio hilo limetekezwa?

Mheshimiwa Spika, katika azimio namba 7 lililohusu kuwajibishwa kwa Mawaziri na watendaji wakuu wa wizara na Bodi ya Tanesco lilisema kwamba, nanukuu;

“KWA KUWA, vitendo vya kijinai wanavyohusishwa navyo viongozi wa umma na maafisa wa ngazi za juu serikalini vinakiuka pia maadili ya viongozi wa umma na kuwanyima viongozi na maafisa hao uhalali wa kuendelea kushikilia nafasi za mamlaka katika uongozi wa umma;

HIVYO BASI, BUNGE LINAAZIMIA KWAMBA, Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa TANESCO wawajibishwe, kwa kuishauri mamlaka yao ya uteuzi kutengua uteuzi wao;"

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais bila ya kujali nini Bunge lilikwisha azimia katika kikao ambacho na yeye alikuwa sehemu ya azimio hilo, lakini bado akamteua Mhe Prof. Muhongo kuendelea kuiongoza wizara hii. Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona jambo hili kama ni dharau sana kwa Bunge na ni fedheha binafsi kwake.

Mheshimiwa Spika, Bunge katika azimio namba 8 la taarifa ya ukaguzi maalum kuhusiana na miamala iliyofanyika katika akaunti ya 'escrow' ya tegeta pamoja na umiliki wa kampuni ya Iptl iliazimiwa kwamba

"HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali itekeleze Azimio husika la Bunge mapema iwezekanavyo na kwa vyovyote vile kabla ya kumalizika kwa Mkutano wa Bunge la Bajeti Serikali iwasilishe taarifa ya utekelezaji wa mapitio ya mikataba ya umeme"

Mheshimiwa Spika, Azimio hili linashabihiana na azimio namba 13 lililoazimiwa na Bunge wakati wa majadala wa taarifa ya kamati teule ya Richmond lililosema kwamba;

"..... Kamati Teule inatoa wito kwa Serikali kuondokana na utaratibu huu usio na tija kwa kuzihusisha Kamati za Kudumu za Bunge kwenye hatua za awali za maandalizi ya mikataba hiyo. Aidha, Kamati Teule inatoa wito kwa Kamati zote za Bunge zihakikishe kuwa zinapitia mikataba mikubwa na ya muda mrefu ya kibiashara chini ya sekta zao ili kuliondolea Taifa mizigo isiyo ya lazima. Pale ambapo upatikanaji wa mikataba hiyo unakwamishwa kwa urasimu usio wa lazima Kamati zitumie utaratibu uliotumiwa na Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara ya kuunda Kamati Teule yenye ufunguo wa mikataba iliyofichika".

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imelazimika kunukuu maazimio hayo kutokana na ukweli kwamba Serikali imeshindwa kabisa kutekeleza maazimio ya Bunge, na badala yake mikataba hiyo inaendelea kutekelezwa kama ilivyoingiwika, mfano mzuri ni TANESCO kuendelea kuilipa IPTL fedha za capacity charge mpaka sasa. Jambo hili linazidi kuliondolea shirika hilo la umeme uwezo wa kuwahudumia wateja wake kwani haliwezi kuwekeza zaidi katika miundombinu za kusambaza umeme kutokana na kutokuwa na fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine wa mikataba yenye mashaka ni ule wa Mchuchuma na Liganga ambao NDC iliingia ubia na kampuni ya kichina ya HONGDA SICHUAN LTD na kuunda kampuni ya Ubia ya Tanzania China Internatinal Mineral Resource Ltd- TCIMRL katika kampuni hiyo ya ubia HONGDA SICHUAN LTD inamiliki asilimia 80 na NDC inamiliki asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wabia wanakuja mikono mitupu bila hela, sasa mbia mkubwa anatafuta mtaji kwa kutumia rasilimali za Kampuni ya ubia kama dhamana. Hizi rasilimali za Kampuni ya ubia ni zile zinazotakiwa kuchakatwa na kuuzwa, katika mazingira yoyote yale tukakubali vipi kuwa ubia wa njia hii unainufaisha nchi?

Mheshimiwa Spika, kama tunaweza kutumia rasilimali zetu kama dhamana ni kwanini tuingie ubia na tusitoe ajira kwa wataalamu waliobobea katika fani hizo na sisi tukawa na umiliki wa asilimia 100?

Kambi Rasmi ya Upinzani inasema mikataba ya jinsi hii ndiyo itakayoliangamiza taifa letu, ni kwa nini wataalam wanaoingia mikataba ya namna hii wanatakiwa kuendelea kuwa maofisini?

Mheshimiwa Spika, licha ya ubabaishaji wa Kampuni hiyo ya Kichina bado ina uhakika kwamba mkopo wa kutumia rasilimali zetu ukipatikana ianze kuiuzia Tanesco umeme wa 600MW, hoja ya msingi je uhalali wa TANESCO kununua umeme wa Mchuchuma na Liganga utakuwa wapi?

3. UAGIZAJI WA MAFUTA BILA USHINDANI

Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini wa Serikali ya Awamu ya Nne katika mabadiliko ya mwisho George Simbachawene, aliagiza mafuta kwa ajili ya miezi ya Septemba, Oktoba na Novemba 2015 bila ya ushindani.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa waziri huyo ambaye sasa ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), ulisababisha mafuta hayo kununuliwa kwa Sh40 bilioni, ambayo ni mara mbili ya bei ambayo ingetumika kama zabuni zingeshindanishwa. Aidha, uamuzi huu ulisababisha wananchi kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kutokana na pamoja na mambo mengine kuongezeka kwa gharama za uagizaji.

Mheshimiwa Spika, wakati waziri akifanya uamuzi huo, tayari Ewura ilikuwa katika mchakato wa tenda za kuagiza mafuta hayo na tenda hizo namba 37, 38 na 39 za Septemba, Oktoba na Novemba, ambazo tayari zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya kushindanishwa.

Mheshimiwa Spika, historia inaonesha kuwa Sekta ya mafuta ndiyo kimekuwa kichaka kikuu cha kuficha ufisadi mkubwa, kwani waziri utetezi wake ni kuwa alifanya kwa nia njema. Hiyo nia njema ya Mhe Waziri ambayo haikuzingatia ushindani na kupuuza ushauri wa mamlaka husika inapimwa vipi? Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa; *“Uamuzi wa waziri kupuuza ushauri wa Ewura ambayo ni mamlaka ya udhibiti, unaonyesha ipo haja ya uchunguzi juu ya nini kilimsukuma kuchukua uamuzi huu,”* Hapa lipo jipu linalohitaji kutumbuliwa.

4. USHAURI WA JUMLA KATIKA SEKTA YA NISHATI

Mheshimiwa Spika, Unaposema Wizara ya nishati na madini kwa watanzania wengi jambo linalokuja vichwani mwao ni uzalishaji na uuzaji wa umeme wanaotumia katika shughuli zao za kila siku za uzalishaji na matumizi ya majumbani. Japokuwa wizara hii ina majukumu makubwa ya kuhakikisha rasilimali ya madini iliyopo hapa nchini, ile ambayo imeanza kuvunwa na ambayo hadi sasa haijaanza kuvunwa inatumika katika hali ambayo inatakiwa iwanufaishe watanzania wa sasa na wale ambao hawajazaliwa

Mheshimiwa Spika, Umeme kama kichocheo cha maendeleo ya kukua kwa uchumi na vile vile kuongezeka kwa kipato cha wananchi kwa kuweza kumiliki na kuzitumia vyema rasilimali zinazowazunguka, hivyo basi hata rasilimali zingine kama madini haziwezi kuwa na thamani kama hakutakuwa na umeme wa kuwezesha kuzitoa huko ziliko na kuzipatia thamani inayostahili.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano ambao ni muendelezo wa miaka mitano iliyopita unakusudia kuwa Tanzania iendeshwe na uchumi wa viwanda. Katika kufika huko umeme wa uhakika katika sekta ya uzalishaji viwandani ni muhimu sana. Hatuwezi kuanzisha na kuendesha viwanda kwa kuwa na umeme usiokuwa na uhakika, kufanya hivyo bidhaa zitakazozalishwa zitakuwa ni ghali sana kwa kulinganisha na uzalishaji bidhaa kama zetu toka nchi zingine jambo ambalo zitashindwa kushindana kwa bei sokoni.

Mheshimiwa Spika, Katika sekta ya Nishati, Mpango uliweka lengo la kuzalisha 2,780 MW za Umeme kwa kipindi cha miaka 5. Maana yake ni kwamba kila mwaka ilitakiwa kuzalisha 556 MW ili kufikia lengo lililowekwa na Mpango.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji- kwa kipindi cha miaka 5 zimeweza kuongezeka 496.24 MW katika uzalishaji wa umeme nchini. Hii maana yake ni kwamba kila mwaka tuliongeza uzalishaji wastani wa 100 MW za umeme nchini. Kwa mwenendo huu ili kufikia lengo la kuzalisha 2,780 MW tunahitaji miaka 13 ili kuweza kufikia lengo la Mpango wa miaka 5 ya awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili ni kwanini haikutekeleza lengo la Mpango wa Maendeleo la kuzalisha 2,780 MW za umeme?

5. MPANGO WA UMEME WA DHARURA

Mheshimiwa Spika, Mpango wa umeme wa dharura unaweza kutafsiriwa kama ni mapungufu ya sera ya nishati kutokuwepo kwa mpango wa muda mrefu ambao unaambatana na uzalishaji utakaoangalia mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Kutokufanya vizuri kwa shirika letu la umeme kwa kiasi kikubwa kumetokana na Serikali kuingia mikataba na makampuni binafsi ili kuzalisha umeme wa dharura na kuliuzia shirika letu la umeme.

Mheshimiwa Spika, Hadi sasa mitambo ya kukodisha ambayo inazalisha umeme na kuuza kwa Tanesco ni; mtambo wa gesi wa Symbion 112MW, Aggreko Ubungo 50MW, Aggreko Tegeta 50 MW, Symbion Dodoma 50MW. Mipango mingine ya muda mfupi ni pamoja na Jacobsen (gas) awamu ya kwanza 100 MW ilikuwa USD 124 million Jacobsen awamu ya pili 150 MW ilikuwa USD 165 million.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya uzalishaji wa umeme imekuwa ndiyo sekta yenye ukiritimba, jambo linalopelekea kuwa sekta yenye rushwa kubwa kubwa, jambo hilo linasababisha wawekezaji wengi wanaotaka kuzalisha umeme kushindwa kufanya hivyo. Mfano mzuri ni mvutano mkubwa uliokuwepo kati ya RUBADA na TANESCO kuhusu uzalishaji wa umeme wa maji kwenye mabonde ambayo yanamilikiwa na Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Moja katika ya rasilimali kuu za Bonde la Rufiji ni chanzo cha uzalishaji umeme wa maji, kwa utafiti uliofanywa na RUBADA mwaka 1984 kwa kutumia kampuni ya Norway ya Norconsult kwenye Rufiji Basin Hydropower Master Plan ilionesha kuwa bonde lina vyanzo vikuu vinane vya uzalishaji wa umeme na vyanzo hivyo ni; Stiegler's Gorge, Mpanga, Ruhudji, Mnyera, Iringa, Lukose, Kihansi and Kilombero¹.

Mheshimiwa Spika, Bonde la Mto Rufiji linauwezo wa kuzalisha umeme wa mpaka 2729MW bila ya kuathiri shughuli zingine za kiuchumi. Lakini kwa sasa Bonde la Mto Rufiji lina mabwawa matatu tu yanayotumika kwa ajili ya uzalishaji wa umeme ambayo ni Kidatu, Kihansi na Mtera ambayo yanazalisha umeme wa 460 MW tu.

¹ Rufiji River Basin Upstream Downstream Linkages - Report of the Workshop held at Morogoro on 26 – 28 March, 2001

Mheshimiwa Spika, Inasadikiwa kwamba Tanzania inauwezo wa kuzalisha umeme wa maji wa 4700MW kwa kutumia mabonde yake ya mito sita, ambayo ni;Rufiji, Pangani, Kagera, Malagarasi, Ruvuma na Rumakali .

Mheshimiwa Spika, kwa Bonde la Mto Rufiji kuhusu uzalishaji wa umeme hapa nchini, mradi wa STIEGLER'S GORGE pekee toka miaka ya 1980 upembuzi yakinifu ulikwishafanywa na kuonekana kuwa ndio chanzo ambacho kingeweza kuzalisha umeme wa kutosha kwa mahitaji ya matumizi yote ya viwandani na majumbani kwa gharama nafuu. Chanzo hiki ndicho kilikuwa chanzo cha uhakika kwa kuiweka Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa Kati.

Mheshimiwa Spika,Kwa mujibu wa upembuzi yakinifu uliofanyika miaka hiyo ya 80 inaonesha kuwa mbali ya Stiegler's Gorge RUBADA inavyanzo vingine vya kuzalisha umeme wa maji, ambavyo ni:-

1. Mpanga linauwezo wa kuzalisha..... 165MW
2. Ruhundji linauwezo wa kuzalisha..... 685MW
3. Mnyera 485MW
4. Lukose130MW
5. Kilombero (Kingenenas&shughuli falls)...464MW

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuelezwa toka upembuzi huo ufanyike ni hatua gani tena imeishafanyika kuona vyanzo hivyo vinatumika kuzalisha umeme kwa matumizi ya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, Miradi ya uzalishaji umeme wa maji kama huu tunaousema wa Stiegler's Gorge zipo pia katika nchi za Brazil kwenye bwawa la Itaipu linalozalisha 10,200MW, China yenye mabwawa matatu yanayozalisha 22,500MW na nchini Venezuela yenye bwawa la Guri lenye kuzalisha umeme 10,200MW²

Mheshimiwa Spika, Umeme uzalishwao kwa kutumia nguvu za maji (hydroelectric power) huu ni uzalishaji rahisi na unatunza mazingira, tofauti na aina zingine za uzalishaji wa umeme ambazo kwanza sio endelevu.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa ni dhahiri toka utafiti ulipofanyika hadi sasa ni muda mrefu sana na Serikali imekwishatumia mabilioni ya fedha kukodisha mitambo ya kuzalisha umeme, jambo ambalo kama uamuzi

2Kiwia, J. 2013: River resources towards Sustainable Development of Tanzania. A contribution of Hydropower to the energy security in Tanzania: Case study, Rufiji River basin. Master thesis in Sustainable Development at Uppsala University, No. 158, 31 pp. 30 ECTS/hp.

ungefanyika kabla kwa sasa tusingekuwa tunahangaika na matatizo ya umeme kwa utafiti uliofanyika wa chanzo hicho cha Stiegler's Gorge tungekuwa na umeme wa kutosha na pengine tungekuwa tunauza kwa majirani zetu.

6. KAMPUNI YA KUZALISHA UMEME WA MAJI -Aldwych International Ltd

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Aldwych International Ltd ya Uingereza ndiyo iliyokuwa inashughulika na kuendeleza mradi wa umeme wa Ruhudji toka mwishoni mwa mwaka 2006. Mradi wa Ruhudji wa uzalishaji 360 MW, kwa mujibu wa Power system Master Plan (PSMP) mwanzoni ulipangwa kumalizika 2014. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuelewa hadi sasa utekelezaji wa mradi huo na Kampuni tanzu ya **Aldwych International Ltd ambayo itaingia ubia na Tanzania iitwayo** Ruhudji Power Development Company Limited, (RPDC) umefikia kiwango gani? muda mrefu inatakiwa kuwa makini na aina ya mkataba **"Implementation Agreement and Power Purchase Agreements"** utakaoingia isije ikawa kama mikataba iliyopo ya umeme wa dharura.

Mheshimiwa Spika, Ni ukweli kuwa mizania ya TANESCO inaonesha kuwa shirika hilo limekuwa likifanya biashara kwa hasara kutokana na gharama za uzalishaji kuwa kubwa kuliko bei ya kuuzia umeme huo hasa ni kwa umeme unaozalishwa na wazalishaji binafsi na kuiuzia TANESCO.

7. SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA-TPDC

Mheshimiwa Spika, Shirika hili la mafuta ndilo lililo na jukumu la msingi la kuhakikisha kuwa raslimali ya mafuta na gesi iliyo hapa nchini inajulikana ilipo na inajulikana kiasi cha hazina kilichopo na inavunwa na nani na watanzania watanufaika vipi na raslimali hizo. Katika kutekeleza hayo yote shirika kwa mwaka wa fedha 2015/16 liliomba kiasi cha shilingi bilioni 12 kama fedha za maendeleo, lakini hadi kamati za Bunge zinakutana hakuna hata shilingi iliyokuwa imetolewa na hazina kama fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha TPDC imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za maendeleo zikiwa ni fedha za ndani, kati ya fedha hizo shilingi milioni 700 ni ujenzi mtandao wa kusambaza gesi asili kwa mikoa ya Mtwara na Lindi na shilingi milioni 800 ni mradi wa kuchakata gesi asili na kuwa kimiminika kwa ajili ya kuisafirisha nje na ndani ya nchi ikiwa imesindikwa, na shilingi bilioni 9.2 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani imeeleza hapo awali kwamba kazi ya kusimamia kwa kuelewa rasilimali ya mafuta na

gesi ilipo na ni kiasi gani kilichopo ni kazi inayohitaji rasilimali. Kitendo cha kukosa fedha kwa ajili ya kutekeleza jukumu hilo ni dhahiri kwamba makampuni yanayojihusisha na biashara hiyo, ambayo kwayo ni lazima yawe na fedha za kutosha ni rahisi kuiweka TPDC mfukoni mwake na mwisho wa siku watanzania wakakosa kunufaika na rasilimali hizo.

Mheshimiwa Spika, katika biashara yoyote kuonesha hali yoyote ya unyonge maana yake ni kuweka haki zako rehani, na vivyo hivyo TPDC kukosa fedha za miradi ya maendeleo ni kuweka sekta hii ya mafuta rehani.

Mheshimiwa Spika, Ukosefu wa fedha unaolikumba shirika hili ndio unaopelekea mapato ya gesi kutokukusanywa kwa kadri mikataba na sheria zinavyosema. Kwa mujibu wa taarifa ya TPDC inaonesha kuwa Songas inadaiwa jumla ya shilingi 50,275,344,006/-na Pan African Energy inadaiwa jumla ya shilingi 60,665,839,011/-. Kwa kampuni zote hizo zinadaiwa na TPDC jumla ya shilingi bilioni 110.94 Je, kwa mwendo huu gesi hii inaweza kuwa na manufaa kwa wananchi, Kama madeni yanashindwa kudaiwa kwa kusimamia mikataba iliyopo?

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni kwamba TPDC imeshindwa kupokea Gawio lake toka kwa songas lenye thamani ya dola za kimarekani 467,997 na hivyo kuzidi kuwa hoi kifedha. Kambi Rasmi ya Upinzani inaliangalia hili la TPDC kushindwa kupata stahili zake kutoka kwenye makampuni hayo ya gesi kutokana na ukweli kwamba mikataba iliyoingiwa pengine kuna vifungu vinavyoshindwa kutoa kazio la mikataba au ni kutokana na watendaji kuwekwa kwa mtindo wa kubebana na hivyo kushindwa kutimiza majukumu yao ya kimsingi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema Serikali wakati inajumuisha itoe majibu kwa hoja zote tajwa kwani Katika Bajeti zetu za nyuma tulizungumzia kuhusiana na muundo mpya wa utendaji wa TPDC ambao ulikuwa unatia mashaka lakini ulipata Baraka zote za Wizara ya Nishati na Madini.

8. SEKTA YA MADINI

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu imejaaliwa wingi wa madini ya kila aina, hata hivyo, madini haya hayatatusaidia sana kama hatua madhubuti hazitachukuliwa dhidi ya mapungufu yaliyomo kwenye sera ya madini inayojenga mazingira mazuri kwa wageni kumiliki utafutaji na uchimbaji madini hapa nchini dhidi ya ushiriki wa wazawa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mapungufu hayo kama yalivyobainiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani ni:

- a. Serikali imekabidhi utafutaji na uchimbaji madini mikononi mwa sekta binafsi ndani ya utandaawazi ulimwenguni, pasipo kuzingatia kuwa sekta binafsi ya Tanzania bado ni changa kushindana na makampuni ya kimataifa.
- b. Kuwalipisha wazawa na wageni ada na tozo sawa kwenye madini kama vile wageni wana haki sawa na wazawa, kwenye rasilimali zinazopatikana nchini Tanzania.
- c. Serikali kutumia misamaha ya kodi kwenye sekta kama njia ya kuvutia wawekezaji badala ya kutengeneza mazingira wezeshi, kama vile nishati na miundombinu ya uhakika katika maeneo ya uchimbaji na hivyo kupelekea sekta kutokutoa pato stahiki kwa nchi. n.k

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali, kwanza kurekebisha mapungufu ya kisera kwani Duniani kote rasilimali zinazoisha kama madini kipaumbele kinawekwa kwa wazawa badala ya wageni. Kwa njia hiyo ndipo rasilimali hizi zitakuwa na thamani na faida kwa watanzania.

9. WACHIMBAJI WADOGO WADOGO

Mheshimiwa Spika, unaposema sekta ya madini, kwa uelewa wa haraka wa watanzania waliowengi maana yake ni wachimbaji wadogo. Hii inatokana na ukweli kwamba wachimbaji wadogowadogo ndio ambao mchango wao unaonekana wazi katika maendeleo ya nchi yetu, hata kama sio kwenye ukokotozi wa pato la taifa. Lakini ukweli ni kwamba maisha ya watu wengi yanabadilishwa na wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa ruzuku kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili kuwawezesha kuimarisha mazingira ya kazi zao. Lakini kumekuwa na malalamiko kuwa utoaji wa ruzuku hiyo hauna utaratibu unaoeleweka kwani walengwa hawanufaiki na fursa hiyo. Malalamiko haya yanatolewa na wachimbaji wadogo wanaotoka kanda ya ziwa (Shinyanga, Geita, Mwanza, Mara, Simiyu na Kagera) ambao ni takriban 80% ya wachimbaji wadogo nchi nzima. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza utaratibu unaotumika kwao kupatiwa ruzuku hiyo ya Dolla za Marekani 100,000 kwa kila mwaka, bila ya kuwepo uratibu na utaratibu unaoeleweka lazima upendeleo utakuwepo kwa watu walio karibu na watendaji wa wizara katika kupata fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wapo karibu kila sehemu ya nchi yetu, na malalamiko ya wachimbaji hao kwamba hawatendewi haki na Serikali kwa kuwatoa au kuwafukuza katika maeneo ambayo wamegundua kuwa kuna madini. Kilio hicho kipo pia katika mgodi wa Busekela Mkoa wa Mara,

Wilaya ya Musoma Vijijini unaomilikiwa na Kampuni ya Dolphine Mines, lakini wachimbaji wanaozunguka mgodi huo wanasumbuliwa sana japokuwa mgodi huo unajulikana ni wa wachimbaji wadogo, lakini Serikali inashirikiana na Kampuni hiyo ya Dolphine kuwanyanyasa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Aidha huko huko Musama Vijijini, Jimbo la Butiama kuna mgodi ambao upo katika kijiji cha Nyamikoma, Kata ya Kyanyari kuna Kampuni ya madini ya M/S HENAN AFRO ASI-GEO ENGINEERING (T) Co. LTD ambayo sasa ni takribani miaka 8 wanafanya utafiti na muda wa utafiti ulitakiwa umalizike mwaka huu mwezi wa Mei, lakini Mkuu wa wilaya alitoa kibali bila ya utaratibu cha kuwaongezea muda wa utafiti kwa barua yake ya tarehe 27/4/2017 yenye Kumb. Na. AB. 128/270/01/A/66 kwenda kwa Afisa Tarafa wa Tarafa ya Makongoro. Utafiti huo umeharibu sana miundombinu ya barabara na mazingira.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo wa Geita wamekosa maeneo ya kufanyia shughuli zao kutokana na ukweli kwamba maeneo waliyokuwa wanafanyia shughuli zao yamehodhiwa na Mgodi wa Geita Gold na watu wengine ambao wamepewa umiliki na Serikali lakini maeneo hayo hayatumiki.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia wanachi maeneo ambayo hayatumiwi na mgodi ili wajasiriamali waweze kufanyakazi yao.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine ambalo wachimbaji wadogo na wananchi wa Geita wanakutana nalo na Mhe. Makamu wa Rais alitoa ahadi kwamba mabaki ya mchanga unaotoka migodini (Magwangala) watapewa wananchi ili wafanye uchenjuaji upya wa kutafuta dhahabu kutoka kwenye mchanga huo. Ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tarime ina mgodi wa North Mara ambao sasa unaitwa ACCACIA, ulianza rasmi mwaka 1994 lakini ulikuta wananchi katika eneo hilo la Nyamongo wakiwa wanachimba madini eneo la Nyarugusu na Nyabirama. Baada ya wawekezaji kupewa leseni, Dar es Salaam walitwaa eneo hilo bila kuwaachia wananchi wa Tarime hata eneo la mita tano kuchimba.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni wananchi kuuawa kila mara kwa kisingizio cha kuingia mgodini. Tangu mwaka 1994 zaidi ya watu 400 wamekwisha uawa na wengine wengi wamebaki na vilema vya maisha na bila kutafuta suluhisho. Mgodi wa Nyamongo tofauti na migodi mingine uko katikati ya makazi ya watu, hivyo wananchi walitakiwa kuhamishwa kwa kulipwa fidia ili kupisha shughuli za uchimbaji kama inavyosema Sheria ya madini ya mwaka

2010. Lakini hadi sasa watu wanaishi mita takriban mbili kutoka mgodini kinyume cha sheria inayosema wawe umbali wa mita 200 kutoka eneo la mgodi.

Mheshimiwa Spika, ukifanyika ulipuaji wa miamba athari kubwa zinawakumba wakazi hao ikiwemo kuathirika kiafya kutokana na vumbi kali, wengine kupatwa na mistuko ya moyo, nyumba zao kuwa nyufa n.k

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kuhusu Kamati ya Kupitia Matatizo yote yanayowakabili wananchi wa Nyamongo na Kampuni ya ACCACIA iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka taarifa hiyo iharakishwe ili kunusuru majanga yasiendelee kwani tayari mauaji yanaendelea, ambapo kijana mmoja alipigwa risasi na askari hivi karibuni.

10. MALALAMIKO YA KAMPUNI YA BISMARCK HOTEL (MINING) LIMITED

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa taarifa ilizonazo ni kuwa kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu kati ya Kampuni ya uchimbaji madini ya Bismark Hotel (Mining) Limited dhidi ya Kampuni za madini za Pangea Minerals Limited, Barrick Exploration Africa Limited na Acacia Mining PLC (zamani Barrick Gold PLC) ambapo kampuni hizo za kigeni ziliingia kwenye makubaliano ya pamoja na kampuni ya Bismark ya kupangisha eneo la kuchimba madini la Mgusu huko Geita mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu kwa upande mmoja unaihusisha Wizara ya Nishati na Madini ambapo imedaiwa kutoa tafsiri tofauti ya kifungu cha 15(2) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kuhusiana na muda wa eneo lililokwisha muda wake wakati wa kuhuisha leseni za utafutaji madini kuwa wazi kabla ya kuruhusiwa maombi mapya katika eneo husika. Hii ni kutokana na matakwa ya kisheria kutoa miezi minne kabla ya kutoa leseni nyingine katika eneo ambalo leseni yake imefikia kikomo.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha kuwa sehemu ya eneo la Mgusu leseni yake ilifikia kikomo lakini kabla ya miezi minne kumalizika ikatolewa leseni mpya kwa Barick Gold/Acacia Mining PLC badala ya kampuni ya Bismark ambayo ilitii matakwa ya kisheria kusubiri muda wa miezi minne umalizike kabla ya kupeleka maombi mengine Wizarani kuomba kuhuisha leseni yao ya awali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kutoa kauli hapa Bungeni kutokana na sakata hilo kwa kuwa serikali yenyewe kupitia Wizara ya Nishati na Madini imekuwa ikitoa mara kwa mara tafsiri tofauti ya kifungu cha 15(2) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Aidha Waziri atoe kauli mbele ya Bunge lako tukufu kuhusu hatua gani zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya Eng. John M. Nayopa ambaye ametuhumiwa kuhusika katika sakata hili

wakati wote na taarifa zake kupelekwa TAKUKURU na kwa Mwanasheria Mkuu wa serikali.

Mheshimiwa Spika, ni vema na ni sahihi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuishauri Wizara kuhakikisha inalimaliza jambo hili kwa wakati ili kuhakikisha pande zote mbili haziendelei kutumia gharama kubwa wakati huu ambapo bado inaonekana kuna mgogoro na pia kuhakikisha kuwa mwenye haki yake katika jambo hili anaipata kwa wakati.

11. TAKA SUMU ZINAZOTOKA KATIKA MGODI WA GEITA NA TATIZO LA MPAKA KAKOLA

Mheshimiwa Spika, mtaa wa Nyakabale, kata ya Mgusu ni mtaa uliokuwepo hata kabla ya uwepo wa Kampuni ya uchimbaji madini ya Geita kuanza shughuli zake katika wilaya hiyo. Katika umilikishaji Mgod, ilikuja kubainika kuwa Kata ya Mgusu imo ndani ya mipaka ya Mgod na pia wako karibu na shughuli za mgodi.

Mheshimiwa Spika, katika shughuli za mgodi, lilichimbwa bwawa kubwa ambalo linatumika kumwaga taka zitokanazo na uchenjuaji wa dhahabu. Taka sumu hizo zimekuwa na madhara makubwa sana ya kiafya kwa wakazi wa Mtaa wa Nyakabale. Kwa kuwa imeshindikana kwa mgodi kutoa fidia iliyo timilifu kwani Mgod unadai kuwa eneo hilo unalimiliki kihalali wakati makosa ya yalifanywa na Serikali kwa kujua au kutokujua wakati wanatoa haki ya umiliki kwa mgodi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulichukulia kwa umuhimu wa kipekee suala la ulinzi wa afya za wakazi wa Mtaa huo wa Nyakabale. Ni muhimu sana kwani uwepo wao hapo sio kwa bahati mbaya bali ni haki yao kutoka kwa mababu zao.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa wakazi wa Mtaa wa Nyakabale, kwa mkoa wa Shinyanga, Jimbo la Msalala Kijiji cha Kakola kinakabiliwa na tatizo la Mgod wa Bulyanhulu kuweka mipaka kuzunguka kijiji kizima wakati wao wanafanya shughuli zao katika eneo dogo tu. Jambo hili linawafanya wanakijiji cha Kakola kukosa huduma stahili, na wao kuweza kuendeleza eneo hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa suluhisho kwa wanakijiji hao, kwani makosa yalifanywa na Serikali wakati wanatoa ardhi kwa mgodi. Sambamba na hilo wakazi wengi katika kijiji hicho wanafanya kazi za uchimbaji madini, hivyo hawawezi kupewa leseni ya kufanya kazi hiyo kwani kijiji kizima inaonesha kinamilikiwa na mgodi wa Bulyanhulu.

12. WAKALA WA USAMBAZAJI UMEME VIJIJINI-REA

Mheshimiwa Spika, wakala huyu alianzishwa kwa sheria Na 8 ya mwaka 2005 na alianza kazi rasmi Oktoba mwaka 2007, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2003. Lengo likiwa ni kuwapatia wananchi waishio vijijini nishati bora. Pamoja na umuhimu wa wakala huyu bado serikali haijaonyesha kwa vitendo kuwa ina nia ya kusaidia wakala huyu ili aweze kutimiza majukumu yake kikamilifu na hasa linapokuja suala la kuupatia fedha kama zinavyoombwa na zinavyopitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 wakala alitengewa jumla ya **shilingi 420,492,701,200/-** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Lakini kwa mujibu wa taarifa ya utendaji ya Wakala ni kwamba hadi Desemba 2015 zilikuwa zimepokelewa jumla ya **shilingi 141,163,133,226/-** tu ambazo ni sawa na **asilimia 34**. Kati ya fedha hizo hakukuwa na fedha zozote zitokanazo na tozo ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa takwimu za wakala wa Uagizaji mafuta kwa pamoja (PBPA) zinaonesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2015/16 wakala uliingiza mafuta ya Petrol jumla ya tani 571,681, mafuta ya Diesel tani 1,052,129 na mafuta ya taa tani 12,238.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria ya fedha iliyopitishwa na Bunge lako tukufu ilitoa haki kwamba kila lita moja ya mafuta ya petrol na mafuta dizeli ikatwe **shilingi 100** na **shilingi 150** zikatwe kwa kila lita moja ya mafuta ya taa, na zipelekwe kwa wakala wa umeme vijijini kwa ajili ya kuimarisha usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa mahesabu ya tani hizo zilizoagizwa na wakala ni kwamba tozo za mafuta ya petrol na diesel kwa jumla ya tani 1623810 ni shilingi **162,381,000,000/-** na kwa tani 12,238 za mafuta ya taa sawa na shilingi **1,835700,000/-**. Na hivyo jumla ya fedha za tozo tokana na mafuta ni **shilingi 164,216,700,000/-**

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kwa mwelekeo gharama za miradi ya umeme ambayo inatekelezwa na makandarasi mbalimbali ni dhahiri fedha hizo kama kweli zilitolewa ni uhakika kwamba madeni inayodaiwa wakala yasingekuwepo.

Hivyo basi, **Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni** inamtaka Mhe Waziri alieleze Bunge ni kiasi gani hadi sasa cha fedha za tozo ya mafuta kati ya fedha tajwa hapo awali kimepelekwa REA.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha REA imetengewa jumla ya **shilingi 587,613,169,000/-** zikiwa na feha za maendeleo, na kati ya fedha hizo **shilingi 53,213,169,000/-** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya wakala inaonesha kuwa kuna miradi inayoendelea ya kuweka umeme ya kutoka mwaka wa fedha 2015/16 na bado REA haijamaliza kuwalipa wakandarasi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2016/17 REA imetengewa jumla ya **shilingi 587,613,169,000/-** kama fedha za maendeleo. Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2015/16 kuna miradi ya umeme iliyokuwa inatekelezwa kwa mwaka huo na wakandarasi hawakulipwa, na hivyo kufanya Ankara ambazo hazijalipwa (**outstanding invoices**) zenye thamani ya **shilingi bilioni 94**, na miradi mipya ambayo inatakiwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka huu wa 2016/19 ina thamani ya **shilingi bilioni 512.143**.

Mheshimiwa Spika, kama fedha za miradi ya nyuma zitalipwa, miradi ya mwaka huu itakuwa na **nakisi ya shilingi bilioni 18.63** kwa maana kuwa Ankara zisizolipwa ukijumlisha na miradi mipya ukilinganisha na bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa mwaka huu.

13. SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA- STAMICO

Mheshimiwa Spika, STATE MINING CORPORATION (STAMICO) ni shirika la umma lililo chini ya wizara lilianzishwa chini ya sheria ya makampuni sura 257 ya mwaka 1972 na pia sheria hiyo ikafanyiwa marejeo au marekebisho 2014. Sera mpya ya madini ya mwaka 2009 ambayo iliifuta sera ya madini ya mwaka 1997, lengo kuu la sera hiyo mpya ilikuwa ni kuifanya serikali kushiriki katika uwekezaji wa madini kwa kupitia taasisi zake kama sera hiyo inavyosema.

Mheshimiwa Spika, ili kwenda sambamba na sera hiyo ya madini ya mwaka 2009, Bunge lilitunga sheria mpya ya madini ya mwaka 2010 ambayo iliweka kifungu ambacho kinaipa haki Serikali kupitia taasisi zake kujihusisha na uwekezaji katika madini. Katika kufanya hivyo, STAMICO ikawa ndio taasisi ya Serikali inayoendesha jukumu hilo na likafanyiwa maboresho ya kimuundo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuwekeza katika sekta ya madini na kuweza kuwa na ushindani katika sekta kunahitaji mtaji mkubwa sana. Hivyo basi kitendo chochote cha kutokuwezesha vya kutosha STAMICO ni kuipa uhuru wa kuendelea kupokea mshahara bila ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika maombi ya fedha kwa mwaka 2016/17 inaonesha kwamba STAMICO imetengewa fedha za matumizi ya kawaida tu, na fedha hizo kwenye kitabu cha IV cha Matumizi ya Wizara na taasisi zake kwa

kulinganisha takwimu hizo utakuta tofauti ya shilingi 36,265,000/- (**Randama Tshs 4,634,402,000/- Vol. IV inaonesha Tshs.4,670,667,000/-**)

Mheshimiwa Spika, Dhana ya uanzishwaji wa STAMICO kwa mujibu wa sheria ilikuwa ni kuwa itakuwa na uwezo wa kushindana au kufanya biashara ya uchimbaji wa madini kwa niaba ya Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kwa kuwa kila kitabu kina zama zake, kwa sasa hiyo dhana ya STAMICO kuwa ya kibiashara imepitwa na wakati na ili kuifanya kuwa hivyo itabidi bajeti zetu za Serikali za miaka kama 20 ndizo ziwekezwe STAMICO, na ukweli jambo hilo haliwezekani.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha kuwa STAMICO ilikabidhiwa mgodi wa TULAWAKA ukiwa unafanya kazi kwa maana ya mitambo na magari na fedha kwa ajili ya pale mgodi utakapofungwa kurudisha mazingira katika uhalisia wake kwa mujibu wa hitajio la sheria ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua Annual turnover ya Mgodi huo tangu uchukuliwe na STAMICO ni kiasi gani? Aidha, Kambi inataka kujua ni shilingi ngapi Kampuni ilipewa na AFRICA BARRICK GROUP kama fedha za kufunga Mgodi kama mgodi huo ungetumiwa na Kampuni ya ABG hadi mwisho? Je, kwa hali ilivyo sasa mgodi huo unatakiwa kufungwa lini?

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa kwa Tanzania rasilimali madini ambayo hadi sasa imewekezwa na kuchimbwa na makampuni makubwa toka nje ni chini ya asilimia 5 ya rasilimali yote ya madini ambayo bado haijachimbwa. Hivyo basi, kwa mujibu wa taarifa ya Mtafiti wa masuala ya madini James Morrissey juu ya jinsi gani rasilimali zinavyoweza kuwa chachu ya maendeleo; kwamba ni lazima thamani kubwa ya rasilimali ibaki kwenye nchi husika kama mapato kwa Serikali. Jambo hili ni tofauti na hali halisi ilivyo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukosa rasilimali za kutosha kwa STAMICO kufanya kazi, imeilazimu STAMICO kuchukua migodi ambayo wahusika wamemaliza kuchimba au kiasi kikubwa cha rasilimali kimeondolewa na mabaki ndiyo STAMICO inapewa, **kwa lugha rahisi ni kuwa STAMICO inakuwa kama fisi ambaye kazi yake ni kuvizia mifupa baada ya simba au chui kula minofu yote**. Utaratibu huu unaliingizia Shirika letu hasara kubwa kwani mgodi unapofungwa, inawalazimu kuhakikisha eneo husika linatimiza masharti ya Kimazingira la kurudisha eneo hilo katika hali yake ya kiuhalisia.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwa ili Tanzania inufaike na Raslimali zetu za madini, ni dhahiri kuwa hatuwezi kushindana na makampuni ya kimataifa kama vile Geita Gold Mine, **AngloGold**

Ashanti, ACACIA, RESOLUTE, Anglo American, Anglo Platinum, De Beers, Empire Zinc Company, Energy Resources of Australia n.k. Ni ukweli kwamba kama mshindani wako umemshindwa basi inabidi uungane nae.

Hivyo basi, Mheshimiwa Spika, ni ushauri wa Kambi Rasmi kuwa STAMICO badala ya kulazimisha kuwa itakuwa ni kampuni ya taifa kuwekeza kwenye madini ni bora Serikali ifanye utaratibu wa kupata hisa kwenye makampuni hayo ya madini na sisi tuweze kuwa na uwakilishi kwenye bodi zao za uendeshaji pamoja na timu za utawala wa Kampuni hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo ni dhahiri kama nchi mbali ya makampuni ya nje kuchimba madini ni dhahiri kile tulichokuwa tunakikosa kama nchi cha kuelewa ukweli wa kinachopatikana, tutakuwa katika hali ya uelewa wa nini kinaendelea katika uzalishaji na stahiki ya nchi itapatikana kama mikataba inavyosema.

14. SEKTA YA UZIDUAJI (EXTRACTIVE INDUSTRIES)

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2015 Bunge lako tukufu ilipitisha miswada mitatu ya sekta ya uziduaji (Extractive industries). Miswada hiyo ni Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2015 (The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act 2015, Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015. (The Oil and Gas Revenue Management Act 2015), Sheria ya Petroli ya mwaka 2015- (The Petroleum Act 2015).

Kwa utaratibu wa kawaida ni wajibu wa serikali kuhakikisha kuwa sheria zinazopitishwa na bunge hili zinatekelezwa kwa haraka na kwa umahiri. Kambi ya upinzani ingependa kutaarifu bunge lako tukufu kuwa mwaka mmoja baada ya kupitishwa kwa sheria ya Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2015 (The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act 2015, haijaanza kutekelezwa.

Hii inatokana na Wizara ya Nishati na Madini kuendeleleza urasimu, kung'ang'ania na kuhodhi madaraka iliyopewa Kamati tekelezi (TEITI Multi Stake Holder Group) kwa mujibu wa sheria hii. Kambi ya upinzani inaomba itoe mifano kuonyesha jinsi gani kucheleweshwa kwa sheria hii inahatarisha ukuaji na usimamizi wa sekta.

Kifungu namba 4 ya sheria hii inasema ifuatavyo:

(1) There shall be a Committee to be known as the Tanzania Extractive Industries(Transparency and Accountability) Committee

(2) The Committee shall be an independent Government entity which shall be an oversight body for promoting and enhancing transparency and accountability in the extractive industry.

Mheshimiwa Spika, Licha ya kipengele hiki kutambua nafasi ya kamati tekelezi (TEITI MSG) chini ya Jaji Mstaafu Mark Bomani, kwa ucheleweshaji huu imenyimwa fursa ya kusimamia na kuhakiki mapato ndani ya sekta hii. Kamati hii haina meno wala ujasiri wa kuwahakikishia Watanzania kuwa inathibiti vilivyo rasilimali zake.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Septemba 2015 Tanzania ilifungiwa na bodi ya kimataifa inayosimamia uwazi katika sekta ya uziduaji (Extractive Industry Transparency Initiative). Kwa barua iliyoandikwa na Mwenyekiti Mhe Claire Short uamuzi huo ulichukuliwa baada ya Wizara ya Nishati na Madini kuchelewesha mchakato wa kupatikana kwa mkaguzi wa mahesabu kwa mahesabu ya 2012/13. Hii iliitia Tanzania aibu mbele ya jumuiya ya kimataifa hasa kwa kuwa tumekuwa tukijitambulisha kuwa mfano wa uwazi na uwajibikaji. Tatizo la manunuzi litatuliwa tu kama kamati tekelezi (MSG) itapewa mamlaka kamili ya kusimamia manunuzi yake bila kuingiliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati tekelezi (MSG) imeshindwa kuajiri ndani ya sekretariati yake, wataalamu wake wenyewe na kutegemea wafanyakazi toka serikalini. Utamaduni ya kutumia wafanyakazi toka Wizara ya Nishati na Madini inaifanya kamati hii kutoweza kuzisimamia serikali na makampuni ipasavyo. Hii pia inatokana na Kamati hii kunyimwa uhuru wa kusimamia rasilimali yao wenyewe hata zile zinazotokana na wafadhili kama EU, Benki ya Dunia na Canada. Kwa utaratibu ulioko kila kitu lazima kiidhinishwe na Wizara ya Nishati na Madini ingawa fedha wanaziomba kamati tekelezi (TEITI MSG) kutoka kwa wafadhili.

Mheshimiwa Spika, Mwishoni mwa Machi 2015, Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT) iliitaka African Gold Mine (kwa sasa Acacia) kuilipa Serikali kodi ya Dola za Marekani 41.25 milioni (zaidi ya Sh89 bilioni), baada ya kugundua udanganyifu katika ulipaji wa kodi kwa miaka minne mfululizo.

Hata hivyo ripoti zilizochapishwa na kamati tekelezi (TEITI MSG) katika miaka yote hiyo hazigundua mapungufu hayo. Hii inaonyesha udhaifu mkubwa katika uendeshaji na usimamizi wa ukaguzi wa mahesabu ya sekta ya madini na mafuta. Ni maoni yetu kuwa hii ingeweza kuepukika ikiwa kutakuwa na wafanyakazi wenye weledi pamoja na rasilimali za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Wakati taasisi nyingi za serikali zinakosa rasilimali fedha, kamati Tekelezi (TEITI MSG) ni chombo kinalalamikiwa na wafadhili kwa kurudisha kapuni fedha kwa kushindwa kuzitumia. Hii inatokana na kutoka

wataalamu wa kutosha na uoga wa kufanya maamuzi ndani ya secretariat. Pia inatokana na urasimu wa kuidhinisha matumizi ndani ya Wizara ya Nishati na Madini.

Kwa mwaka 2015/16 pekee, Umoja wa Ulaya na Shirika la maendeleo Canada zilitoa takribani Euro 1,400,000. Nusu ya fedha hizi zinarudishwa kwa wafadhili bila maelezo ya kuridhisha, huku ikionyesha udhaifu mkubwa wa watendaji kutimiza wajibu wa kuimarisha kazi ya udhibiti wa mianya ya kupotea mapato ya serikali.

15. WAKALA WA JIOLOJIA TANZANIA (GST)

Mheshimiwa Spika, wakala wa Jiolojia Tanzania ulianzishwa chini ya sheria ya wakala wa Serikali Namba 30 ya mwaka 1997 (CAP 245) kupitia katika tangazo la Serikali Namba 418 la Desemba 09,2005, na kuzinduliwa rasmi mwaka Juni 23, 2006. Aidha, ni kwamba tangu enzi za Mkoloni kitengo cha maabara ya madini kilikuwepo na kilianzishwa rasmi mwaka 1925 na kilikuwa kinafanya kazi zake kikiwa hapa Dodoma na majukumu yake ya msingi hadi leo hayajabadilika sana bali yameboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya wakala huyo ni pamoja na kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kutunza takwimu na taarifa mbalimbali za jiosayansi, kutengeneza ramani mbalimbali za jiosanyansi zinazoainisha uwepo wa madini ya aina mbalimbali, kusambaza ramani, taarifa na takwimu kwa wadau ili ziweze kutumika kwa shughuli mbalimbali, kutoa ushauri wa kitaalam kwa wachimbaji madini wakubwa na wadogo na pia kwa kwa sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji ya Wakala kwa mwaka wa fedha unaomalizika wa 2015/16 unaonesha kuwa katika fedha zilizotengwa za matumizi mengineyo ya **shilingi 4,433,482,000/-** lakini hadi mwezi March, 2016 ni jumla ya shilingi bilioni 1 tu sawa na asilimia 22.55. Aidha, wakala haukutengewa fedha yoyote kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa mwaka wa fedha unaotarajiwa kuanza mwezi wa saba wakala unaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 4,417,444,000/-** lakini kama ilivyokuwa mwaka jana haikutengwa hata shilingi moja kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kabisa kwamba Tanzania imebahatika kuwa na madini ya kila aina, hivyo basi ni jukumu la wakala huyu kufanya utafiti na kubaini kila eneo lina madini ya aina gani na kwa kiasi gani na matumizi ya madini hayo na ni njia gani inatakiwa kutumika katika uchimbaji wake. Kitendo cha Serikali kutokutoa fedha yoyote kwa ajili ya kupata vifaa vya kisasa vya kutafuta na kupimia sampuli za miamba au udongo kwa kulinga aina ya madini yanapopatikana ni kuifanya sekta ya madini kuendelea kuhodhiwa na wale wenye uwezo wa kifedha tu.

Mheshimiwa Spika, Kwani makampuni makubwa yanapata leseni ya kuchimba aina moja ya madini lakini ukweli ni kuwa katika mchakato wa kuchimba madini hayo, yanakuwemo madini mengine yanayoambatana na madini yaliyooombewa leseni, hivyo nchi ndiyo inapoteza na inakuwa ni faida kwa wenye leseni kwani wanachukua madini hayo bure kabisa. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba Wakala huyu ili kazi yake iwe ya manufaa kwa Taifa na kwa jamii ni lazima apatiwe fedha za maendeleo ili rasilimali hizo ziweze kujulikana zilipo, na kiasi kilichopo na pia thamani yake ijulikane na hivyo mfanyabiashara apate stahili yake na Serikali ipate stahili yake.

Mheshimiwa Spika, kutokuwezeshwa kwa wakala huyu maana yake ni kwamba tutaendelea kuona kwamba rasilimali za madini tulizonazo hazitusaidii kama nchi.

16. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ina wajibu muhimu wa kusimamia maendeleo endelevu ya rasilimali za nishati na madini ili kuwezesha maendeleo ya nchi na kuboresha maisha ya wananchi. Hata hivyo mpaka sasa haijawezesha upatikanaji wa nishati kwa bei nafuu wala haijahakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, hali hii inahitaji mabadiliko makubwa ya kimfumo na kufungua ukurasa mpya kama taifa kuepusha laana ya rasilimali. Nyenzo mojawapo ya mabadiliko ya kimfumo ni katiba ya wananchi na si katiba inayopendekezwa. Katiba mpya itaweka misingi bora ya nchi na wananchi kunufaika na rasilimali badala ya sheria dhaifu, mikataba mibovu na mianya ya ufisadi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha,

.....
John John Mnyika (Mb)
Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-
Wizara ya Nishati na Madini
19.05.2016

SPIKA: Sasa Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na uchangiaji. Tutapata wachache asubuhi hii lakini tutaendelea jioni na kesho pia. Mheshimiwa David Silinde uwe mchangiaji wa kwanza.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, Asante sana kwa kunipatia fursa hii ya mimi kuwa mchangiaji wa kwanza katika hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Momba na niwashukuru sana vilevile Mahakama Kuu kwa kuhalalisha Ubunge wangu siku ya tarehe 16, baada ya Mgombea wa Chama cha Mapinduzi kunikatia rufaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa hayo yote. Sasa niwambie wananchi kwamba tumerudi kwa ajili ya kazi moja tu kuhakikisha Momba inaendelea mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimesoma Hotuba ya Waziri kidogo ilichelewa, lakini nimepitia Hotuba ya Kamati pamoja na Hotuba ya Kambi ya Upinzani. Kwa mara ya kwanza katika Bunge hili niseme kabisa kwamba Kamati ya Nishati na Madini imejitahidi sana kutoa taarifa inayoelezea matatizo yaliyopo kwenye Sekta nzima ya Nishati pamoja na Madini, niwapongeza sana Kamati ya Nishati na Madini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukizungumza kila mara na Serikali ya Awamu ya Tano imekuja na kaulimbiu ikisema itakapoingia madarakani itapitia mikataba yote na makampuni yote yanayochimba na kuzalisha madini ndani ya nchi yetu, lakini mpaka sasa, hatujasikia mapitio ya mkataba kwenye kampuni yoyote. Hatujasikia na ni kauli ambayo ilitoka kwa Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli. Sasa kwa nini tunaliulizia hili jambo kwa sababu sekta ya madini ndiyo sekta ambayo sisi kama Taifa tumeibiwa sana! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, makampuni haya tangu yameanza kuzalisha madini hayajawahi kupata faida na haya yamekuwa yakizungumzwa ndani ya Bunge tangu Mabunge yaliyopita. Bunge la Tisa, la Kumi mpaka hili la Kumi na Moja tunajadili mambo yaleyale na mifano midogo tunayo. Tuna mfano wa Mgodini unaozalisha Almasi wa *Williamson Diamond* pale Shinyanga, umeanza kuzalisha mwaka 1940, leo tunapojadili ni miaka 76, lakini mpaka leo hawajawahi kupata faida, hawajasitisha uchimbaji wa madini na ukiangalia kwenye malipo yao ya kodi ndani ya hili Taifa hakuna chochote kinachofanyika. Haya ndiyo tunayosema, kile kilichoahidiwa na Serikali ya Awamu ya Tano cha kupitia mikataba, ndiyo kilitakiwa kifanyike sasa, kwa sababu haiwezekeni watu miaka 76 hawapati faida, lakini hawaondoki, wako pale pale. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa haya ndiyo maswali ambayo tulikuwa tunahitaji kupata majibu kutoka kwenye Wizara ya Nishati na Madini ambayo iko chini ya Mheshimiwa Waziri Sospeter Muhongo. Kwa hiyo tunahitaji hayo majibu. Tunahitaji majibu juu ya kampuni ya ACACIA ambayo hata Kamati imeeleza, Mahakama ya Usuluhishi imewaambia walipe kodi ya mapato karibu bilioni 89 ambazo walikuwa wamezikwepa kwa kipindi cha miaka minne, lakini mpaka leo kampuni hiyo hiyo inashindwa kulipa na Serikali haijasema, haijatoa kauli na haijachukua hatua yoyote. Sasa haya ndiyo mambo tunayosema, huwezi kuita hapa kazi tu, wakati unashindwa kusimamia makampuni ya namna hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya tunataka kazi iendane na kukamata hawa watu, walipe hizo bilioni 89 ambazo zimeamuriwa na Mahakama ya Usuluhishi kuhakikisha kwamba Taifa letu linapata hiyo faida. Kwa hiyo, nategemea Mheshimiwa Waziri Sospeter Muhongo atatupatia majibu kwenye majumuisho yake hizi bilioni 89 zilizoamriwa kulipwa kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nini mpaka sasa hivi, Serikali inashindwa kuzipata fedha hizi?

Mheshimiwa Spika, lakini, kuna mambo mengine ambayo tulikuwa tumeyajadili. Kwenye Mabunge yaliyopita Bunge liliamuru kwamba makampuni ya uzalishaji wa madini yajisajili kwenye soko la hisa la ndani ya nchi, siyo yafanye *cross listing*. Unajua, watu wanashindwa kuelewa haya makampuni yamejisajili London yamejisajili kwenye masoko ya nje ambako sisi Watanzania wa ndani hatuwezi kupata taarifa juu ya mwenendo wa haya makampuni, huku ndani tunapata tu taarifa za kawaida na kinachotokea nini? Kule wanapata faida, lakini kwenye taarifa za ndani za Taifa letu hakuna faida yoyote inayoonekana juu ya makampuni haya yanayochimba madini katika hili Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunahitaji kupewa majibu juu ya maazimio ya Bunge, juu ya kauli ya Rais ambayo ndiyo ahadi kwa Watanzania lini mtapitia mikataba ya makampuni yote yanayozalisha madini nchini. Kwa sababu madini yaliyoko ndani ya nchini yetu yanakwisha wala siyo kwamba yatakaa milele, ni *Non Renewable Resources* na kila mmoja anajua hiki kitu. Kwa hiyo, sasa hatutaki kupata mashimo kama yalivyo kwenye *Resolute* kama tunavyoona kule Tulawaka kwamba Taifa limebakiwa tu na mashimo ambayo sisi kama Taifa hatukupata faida ambayo tulikuwa tunatarajia kutoka na mikataba ambayo sisi tulikuwa tumeingia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo tungependa kupata ufafanuzi, Rais wakati anazindua mradi wa pili, kule Kinyerezi aliahidi kwamba atahakikisha mkataba wa *IPTL* wa kulipa *capacity charge*, yeye katika Serikali yake, huo mkataba anauvunja na hatalipa ameyasema hayo Mheshimiwa Rais. Sasa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaliona hili kwamba mpaka sasa ni

hatua gani mmechukua kuhakikisha haya Makampuni hayaendelee kulipwa *capacity charge* yawe yanazalisha umeme, yasiwe yanazalisha umeme? Hebu fikiri, milioni 300 za Kitanzania zinapotea kila siku kampuni izalishe umeme ama isizalishe, hii hasara hatuwezi kuendelea kuwa nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, makampuni haya yalikuja kwa lengo moja tu, kuzalisha umeme wa dharura, lakini mpaka sasa hivi siyo kwamba tuna udharura, udharura haupo sana kama kipindi ambacho kilikuwepo. Sasa hivi tuna uhakika na kile tunachokifanya, lakini mpaka leo haya mambo yanaendelea, sasa tunataka tuambie, maana yake tunajua kauli ya Rais ndiyo kauli ya Serikali, ndiyo msimamo wa wananchi, kwamba tunataka kuona makampuni yote yanafungiwa na maazimio yote ya Bunge yanafuatwa na yanapatiwa mkakati wake.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambolo ningependa kulizungumzia, Kamati vile vile imelisema na mimi nilitaka niliseme. Kampuni ya Dangote ilikuja kwa lengo zuri kabisa na naamini bado lengo ni zuri. Imekuja kwa lengo la kuzalisha saruji ndani ya nchi yetu, lakini mpaka leo tunapojadili kampuni ile haitatumia gesi ya nchini, haitumii na wala haitatumia gesi kwa sababu mitambo yake ile imetengenezwa kwa ajili ya kutumia makaa ya mawe. Lakini cha ajabu ambalo Watanzania hawajui, makaa ya mawe yale sio yanayotoka Liganga na Mchuchuma kule. Makaa ya mawe yale yatatoka Msumbiji ambako ni karibu kabisa na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, sasa unajiuliza haya maswali kila siku kwamba tunazalisha gesi na gesi ipo kwa wingi lakini tunashindwa kwa sababu moja tu, tumeambiwa wameshindwa kukubaliana juu ya bei halisi, kwamba Dangote anataka senti kadhaa tu. Tunaamini sasa gesi ili iwe faida kwa Taifa, gesi hii ndiyo itumike kwenda kwenye Kampuni ya Dangote, Serikali ipate faida kutokana na mauzo ya gesi ili sisi kama wananchi tuweze kujitegemea huko tunakokwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, miradi ya REA. Waziri hapa amesema kumeongezeka kwa bajeti, nakubaliana, kwamba imetoka karibu bilioni 357 mpaka mnakwenda kwenye 500. Hata hivyo, changamoto ni nini, mwaka jana, mwaka 2015/2016, tulitenga karibu bilioni 357 kwenye Bunge hili hili la bajeti, lakini mpaka sasa hivi tunapojadili kwenye bajeti ile fedha zilizotoka hazijafika hata asilimia 70. Sasa leo unaleta tena 534, of course umeongea vizuri kwamba hapa hakuna cha MCC, its okay, lakini hela hizi zitafika kwa asilimia 100? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Momba kule mlipoleka miradi ya umeme tukaahidi Halmashauri ya Momba itapata umeme wa REA kufikia mwaka jana 2015 Juni, lakini mpaka leo tunapojadili, mwaka mzima, Momba hakuna umeme. Nguzo zipo pale zimesimama, miradi ya REA haiendelei. Sasa hii changamoto tusiwadanganye Watanzania kwa kutaja viwango vya fedha, tunataka utekelezaji unaoendana kwa vitendo, tuambiwe hela inayokwenda kufanya kazi, kwa hiyo hicho ndicho tunachokitaka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, unaweza kusema hapa REA tumetenga trilioni moja, *its okay*, trilioni moja itafikiwa mwisho wa mwaka? Je hizo Bilioni 357 za mwaka 2015/2016 zimefika kwa asilimia 100? Mheshimiwa Muhongo kwenye *facts* za *data* najua yeye ni mzuri sana, lakini ngoma ipo kwenye utekelezaji, twende tufanye utekelezaji, ndiyo Taifa tunachotaka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kwenye *issue* ya vinasaba, tumekuwa tukijadili kila mwaka. Vinasaba vilikuwa vimeletwa kwa kazi moja tu, lengo ni kupunguza uchakachuaji...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa...

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Silinde, umeunga mkono hoja? Haya, tumemaliza CHADEMA sasa twende CUF, Mheshimiwa Maftaha, Mbunge wa Mtwara Mjini, halafu tutahamia CCM sasa. (Kicheko)

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Nishati na Madini. Kabla sijaanza kutoa salamu za Wanamtwara na maagizo ya Wanamtwara kwa Wizara hii, naomba kwanza nitoe masikitiko yangu kwa kiasi kikubwa sana. Mheshimiwa Waziri hapa wakati anawasilisha hotuba yake kazungumzia mambo mengi yanayohusu gesi, mambo mengi yanayohusu petroli na mambo mengi yanayohusu mafuta ambayo ndiyo chachu ya uchumi wetu wa sasa hivi hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, masikitiko yangu, nilikuwa napitia gazeti leo hii, gazeiti la *The Citizen*, CAG ameeleza masikitiko yake makubwa kabisa na naomba ninukuu, halafu nimuulize Mheshimiwa Waziri swali langu. Amesema hivi:

"It was unfortunate that NAOT does not have a single expert in auditing accounts related to oil and gas despite trillions of cubic feet of fossil fuel reserves having been discovered in Tanzania".

Mheshimiwa Spika, gazeti la leo, kwamba anasikitika na anaeleza, analiambia Taifa hili kwamba pamoja na umuhimu wa gesi na mafuta tuliokuwa nayo na wingi wake wote, lakini hana mamlaka ya kwenda kukagua, sasa sijui tatizo ni nini? Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa majibu atueleze kwa nini *account* zile zinazotokana na visima vya mafuta na gesi havikaguliwi na CAG.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuzungumzia suala zima hili la umeme vijijini. Ile Mikoa ya Kusini tuna bomba la gesi na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alizungumza katika mihadhara yake mingi sana kwamba Wanamtwara na Lindi watakuwa wananufaika na gesi kupitia mle lilimopita bomba la gesi kupitia Sekta ya Umeme.

Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa ninavyozungumza ule unaitwa mkuza wa bomba la gesi ambalo Serikali imekuwa inaahidi kupitia miradi yake ya REA Awamu ya Kwanza, REA Awamu ya pili, mpaka hivi sasa tunakwenda kwenye REA Awamu ya tatu bado vijiji vile vyote havijapata umeme huu pamoja na ahadi nyingi na majigambo makubwa ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri ya kwamba, ni lini sasa atahakikisha kwamba maeneo yote yanayopita bomba la gesi, mkuza wa gesi, anatekeleza ahadi yake ya kupeleka umeme? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili la wananchi wa mikoa ya kusini kunufaika na gesi. Hata hivyo, nitoe masikitiko yangu makubwa sana, kwamba tumekuwa tunazungumza sana, tumekuwa tukiahidi sana, tukieleza sana, kuliko kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia mpango wa TPDC wakati tuko kwenye Kamati, lakini juzi taarifa yao tumekuwa tunapitia. Kuna mkakati ambao Serikali wameweka wa kuhakikisha kwamba gesi inayotoka mikoa ya kusini, Mtwara na Lindi inafika Dar es Salaam, baadaye itapelekwa mikoa mingine ya kaskazini kwa mfano Tanga, Mwanza na maeneo mengine. Katika mkakati ule pia wameeleza kwamba hii gesi itakuwa inapelekwa kwa ajili ya matumizi ya majumbani kuanzia Dar es Salaam, lakini cha ajabu ukipitia taarifa ile ya TPDC mikoa ya kusini, Mtwara na Lindi haipo.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja na majibu yake atueleze wananchi wa Mtwara na Lindi mkakati ukoje. Kwa sababu niliuliza swali hili wakati tunasikiliza taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini tulivyowaita kwenye Kamati yetu hii ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na wakasema kwamba watakwenda kulishughulikia. Naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba asije akawa anazungumza tu wakati kwenye maandishi kule hakuna na Wanamtwara na Wanalindi pia wanasubiri majibu stahiki kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia suala zima ambalo Mheshimiwa Silinde ameligusia hapa, la kuwapa wawekezaji ambao wapo mikoa hii ya kusini nishati hii ya gesi waweze kutumia kama nishati. Leo hii tuna kiwanda ambacho kilitarajiwa kujengwa Mtwara maeneo ya Msangamkuu, ni kwa miaka minne hivi sasa yule mwekezaji anaomba apewe gesi ili aweze kujenga kiwanda cha saruji, mpaka leo tunavyozungumza ni danadana tu kwenye Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, niombe sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba wawekezaji hawa ambao wana nia ya kuwekeza Mikoa ya Kusini wanapewa nishati hii ya gesi ili waweze kuondoa umaskini ambao wananchi wa mikoa hii ya kusini umekuwa unatutawala kwa muda mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi, Mheshimiwa Silinde kazungumza, mwekezaji Aliko Dangote, kwa muda mrefu sana amekuwa akiomba gesi ili aweze kuitumia kama nishati. Mheshimiwa Silinde kazungumza kwamba ananunua makaa ya mawe kutoka Msumbiji, sio Msumbiji Mheshimiwa Silinde, ananunua makaa ya mawe kutoka *South Africa*. Meli inakuja Mtwara ku-gati kutoka *South Africa* ambayo mwekezaji huyu Aliko Dangote anatumia kama nishati wakati Mtwara tuna gesi iko kedekede, *cubic meter* za kutosha, kwa nini asipewe hizi gesi sambamba na kwamba yuko tayari kuuziwa, lakini Wizara mpaka leo inaleta danadana? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, wananchi wa Mtwara na Lindi waliandamana kwa kiasi kikubwa sana wakidai manufaa ya gesi, kwamba kwa namna gani hii gesi itaanza kuwanufaisha wananchi wa mikoa ile. Na madai yetu yale yalipotoshwa sana, watu walifikia wakati, wengine viongozi kabisa wa Kitaifa wakiwabeza wananchi wa kusini kwamba wao wanahitaji kutumia gesi peke yao. Madai yetu yalikuwa ni kwamba gesi inayotoka mikoa hii, kwa sababu inaanzia pale, kwanza tunufaike kwa kupata mrabaha. Nimepitia na nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, wakati anawasilisha sijaona hata sehemu moja na sijamsikia anasema kwamba mrabaha kiasi gani utabakizwa Mtwara na mikoa ile ya kusini ya Mtwara na Lindi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini cha ajabu kabisa kule kwenyewe inakotoka hii gesi, Msimbati, hata barabara ya kufika Msimbati ni kizungumkuti. Kwa nini Wizara na Serikali isitenge bajeti ya kujenga angalau barabara ile kiwango cha lami kutoka Mtwara Mjini mpaka kule Msimbati? Wananchi wa kusini wakidai haki hizi mnawapiga mabomu, mnatuletea Wanajeshi na kwamba sisi hatuipendi Serikali. Tunachosema ni kwamba, Serikali ihakikishe kwamba manufaa yanayotokana na gesi hii na sisi wananchi wa kusini tuweze kunufaika nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, upotoshwaji unaofanywa wa kwamba tunataka tuitumie gesi peke yetu si kweli. Nazungumza haya kwa sababu tuna ushahidi wa kutosha sana, tuna ushahidi wa kutosha. Sisi wote ni mashahidi, kwa kiasi kikubwa Korosho inazalishwa Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani, lakini korosho ile kwa taarifa za mwaka jana na miaka mingi mfululizo limekuwa ni zao ambalo linaingizia Taifa pesa nyingi sana. Mwaka jana, 2014/2015 limekuwa ni zao la pili, lakini zile pesa zinazokusanywa na mapato ya korosho zote zinapelekwa Hazina zinanufaisha Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, tunachosema Wanakusini, tunachosema Wanamtwara na Lindi ni kwamba tunufaike na fursa za ajira na isiwe Serikali na Wizara inaondoa fursa hizi. Kwa sababu unapomnyima mwekezaji huyu kutumia gesi, kwa mfano, Aliko Dangote akiagiza makaa yake ya mawe kutoka *South Africa* anakodi meli, gharama zinakuwa ni kubwa, mwisho wa siku simenti inakuwa bei mbaya. Tunaomba sana wananchi wa Mtwara na Lindi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la ajabu sana, Serikali hii imekuwa ni *sharp* sana katika kuondoa rasilimali za kimaendeleo Mikoa ya Kusini kuliko kupeleka kwingine. Nimekuwa nazungumza hili kwa muda mrefu sana. Bomba la gesi limejengwa kwa miezi 18 tu. Kwa miezi 18 pesa zilizotumika zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni mia mbili kama na hamsini na tano, lakini tunavyosema kwamba, tunahitaji maendeleo yaletwe kusini yanachukua muda mrefu sana. Suala la kufanya *negotiation* ya mkataba tu kwamba huyu mwekezaji wa Kiwanda cha Mbolea Mtwara, Dangote na yeye mwekezaji wa simenti inachukua muda mrefu, kwa nini? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka haya maswali yangu yaweze kupatiwa majibu. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Maftaha. Ulipokuwa unaongea nikawa najiuliza, kumbe ndiyo maana Murad hayupo hapa! (Makofi)

Mheshimiwa Ally Keissy, atafuatiwa na Mheshimiwa Shabiby.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani za dhati kwa kunipa nafasi. Namshukuru sana Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kumteua Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo kuwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemari kuwa Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wote. (Makofi)

Ndugu zangu, hili Bunge tusifanye vichekesho au viigezo, tukumbuke Bunge la Tisa, sikuwa Mbunge, nilikuwa naangalia kwenye TV. Hapa Bungeni alikuwa rafiki yangu, kipenzi wangu, Waziri Mkuu anaitwa Edward Ngoyai Lowassa. Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa alijiuzulu kutokana na kashfa ya *Richmond*, hapa Bungeni. Cha ajabu jamaa wa pili hao hao wamemchukua kumpa tiketi agombee Urais awe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wanaona ajabu wakati si kweli kama Mheshimiwa Sospeter Muhongo alihusika na *Escrow Account* ila alisingiziwa kwa ufasadi wenu ninyi baadhi ya Wabunge, tunalijua hilo, lakini Mheshimiwa Edward Lowassa hapa alitolewa, alijiuzulu, lakini ninyi mkamkumbatia mkatembeza nchi nzima, je angekuwa Rais nchi hii ingekuaje? Ndugu zangu mnasahau matapishi yenu? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sipendi kuwakashifu ninyi rafiki zangu, lakini mnashika pabaya lazima tuwaambie ukweli, mnakuwa na akili ya kusahau kama vile kuku wa kizungu au samaki anakwenda kunasa kwenye nyavu. Leo siku hata tano haijapita unasahau unataka ripoti ya kumkashifu Mheshimiwa Sospeter Muhongo na Magufuli kumchagua kuwa Waziri wa Nishati na Madini, akupe wewe kuwa Waziri, wakati ninyi hapa mmemtembeza Lowassa nchi nzima na Bunge hilihili, nchi nzima walifahamu kwamba amejuzulu kutokana na kashfa ya *Richmond*, sasa si ajabu hii? Mnasahau... (Makofi)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Toa taarifa nitakujibu!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, Taarifa!

TAARIFA

SPIKA: Mheshimiwa Esther taarifa!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, napenda nimpe ndugu yangu Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy taarifa kwamba, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa alijiuzulu, *it's a collective responsibility*, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alijiuzulu, akaja akapewa tiketi ya Urais CCM na akachaguliwa kuwa Rais. Kwa hiyo, atafute hoja nyingine ajenge na sio ya Lowassa kujiuzulu. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Keissy endelea!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Hiyo ya Rais Mwinyi usizungumze, Rais Mwinyi alikuwa amelala nyumbani kwake...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge
waliongea bila utaratibu)*

MHE. ALLY K. MOHAMED: ...kule Magereza Shinyanga ni tofauti kabisa, wala hakuwa fisadi kama unavyofikiria wewe. Unamsingizia, Mwinyi hakuwa fisadi, Mwinyi alijiuzulu kutokana na kashfa ya Magereza Shinyanga, tofauti kabisa na rafiki yangu. Achana na ninyi, mlimtembeza mtu mnamjua kabisa mtu kajiuzulu kwa sababu ya rushwa, mkamtembeza nchi nzima, mtacheka wenyewe. Nimeshawapasha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Wizara ya Nishati na Madini, hasa REA, imesaidia kabisa katika vijiji vyetu kupata umeme. Ninachoiomba Serikali, iwapatie pesa ya miaka mitatu ya nyuma, REA walikuwa hawajapata pesa, wanadai karibu bilioni 272 maana yake Wakandarasi wako vijijini wanadai hizo pesa mpaka sasa. Haiwezekani hizi hela za mwaka huu, bajeti ya mwaka huu, bilioni zaidi ya 500 waanze kuzimegua ili kuwalipa Wakandarasi ambao wapo kazini, lazima tuhakikishe kabisa kwamba wanapewa hela zao za miaka mitatu ya nyuma, bilioni 272 Wakandarasi wakalipwe ili awamu ya pili ikamilike bila matatizo yoyote na hizi Milioni 540 zifanye kazi kwa vijiji vyote katika nchi hii kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nataka kuzungumzia alipoishia jirani yangu Mheshimiwa Silinde, kuhusu vinasaba. Vinasaba vimepitwa na wakati, vinasaba tumezungumza mara nyingi hapa, tuliruhusu vinasaba kwa sababu ya tofauti ya bei ya mafuta. Leo bei ya mafuta inalingana nchi nzima, nani atachakachua? Tuliamua hapa mafuta ya taa yapande bei ili wasiwe wanachakachua na mafuta ya taa kweli yameteremka hayaagizwi tena nchini kutokana na kwamba walikuwa wanachakachua kwa sababu bei ya mafuta ya taa, bei ya *diesel* vinalinganalingana.

Mheshimiwa Spika, tunaona uchungu, yule wa vinasaba kutokana na mafuta yanayoingia nchini kwa mwaka mzima zaidi ya lita bilioni mbili, anachukua zaidi ya bilioni tisa kwenye gharama ya vinasaba. Huyu wa vinasaba faida yake ni bilioni 14. Usimamizi wa EWURA unachukua zaidi ya bilioni 13.9, wakati ukaguzi wa mafuta TBS yenyewe inachukua bilioni 2.8 kwa ajili ya kudhibiti mafuta kama yana ubora. Sasa vinasaba vina faida gani?

Mheshimiwa Spika, halafu cha ajabu, EWURA hao hao wako chini ya Idara ya Maji wakati vipato vyao vyote vinachukuliwa katika Wizara ya Nishati na Madini. Wenyewe ukiwauliza hawahusiki kabisa moja kwa moja na Wizara ya Nishati na Madini, lakini mapato yao, kila kitu wanachukua kutoka Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilizungumza Bunge lililopita kabla halijaahirishwa. Mpaka hawa jamaa wakawa wanatumia pesa kwenda gym, wanalipa kila mfanyakazi wa EWURA Dola 400, akienda gym asiende gym. Wanajipangia mishahara wanavyotaka, wananyanyasa watu wanavyotaka. Hivi vinasaba vimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TRA kukagua magari ya mafuta, TRA wana vituo njiani (checkpoints) tatu au nne, lazima magari yapite, TRA ikague mafuta kama yameteremshwa njiani au hayajateremshwa njiani. Kama watumishi wa TRA ni wabovu wanagongesha mihuri, je hao EWURA ndiyo watakuwa waaminifu kama malaika? Ni kuongeza mzigo kwa walipakodi kupandisha bei ya mafuta bila sababu. Nashauri hizi pesa za EWURA ziende REA moja kwa moja kutatua matatizo ya umeme vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka mzima pamoja na usimamizi, EWURA wanachukua shilingi 18 na senti 85 kutoka kwenye gharama za vinasaba, halafu wanachukua shilingi sita kwa ajili ya usimamizi, jumla bilioni 42 . Hizi pesa zikienda REA kule zitasaidia kutatua matatizo ya umeme vijijini, kuwalipa Wakandarasi. Kwa hiyo, naomba Serikali irudie upya hivi vinasaba, iangalie kama vina umuhimu ama havina umuhimu. TRA ndio wasimamizi wa mafuta kama yanavuka mipaka au hayavuki mipaka.

Ndugu zangu na uchakachuai ulipitwa na wakati, tulikuwa tunachakachua kwa sababu mafuta ya taa yalikuwa chini kabisa, mia tano, mia sita, tumeongeza ile bei ili wananchi wapate umeme vijijini, sasa nashangaa bado wanaendelea na vinasaba ili kuumiza wananchi wetu na havina faida wakati huu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, hawa jamaa wa REA tuwape pesa kama inavyotakiwa. Hizi pesa ziende moja kwa moja REA zisipitie Hazina. Zikipitia Hazina zinakuwa na vigezo, miaka mitatu mfululizo, REA hawakupata hela kama inavyopangwa, miaka mitatu nimepiga hesabu hapa ni milioni 272, REA hawajapata hela. Wakandarasi wanadai kule vijijini, wanadai tozo kule vijijini, lakini sababu pesa ziko Hazina, hizi pesa zimeshatoka kabisa sasa kwa nini zisiende moja kwa moja REA ili REA wafanye kazi na tuwawajibishe kama hela hawajawapa wakandarasi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile naishauri Serikali, kwanza naishukuru sana kupunguza tozo ya umeme ili wananchi wetu wapate, lakini vilevile ndugu zangu wa mijini wamekaa wanaiba umeme, tatizo kubwa. Ni tatizo kubwa, haiwezekani mtu ana AC tatu, ana kiwanda hawafuatilii, Serikali kama wanashindwa REA peke yake kufuatilia TANESCO watafute JKT wapite nyumba kwa nyumba hasa mijini. Watu wa mijini wamekuwa wezi wakubwa wa umeme, wanaiba umeme mchana kutwa, Manzese wanasaga usiku wanaiba umeme,

viwanda vidogovidogo wanaiba umeme, wanaoumia ni watu wa kijijini ambao hawana utaalam wa kuiba umeme.

Mheshimiwa Spika, mpaka baadhi ya watu wakubwa Serikalini wanaiba umeme, mashule makubwa makubwa yanaiba umeme, mahoteli yanaiba umeme. Ndugu zangu hatuwezi kufika, tuibe umeme, tuibe na maji, halafu hapa tunakuja tunalalamika tunataka kila kitu wakati sisi wote tunasaidia wizi.

Mheshimiwa Spika, unakuta Mbunge anamwona mtu anaiba umeme, hatoi ripoti, bado anamsaidia, tuna kazi ya kuilaumu Serikali, hatuipigi vita kwa njia ya namna hiyo, tumsaidie Rais Magufuli kutumbua majipu hata katika wizi wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mkurugenzi wa TANESCO, Mkurugenzi wa REA, wanafanya kazi, inabidi tuwaunge mkono. Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo usisikie maneno ya majungu, mimi nilikuwa kwenye Kamati ya *Public Account Committee*, ni uzushi yule James Rugemalila alikuwa anadaiwa kodi, ndipo tuliamua alipe kodi; hana kashfa yoyote, kashfa kama mnayo nyie kwa majungu yenu hatoki na anakaa pale kwa niaba ya Serikali ya CCM. Ataendelea kufanya kazi na katika Mawaziri wachapakazi hakuna kama Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, hana siasa. Mnataka kwenda kwa vigezo vya rushwa, huyu hali rushwa, wala kashfa ya *ESCROW Account* hamkumwona hata kapewa kiroba cha hela waliopewa hela walitajwa humu yeye hahusiki.

Mnamsakama bure hamfanyi lolote, aliyemchagua Rais Magufuli kwa niaba ya Serikali ya CCM, kwa hiyo hawezi kubanduka atachapa kazi. Ngojeni na ninyi wananchi watawachagua na kutokana na uongo wenu wameshawagundua hamuwezi. Mmeshapigika huko nje mnaleta fitina za uongo hapa, hamkubaliki kwa *speed* ya Magufuli inayokwenda kama umeme. Kwa hiyo, Rais Magufuli *speed* yake hamuipati, shemeji zangu nawaambia ukweli, mliboronga kuchagua mtu aliyekataliwa na Bunge, akajiuzulu, mkamtembeza nchi nzima, sasa safari hii ndugu zangu kaeni chonjo mtapungua siku hadi siku. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mlichokoza wenyewe jamani, jamani taratibu tufike au siyo. Haya, ahsante sana Mheshimiwa Ally Keissy hayo ndiyo mawazo yake, msimlaumu wala msimshutumu. Mheshimiwa Ahmed Shabiby mchangiaji anayefuata na Mheshimiwa Stephen Masele ajiandae. *(Kicheko)*

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kunipa nafasi na mimi kuwa mmojawapo wa wachangiaji katika hotuba hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpungeze Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wetu Profesa Sospeter Muhongo pamoja na Naibu wake. Pamoja na kuwa ni mgeni lakini tunaona ana nia njema katika Wizara hii na Taifa hili. Vilevile nimpungeze Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na wote katika Wizara ya Nishati na Madini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitaanza na REA, cha kwanza nitapingana kidogo kuunga mkono juu ya hoja ya ndugu yangu Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy, kwamba REA wanafanya vizuri kwa sababu moja. REA katika mipango yao ya kugawa umeme vijijini wana upendeleo, hili liko wazi, kwa wale Wabunge waliopita, Bunge lililopita wameona, katika ile miradi ya awamu ya pili. Kuna baadhi ya wilaya na majimbo yana vijiji mpaka sitini; kwa mfano Majimbo ya Karagwe na Bunda.

Mheshimiwa Spika, ukija Jimbo la Gairo lina vijiji vinne na havijawaka umeme hata kimoja. Karagwe kuna vijiji 110, ukija Bahi kuna vijiji viwili, hapa Dodoma hakijawaka hata kimoja, sasa nataka kujua, hawa REA wanafuata vigezo gani? Wanataka sisi Wabunge tukashinde ofisini pale kwa Meneja au kwa ndugu yangu yule Msofe tuanze kuomba umeme, tusifanye kazi nyingine? Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ameliona hili ndiyo maana safari hii hata vijiji hajavitaja humu kwa sababu nafikiri nia yake labda ni kwenda kugawa keki hii kwa kila mwananchi na kila Wilaya au kila Jimbo wapate sawa, wasirudie yale. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wameandika Gairo vijiji 27 ndani ya kitabu cha Wizara, nimekwenda kule na Waziri aliyepita, Mheshimiwa Charles John Mwijage, nimekwenda na Mheshimiwa Simbachawene, hawaelewi, wala watu wa REA hawajui wakati wapo Wizara ya Nishati wanaishia vijiji vinne. Kwa kweli mwaka huu ndio utakuwa wa mwisho wangu kuunga mkono hii habari ya REA.

Mheshimiwa Spika, REA hawana maana kabisa katika ugawaji wa umeme vijijini. Hata kama pesa hawapewi basi tupewe hata maneno kwamba utawekewa kijiji hiki, kijiji hiki, tubaki tunadai, sasa hata pa kudai hakuna. REA ni tatizo kubwa na ninyi Wabunge wageni mtaliona tatizo hilo, bado hamjaliona. Mwaka huu nasubiri kwa sababu nimeangalia sana kwenye hotuba ya Waziri hivi vijiji sijaviona humu mwaka huu tumetajiwa tu idadi ya pesa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, mimi ni mfanyabiashara na katika biashara zangu nafanya biashara nyingi mojawapo ikiwa ya mafuta. Na-declare interest na humu ndani kuna watu wengi kuna Walimu, wakulima, wafugaji, kila mtu ana fani yake. Kwa hiyo nisipozungumzia habari ya biashara ya mafuta wakati najua na na-declare interest nitakuwa sijajitendea haki. Kwa wale waliopita Bunge lililopita wanajua kabisa vituko vya EWURA,

wanavifahamu, na ndiyo maana hata Mbunge, Mheshimiwa David Silinde nafikiri alikuwa anataka kuizungumzia lakini muda ulikwisha.

Mheshimiwa Spika, kwanza lazima tukumbuke hata neno chakachua aliyelileta Bungeni na Tanzania nzima ni mimi hapa wakati nazungumzia habari ya kuchakachua mafuta ya taa, *diesel* na petrol ndiyo hilo likaingia chakachua matokeo, sijui chakachua kitu gani, chakachua kitu gani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, EWURA ilianzishwa wakati ule mafuta ya taa yalikuwa hayana kodi, petroli na *diesel* zilikuwa na kodi ziliyazidi mafuta ya taa karibu shilingi mia sita. Kwa hiyo, wafanyabiashara wengi wakawa wanachukua mafuta ya taa wanayafanya malighafi wanachanganya na *diesel* au na petroli kwa ajili ya kujipatia kipato. Tukaanzisha mfumo wa kuweka vinasaba kwenye mafuta ili mtu akichanganya mafuta ya taa na petroli au na *diesel* anaona kwamba amechanganya na mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, baadaye EWURA walishindwa kabisa kuondoa ule uchakachuaaji kwa vinasaba vyao kwa ajili ya rushwa iliyoko EWURA. Kwa hiyo, Bunge hili likaamua kupandisha mafuta ya taa kwa kuweka kodi kwa sababu EWURA walishindwa kufanya kazi yao. Lakini cha ajabu EWURA wakahamia sasa wakawa wanaendelea kuweka vinasaba kwenye petroli na *diesel*. Sasa wakija kwenye *petrol station* wanakwambia vinasaba vimepungua, kwa hiyo, umeshusha mafuta yanakwenda mgodini au yanakwenda *transit*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini vinasaba wanawekaje? ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge nataka niwaeleze. Mtu yuko Dodoma ananunua mafuta anapiga simu BP, nataka kununua mafuta, BP anamwambia bei yangu hii, anamwambia nimekubali, anamwambia weka hela Dodoma kwenye benki nitazona kwa *internet* hapa Dar es Salaam. Unaweka hela Dodoma benki mtu wa BP anakwambia lete gari, nampigia simu nikiwa Dodoma *Transporter* peleka gari yangu BP kanipakilie mafuta.

Mheshimiwa Spika, *Transporter* anamtuma dereva wake nenda kapakie mafuta labda ya Shabiby BP, dereva akifika pale yuko mtu aliyepewa tenda na EWURA wanaitwa GFI, mtu wa GFI anakuja anamwambia dereva, wakati huo dereva hana elimu yoyote wala hajui vinasaba au anawekewa mkojo wa punda au anawekewa *juice*, anaambiwa umeona hii hivi ndiyo vinasaba hivi usinuse, nakuwekea hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kumbuka vile vinasaba havibadilishi mafuta rangi wala nini, unaletewa Dodoma. Siku ya pili anakuja mtu na gari la EWURA na havionekani kwa macho ameshaambiwa na yule mwenzie kwamba kule nilikoweka nimeweka kidogo nenda kapime. Anakuja anapima kwako, kwanza anakwambia kabisa nipe milioni tatu kama hutaki napima, usipotoa hiyo pesa

na sisi Wabunge wabishi kutoa rushwa anapima, anakwambia vinasaba vipo lakini vimepungua kidogo wakati huvioni kwa macho, hujahusishwa kwenye kuviweka, wala havikuhusu; sasa huu ni wizi.

Mheshimiwa Spika, nikwambie kwa Tanzania kwa mwezi inaingiza *meter tones* laki mbili na elfu hamsini, sawasawa na lita mia tatu na vinasaba mtu wa mwisho anayeweka mwenye gari anachajiwa shilingi kumi na mbili na senti themanini na nane, kila lita moja unayoweka wewe mafuta. Kwa mwezi yule aliyepewa tenda analipwa bilioni tatu na milioni mia nane, kwa mwaka bilioni arobaini na sita, umenielewa.

Mheshimiwa Spika, hii kampuni ya *GFI* imepewa tenda bila kutangazwa kwenye magazeti na mpaka leo tenda hiyo inaendelea. Tafuteni *GFI* imepewa wapi hiyo tenda, haijawahi kutangazwa na imepewa tenda mpaka leo hii. Tusizungumze hapa tunasema sijui hii kampuni ya nani, hii kampuni ni ya wao wenyewe na ukimchukua leo Kalamagozi wa *EWURA* na yule Kaguo utaona anavyojieleza, wanajieleza kuliko hata waandishi wa habari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya magazeti hayawezi kuandika *EWURA* vibaya, baadhi yao, yanayopewa matangazo, kwa sababu ukiandika vibaya tangazo hupewi. Ukiandika vibaya habari ya *EWURA*, hupati tangazo. Hivi leo bilioni arobaini na sita hii ukiigawanya hata kama tununue madawati tu tunapata madawati laki saba.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii mpaka nipate jibu sahihi la hawa watu wa *EWURA*. Ahsante sana. (Makofi)

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambayo anafanya ya kujenga nidhamu ya nchi yetu na kurejesha nidhamu ya Utumishi wa Umma na nidhamu ya wananchi kutii sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo kwa kazi nzuri ambayo anaifanya ya kusukuma mbele Sekta ya Nishati na Madini nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wote sisi ni mashahidi, Wizara hii ina changamoto nyingi sana kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamezieleza, lakini wizara hii haihitaji malaika wa kwenda kufanya kazi pale. Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo ameonesha ubora na anastahili kupewa *support*, anastahili kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge na tutakuwa tumelitendea haki Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimefanya kazi na Mheshimiwa Muhongo, namwelewa, tunapozungumzia moja ya Mawaziri makini nchi hii ni mmojawapo. Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Leo Mheshimiwa Rais ameeleza wazi anataka Tanzania iwe nchi ya viwanda, Mheshimiwa Rais ameeleza wazi, anataka asilimia 30 ya ajira za vijana zitokane na viwanda. Sasa Wizara hii na Hotuba ya Mheshimiwa Muhongo ndiyo ambayo itatupeleka kwenye kuwa na Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, leo Waziri wa Viwanda na Biashara hata aseme ataleta viwanda elfu ngapi, kama hakuna nishati ya umeme ni sawa na kazi bure na Waziri ameonyesha kwa vitendo kwa kutenga asilimia 94 ya bajeti yake kwenye maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na niseme tu kwamba kwenye REA kila mtu anafahamu kazi inayofanywa ni nzuri, lakini changamoto zipo, najua ataendelea kuzitatua. Nimpongeze pia kwa kuteremsha gharama za umeme, Watanzania wengi wanalia gharama za umeme ziko juu na nakumbuka aliahidi kwamba atalifanyia kazi atapunguza gharama za umeme leo ametekeleza.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwenye viwanda nchini moja ya changamoto kubwa ambayo wanahangaika nayo ni *bill* zisizoeleweka ambazo wanapelekewa na TANESCO kwenye maeneo husika. Ziko *charge* nyingi ambazo viwanda vinapelekewa ambazo zinakatisha tamaa uwekezaji wa viwanda vilivyopo na hata hivyo vinavyokuja. Nina hakika kama bili hizi zitaendelea kuwa hivyo, basi kutakuwa na changamoto kubwa ya bidhaa zinazozalishwa nchini kushindana na bidhaa za masoko za kutoka nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliahidi kwa Watanzania kwamba atafanya mahesabu na atahakikisha hata nguzo za umeme itafika mahali atatutangazia atazigawa bure, tunasubiri ahadi hiyo na nina uhakika anaweza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo Tanzania, Mheshimiwa ameeleza kwenye hotuba yake, inazalisha megawati 1,400. Ili tuweze kuwa nchi kweli ya kipato cha kati, ili tuweze kuwa Taifa la Viwanda ni lazima tuongeze *speed* ya uzalishaji wa umeme. *Speed* ya uzalishaji wa umeme ni kuwekeza kwenye miradi ya uzalishaji hasa kupitia gesi asilia. Leo Tanzania tunazalisha gesi yetu wenyewe na Mungu ametusaidia, tusingekuwa na hii gesi na tusingekuwa na uimara wa Mheshimiwa Profesa Muhongo kusimamia bomba la gesi likamilike kwa kutegemea mvua haya malengo yote tusingeweza kuyafikia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie, Taifa la Uturuki leo linaongoza kwa uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwenye soko la Ulaya, ni kwa sababu wana umeme wa kutosha na hata hiyo gesi yenyewe hawana, wanaagiza kutoka kwenye Mataifa yenye gesi. Uturuki peke yake inazalisha *megawatt* 60,000 za umeme. Afrika Kusini inazalisha megawati 80,000 za umeme. Unapokwenda kule kama Waziri unamwambia mwekezaji kama *Toyota* njoo uwekeze kiwanda cha *ku-assemble* magari Tanzania atakuomba megawati 5,000 peke yake, huna, safari yako haina maana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Bunge hili litatenda haki kwa Watanzania endapo tutafikiri kimkakati namna gani Tanzania itazalisha umeme wa kutosha ili kuweza kukidhi mahitaji ya majumbani lakini pia tuweze kukidhi maendeleo ya viwanda tunayoyazungumza.

Mheshimiwa Spika, umeme tulionao huu vikiunganishwa migodi mitano tu Tanzania tutaingia kwenye mgao. Leo iko migodi hapa inazalisha yenyewe umeme. Tukiunganisha viwanda vikubwa tutaingia kwenye mgao. Kwa hiyo, bado tuna kazi ya kufanya, bado tuna kazi ya kumpa ushirikiano Waziri kwa jitihada ambazo amezionyesha kwenye bajeti hii ili tuweze kufikia hayo malengo tunayoyataka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa leo Tanzania tunazalisha kupitia *TANESCO*, malengo yetu kama nilivyosikia kwenye hotuba tunatakiwa tuwe na *megawatt* 2,500, tunatakiwa tuwe na *megawatt* 10,000 ifikapo 2025. Tutafikishaje *megawatt* 10,000 kama hatuvutii uwekezaji binafsi kuja kuwekeza katika Sekta ya Umeme? Serikali peke yake kuzalisha *megawatt* 100 za umeme ni zaidi ya Dola za Marekani milioni mia moja na! Tukitaka *megawatt* 10,000 leo tunahitaji zaidi ya dola bilioni 10 za Marekani labda ni bajeti yetu hii ya miaka 10 ijayo tusifanye jambo lingine lolote. Kwa hiyo, lazima Serikali tuwe na mikakati ya kuhakikisha kwamba tunawekeza katika umeme sawa, lakini tuvutie pia sekta binafsi kuwekeza katika miradi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwenye Sekta ya Madini, zipo jitihada kubwa Wizara inafanya, niwapongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuendeleza jitihada za kuwainua wachimbaji wadogo Tanzania, nimpongeze Naibu Waziri kwa kazi kubwa ya kusuluhisha migogoro ya Nyamongo, lakini bado ziko changamoto ambazo tunatakiwa kuzishughulikia na bado katika uwekezaji mkubwa pia tunahitaji kuwa na migodi mipya.

Mheshimiwa Spika, tulipitisha miaka miwili iliyopita hapa sheria inayotoza kodi kwenye vifaa vya utafiti. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri ni mjiolojia bingwa duniani, tunapoweka sheria hizi za fedha za kutoza kodi kwenye vifaa vya utafiti ni sawasawa unasema tunataka kilimo cha kisasa halafu tunakwenda kuweka kodi kwenye matrekta, tunakwenda kuweka kodi kwenye mbegu.

Mheshimiwa Spika, kwenye uzalishaji wa migodi mipya haiwezi kutokea migodi mipya Tanzania endapo utafiti utakufa, endapo makampuni yanayofanya utafiti yatapunguza bajeti ya kufanya utafiti. Mheshimiwa Waziri naomba hili alifanyie kazi tupitie upya hizi sheria hasa kwenye eneo hili la utafiti ili kuweka unafuu wa utafiti na hatimaye nchi yetu iweze kupata viwanda vipya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuiwezesha Tanzania kupata mradi mkubwa wa kujenga bomba la mafuta kutoka Uganda. Nafahamu jitihada zako, nafahamu jitihada za Serikali. Miradi hii itasaidia sana kukuza uchumi wa Taifa letu. Nimwombe aendeleo na jitihada, natambua Uganda imetuomba Tanzania tupeleke bomba la gesi, natambua Kenya tume-sign makubaliano nao ya kuwauzia megawatt 1,000. Leo wapo Watanzania wanajiuliza kwa nini shilingi haina nguvu? Wachumi wanasema unapoingiza zaidi kuliko kupeleka nje zaidi maana yake unadhoofisha shilingi yetu. Tukiweza kuuza megawatt 1,000 za umeme Kenya tutaingiza mapato ya kigeni mengi ambayo yatasaidia hata kuimarisha shilingi yetu.

Mheshimiwa Spika, miaka mingi tangu uhuru tumetegemea mazao ya mashambani; pamba, tumbaku, madini kidogo bei imeshuka, uzalishaji umeshuka; lakini tuna bidhaa, tuna zao jipya la gesi ambayo tunaweza tukazalisha megawati 1,000 ambazo Kenya wanazihitaji na tuka- export megawatt 1,000 tukapata mapato mengi ya kigeni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Massele. Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji jioni kadri orodha zetu zilivyoletwa hapa na Wanadhimu wa Vyama, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mwendelee tu kujiandaa. Kwa upande wa CUF, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atakuwa miongoni mwa walio mwanzo, kwa upande wa CHADEMA, Mheshimiwa

Salome Makamba atakuwa miongoni mwa walio mwanzo mwazo, kwa upande wa CCM, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Suleiman Saddiq na wengine watafuatia. Kuanzia saa kumi kamili nitaomba kila ambaye yumo kwenye orodha awepo kwa wakati.

Mheshimiwa Massele aliyemaliza kuzungumza sasa hivi ambaye ni Katibu wa Wabunge wote vijana anaomba Kamati ya Uongozi ya Caucus yao ya vijana wakutane pale ukumbi 227, Kamati ya Utendaji ya Wabunge vijana ukumbi 227, mkutane mara baada ya mkutano huu.

Baada ya hayo, naomba sasa nitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni ya leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (John A. Chenge) alikalia Kiti

HOJA ZA SERIKALI

NDG. ZAINABU ISSA – KATIBU MEZANI:

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 - Wizara ya Nishati na Madini

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kikao chetu. Tuna wachangiaji hapa, acha tuanze; nimwone Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza jioni hii ya leo kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, bado ananiwezesha kusimama kwenye Bunge lako Tukufu, nikitoa mchango wangu katika Wizara mbalimbali; ni kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu aliyenifanya nisimame hapa niwawakilishe Wanaliwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema ukweli, sina wasiwasi na dhamira ya Waziri wa Nishati na Madini. Kwanza nakubaliana naye kwa taaluma yake, masuala ya uweledi na ufanisi hilo sina ujuzi nalo, lakini kwa taaluma yake namfahamu vizuri. Wasiwasi wangu ni kwenye utekelezaji, na uwezo wa kuyatekeleza haya ambayo yameanishwa kwenye hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuweka rekodi sawa nataka niwaeleze Waheshimiwa Wabunge walioko humu ndani, wasione Wabunge wa Kusini wamekuwa walalamikaji sana humu ndani, kwamba kila Mbunge wa Kusini akisimama analalamika kama vile tumeonewa! Kwa kuweka rekodi sawasawa nataka niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge, Reli ya Tanga – Dar- es-Salaam iling'olewa kutoka Mtwara– Nachingwea, wakati ule Mkoa wa Lindi tulikuwa tunalima pamba, mkonge, karanga pamoja na korosho. Wajerumani wakatuwekea ile reli, ili kuharakisha maendeleo, lakini tulivyopata uhuru reli ile ikang'olewa, ndipo umaskini wa watu wa kusini ulianza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapokuja kulalamika tumeona Mwenyezi Mungu ametupa neema hii ya gesi, sasa ni lazima watu ambao tumeshafanyiwa huko nyuma tuwe waoga. Ndio maana mtu wa Kusini akisimama leo hapa, haiamini hii Serikali ya Chama cha Mpinduzi kwa sababu, wameshatufanyia mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye madini. Sera ya Madini bado sijaelewa, hata wananchi wangu wa Liwale nafikiri bado hawajaelewa Sera hii imekaakaaje, hasa pale ambapo ardhi ya wanakijiji inapokuja kugundulika pana madini; hawa wananchi wa ardhi ile bado hawaelewi hatima yao na nafasi yao katika rasilimali ile iliyopatikana pale kwenye ardhi yao. Kwa sababu, ninavyofahamu mnufaika wa kwanza wa rasilimali inayopatikana ni lazima awe yule inayomzunguka pale alipo. Pamoja na kwamba, hizo rasilimali ni za kitaifa, lakini mnufaika wa kwanza anapaswa awe yule inayomzunguka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii kwa Liwale imekuwa ni kinyume chake, sisi Liwale tuna machimbo ya madini yako kwenye Kata ya Lilombe, katika Kijiji cha Kitowelo. Pale wanachimba madini ya *sapphire* na dhahabu, lakini Ofisi ya Madini iko Tunduru, ndiko mahali ambako kinapatikana kibali cha uchimbaji. Aidha, wachimbaji wadogo ili kupata leseni inabidi uende Tunduru, sasa unafikaje huko Tunduru, sielewi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ukishapata hicho kibali, unakwenda moja kwa moja msituni, machimbo, wanachimba, wakishachimba wanakwenda moja kwa moja Tunduru kwenye mauzo; Halmashauri ya Kijiji na Wilaya haina habari! Nilivyofika kule kwenye machimbo nikalazimika kumtuhumu hata Mkurugenzi wa Halmashauri, pengine naye anajua chochote. Haiwezekani madini yatoke pale Lilombe, wana Lilombe hawajui, Halmashauri haijui, haipati hata thumni! Sasa leo nimesikia ofisi hii imesogezwa imepelekwa Nachingwea! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Lilombe mpaka Liwale Mjini ni kilometa 60, kwa hiyo, hayo yanayofanyika Lilombe Halmashauri haijui! Sasa hii Sera ya Madini, Mheshimiwa Waziri, atakapokuja nitaomba ufafanuzi kidogo, hii inakuwaje kuwaje? Hawa wachimbaji wadogo tunawasaidiaje? Kwa sababu, nimekwenda mimi kwenye yale machimbo nimemkuta mmiliki mmoja, mchimbaji mdogo, kuna bwana mmoja pale, nafikiri yule alikuwa IGP, Mheshimiwa Mahita! Yeye ana vitalu vyake pale, lakini yeye mwenyewe hayupo pale upo Tunduru!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana wale wachimbaji wakipata madini wanampigia simu, anakuja kuchukua anakwenda au pengine wampelekea ananunua anakwenda, lakini Halmashauri pale haipati chochote, wala kijiji kile hawapati chochote, wanaachiwa mashimo tu na ile ardhi ipo pale! Sasa hapo Waziri atakapokuja naomba anisaidie, hii Sera ya Madini ikoje kwa sababu, sisi ndiyo kwanza tunaingia kwenye hiyo fani kwa sababu, mgodi wetu ule ni mdogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirejee kwenye umeme. Wilaya ya Liwale ilibahatika kupata umeme miaka ya 77, ndiyo Wilaya ya kwanza kwenye Kanda za Kusini na Nyanda za Juu Kusini kupata umeme wakati ule Mzee Kawawa akaambiwa umeme amefunga kwenye mikorosho, lakini umeme wenyewe ni ule wa mwisho saa nne, mpaka leo miaka 40 bado umeme ni ule ule wa mafuta!

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa wametuonea huruma wakachukua ile mashine kutoka Ikwiriri wakaipoleka Liwale, mashine kuukuu iliyotoka Ikwiriri wakaipoleka Liwale ku-subsidise ile mashine ya zamani ya Mzee Kawawa; lakini kulingana na jiografia ya Liwale, umeme ule wa mafuta, masika kama saa hizi Liwale hakufikiki na mafuta hakuna! Kwa hiyo, mafuta yanapokosekana Liwale inabaki giza, lakini siyo hivyo tu, kutoka Liwale kuja Nachingwea ni kilomita 120. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna hii Miradi ya REA; umeme wa REA katika Wilaya ya Liwale, ambayo ina vijiji 76 sisi tuna vijiji vitano tu! Tuna Mangirikiti, Kipule, Likolimbora, Mihumo na Darajani, hivi vipo ndani ya kilomita tano kutoka Liwale Mjini, lakini nje ya hivyo zaidi ya hapo hakuna kingine tena kinachopata umeme. Siyo hivyo tu, umeme huu wa gesi umeishia Nachingwea! Nachingwea Liwale kilomita 120, lakini mpaka leo sijaelewa huu mradi wa umeme wa kutoka Nachingwea kufika Liwale umefikia hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembea kutoka Liwale kuja Nachingwea katika Vijiji vya Kiangara, Vibutuka, Nagano mpaka Mikunya; nguzo zimewekwa pale, zingine zimechimbwa, zingine huku zinaanguka huku zinachimbiwa, haieleweki, haielezeki, ukimuuliza meneja hakuna anachosema! Mara pesa

bado, hajeleta mkandarasi, hapo alipofikia bado hajalipwa, sijui imekuwa kuwaje, haeleweki ile REA pale Liwale mwisho wake ni lini? Hivi sisi tutabaki gizani mpaka lini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka niseme, kama ingekuwa enzi zile za zamani kwamba, ukitoa shilingi inaleta *reflection* yoyote, ningekuwa natoa shilingi kila Wizara hapa, maana sioni Wizara hata moja ambayo nikasema Wizara hii ina nafuu kwa Liwale. Hata hivyo, hata nikitoa shilingi haina maana yoyote kwa sababu, tumeona hapa mambo yenyewe yanavyokwenda mwisho wa yote tunapiga kura wape, wape, basi; haina maana yoyote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, namwomba Mheshimiwa Waziri, kweli atutendee haki, atuondoe gizani; sisi umaskini wetu umechangiwa na haya mambo ya barabara na haya mambo ya umeme, huu ndio unatuletea umaskini, leo hii Liwale hakufikiki, huu umeme wa mafuta magari hayaendi! Hivi huu umeme wa mafuta utafika lini? Halafu umeme wenyewe mwisho saa nne! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana, sana Waziri... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wetu ndiyo huo!

Mheshimiwa Salome Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Omar Kigua ajiandae.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati na Madini. Naamini nafasi hii haijaja kwangu kwa bahati mbaya kwa sababu, natokea Mkoa wa Shinyanga ambao umebarikiwa kuwa na baraka ya madini kwa sababu, nina migodi mitatu mikubwa; migodi miwili ya dhahabu, Mgodini wa Bulyanhulu na Buzwagi iliyoko Jimbo la Msalala na Jimbo la Kahama. Nimebarikiwa kuwa na Mgodini wa *Williamson Diamonds* ulioko Mwadui Shinyanga, lakini pia nina mgodi, *medium scale mining* wa El-Hilary ulioko Bugarika, Kishapu, ukiacha migodi mbalimbali midogo midogo inayohusika na uchimbaji na uchenjuaji dhahabu ambayo imezunguka Mkoa mzima wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Shinyanga ni Mkoa ambao unachangia takribani asilimia tisa ya pato la Taifa hili na hii ni baada tu ya Mkoa wa Dar-es-Salaam na hii inatokana na uwepo wa nishati na madini katika mkoa huo. Pamoja na baraka hizi ambazo Mkoa wangu wa Shinyanga umebarikiwa kuwa nazo leo nikisema niondoke na watu wachache hapa kwenda kuangalia

hali halisi ya mkoa huu, ukilinganisha na baraka hizi ambazo tunazo, mambo yanayoendelea kule ni mambo ya kusikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Shinyanga hasa maeneo ya uchimbaji, walipoletewa habari hii ya uwekezaji wa sekta ya madini walifikiri kwamba, itakuwa ni faraja kubwa kwao na itawakwamua na umaskini, lakini kwa bahati mbaya watu hawa, badala ya mijadala ya kuwahamisha ili kuweza kuwapisha wawekezaji kufanyika kama inavyoelekeza Sheria ya Madini ya mwaka 2002 na 2008 badala yake watu hawa walihamishwa kwa kufukuzwa kama wakimbizi kwenye ardhi yao wenyewe. Mbali na hivyo, watu hawa walilipwa fidia ambayo *intervention* ya Serikali katika ulipaji wa fidia hizi, ikawa ni kinyume na matarajio ya wakazi hawa, hasa maeneo ya Kakola, ambako kuna mgodi wa Bulyanhulu na maeneo ya Kahama Mjini ambako upo mgodi wa Buzwagi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa mpaka leo wamekuwa na kilio cha muda mrefu. Zaidi ya miaka 10 wanalalamika kuhusu *unfair compensation* iliyofanyika kwenye maeneo yale, lakini Serikali ambayo tunaamini kwamba, inaweza kushughulikia matatizo yao haioni umuhimu wa kushughulikia matatizo hayo na wale wananchi wa-*feel* kweli Serikali ipo kwa ajili ya kuwatumikia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Shinyanga ni wapole na ni watulivu, pamoja na maumivu makali waliyoletewa kwa sababu ya *unfair compensation*, malipo ya fidia ambayo hawakuridhika nayo, walikubaliana kuvumilia mgodi wakiamini ipo siku Serikali itakuja kutatua matatizo yao. Pamoja na Serikali kutokutatua matatizo yao na kuwaahidi kwamba, watapata kazi kwenye migodi ile, mpaka leo wananchi wale hawapati ajira na wakifanikiwa kupata ajira basi, watapewa zile ajira ambazo mwisho wa siku zitawaacha katika hali ya umaskini mkubwa na utegemezi wa hali ya juu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaozunguka eneo la mgodi wakipata kazi kubwa katika migodi hii ambayo tunaamini ni ya wawekezaji watapata kazi ya kufagia, kufyeka, upishi na hakuna *program* zozote za msingi ambazo ni madhubuti zimewekwa na Serikali zinazoweza kuwaendeleza wananchi wale! Japokuwa tunasema wamefanya kazi kwa muda mrefu tuna-*assume* kwamba, wana-*on job training*, basi angalau i-*certify* ujuzi walionao ili siku moja watu wale waweze kuja kupata kazi ambazo zitawaingizia kipato na cha akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikitishwa sana na matukio yaliyojitokeza kwenye Mgodi wa Bulyanhulu miaka ya 2000, 2002, 2005; wafanyakazi wale walipata ulemavu, wengi wao wakiwa ni ma-*operator*. Wale ambao tulipata bahati ya kwenda kutembelea migodini kuna Watanzania wenzetu wanaofanya kazi ya ku-*operate* mitambo katika migodi ile, lakini pamoja na

maradhi waliyoyapata kwa sababu ya kufanya kazi ngumu na nyingine zikiwa *underground*, watu wale walipelekwa kutibiwa na mgodi na wakiwa wanaendelea na matibabu yale, wale watu walirudishwa kazini na kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi zao ziko Mahakamani. Mpaka leo wanahangaika wengine wanakufa kwa sababu ya magonjwa, lakini Serikali inayojiita Serikali sikivu, sijaona hatua mahususi, hatua madhubuti za kusaidia kutetea watu hawa na leo hii tunajisifu hii ni Serikali ya Hapa Kazi Tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mbali suala la watu kufukuzwa kazi, kuna watu ambao leo migodi ya Tanzania, migodi ya wawekezaji imekuwa ni Serikali ndani ya Serikali ya Tanzania. Wafanyakazi wanapokosea katika migodi ile adhabu wanayopewa bila kujalisha ukubwa wa kosa alilolifanya anapewa adhabu ya kufukuzwa kazi na anafungiwa haruhusiwi kufanya kazi mahali popote pale maisha yake yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala limewaathiri watu wengi ambao kama nilivyotoka kusema awali, wananchi wa Mkoa wa Shinyanga maisha yao yote yamekuwa ni maisha ya madini. Unapomwambia kwamba, haruhusiwi kufanya kazi tena ina maana unamzuia yule mtu kupata kipato halali na hakuna adhabu Tanzania hii, labda kama ni adhabu ya kifo, inayomfanya mtu kupewa adhabu ya milele, lakini hicho ndiyo kinachoendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo migodi inafungwa! Tumeona Mgodi wa Tulawaka umefungwa na Mgodi wa Buzwagi huenda mwakani ukaanza *closure plan* na migodi mingine itafungwa. Kinachotokea nyumba zinazozunguka migodi hii zimekuwa zikipata athari kubwa ya uwepo wa migodi hiyo, kama athari za milipuko na athari za kemikali inayoweza kuvuja kutoka migodini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo Tulawaka imeshafungwa na Buzwagi itafungwa. Vijiji vya Mwendakulima, Vitongoji vya Ikandilo, Chapulwa, Mwime, Mbulu, Kakola, kule Msalala watu wanalia, nyumba zao zimepata *crack*, zimepasuka kwa sababu ya athari ya milipuko! Nimewahi kushiriki kwenye Kamati kwa ajili ya kuangalia athari za milipuko na Kamati hizi zilishirikisha watendaji wa Serikali ambao ni Majiolojia na Maafisa Madini. Afisa Madini anakuja kwenye Kamati ya Uchunguzi wa Athari ya Milipuko na kalamu na karatasi; utawezaje kuchunguza athari ya milipuko kwenye nyumba bila kuwa na vifaa ambavyo vinaweza kukupa data zinazoeleweka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea ku-improve sekta ya madini na uwekezaji, tunaongelea kuwapa vifaa Wataalam wa Serikali ili tuweze kupata ripoti ambazo zipo *impartially*, ambazo zinaweza kusaidia na kutetea maslahi ya wafanyakazi wetu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda Nyamongo kuna kesi, hata leo ukifungua kwenye google, kuna kesi inaitwa the *Tigiti River*; ile kesi watu waliripoti, Wabunge walipiga kelele Bungeni na mto ule ulikuwa unatiririsha maji yanayotoka mgodini ambayo yalisemekana kwamba yana sumu, yalitiririshwa kwenda kwenye vijiji na ng'ombe wakafa na watu wakaathirika, lakini Serikali ikapuuza kelele za Wabunge, kama ambavyo mnafanya sasa! Matokeo yake ripoti ya Umoja wa Mataifa na Mataifa mbalimbali ndiyo iliyofanyiwa kazi. Hivyo, leo tutaendelea kupiga kelele humu ndani na kama kawaida Serikali itapuuza, lakini naamini sisi tukiongea msipofuatisha na mawe yataongea na ipo siku mtatekeleza matakwa ya wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekee kwenye suala la uchimbaji holela. Katika Wilaya ya Bukombe kuna Pori la Kigosi Moyowosi na Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009 inasema, hairuhusiwi kuchimba madini hasa ya dhahabu *except for strategic minerals*. Lakini leo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, muda wetu ndiyo huo!

Tunaendelea na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Kigua na Mheshimiwa Ignas Malocha ajiandae.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe kwa kuniona na kunipa nafasi hii niweze kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, Profesa msomi, Mheshimiwa Muhongo ambaye kwa kweli, binafsi yangu kwa aliyonifanyia kipande cha Chalinze, sina shaka kusema Mungu azidi kumzidishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu iliyopita katika vijiji 67 vya Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze tumefanikiwa kupata umeme karibu vijiji vyote kupitia mpango wa REA isipokuwa vijiji 15 ambavyo vimebakia, ambavyo nina imani kabisa Mheshimiwa Waziri atakapokuja kusimama hapa na kueleza juu ya mkakati wake wa kuimarisha umeme vijijijini, basi Chalinze nina hakika kabisa ataviangalia hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaoishi vijiji vya mbali kama kule Kwa Ruombo, Kibindu, Lugoba, Mkange, wanaonisikiliza wote katika Jimbo la Chalinze kule Pela, Msoga, Tonga na maeneo mengine mbalimbali hakika kabisa watakuwa wameyasikia haya. Kwa kweli Profesa najua kwamba, ramani ya eneo lile siyo mgeni nalo, basi atafanya mambo yale ambayo ametufanyia katika miaka mitano iliyopita. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo, jambo la msingi nataka nimkumbushe Waziri na najua kwamba analifahamu, lakini sio mbaya nikatumia nafasi hii kumkumbusha. Pale Chalinze wakati wanaweka *transformer*, ile inaitwa *power transformer*, kwa ajili ya kuongeza nguvu za uzalishaji wa umeme Chalinze na maeneo yake walitufungia *transformer* yenye MVA 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu na takwimu za wasomi wa elimu ya umeme katika Jimbo letu la Chalinze wakiongozwa na ndugu yangu Mkuu wa TANESCO pale Chalinze inaonesha kwamba, matumizi ya sasa ya Jimbo la Chalinze ni *almost* karibu MVA 10, kwa hiyo, maana yake tunayo nafasi nyingine iliyobakia ya MVA 35 ambayo Mheshimiwa Profesa Muhongo akiangalia vizuri hii anachotakiwa kufanya ni kuweka tu nyaya pale na wananchi wa Chalinze wale wapate umeme wa uhakika zaidi; hatuna tunalomdai zaidi ya umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nataka nizungumzie pia tatizo kubwa ambalo nililizungumza katika Bunge lililopita juu ya tatizo lililoibuka katika Kijiji cha Kinzagu na Makombe juu ya hati alizopewa mwekezaji. Sisi tulilalamika sana, lakini tukaambiwa kwamba, kuna utaratibu Wizara inaweza ikatoa hati ya mtu kwenda kufanya uchimbaji wa madini katika vijiji hata kama hao wataalam wa Wizara hawajafika kijijini hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie ukweli na Bunge lako lisikie na Watanzania waamini hili ninalolisema. Hati iliyotolewa, aliyopewa mwekezaji katika Kijiji cha Kinzagu na Makombe imeacha kipande ambacho nafikiri kina ukubwa, labda wa jumba hili la Bunge! Kijiji chote kipo ndani ya ardhi ya mwekezaji! Wale watu wamezaliwa pale, wameishi pale, wamekulia pale na waliokufa wamezikwa pale! Leo hii wanapowaambia kijiji kizima kiondoke, nini maana ya mimi kuwa Mbunge pale kama sio kutetea watu wangu ambao wamenipigia kura. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Profesa Muhongo, hata kama sheria hizo zipo nataka atambue kwamba, sheria hizo kwa watu wa Chalinze ni *bad law* na kwamba, tutazipigania kuhakikisha kwamba hizo sheria zinaondolewa, lakini muhimu yeye mwenyewe atakapokuja kufanya majumuisho, akatuambia ni mpango gani walionao katika hili. Kidogo nimepata nafasi ya kusoma sheria, natambua kwamba, hata kama mtu

amepewa hati hiyo wanakijiji wanayo haki ya kukataa huyo mtu asipewe access ya kufanya uchimbaji wake na mwendelezo huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine hapa tunazungumzia maendeleo, ninachokiona Serikali yangu inajaribu kunigombanisha nao pia, kwa sababu, mimi kama mwakilishi wa wananchi sitokubali! Nasema tena, sitokubali kuona watu wangu wa Kijiji cha Kinzagu na Makombe wanaondolewa ili kupisha bepari ambaye anataka kuja kuwekeza katika eneo lile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nizungumzie pia, matatizo ambayo wanayo wananchi wa eneo la Kata ya Mandela. Niliwahi kusema hapa na leo narudia tena, tulimwomba Mheshimiwa Waziri aangalie sana kuna Kijiji kinaitwa Ondogo ni kijiji ambacho wanaishi watu wanaotegemea maisha yao katika ukulima. Kama unavyojua ukulima sio shughuli ambayo inafanyika muda wote, ni shughuli ambayo inafanyika, jua likizama watu wanarudi nyumbani.

Pale nataka nikuhakikishie Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais aliyemfanya yeye leo hii akawa Waziri alichaguliwa kwa asilimia 100 katika Kijiji cha Ondogo; Bwana John Pombe Magufuli alichaguliwa kwa nini, ni baada ya mimi na viongozi wenzangu wa chama, kwenda pale kuchapa maneno na kuwahakikishia wananchi wale kile kilio chao cha *transformer* tu ya KV 20 itapatikana na wale wananchi watapata umeme wa uhakika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba, hapa nilipo nimeshapewa taarifa kwamba, kama hiyo *transformer* haitakuja pale, 2020 nikatafute sehemu nyingine za kuombea kura kwa sababu, pale sitopata hata moja. Kwa maana hiyo ya kwamba, sitopata hata moja, maana yake Mheshimiwa Rais pia naye hatopata hata moja! Mimi natokea Chama cha Mapinduzi, naomba ku-*declare interest* kukipigania chama changu ni wajibu wangu na nina imani katika jambo hilo. Nataka pia Mheshimiwa Waziri aangalie sana pale ambapo tulipata asilimia mia moja ya kura zote ili baadaye tusije kupata sifuri ya kura zote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Muhongo kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, lakini pia kwa juhudi kubwa ambazo Wizara yake inafanya. Tunao mradi pale, mkubwa, wa Bwala la Kidunda ambao katika bwawa hilo pia, tunatarajia kwamba, ipo sehemu ambayo itatoa umeme na umeme huo utafaidisha Vijiji vya Magindu, Kijiji cha Chalinze, kwa maana ya Bwilingu, lakini pia na maeneo mengine ya Mikoroshini na Kata ya Pera pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri, yeye na Wizara ya Maji wanapokwenda kusimamia, kuhakikisha kwamba jambo hili wanalifanyia kazi, basi ningepomba jambo la umeme kwa wananchi wangu wa Chalinze nao pia muwaangalie kupitia mlango huo, kama ambavyo mipango thabiti ya Chama cha Mapinduzi tumeipanga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Naomba kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri na kumtakia kila la heri katika safari yake ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana, tunakushukuru. Tunaelekea Kilindi, Mheshimiwa Omary Kigua!

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa jioni ya leo niweze kusema machache, hususani katika Wizara hii iliyopo mbele yetu. Naomba nichukue fursa hii kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuiletea maendeleo nchi yetu. Watanzania ni mashahidi kwamba, Profesa Muhongo na Naibu wake wanafanya kazi iliyotukuka na sote hatuna budi kumpa pongezi na kum-support afanye kazi ya ziada. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa sio busara pia, kutokumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuhakikisha kwamba, Tanzania inapata bomba lile ambalo linatoka Uganda hadi Tanga. Bomba hili litatoa fursa ya ajira kwa vijana wetu, ndugu zetu, kabla na baada. Naomba niseme kwa niaba ya wachangiaji au Wabunge wa Mkoa wa Tanga, nikupe shukrani za dhati sana katika hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa naomba nichangie kuhusu REA, Umeme Vijijini; Waziri na Naibu Waziri ni mashahidi, mara nyingi nimekuwa nikizungumza nao na kupeleka ushahidi kwamba, Jimbo la Kilindi lina vijiji visivyopungua 102, lakini katika vijiji hivyo ni vijiji 20 tu, tena vilivyopo usoni mwa Makao Makuu ya Kata. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anaangalia suala la umeme wa REA vijijini, basi ajue Wilaya ya Kilindi wana changamoto kubwa sana. Naomba vijiji vilivyobaki, kama siyo vyote, tuweze kupata hata nusu ya vijiji hivyo kwa sababu, wananchi wa Jimbo la Kilindi wanahitaji umeme kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia sambamba na mambo ya umeme hapo hapo, ni kwamba umeme uliopo Kilindi uliletwa kwa ajili ya wakazi wachache sana. Jimbo lile sasa hivi lina wakazi takribani laki tatu, umeme ule unakatika mara kwa mara, wakati mwingine hata wiki umeme unakuwa haupatikani! Nashauri basi, kwamba Wizara iangalie namna gani inaweza ikaboresha ili wananchi wa Wilaya ya

Kilindi waweze kupata umeme wa uhakika. Najua hilo kwamba, kuna utaratibu wa kuleta umeme kwa kiwango kikubwa, basi na Wilaya ya Kilindi kwa ujumla iweze kunufaika na mpango huu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, napenda kuzungumzia suala la madini. Wilaya ya Kilindi imebahatika kuwa na madini ya dhahabu na *ruby* yanapatikana kwa kiwango kikubwa sana pale, lakini nimepitia kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijaona ni wapi! Sasa Serikali inatia msisitizo kuweka nguvu ili wananchi wa Kilindi waliobahatika kwa nguvu ya Mwenyezi Mungu kupata madini yale waweze kunufaika na madini yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwamba kuna utaratibu wa kupima, Mheshimiwa Waziri, Ukanda wa Ziwa unajulikana kwamba ni Ukanda wa *Green Belt*. Mzungumzaji aliyepita hapa amezungumza kwamba, migodi mingi kule inafungwa, Kilindi ina dhababu nyingi sana, kwa nini sasa tusiharakishe upimaji katika Jimbo la Kilindi ili wawekezaji wanaokuja kwa ajili ya dhahabu na *ruby* wakimbilie katika Wilaya ya Kilindi, hivyo wananchi wa Kilindi wanufaike na Taifa kwa ujumla. Naomba, Mheshimiwa Waziri aliangalie hili kwa jicho la tatu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kuzungumzia juu ya Sheria za Madini, Wilaya ya Kilindi kuna migogoro mingi; Mheshimiwa Waziri kwa sababu, utaratibu wa kutoa *license* mtu anaweza kupata *license* yupo Mwanza, yupo popote pale, lakini naamini na anafahamu hilo kwamba, wagunduzi wa madini mara nyingi ni wananchi au wakulima wa maeneo yale. Sasa inapokuwa mtu huyu kaja na *license*, amemkuta mwenyeji pale ambaye vizazi vyote kazaliwa pale, kazekea pale, halafu anamwambia azungumze naye namna ya kumpisha ili aweze kuchukua madini pale ardhini! Mtu alikuwa analima mahindi, leo kaambiwa kwamba, pana dhahabu, hivi ni rahisi kuondoka eneo hilo? Siyo rahisi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sheria hii iangaliwe kwa jicho lingine tena kwa sababu, wananchi wa maeneo haya wanadhani ndio wanapaswa kupata fursa ya kunufaika na madini yale. Hatukatai kwamba, wawekezaji wasije Tanzania, lakini utaratibu uwape fursa wananchi wa maeneo yale kwa sababu, migogoro ya mara kwa mara imetokea na Mheshimiwa Waziri ni shahidi. Nimeshakwenda ofisini kwake nikamwambia kwamba, tunahitaji Ofisi ya Madini katika Wilaya ya Kilindi ili iweze kusimamia taratibu za madini Wilaya ya Kilindi. Ni kwamba, ofisi ya madini ipo Handeni, lakini umbali kutoka Wilaya ya Handeni mpaka Wilaya ya Kilindi ni umbali mkubwa unahitaji gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tu hakuna ulazima wa kujenga ofisi pale, tusogezee maafisa watakaoweza kuwahudumia wananchi kwa sababu, wananchi wa Kilindi na wenyewe wanayo fursa ya kupata huduma ya madini pale. Hii pia itapunguza migogoro ya ardhi ya mara kwa mara. Mheshimiwa Waziri naomba wakati ana-*wind up* aweze kunipa majibu katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuchangia ni suala la REA. Inavyoonekana hapa wale wakandarasi, makampuni yale yanayosambaza umeme vijijini, inaonekana wamepewa maeneo mengi sana. Nilipokuwa nazungumza na Meneja wa Wilaya ya Kilindi aliniambia, mtu anayesambaza umeme vijijini amepewa Mkoa wa Morogoro na Mkoa wetu wa Tanga na Mkoa mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wakati umefika wa kuwapunguzia wale *work load* ili waweze kufanya kazi hizi kwa ufanisi wa hali ya juu sana. Wakati mwingine tutakuwa tunawalaumu hawa watu, lakini hawafanyi kazi kwa ufanisi kwa sababu, kazi hizi wanazopewa vijiji vinakuwa vingi sana. Nashauri na naamini kabisa kwamba, kwa *phase* ya tatu, basi kazi zitakwenda kwa haraka ili wananchi waweze kufaidika na umeme huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la kumsaidia Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla kwamba, tunatakiwa tuongeze wigo wa mapato. Wigo wa mapato upo katika maeneo haya ambayo nayazungumzia, hususani ya madini. Siku moja Mheshimiwa Waziri nimeshawahi kumwambia kwamba, watu wanagawana milioni 200, mia 300 Kituo cha Polisi, maana yake Serikali inapoteza mapato! Hebu, Wizara ya Madini ione namna ya kuweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba, mapato haya yanayopotea ya Serikali, basi yanadhibitiwa. Haiwezekani mtu anayechimba pale, mwekezaji mdogo apate milioni 300 wakagawane Kituo cha Polisi, usalama hapo uko wapi? Wizara ya Madini iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wakati umefika, Mheshimiwa Waziri aone na kunisikiliza kwa sababu maneno haya ninayozungumza siyo yakwangu mimi, ni ya Wapigakura wa Wilaya ya Kilindi. Naamini wananisikiliza na wanajua Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi itawasikiliza na itawaletea Ofisi Wilaya ya Kilindi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni juu ya hawa wachimbaji wadogo wadogo na wakubwa wa madini, wamekuwa wakifanya shughuli hizo wakati mwingine wakiathiri mazingira. Kwa mfano, katika Kata ya Tunguli, kuna mwekezaji pale ambaye anafanya shughuli za madini, lakini kwa taarifa nilizonazo ni kwamba, maji yanayomwagika...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, muda wetu ndio huo.

Tunaendelea, Mheshimiwa Ignas Malocha, atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Saddiq na Mheshimiwa Joyce Sokombi!

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Hapana! Samahani Japhary Michael ajiandae.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuungana na wenzangu katika kuchangia Wizara hii. Kabla ya yote niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ndugu yangu Profesa Muhongo, Naibu Waziri na Katibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi siyo za unafiki, zinadhihirisha uwezo alionao, hasa kwa sisi ambao tulikuwamo katika awamu ile ya kwanza na awamu hii, tulikuwa tunamlilia arudi aokoe jahazi juu ya Wizara hii. Mwenyezi Mungu ameturudishia, ni haki yake kuwepo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote tunatambua umuhimu wa nyenzo muhimu hii ya umeme kwamba, umeme ni nyenzo muhimu katika maendeleo. Umeme unaongeza uchumi, unaongeza ajira, unaboresha huduma mbalimbali, ni chanzo muhimu cha uchumi katika njia zote za uchumi; bila umeme hakuna viwanda, hakuna maendeleo, hakuna ustaarabu! Hivyo ni wajibu wa Serikali kuhakikisha umeme huo unamfikia kila Mtanzania mahali popote alipo, ili aweze kufaidika na kupata huduma zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa masikitiko yangu makubwa kwa upande wa umeme wa REA. Tumekuwa na REA I, REA II na sasa hivi tunakwenda REA III, lakini ni jambo la ajabu sana Wilaya yangu ya Sumbawanga pamoja na ukubwa wote vijiji karibu 150, watu zaidi ya laki nne na nusu, hakuna hata kijiji kimoja chenye umeme! Sasa Mheshimiwa Waziri, kama wewe ndiy ungekuwa Mbunge, sijui ungejisikiaje na wananchi wako wangekuelewaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kwanza mwelewe kwamba, wilaya yangu ina kanda mbili, kanda ya kwanza iko Ufipa Juu, unaanzia Sumbawanga kwenda Tunduma na ukanda wa pili unaanzia Stalike, kule tunapakana na Mheshimiwa Lupembe, mpaka huku tunapakana na ndugu yangu, Mheshimiwa Silinde. Sasa nianze na ukanda wa juu. Ukanda wa juu zipo kata 13 ambazo zinatakiwa kupitisha umeme, nimeona nitaje kata maana nikitaja vijiji ni vingi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kata ya Msandamungano, Sandulula, Jangwani, Mpwapwa, Kaengesa, Kanda, Lyangalile, Mpui, Ikozi, Kalambanzite, Lusaka, Laela, Kasanzama, Myakula, Mlangalua; hizi ni kata za Ukanda wa Ufipa juu, lakini zipo Kata za Ukanda wa Ziwa Rukwa, maana kata yangu ina maeneo mawili tofauti, ndiyo maana mara nyingi nimekuwa nikilalamika jiografia ya hii Kata! Ukanda wa Ziwa Rukwa tunazo Kata 13 ambazo zina vijiji vingi; hakuna hata kata moja iliyopata umeme, ambayo ni Muze, Mto Wiza, Milepa, Ilemba, Kapenta, Kaoze, Kilya, Jamatundu, Kilangawana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maeneo ni makubwa. Ninapotaja hizi kata, nataja kwa sababu ni kata, lakini maeneo mengine kata moja inaweza ikagawanyika kuwa kata tatu kwa ukubwa wa kata jinsi ulivyo, lakini unashangaa ni vigezo gani vinatumika kutopeleka umeme katika maeneo haya! Sijajua kwa nini Serikali, mara nyingi, imekuwa ikifanya Wilaya ya Sumbawanga Vijijini kuwa ni ya mwisho katika kupeleka huduma mbalimbali! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata suala la barabara tumekuwa karibu wa mwisho kuletewa barabara, sijui mlishatazama namna gani; kwa maana hiyo, lazima Waziri anieleze sababu za msingi za kutifikisha umeme katika maeneo hayo. Tena eneo hilo la ukanda wa chini ni eneo lenye uchumi mkubwa, jamani umeme unahitajika! Watu wa kule wana uchumi mkubwa, yapo maeneo mnapeleka umeme, nguzo zimesimama, watu hawataki kuingiza ndani ya nyumba kwa sababu hawana fedha! Sasa mnapeleka tu kama *formality* wakati umeme unatakiwa kujizungusha urudishe pesa! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maeneo ninayosema haya ni maeneo ya watu wenye uchumi mzuri, ukipeleka umeme wataingiza umeme kwenye nyumba zao, wataufanyia shughuli za maendeleo, wataongeza uchumi wao, wataongeza uchumi wa Taifa; kwa nini hamtaki kufanya hivyo? Nataka unapokuja hapa unipe vigezo vinavyokufanya usipeleke umeme katika maeneo haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie umeme tunaoutumia Mkoa wa Rukwa. Mkoa wa Rukwa wote tunatumia karibu *megawatts* tano kwa mkoa mzima na umeme huo mwingine tunaupata kutoka Zambia na mwingine unakuwa ni umeme wa *generator*. Ninachotaka kusema, tunavyo vyanzo vingi vya kuweza kuongeza umeme katika Mkoa wetu wa Rukwa. Kwa mfano, nikitaja umeme unaotokana na maji, Mto Nzovwe una maporomoko makubwa na ulishafanyiwa utafiti kwamba, unaweza kutoa *megawatts* nane ambazo zikiongezeka katika Mkoa wa Rukwa unaweza ukawa na *megawatts* nyingi zinazoweza kusambazwa na viwanda vikaweza kutekelezeka vizuri zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa ni kwa nini hawataki kuutumia mto huo ambao ulishafanyiwa utafiti na haukauki na bahati nzuri Mkoa wetu wa Rukwa ni karibu kila mwaka una mvua. Kwa nini wasitumie maporomoko hayo ambayo yameshafanyiwa utafiti wa kutoa *megawatts* nane! Kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri aje anieleze, ni kwa nini hawataki kutumia njia nyingine ya kupata umeme katika Mkoa wetu wa Rukwa ambao gharama yake inakuwa ni ndogo kuliko hata umeme wa *generator*? Sijui wataalam wetu, nashindwa hata kuwaelewa! Tatizo hili ni kutozunguka, kutotembea! Yapo maeneo mlishayatenga, mnarudia rudia, maeneo mengine hamtaki kwenda! Mnazunguka, mnarudia maeneo yale yale! Sijui ni kwanini? Sisi sote ni Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni juu ya utafiti. Lazima nchi yetu ijielekeze kwenye utafiti katika mambo mbalimbali kwa sababu, yapo maeneo mengi yana rasirimali, lakini nchi hii haijagundua! Ndiyo maana hata juzi nimekuja kugundua Mtwara mmegundua gesi, mmegundua mafuta, lakini rasilimali hizo zipo maeneo mengi ila hamjaweka upendeleo wa kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia kuzungumzia juu ya Ziwa Rukwa. Ziwa Rukwa halina tofauti na Ziwa Albert la Uganda, jiografia ni ile ile na bahati nzuri nimeshafika, lakini nataka anieleze ni utafiti gani umeshafanyika wa Ziwa Rukwa ili kuangalia kuna kitu gani na mkishajua maana yake mtaweza kulitunza. Ndiyo maana mmelitelekeza, hamna habari nalo, suala la mazingira hamna habari, lakini naamini upo uchumi mkubwa katika eneo lile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala lingine la utafiti, kuna shamba ambalo nimekuwa nikizungumzia mara kwa mara, Shamba la Malonje. Yule Mtaalam wa Kenya alilizungukia lile shamba akasema, lile shamba, 1/8 ya lile shamba lina madini ya kopa, lakini watafiti wetu hawajakwenda kuangalia ni kitu gani kinafanyika! Matokeo yake mwekezaji akija anang'ang'ania kwa sababu, anajua pale kuna faida kwa baadaye. Kwa nini, watafiti hamtaki kufanya kazi inayostahili, ili kuweza kuboresha nchi yetu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka tu kusisitiza kwamba, Mheshimiwa Waziri sisi sote tunafahamu uwezo wake na msukumo wake. Siwezi kuunga mkono kwa sababu, wananchi watanishangaa! Huna umeme hata kijiji kimoja, vijiji 150, halafu leo hii unasema unaunga mkono, watakushangaa! Mpaka nipate maelezo ya Mheshimiwa ndipo naweza kuunga mkono hoja, lakini kwa sasa siwezi kuunga mkono hoja wananchi watanishangaa, kwanza ni aibu kubwa, ni aibu kubwa! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasisitiza Mheshimiwa Waziri anieleze ni kwa namna gani atapeleka umeme katika Wilaya ya Sumbawanga Vijijini? Mkija Sumbawanga Mjini mnadhani ndio Sumbawanga Vijijini, hata Kijiji kimoja! Ni aibu kubwa sana. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Anafuata Mheshimiwa Saddiq.

Hebu subiri kidogo, nina tangazo la dharura kidogo; Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge, mnatangaziwa kwamba, saa 12.00 jioni ya leo kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi kwenye Ukumbi wa Spika, Ghorofa ya kwanza, naomba mhudhurie bila kukosa. Ahsanteni.

Mheshimiwa Saddiq, atafuatiwa na Mheshimiwa, jirani yake, Mheshimiwa Ndassa.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote naomba kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais kwa kumteua Profesa Muhongo kuwa Waziri wa Nishati na Madini; naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri maneno ambayo yanazungumzwa aachane nayo, akaze buti tusonge mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yake ambayo amefanya tumeiona, tuna matumaini makubwa na yeye. Labda niseme neno dogo katika eneo hili, niwaombe watendaji wanaomsaidia Mheshimiwa Waziri waoneshe mshikamano na upendo mkubwa kwa Waziri, wafanye kazi kama Waziri anavyofanya ili eneo hili sasa lisonge mbele. Wapo watendaji katika eneo hili inaonekana hawana speed ya Waziri mwenyewe. Niwaombe watendaji wa Wizara husika msaidieni Waziri, sisi Wabunge tuna imani naye, tusonge mbele, tulete maendeleo katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la umeme hususani umeme wa REA, vijijini. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri anaendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika yale maeneo ambayo huwa naonana naye na kuwasiliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu ambao unajitokeza katika mpango wa REA wa Awamu ya Pili. REA Wilaya ya Mvomero ipo kwenye tarafa zote nne. Na katika tarafa zote nne hizi kuna baadhi ya vijiji mradi ule unaendelea na baadhi ya vijiji mradi bado. Tumewasiliana mara nyingi na Msaidizi wa Waziri, tumewasiliana na Msofe wa REA, lakini bado yapo matatizo ya hapa na pale. Naomba Mheshimiwa Waziri aelewe kwamba, lile eneo la Kata ya Mtibwa,

Wilaya ya Mvomero, katika Vijiji vya Kiduduwe, Kisara na Kunke, yule mkandarasi ambaye yuko pale leo ni miezi mitatu hajawalipa mafundi ambao wanafanya kazi ya kusambaza umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafundi wale wapo zaidi ya 20 wanahangaika hawajalipwa na baadhi ya maeneo nguzo wameanza kuziondoa ambazo mwanzo walisambaza. Suala hili nilishamweleza Mheshimiwa Waziri, naomba hatua sasa zichukuliwe, lakini kuna maeneo ambayo umeme huu unasambazwa, ni maeneo ya barabarani peke yake, hakuna umeme unaokwenda vijiji vya ndani, umeme unalenga barabara kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Langali kuna vijiji vitatu, umeme ubaki kijiji kimoja kitongoji kimoja; tunaomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko, gharama ya kupeleka umeme Mgeta ni kubwa. Inakuwaje leo umeme unakwenda kijiji kimoja wakati mamilioni ya fedha yametumika? Mheshimiwa Waziri tunaomba atusaidie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika eneo la Kibati, Kijiji cha Ng'ai waliweka nguzo, wameziondoa, wanasema nguzo ni chache, sasa hivi wanaendelea kutafuta nguzo. Naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, ili ile azma yake na azma ya Serikali itimie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida moja mbayo ipo, Mheshimiwa Waziri, wale ambao walipewa mkataba na REA na wao wame-subcontract kwa mafundi wengine na kampuni nyingine na wale ma-subcontractor na wao inaonekana uwezo ni mdogo. Tunaomba Serikali iliangalie hili, uwezo wa ma-contractor wanaopeleka umeme vijijini, hasa wale wanaopewa subcontract, uwezo wao ni mdogo.

Mheshimiwa Waziri, tunaomba eneo la Kibati, Mgeta, Turiani na sehemu za Mtibwa, watusaidie umeme ufike maeneo ambayo bado. Naomba ku-declare interest mimi ni mfanyabiashara wa mafuta naomba na mimi niseme mawili, matatu. (Makofi)

MWENYEKITI: Mafuta ya kula ya petrol?

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa leo tunaongelea mafuta ya petrol, mafuta ya kula wakati wake umeshapita. Naomba ku-declare interest na mimi ni mfanyabiashara wa mafuta ya petrol, ziko changamoto nyingi ambazo tunaona ni vyema tukazisema, ili Serikali izifanyie kazi. Changamoto ya kwanza, ni katika utaratibu mzima wa mafuta yanavyoagizwa, kwa maana ya bulk wale wanaoleta, sisi tunaunga mkono azma ya Serikali kuleta mafuta kwa utaratibu wa bulk, hilo mimi sina tatizo nalo na naliunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo lipo ni eneo ambalo mafuta yale yanaingia kwenye *depot*, kwa maana ya ghala. Sasa kwenye ghala unayatoa mafuta unayapeleka kwenye *petrol station*, hapo sasa ndipo ambapo tatizo linaanzia na EWURA lazima wajue changamoto hiyo. Sisi wengine hatuendi kule tunafanya utaratibu wa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wameongea na mimi naomba niseme. Tatizo lililopo ni kwamba, EWURA wao wanakwenda kumkaba moja kwa moja mlaji hawahangaiki na mpishi wa jikoni! Mpishi wa jikoni ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpishi ni yule *depot* ambaye yeye ndiye amepata mafuta yale. Sasa yule mpishi, ambaye kapika chakula kile, wao hawahangaiki naye wanakwenda kuhangaika na mlaji na wanamsulubu sana mlaji! Naomba EWURA waliangalie hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu utaratibu huu ulikuwa unasimamiwa na SGS, SGS walisumbua sana sekta hii. Mheshimiwa Rais Mkapa aliwatimua SGS na waliondoka kwa sababu walikuwa wanafanya mambo ambayo leo yanafanywa tena na EWURA; naomba Mheshimiwa Waziri aangalie matatizo ambayo yalikuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikukabidhi gazeti hili uweze kulipeleka kunakohusika. Taarifa iliyotolewa humu ni taarifa ya TRA, afisa ambaye ametoa takwimu hizi anasema, leo kwenye Taifa letu fedha hizi zinapotea kwa sababu ya urasimu wa EWURA. Naomba sasa tubadilike, tubadilike katika eneo hili na wenzetu wa EWURA nao wabadilike, wabadilike ili tulete tija katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niseme suala moja, TRA sasa hivi wao wanajua sehemu mbili ambazo zinapoteza mapato ya mafuta; sehemu ya kwanza ni *transit*, sehemu ya pili mafuta yanayokwenda ndani ya nchi, hususani kwenye migodi. Upande wa mafuta yanayokwenda kwenye migodi TRA wameweka *monitored by track system*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana mafuta yanayokwenda migodini sasa hivi yako *monitored* tayari na yale ya *transit* yanalipiwa ushuru sasa hivi na wahusika wenyewe, sasa tunahangaika nini kama hayo mambo sasa hivi TRA wenyewe wanayashughulikia na wao wana-*monitor* mambo haya? Naomba EWURA wakae chini, waangalie upufungu wao, lakini wafike mahali waangalie na ubinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokifungia kituo cha mafuta unapoteza ajira za watu. Kituo kinafungwa mwaka mzima, yule mwenye kituo unampotezea mwelekeo wake, Serikali inakosa mapato, lakini yule uliyemfungia kituo ni mlalahoi au ni mjasiriamali anayehangaika kuuza mafuta rejareja, kwa nini

usihangaikie na wale wanaoshughulika na vinasaba? Usihangaikie na wale wenye maghala ya mafuta? Kwa hiyo, wenzetu wa EWURA hebu liangalieni hili, mimi sina ugomvi na EWURA! Sina ugomvi kabisa na EWURA, lakini nawaomba changamoto zilizopo tuzifanyie kazi. Naomba sana changamoto zilizopo tuzifanyie kazi ili twende sambamba, wote nia yetu ni moja, tuhangaikie Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri, kuna suala la *oil refinery* ya Uganda kusafisha mafuta ghafi...

(Hapa kengele ilililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa...

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ndassa, Richard!

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Nianze moja kwa moja, sitaki nipongeze, niende Ukurasa wa 78 wa Kitabu cha Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana kwa sababu, ametenga asilimia 94 kwa ajili ya maendeleo, lakini hasa kwenye Sekta ya Nishati. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, lakini ili tuipate hiyo trilioni moja nashukuru kwa sababu, bahati nzuri nyuma yangu hapa kuna Waziri Mkuu na ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisikilize vizuri, naomba mumshtue hapo! Hili Jimbo la Ruangwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Shabiby, hili Jimbo la Ruangwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, eneo lote lile lipate umeme, lakini na maeneo mengine ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tuliomo humu ndani tunaomba sana Serikali hii, asilimia 94 ambayo ni sawa sawa na trilioni moja; Mheshimiwa Waziri wa Fedha tumekuwa tukisema mara nyingi sana humu ndani kwamba, pesa hizi zitoke, lakini bahati nzuri au mbaya pesa hizi hazitoki! Hata zile fedha ambazo tumeziwekea uzio na zenyewe mnazipeleka sehemu nyingine, lakini ili nchi hii iendelee na ili iwe ya viwanda lazima tuwe na umeme wa kutosha. Tutaimba nyimbo hapa, lakini kama hatuna umeme wa kutosha, umeme wenye uhakika, hatuwezi tukafikia yale malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hapa, Serikali kupitia Waziri Mkuu, mtakapokaa kwenye vikao vyenu huko hii trilion moja iliyoombwa na Wizara ya Nishati na Madini itoke ili kusudi huyu Waziri wa Viwanda anapozungumzia viwanda, lazima apate umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukipata umeme wenye uhakika REA wakasambaza umeme vijijini wale vijana wanaokuja mjini hawatakuja mjini tena kwa sababu kuna umeme vijijini. Naomba sana Serikali zile pesa ambazo tulikuwa tumetenga kwa ajili ya umeme Tanzania, tozo, pamoja na zile ambazo zilibaki mwaka jana, lazima wapelekewe wenzetu wa TANESCO ili kusudi waweze kufanya kazi yao vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili na hili nimekuwa nikilisema mara kwa mara, Serikali imeshindwa kulipa TANESCO madeni yake, sijui tatizo ni nini! Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, hii si Serikali kwa Serikali, hivi hawawezi kukaa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha wakaondoa hili deni ili kusudi vitabu vya TANESCO viwe visafi! Maana kila siku tunakuta madeni, madeni, madeni! Hebu wakae chini hili tatizo walimalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie bomba la gesi; huu ni ushauri kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Bomba hili lina gharama kubwa, linatakiwa liwe na ulinzi wa kutosha na wasiweke pale Waswahili, waweke Jeshi la Ulinzi liende lisimamie ulinzi wa bomba lile kwa sababu, gharama yake ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu, mitambo ya kusindika gesi, LNG; bado hatujachelewa, tuongeze speed kwa sababu, huwezi ukazungumzia *trillion cubic meters* za gesi tuliyonayo, wamesema 57 *trillion*, halafu huna mtambo wa kusindika hiyo gesi! Lazima tuwe na mtambo wa kusindika hiyo gesi, vinginevyo tutabaki hapa, hata manufaa yatakuwa hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bomba la mafuta la kutoka Uganda kuja Tanzania, Tanga. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuchangamkia, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, hii ndiyo fursa yenyewe, tusiiachie hata kidogo, lakini lazima kuwe na ulinzi wa kutosha katika usimamizi wa ujenzi wa bomba hili la mafuta kutoka Uganda kuja Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, REA. Niwapongeze sana REA kwa kazi nzuri sana wanayofanya na niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwa umoja wetu, kwa kazi nzuri sana aliyofanya REA, hata kama huwapendi kwa sura zao, basi wapende kwa matendo yao, wamefanya kazi nzuri mno. Cha msingi hapa, sisi kama Wabunge, ni kuibana Serikali, ili itoe pesa za kutosha ili miradi iliyobaki ya REA II na REA III tunayokwenda kuanza, iweze kukamilika ndani ya muda

unaotakiwa. Lazima tuibane Serikali humu ndani na tuishauri Serikali kwamba, kwa sababu, tunakwenda kwenye REA III tuibane Serikali ili kusudi iweze kutoa pesa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo dogo upande wa REA, lakini ni vizuri wakarudi nyuma ili wajifunze kwamba, tulifanikiwa REA I, kulikuwa na matatizo gani? Changamoto zilizopo, tumekwenda kwenye REA II changamoto ni zipi tulizoziona? Sasa tunakwenda kwenye REA III zipo changamoto nyingi, hasa urukaji wa vijiji na vitongoji; wanaweka umeme hapa, wanaruka, wanakwenda wanaruka, wanaruka, wanaruka!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kwa sababu, wanapita kuangalia ni wapi wameweka umeme, ni vizuri kama ni kijiji kimoja basi kijiji chote kiweze kupata umeme. Si vizuri sana wanaweka umeme kwenye nyumba, wanaruka wanakwenda kuweka kwenye nyumba hii, wanaruka! Si vizuri sana, tungependa sana umeme kwenye kijiji X umeme uwepo. Kwenye maeneo ya Jimbo langu, nilishawasilisha kwa Ndugu Msofe maombi, sitaki niseme hapa, lakini nimwombe sana, maeneo ambayo yamerukwa, vijiji ambavyo vimerukwa, naomba katika awamu ya III umeme uweze kupatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho. Naomba kusesitiza tena, najua Waziri wa Fedha hayupo, lakini najua Waziri wa Nishati yupo na Waziri Mkuu ananisikiliza. Pesa tunazokubaliana humu kwamba, pesa hizi zinatakiwa zitumike kwa kazi fulani, naomba zitumike kwa kazi hiyo hiyo, zisitumike kwa kazi nyingine na haya ni makubaliano ya Bunge. Nasisitiza tena, tukikubaliana kwamba, pesa hizi zinakwenda kwa ajili ya umeme, kama ni tozo za mafuta ziende zikasaidie kule, kusaidia wananchi wetu ili waweze kupata umeme wenye uhakika, basi ziende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila umeme wenye uhakika hakuna maendeleo, bila umeme wa uhakika hakuna viwanda. Mheshimiwa Mwijage, ni vizuri wakakaa kwa sababu huko mbele bila umeme wa uhakika, viwanda tunavyozungumza Dar-es-Salaam au maeneo mengine vijijini, havitapatikana! Ni lazima tupate umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.

Tunaendelea, ngoja tuhamie kidogo upande wa CHADEMA. Ninao hawa wawili kwa dakika tano tano kila mmoja. Mheshimiwa Marry Deo Muro dakika tano na Mheshimiwa Japhary Michael dakika tano. Watafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema.

Tuanze na Mheshimiwa Muro!

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na ninayo machache ya kuchangia kwenye Wizara hii. Kwanza namshukuru Mungu kuwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuchangia eneo la mwanamke na nishati; nimeamua kuchangia eneo hili kwa sababu nimeona ni jinsi gani mwanamke anahangaika na nishati kuanzia asubuhi mpaka jioni na saa nyingine ashindwe hata kutayarisha chakula kwa kukosa nishati. Nafahamu kabisa kwamba, ndani ya jengo hili wanaume wengi wanakuta chakula kiko mezani, hawajui mwanamke amehangaika kiasi gani mpaka akifikishe mezani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia safu ya uongozi kwenye nishati naona ni wanaume wawili wamekaa pale, lakini hakuna mwanamke ambaye angesimama kwa niaba ya wanawake wa Tanzania ambao wanahangaika siku nzima kutafuta kuni ili waweze kutayarisha chakula kwa ajili ya familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za katikati hapo nyuma, kulikuwa na mradi unaitwa *biofuel* ambao tulitarajia kabisa ungeweza kutumia gharama ndogo ya kumfikia kila mwanamke alipo, akapata moto poa, ambao ungeweza kumrahisishia kupika na kufanya kazi za upishi kwa urahisi, lakini mpaka sasa hivi hatuoni dalili zozote za ule mradi wa mibono ambao ungeweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kueneza vijiji vingi nishati mbadala. Tunaona kuna *biogas* na zimetengewa pesa hapa bilioni 3.2, lakini ukiangalia kwa Tanzania ilivyo kubwa, mpaka akafikiwe mwanamke aliyeko kule kijijini pembezoni, akapate *biogas* itakuwa ni karne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mwanamke ataendelea kulia machozi jikoni huku akichochea vyungu, akichochea sufuria, ili mwanaume akae ale mezani, ambaye haingii jikoni na mwanaume hapati uchungu kwa sababu siye anayepika! Mwanamke ndiye anayehangaika, apike, atafute wapi kuni, atatafuta mkaa, atatafuta chochote kile, lakini chakula kiive! Namwomba Waziri anapokuja angalau atuambie amemuangaliaje mwanamke wa Kitanzania? Jinsi gani anaweza akasaidika na bajeti hii ambayo ameileta mezani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, atakapokuja kujibu, naomba Waziri aje na majibu sahihi, sana sana atuambie labda ule mradi wa *biofuel* umeishia wapi? Watu walishaanza kulima na mibono ilishaletwa mpaka majiko, umeishia wapi? Leo ukija kwenye bajeti hii ya 3.2 *billion* kwa Tanzania nzima wakati unaweza ukatumia *biofuel* ikaenda kwa haraka na kwa nafuu zaidi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Mkoa wangu wa Pwani. Mkoa wangu wa Pwani, Wilaya ya Kibaha, kuna mradi ambao ulikuwa unaendelea wa TANESCO wa Gridi ya Taifa, walitathminiwa wakaambiwa kwamba watalipwa. Ni Vijiji vya Kiluvya, Mwanalugali na Mikongeni, lakini tangu wametathminiwa kwenye mpango wa miaka mitano ilielezwa kwamba, wamelipwa lakini mpaka sasa hivi hawajalipwa na kinachoendelea hatuelewi! Wananipigia simu kila siku wanasema utakaposimama, tuulizie kwa Waziri, Je, hela zetu tutalipwa? Kama hatulipwi, tuendeleze maeneo yetu? Kwa hiyo, Waziri atakapokuja kujibu, ningependa kupata majibu ya maswali ya Wanakibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuchangia yafuatayo. Kwa mfano, tunaona TANESCO imebeba mzigo mzito sana, inazalisha umeme, inasambaza, inauza! Hivi kweli, hili shirika binafsi litaweza kufanya kazi zote hizo? Kwa nini Serikali isije na mpango mwingine ambao uta-*faster* maendeleo ya Tanzania tunapoelekea kwenye Tanzania ya viwanda? Nadhani kungekuwa na mpango wa ziada wa kuisaidia TANESCO isifanye kazi zote peke yake; kuzalisha, kusambaza, kuuza, ndiyo maana unakuta saa nyingine...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Japhary Michael, atafuatiwa na Mheshimiwa Lema.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea hapo alipoishia mchangiaji aliyepita ambaye amenipa muda wake wa dakika tano, naomba niongelee mambo machache sana ya Jimbo langu la Moshi Mjini katika suala la nishati. Napenda kuongelea kwenye upande wa nishati mbadala kama ilivyoandikwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika page ya 60 na Serikali imeonyesha kwamba, imepitia maeneo ambayo wanadhani kwamba, wanaweza wakawekeza kwenye umeme wa upepo na umeme wa jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni mpango mzuri, lakini sijui kwa nini umechelewa kiasi hiki kwa Taifa letu la Tanzania. Pamoja na yote hayo, nataka nisisitize kidogo kwenye suala la matumizi ya takataka zetu, miji yetu mingi inazalisha takataka nyingi, lakini Serikali haijawa tayari kuwa na matumizi bora ya takataka hizi na matokeo yake tumekuwa tukizalisha maradhi ya kila siku na kuharibu mazingira kila wakati, wakati tunaweza tuka-*control* hiyo situation.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukulia mfano Manispaa ya Moshi; Manispaa ya Moshi tuna mradi wa kutumia jalala letu ambalo ni *semi-land fill* ambalo lina uwezo wa kuzalisha *methane gas* ambayo inaweza ikatumika kupunguza sana matatizo ya nishati ya umeme katika mji wetu wa Moshi. Bahati

nzuri tumeshafanya *feasibility study* na bahati nzuri tumeshapata ushirikiano wa wenzetu wa mji dada wa Tübingen, Ujerumani kwa hiyo, tuko katika hatua nzuri ya kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachohitaji ni msukumo wa Serikali katika hili kwa sababu, haionekani kama vile Serikali imeweka mkazo katika eneo hili. Kwa hiyo, tunahitaji msukumo wa Serikali katika hili, ili wale watu wa Ujerumani watusaidie kufikia malengo yetu kwa sababu tayari tumeshatumia fedha za *own source* katika kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tunahitaji *commitment* ya Serikali kwamba, wenzetu wa Ujerumani wametuaambia kama tuki-raise cost ya mradi, wao wako tayari ku-raise 80% na sisi tu-raise 20%. Uwezo wa halmashauri kufanya kazi hii ni mdogo, lakini tunaamini kama Wizara itaji-commit itatusaidia sisi kupata 20% ili huo mradi utekelezwe mapema zaidi. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aifanye Moshi *pilot area* ya mradi wa *methane gas* ambayo itasaidia sana kuzalisha umeme ili maeneo mengine yaige katika nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala lenye shida katika Manispaa yangu ya Moshi katika Jengo la *Stand* kuhusu suala la umeme. Wananchi wanaomiliki vibanda katika Jengo la *Stand* yetu Kuu, jengo ambalo ni mali ya Manispaa, wametaka kuwekewa LUKU, lakini TANESCO wamekataa kuwafungia LUKU wakisema kwamba, mpaka wapate kibali cha Waziri. Sasa wale wananchi hawako tayari kuletewa bili na *landlord* ambaye ni manispaa. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atoe kibali, ili wananchi wale wa Manispaa ya Moshi wafungiwe zile LUKU ili waweze kuendesha shughuli zao kirahisi kuliko kupata usumbufu usio wa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni suala la *biogas*. Ukiangalia page ya 28 ya hotuba hii, *biogas* imeonekana kuelekezwa zaidi maeneo ya vijijini kupitia mradi wa REA na miradi mingine. Hata hiyo 3.2 *billion* iliyotengwa inaonesha ni kwa maeneo ya vijijini, lakini maeneo ya mjini watu wanafanya *zero grazing*, kwa hiyo, wanapata *resources* ambazo zinafaa kwa *biogas* na hitaji muhimu sana la wananchi, ili kupunguza matumizi ya kuni na ya mkaa ambayo siku zote tumekuwa tukikimbizana na tunagombana na wananchi kwa sababu, wanatumia mkaa na kuni na wengine mpaka tunawafunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba maeneo ya mjini ikiwemo Manispaa ya Moshi mradi huu uwe *considered* kufika katika eneo hili ili wananchi wangu wa Manispaa ya Moshi nao wafaidike na mradi huu wa Serikali. Naamini tukilitekeleza hili tutaweza kukabiliana na hali halisi ya uchafuzi wa mazingira. Bado naamini, Serikali yetu haijawekeza vizuri katika *solid waste*

management ambayo ni teknolojia itakayosaidia sana maendeleo ya nishati katika dunia tunayoishi leo. Ukienda Nchi za Ulaya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea, Mheshimiwa Lema, atafuatiwa sasa na Mheshimiwa Dkt. Mary Ngu.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kabisa nianze bila kusahau na suala ambalo tulikutananalo Arusha na Mheshimiwa Waziri naomba anisikilize sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda Arusha na Kamati ya Viwanda na Biashara na tulivyofika *TANELEC*, mahali ambako tunatengeneza *transformer*, walikuwa na malalamiko ya msingi sana. *TANESCO* ni *shareholder* wa *TANELEC*, yaani kwenye *Board* ya *Directors* ya *TANELEC*, Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* ni mjumbe. Cha kushangaza sana ni kwamba, Kenya wananunua transfoma Tanzania, Msumbiji wananunua transfoma Tanzania, mpaka Malawi, lakini Tanzania ambao ndiyo wanaotengeneza *transformer* na *TANESCO* ambao ndiyo inafanya biashara ya umeme, inanunua transfoma kwa Manji, kutoka India kwa bei mara mbili ya zinazouzwa *TANELEC*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, haya mambo ni mambo ya ajabu kweli, kwamba *partner*, mwenzi wa *TANELEC* ambaye ni *TANESCO* kwenye *Board* anaingia Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO*, wanakwenda kufanya maamuzi ya manunuzi ya transfoma, wanaacha kununua transfoma Tanzania, wanakwenda kumpa *order* Manji kuagiza transfoma ya dola 4,000 au 5,000 wakati pale zinatengenezwa transfoma. Sisi na Wajumbe wote wa Kamati tulihuzunika sana na tulimpelekea Waziri wa Viwanda na Biashara tukamwomba akuone! Hili jambo Mheshimiwa, siyo tu ni jipu, hii ni *cancer* ambayo matibabu yake kwa kweli, lazima yafanywe *very serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini ya *Tanzanite*; ninachokielewa na ninachokiona, Mheshimiwa Waziri ni Mtaalam wa Miamba, lakini ukweli ni kwamba, lazima tutafakari kwenye Wizara ya Nishati na Madini tunahitaji Mtaalam wa Miamba ama Mtaalam wa Biashara ya Madini. Tukiweza kulipambanua hilo vizuri tunaweza tukaisaidia sana Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoongea sasa hivi Madini ya *Tanzanite* yameanguka kwa takribani asilimia 60 mpaka 70! Jiwe lililokuwa likiuzwa shilingi milioni moja mwaka jana mwezi wa 11, leo jiwe hilo linauzwa shilingi 300,000 mpaka shilingi 400,000 hakuna *market*! Sababu ni moja, kuna *confusion* kubwa imekuwa *created* kati ya madini ya *tanzanite*, ambayo ni *cut* na madini ya

tanzanite ambayo ni *rough*. Kwa hiyo, nimwombe sana Waziri, waende wakafanye tathmini ya kutosha; watu wote waliokuwa wakinunua madini Arusha wakisafirisha kwenda nje, wote wame-*shift position* wamekwenda Mombasa, wamekwenda Kenya. Kimsingi ni kwamba, hawataweza kuzuia madini ya *tanzanite* yasiende kwa njia za panya kufika Nairobi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kitakachoonekana, Nairobi ndiyo watakuwa wana-*seal* mzigo. Mzigo utaondokea Kenya, kwa hiyo *tanzanite* yote duniani itaonekana inaondokea Kenya kwenda kwenye Mataifa ambako inanunuliwa kwa sababu, haikufanyika *feasibility study* vizuri ya kuweza ku-*burn* hii *tanzanite* ambayo leo inazuiwa kwenda *rough*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri wataalam wako wanapokuja kufanya utafiti wa biashara ya madini wasije tu watu waliosomea miamba inavyotoa madini, waje watu ambao wako *business oriented*. Leo tunavyoongea Arusha watu wameondoka na kwa sababu ya hii kasi ya Serikali hii watu wanaondoka wanahamisha *investment*. Biashara kubwa inafanyika Mombasa na jiwe la *Tanzanite* ukipita nalo kwenye kengele hapo, *gemstone* haipigi kelele. Kwa hiyo, mawe yataondoka yote Arusha, yatakwenda Mombasa, yatakwenda Nairobi, wata-*seal* mzigo Nairobi, watakwenda Thailand, watakwenda Marekani, itatokea kama ilivyotokea miaka ya nyuma, Kenya ilipewa zawadi ya ndege kwa kuuza madini mengi ya *Tanzanite* wakati Tanzania haijawahi kupewa zawadi hata ya baiskeli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme na mazingira. Tanzania kuna takataka nyingi sana. Amesema Mheshimiwa Japhary kwamba takataka siyo *disadvantage*, takataka ni umeme. Lakini leo nchi hii tuna *claim* kuwa na takataka nyingi mijini badala ya kuzi-*transform* takataka hizi kuwa umeme. Wameongea wenzangu hapa kuhusu *biogas*, kama Wizara ya Nishati na Madini ingekuwa *serious* na *biogas* leo misitu inavyokatwa nchi hii inakatwa kwa sababu hakuna njia mbadala ya nishati ya kupitia tofauti na kuni, lakini ukiangalia maeneo yote ya Usukumani kuna ng'ombe wengi, kuna vinyesi vingi vya ng'ombe ambavyo hivi vingeweza kuwa *transformed* kuwa umeme, vingeweza kuzuia sana uharibifu wa mazingira mkubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala la *biogas* siyo suala la umeme peke yake na kupikia chakula. Ukitaka kuokoa Taifa hili na uharibifu mkubwa wa mazingira, Mheshimiwa Waziri ni shahidi ukiwa kwenye ndege unakwenda Dar es Salaam hapa katikati Morogoro kote kumeanza kuisha. Mawaziri na Wabunge tunanunua mikaa barabarani. Ukiongelea *future* ya Taifa bila kugusa mazingira ni kujidanganya sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana suala la *biogas*, mimi ni shahidi nyumbani kwetu ninakotoka kijijini kwa mama yangu tumemfungia *biogas* ana

ng'ombe wawili, tuna miaka mitatu hajawahi kutumia kuni, tuna miaka mitatu hajawahi kutumia umeme wala hajawagi kununua gesi ya madukani. Kwa hiyo, suala la biogas siyo suala tu la nishati mbadala, lakini nishati ambayo inaweza ikazuia uharibifu mkubwa wa mazingira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, TANESCO wanapobadilisha nyaya utafikiri wametumwa na ibilisi kuja kukata miti. Hakuna watu wanakata miti hovyoyote kama TANESCO. Kila wanapobadilisha waya wanakata miti, mti mmoja kukua unachukua zaidi ya miaka mitano mpaka 15 halafu TANESCO wanakuja kubadilisha waya imetumika muda mrefu wanakata mti wote. Kupanda mti mwingine mpaka ufike kwenye maeneo ulikofika ni miaka mingine kumi, tunaendelea kutengeneza jangwa. Waya za siku hizi nimeziona, ni waya ambazo zina *plastic*, ziko *covered* na *plastic*. Unajiuliza kuna sababu gani ya TANESCO kukata miti hovyoyote badala ya ku-*prune* miti na kuacha waya zipite kawaida na miti iendelee kuwa mapambo ya miji yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri, TANESCO waambiwe kabisa wakitaka kufanya *pruning* ya miti yoyote wawe na *link* kwanza na Halmashuri husika ili tukubaliane na Mipango Miji hii miti inakatwaje, kwa sababu watu wanafanya jitihada. Mheshimiwa Mbowe amepanda miti kutoka KIA mpaka Hospitali ya Machame mpaka Moshi Mjini, juzi TANESCO walikuwa wanabadilisha waya, wanahamisha nguzo mimi nikawakuta wamekata. Nikasimama, nikampigia Mbunge simu, nikamwambia Mbunge miti uliyopanda, amenwyeshea mwenyewe kila kitu mwenyewe, miti imefika mita tatu, mita tano juu TANESCO wanakata miti na waya zinazopita pale ni waya ambazo zina *plastic cover*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba TANESCO wanavyofanya kazi ya kuweka waya mijini na Mheshimiwa Maghembe analijua hilo tukiwa kwenye kikao cha RCC waliliongea hili. Waangalie kabisa kwamba mazingira ni muhimu kuliko kitu chochote katika nchi hii. Hakuna kitu cha msingi kama mazingira. Kwa hiyo TANESCO watusaidie, wa-*communicate* na Halmashuri, tukubaliane namna gani ya ku-*prune* miti na waya zipite bila kuharibu mazingira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu, Waziri Mkuu alikwenda bandarini, alivyofika bandarini akakuta ile *flow meter* imefunguliwa akauliza, alipouliza Waziri Mkuu akawa na hasira kwa sababu anaipenda nchi yake akakamua jipu. Lakini yule mama alisema nimetumiwa *message* na Waziri, sasa Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe tulikutolea maazimio mwaka jana na bado leo tuko na wewe, ina maana ni huruma yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kama ni Mheshimiwa Waziri alimtuma yule mama aongee tu na Waziri Mkuu yule mama mumrudishe kazini kwa sababu

kwa vyovyote vile yule mama kama aliambiwa na boshi wake fungua hiyo *flow meter*, halafu mama akasema nimeambiwa na boshi wangu, Waziri Mkuu akatumbua jipi bila ganzi. Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi nakuheshimu sana, kwa kweli hebu mfikiri yule mama kama ambavyo sisi ama wenzako huko ambavyo wamekufikiria wewe Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulimfungua na mashati hapa lakini mwaka huu tumekuona umekuja na tunashindwa kuongea vibaya dhidi yako kwa sababu wote waliokuja.....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Muda wetu ndiyo huo, tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kawambwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula ajiandae.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa kuongea kwenye sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi na kwa maslahi ya watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kuangaza Tanzania na kuleta maendeleo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwa sababu muda ni mfupi ningependa kushukuru watu wengi lakini niende moja kwa moja kwenye mambo ambayo ni *pressing* kwa Wilaya yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara ni Mkoa wa kilimo na Wilaya ya Hanang ni Wilaya ya kilimo na ufugaji. Umeme wa REA namba moja ulitpelekwa kwa vijiji vinne tu Wilaya ya Hanang na mpaka leo vijiji vile vinne bado havijapata umeme, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze vijiji hivyo vitapata umeme lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tulipata vijiji vichache wakati Wilaya za jirani zinapata zaidi ya 20, zaidi ya kumi nikamwomba vijiji 19 na yeye akaniahidi, naomba uwahakikishie watu wa Hanang kwamba Hanang nayo inathaminiwa kwa hivyo vijiji 19 kuweza kupata umeme na orodha nimekupa. Kwa ajili ya muda mfupi nisingependa kupoteza muda. Ninaomba uone umuhimu wa Wilaya moja kwa REA zote tatu sasa tunaenda kwenye REA tatu imepata vijiji vinne na nafikiri utaona umuhimu wa kuona kwamba Mbunge akilia hapa ana sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Tanzania ni nchi iliyojaaliwa kuwa na vyanzo vingi vya nishati, siwezi kuvitaja kwa kuwa mnavijua, lakini ninafikiri gharama ya kupata nishati kwenye chanzo kimoja vinatofautiana na vingine. Na miaka ya awali ya Tanzania tulikuwa tunapata umeme kutokana na maji. Tabianchi ilipoanza kubadilika tukakumbwa na ukame tukapatwa sasa na dharura za kukimbilia kuweka umeme wa dharura. Mimi nafikiri sasa wakati umefika wa kuwa na mkakati mzuri. Ninajua kuna *power master plan*, lakini ninaomba sana tuangalie *mix* ya hiyo *power master plan* kusudi gharama iwe baadaye si kubwa kwa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba tusifikirie vidogo vidogo, mmefanya kazi kubwa, kuna Kinyerezi I, Kinyerezi II, Kinyerezi III mnafanya kazi nzuri na kuna vyanzo vingine ambavyo mnashughulikia. Mimi bado naamini tufikirie vikubwa na mimi nafikiria hakuna umeme ambao utaokoa Tanzania kama siyo ule wa *Stigler's Gorge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Stigler's Gorge* unaweza ukatoa umeme wa *kilowatts* 2100, tukijielekeza huko wakati wa *master plan* nimeona *Stigler's Gorge* iko kwenye *master plan* lakini iko mbali. Naomba muilete karibu kusudi tuwe Taifa la kufikiria vitu vikubwa. Nitakushukuru sana, najua una uwezo na ukiamua hilo unaweza ukalifanya vizuri na mimi sina wasiwasi, ninajua wakati wa dharura dharura ile ndipo tulipoingia kwenye *IPTL*, kwenye *DOWANS* na mambo ambayo yalileta madhara makubwa kwa Taifa letu.

Kwa hiyo, sasa ni wakati mzuri wa kufikiria kwamba katika ile *master plan* tuwe na mkakati ambao utajielekeza kwenye kuona kwamba tumeamua kuwa nchi ya viwanda na uchumi wa kati. Bila kuwa na umeme wa hakika huko hatutafika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiria kwamba Mkoa wa Manyara ndipo ambapo Mererani ipo. Kutokana na *Tanzanite* ya Mererani Wilaya ya Simanjiro ikatoa eneo la *EPZA* bure na wengine wote wanadai fidia.

Ninaomba sana tuangalie Mererani na tuone jinsi ambavyo tutaweza kuongeza thamani ya *Tanzanite* kwa kuweka viwanda ili tuweze kuwa na faida ya *Tanzanite* kuliko inavyoonekana sasa Tanzania ni nchi ya tatu. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeleta manufaa makubwa ya vito ambavyo vimeletwa na Mwenyezi Mungu nchini kwetu na Mkoa wa Manyara ambao hauna *resources* nyingi isipokuwa ardhi yenye rutuba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana nirudie tena kwamba naomba Wilaya ya Hanang iletewe umeme kwenye vijiji nilivyosema ili tuongeze thamani ya mazao ya kilimo, thamani ya mazao ya mifugo na watu ambao zamani ndiyo walikuwa nyuma kuliko wengine wamekubali kukimbia muwawezeshe

kukimbia kuwakuta watu wa Kilimanjaro na Arusha. Mkoa wa Manyara umejigawa kwa sababu tulikuwa nyuma sana na kwa ajili ya Arusha tukawa tunaonekana tumeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa tuingie kwenye huo mkakati wa kuendelea wa kutuletea umeme na wewe ndiye utakuwa savior, ninakushukuru, ninakupongeza na Mwenyezi Mungu atakupa nguvu zaidi na kuendelea kuwa kwenye hii Wizara, maneno yapo, Upinzani wanasema wao wanaisimamia Serikali naomba tukumbushane hapa kwamba ni jukumu la Wabunge wote pamoja na wale wa CCM kuishauri na kuisimamia Serikali, siyo kazi ya Wapinzani tu. Na sisi ndiyo tuna wajibu mkubwa wa kuishauri na kuisimamia Serikali yetu kuliko ninyi, Ilani ya Uchaguzi ni yetu na kwa hivyo lazima tuisimamie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kama dakika zangu hazikuisha wengine nao wanufaike. Ahsanteni wote. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Dkt. Nagu tunakushukuru. Mheshimiwa Dkt. Kawambwa atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini.

Awali ya yote niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo anaifanya yeye pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara kwa juhudi kubwa ambayo wameionyesha kulitumikia Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yangu kwa kusimamia vizuri Mradi huu wa Umeme Vijijini. Mradi huu ni ukombozi wa wananchi na katika vijiji vile ambavyo umeme umefika wananchi wamepata maana nyingine kabisa ya maisha. Wanafurahia maisha yao, wameanzisha miradi ya uzalishaji, wameanzisha biashara, huduma za elimu na za afya zimeboreka, kwa kila namna mradi huu ndiyo ukombozi wa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya wa umeme vijijini mwaka huu kwa asilimia 50. Hii ni hatua kubwa, hatua adhimu na nina imani kwamba Mheshimiwa Waziri akiendelea kusimamia hivi basi ndani ya miaka hii mitano Serikali ya Awamu ya Tano itamudu kufikisha umeme katika vijiji vyote vilivyobaki 10,000 katika nchi yetu na kwa maana hiyo nchi yetu itakuwa katika hali nyingine kabisa ambayo tunasema kwamba tutakuwa tumejipanga kwa ajili ya kufika mwaka 2025 kama nchi inayoelekea uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuombea Waziri na Wizara na Serikali yetu Tukufu ili wamudu kulitekeleza ndani ya miaka mitano kusibaki kijiji ndani ya nchi yetu ambacho hakina umeme. Najua kwamba hilo litaambatana pia na uzalishaji mkubwa zaidi.

Nimuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ambaye amesisitiza mradi wa *Stigler's Gorge* ambao una uwezo mkubwa, tumezungumzia kwa muda mrefu, Marehemu Baba wa Taifa aliufikiria katika Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili haikuwezekana pia, ya Tatu, nina imani Awamu hii ya Tano chini ya uongozi wako Waziri mradi huu utawezekana ili ndoto ya kufikisha umeme katika vijiji vyote Tanzania ndani ya miaka mitano hii iwezekane. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika REA Awamu ya Pili Jimbo la Bagamoyo lilipata miradi kumi tu, vijiji kumi ndiyo ambavyo vilipata umeme wa REA lakini kinachonisikitisha au kinachotupa tatizo katika Jimbo la Bagamoyo ni kwamba katika miradi hiyo kumi, minne mpaka hivi sasa haijamalizika na mmoja umefutwa. Sasa miradi minne ambayo ilitegemewa ilipofika Juni mwaka jana 2015 iwe imemalizika mpaka hivi sasa haijamalizika, wananchi wana hasira, hawaelewi, hakuna ambacho wanaweza wakasikiliza kutoka kwa Mbunge, wanashindwa kuelewa kwamba wao wanaishi katika nchi gani kama siyo hii hii nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kijiji cha Buma nguzo zimesimamishwa lakini nyaya hazijafungwa. Kwa hivyo kunguru nao wanatembea pale wanafanya ndiyo viotea wanakaa kule, wananiuliza Mbunge, sasa hawa kunguru tutawafanya nini, tuwafuge majumbani kwetu au iweje? Katika kijiji cha Kondo hivi karibuni nguzo zimeenda.

Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa sauti yako ya wiki iliyopita ambayo imefanya kijiji cha Kondo sasa hivi mkandarasi yule ndiyo anajitahidi ameweka juhudi kubwa ya kuweza kufikiza umeme. Lakini kabla ya hapo kila tulilolisema lilikuwa haliwezekani. Kijiji cha Kondo na mradi wenyewe haujaanza mpaka hivi sasa. REA wamejichanganya kwamba Kondo kuna bandari ambayo haijengwi Kondo, bandari inajengwa Pande na inajengwa Mlingotini. kijiji ambacho kimefutwa kwa ajili ya mradi wa bandari ni kijiji cha Pande na wao siyo kwa utashi wao isipokuwa ni mradi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji cha Kondo Mheshimiwa Waziri naomba utumie juhudi yako yote kuweza kuhakikisha kwamba mkandarasi huyu anaanza kufanyaazi mapema iwezekanavyo. Kijiji cha nne ni Matimbwa ambacho sehemu ya umeme imekamilika lakini kuna nguzo 20 ambazo bado hazijafungwa nyanya. Nguzo hizi bahati mbaya ni eneo hilo ndilo ambalo tuna zahanati mpya ya kijiji cha Matimbo. Wenzetu NGO ya Korea imejitolea kutujengea zahanati nzuri ya kisasa katika kijiji kile cha Matimbwa,

wanatushangaa kwamba nguzo ziko pale zimesimama, sehemu nyingine umeme unawaka lakini pale hapawaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba REA ihakikishe kwamba mkandarasi huyu anamsimamiwa vizuri ili kijiji hiki nacho cha Matimbwa mradi wake ukamilike. Pande imefutwa sawa kwa sababu mnatengemea kujenga bandari pale, lakini mradi huu ulishakabidhiwa kwa mkandarasi, imani yangu ni kwamba basi mradi huu ungehamishiwa katika kijiji kingine. Nimezungumza REA bado hatujapata mafanikio, nina imani kwamba kwa juhudi zako Mheshimiwa Waziri bila shaka REA watapata maelekezo ya kuweza kusaidia kuhamisha mradi ule kuupeleka katika kijiji kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimwa Waziri naomba atakaposimama kufanya majumuisho basi ututhibitishie wana Bagamoyo kwamba miradi hii michache itapewa kipaumbele kuweza kumalizwa ndani ya mwaka huu wa 2016. Ni miradi michache tumeipata basi nayo iweze kukamilishwa wananchi waweze kupata huduma hii adhimu ya umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile hatukufaidika kiasi hicho katika REA Awamu ya Pili, mategemeo yangu sasa baada ya mimi kama Mheshimiwa Mbunge pamoja na Madiwani kuwasilisha REA miradi 29 katika Jimbo hili la Bagamoyo kwa ajili ya REA III, nina imani kwamba safari hii tutaonewa huruma na miradi hii yote 29 ambayo tumeiwasilisha itaweza kuingizwa katika utekelezaji katika Awamu hii ya Tatu ya Umeme Vijijini. Mheshimwa Waziri najua kwamba kwenye REA II kulikuwa na tofauti kubwa sana kati ya Majimbo na Majimbo, Wilaya na Wilaya, bila shaka Wilaya zile ambazo hazikuweza kufaidika sana katika REA II basi safari hii utaziangalia kwa jicho la huruma ili nazo ziweze kupiga hatua nzuri zaidi na kuweza kuwakaribia Wilaya zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na umeme vijijini ni jambo moja, lakini umeme wa uhakika nalo ni jambo muhimu sana. Katika Mji wa Bagamoyo na Kata za jirani kama vile Magomeni na Kiromo kumekuzuka tabia kubwa sana ya ukatikaji wa umeme mara kwa mara. Hukai siku mbili umeme umekatika mara kidogo umeme umekatika. Mheshimiwa Waziri nadhani jambo hili linafanya wananchi nao wanakosa faida zile ambazo walikuwa wakizitegemea wazipate kutokana na uwepo wa umeme, naomba Mheshimiwa Waziri Shirika la TANESCO waliangalie jambo hili kwa umakini, kama ni vipuri, kama ni mitambo ambayo imechakaa iwe transfoma au viunganishi vingine, mitambo hii iweze kushughulikiwa kwa umakini, ukarabati na ukarafati uwe mila na desturi ya Shirika letu la TANESCO ili wananchi waweze kupata huduma bora katika upatikanaji huo wa umeme usiwe unakatika mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie jambo moja la mwisho na hili ni kuhusu nishati ya gesi. Katika Wilaya yetu ya Bagamoyo watafiti

wameendelea kufanya kazi kutafuta gesi, wakitarajia kupata gesi katika Jimbo langu Bagamoyo, Kata ya Fukayosi wamefanya kazi sana pale na katika Jimbo la Chalinze Kata ya Vigwaza wamefanya kazi sana pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewa fununu kwamba kuna gesi lakini hatujapata taarifa rasmi naomba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, tunaendelea na Mheshimiwa Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate na Mheshimiwa Kakoso ajiandae.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia bajeti iliyoko mbele yetu. Nitamke bayana kabisa kwamba naunga mkono bajeti hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa karama hii ya uhai na kwamba leo napata fursa ya kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nizungumzie eneo la REA, nitumie fursa hii kupongeza kazi kubwa iliyofanywa na wenzetu wa REA, imefanyika kazi kubwa sana, kazi ambayo ripoti inaonesha kwamba tumefikia kupeleka umeme vijijini sasa kwa asilimia 40, ni jambo zuri. Wakati tumefanya kazi hii vizuri ni ukweli vilevile kwamba zipo changamoto kubwa sana katika utekelezaji wa miradi hii ya REA. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati, kwa hiyo nilipata fursa ya kuzungukia miradi ya REA, vilevile nina hazina ya uzoefu kwa miradi ya REA kule kwenye Jimbo langu. Kubwa tuliloliona ni kwamba kuna changamoto kubwa sana ya kusimamia utekelezaji wa miradi hii. Maeneo mengine yamerukwa kwenye vitongoji, maeneo mengine vijiji vimerukwa bila sababu za msingi na maeneo haya ni maeneo ambayo awali yalikuwemo kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani kwangu vipo vitongoji vimerukwa na bahati mbaya sana vitongoji vilivyorukwa wananchi wamekatiwa mazao yao ili umeme uweze kufika, mimea imekatwa hakuna fidia, lakini mwisho wa siku wanakosa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano na hili Naibu Waziri analijua kwa sababu nililisema tukiwa kweye Kamati, kijiji ninachotoka mimi zimepelekwa nguzo 15, hivi nguzo 15 zinapelekaje umeme kwenye kijiji? Sasa matokeo yake

taasisi muhimu kama zahanati, sekondari, shule za msingi zimekosa huduma hii, ukiacha wananchi ambao wamekatiwa mazao yao. Nadhani hii siyo sahihi tujitahidi katika kusimamia ili tuondokane na kero hii ya wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeliweka tena eneo hili la Kata ya Kigongoi kwa matumaini kwamba linaingia kwenye REA Awamu ya Tatu. Hivyo, naomba miradi hii ya REA tuisimamie iende vizuri, mapungufu yote ambayo yameonekana sasa yasije yakaathiri utekelezaji wa REA Awamu ya Tatu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haingii akilini, kwamba umeme unapelekwa kwenye kijiji lakini wananchi wanaambiwa umeme ulioletwa hauwawezeshi ninyi kuendesha mashine za kusaga unga na mambo kama hayo, tufanye marekebisho, tufanye usimamizi wa karibu ili changamoto hizi ziweze kuondoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine linalokwenda sambamba na hilo ni kukatika umeme katika maeneo ya Mkoa wa Tanga, nilisema hapa eneo la Maramba, mwenzangu Majimarefu akazungumzia kule Korogwe, dada yangu Chatanda akazungumzia Korogwe Mjini na Waziri akatuambia kwamba upo mradi mkubwa wa kuboresha upatikanaji wa umeme, naomba jambo hili lisimamiwe kwa karibu ili tuondokane na tatizo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye eneo la uchimbaji wa madini ya *graphite*. Taarifa zilizopo sasa zinasema Tanzania itakuwa miongoni mwa Mataifa makubwa yanayozalisha *graphite*, tutakuwa ndani ya nchi kumi zinazozalisha *graphite* ulimwenguni. Wakati tukielekea huko nataka tujiulize, tumejipanga namna gani kusimamia eneo hili ili yasije yakatukumba kama yaliyotokea malumbano wakati tunaenda kwenye uchimbaji wa dhahabu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizopo ni kwamba tayari wapo wajanja wachache ambao hawastahili kuajiriwa kwenye sekta hii, makampuni ya nje yamewaajiri watu ambao vibali vyao vinatia mashaka kuajiriwa kwenye sekta hii, taarifa zilizopo zinasema wapo watu wameajiriwa kwa fani ambazo Watanzania wanaweza kuzisimamia. Hivi inakuwaje leo tunaajiri mtu wa sekta ya ununuzi kutoka Australia, kwamba Watanzania hawapo wenye uwezo wa kusimamia mambo haya? Mheshimiwa Waziri naomba tufanye *due diligence* katika mambo haya ili tusije tukaingia kwenye matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa kwamba ipo kampuni imepewa leseni, kampuni hiyo tunaambiwa inatoa asilimia tano ya hisa kwa Tanzania, madini yetu tunapewa asilimia tano, mimi sitaki kulikubali hilo, lakini kama ni kweli Mheshimiwa Waziri hebu lifuatilie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni madini ya vito. Tumelizungumza kwenye Kamati tukajielekeza moja kwa moja kwenye *Tanzanite*, ripoti za kitafiti duniani zinaonesha kwamba madini ya vito asilimia 50 yanazalishwa kwenye ukanda wa Afrika Mashariki. Lakini kwa bahati mbaya sana nchi hizi zimeshindwa kunufaika ipasavyo kwenye madini haya, hapa ndipo linapokuja suala la *Tanzanite*, tumezungumza kwenye Kamati nini cha kufanya, naiomba Serikali imuelekeze Mkaguzi na Mthibiti Mkuu Hesabu za Serikali aende akafanye ukaguzi maalum kule *Tanzanite* ili ripoti hiyo ituwezeshe Bunge kuishauri Serikali ipasavyo, hatujanufaika na *Tanzanite*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Lema pale anasema, sasa jamaa wameondoka kutoka kununua Arusha, *Tanzanite* inafungashiwa Mombasa, nataka wakati tukiyasikia haya turudi kwenye tafiti, taarifa ya Umoja wa Mataifa inasema nini, taarifa ya Umoja wa Mataifa inasema madini haya *gemstone* ndiyo imekuwa kichaka cha magaidi, kujificha kwenye jambo hili. Sishangai kusikia kwamba badala ya watu wale kuwa Nairobi sasa *Tanzanite* inafungashiwa Mombasa, nikisema hivi nafikiri mnaelewa ninasema nini, tuyasimamie madini yetu vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni EWURA, tulifanya uamuzi wa kuanzisha EWURA na tulipoanzisha *work load* ya sekta ya nishati haikuwa kubwa sana, kwa hiyo ilikuwa ni sahihi pengine EWURA kusimamiwa na Wizara ya Maji. Sasa *workload* ya upande wa nishati imepanuka sana, nadhani siyo sahihi kuendelea kuiacha EWURA ikasimamiwa na Wizara ya Maji, nafikiri busara itumike, Mheshimiwa Rais ashauriwe ili ile *instrument* inayoelekeza EWURA kusimamiwa na Wizara ya Maji sasa ibadilishwe na hata ikibidi EWURA igawanywe, tuwe na kitengo kinachosimamia sekta ya nishati ibaki Wizara ya Nishati, na ile inayoshughulikia sekta ya maji ibaki Wizara ya Maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni matumizi ya gesi, tumekuwa tukijielekeza kwenye matumizi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Katimba.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye

amenipa nafasi hii na uhai kuwepo katika Bunge hili, maana tunaishi kwa neema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Sospeter Muhongo wewe ni jembe tu hata wakipiga kelele, tunakuamini wewe pamoja na Naibu Waziri wako na watendaji wengine wote wa Wizara, kazi mnayoifanya inaonekana, hapa tulipofikia pamoja na figisufigisu zilizofanywa, lakini tumefika hapa tulipo kwa sababu ya kazi yako kubwa uliyoifanya. Watanzania wanajua, ndiyo maana wanakuunga mkono na ninaamini watu wenye akili hakuna atakayesimama kukupinga wewe. Kwa hiyo, ninampongeza sana, songa mbele, jeshi kubwa liko mbele yako na nyuma yako, tunakulinda kwa nguvu zetu zote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu Wizara hii, kwa kweli nina kila sababu za kuwapongeza Wizara hii imeonesha dhamira kubwa ya kutaka kutusogeza mbele. Ukisoma hii bajeti fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ni fedha kubwa, hii ni dhamira nzuri ya Serikali kutaka kuinua uchumi wa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini umeme ndiyo kila kitu, hata Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mwijage anaposema anataka Tanzania ya viwanda kila kona, tusipokuwa na umeme wa uhakika hatuwezi kuwa na viwanda. Kwa hiyo, hizi Wizara zinategemeana, niendeleo kusema juhudi zenu ni nzuri na tunakuunga mkono, ukiangalia kwa mfano upande wa REA imeongezeka karibu asilimia 150 utoka shilingi bilioni 350 mpaka shilingi bilioni 535, kwa kweli hii ni dhamira ya dhati kwa Wizara hii. Mimi ninawapongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ninaomba kwa Mheshimiwa Waziri na Serikali hizi fedha zinapotengwa zitolewe, siyo leo tunapitisha bajeti mwisho wa siku zinatolewa asilimia tano.

Ninaomba Serikali ijitahidi hizi pesa zitolewe Watanzania wanahitaji kupata umeme wa uhakika, umeme wa kutosha. Kwa mfano, kule kwetu Kyerwa tangu uhuru ndiyo tumeanza kuona umeme wengine walikuwa wanashangaa umeme ulipowashwa. Bado haujafika mbali, umeme kule kwetu Kyerwa umepita maeneo machache, Mheshimiwa Waziri umefika Kyerwa umeona Watanzania wa Kyerwa namna walivyo na uhitaji wa umeme. Maeneo mengi ya vijijini ndiyo kuna uzalishaji, tunaposema tunataka kujenga viwanda tukipata umeme wa uhakika, hivi viwanda vinaweza vikajengwa vijijini tukazalisha huko vijijini, tukafungua viwanda vidogovidogo na tukaongeza ajira kwa vijana wetu ambao wako mitaani hawana ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninakuomba Mheshimiwa Waziri, jambo hili ninakusifu sana kwa kutotenga vijiji hapa maana kuna kuchomekeana sana hapa, kuna wengine wanapita mlango wa nyuma, kwa sababu hukutaja vijiji ninakuomba wote tukagawane mkate huu sawa, Watanzania ni wamoja na wote tupewe sawa siyo wa kupendelewa, kuna upendeleo na hili naomba mlisimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wengine wakati mwingine wanatoa pesa ili wapewe miradi hilo lipo, ndiyo maana unakuta mwingine amepitishiwa vijiji vyote kwingine hakuna, naomba Mheshimiwa Waziri hata hao watendaji wako hao uwaangalie vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri suala la umeme ni muhimu sana na ili Tanzania iweze kuendelea tuweze kufanikisha malengo tuliyonayo tunahitaji umeme wa uhakika, siyo umeme huu tunasema tunafunga umeme lakini umeme huo siyo wa uhakika. Kwa mfano, kwetu Kyerwa, umeme unawaka lakini huwezi ukawasha mtambo wowote mkubwa, umeme unawaka na kuzimika, kule tunapewa umeme masaa mawili, matatu. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri huu umeme usiangalie mijini tu hata huko vijijini ni muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la gesi, Mheshimiwa Waziri suala la gesi ni muhimu sana kwa Taifa letu na tumshukuru Mungu kwa jinsi ambavyo tumepata gesi ya uhakika. Hii gesi isijikite kwenye umeme tu wataalam wanasema gesi tunaweza tukaitumia kwenye umeme asilimia kumi, kuna vitu vingi ambavyo tunaweza tukavipata kupitia umeme kwa mfano plastiki, kuna nguo ambazo zinazalishwa kupitia gesi naongelea gesi kuna mbolea na vitu vingine hii gesi isije ikapotea bure. Kama tunaweza kuzalisha umeme asilimia kumi, je, hii asilimia 90 tumejiandaa vipi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na hili lazima uliangalie tusije tukasema tuna gesi kumbe gesi yenyewe tunaitumia asilimia kumi tu, kwa hiyo ninaomba mliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Waziri nataka nilisemee Kyerwa tuna madini ya *tin*, haya madini kule kwetu Kyerwa majirani zetu ndiyo wanaoyafaidi, asilimia kubwa hatuyafaidi Watanzania yanavushwa na hilo Mheshimiwa Waziri unalijua, naomba tulisimamie vizuri ili tukafaidi haya madini ni ya Watanzania siyo ya nchi jirani. Serikali hili mnalijua sijui mmejiandaa vipi kwa ajili ya kulisimamia vizuri ili haya madini yasiendelee kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuhusu madini Mheshimiwa Waziri ulifika kule Kyerwa, vijana wetu ambao wanachimba madini wako kwenye mazingira ambayo siyo mazuri tuwaboreshesha mazingira yawe rafiki, tutenge maeneo ambayo ni kwa ajili ya vijana wetu hao wachimbaji wadogo wadogo.

Wakati mwingine hawa vijana wanafanya utafiti, wakishagundua madini hawa wakubwa wanakuja wananunua yale maeneo wale vijana ambao wameanzisha wanaondolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri kama ulivyoongea na wale vijana ukasema utatuma wataalam, waje wapime watenge maeneo kwa ajili ya hawa vijana nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, ninakumini wewe ni mchapakazi ninaomba hili ulisimamie kwa ajili ya vijana wetu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako, tunaendelea Mheshimiwa Moshi Kakoso baadaye Mheshimiwa Zainab Katimba halafu tutaenda upande mwingine.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii nichangie Wizara hii muhimu ya Nishati na Madini. Nianze juu ya umeme katika Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi una umeme usio na uhakika. Nilikuwa naomba Wizara kupitia Waziri aangalie umuhimu wa kuboresha miundombinu ya umeme katika Mkoa wa Katavi. Mkoa huu umekuwa ni chaka la kupelekewa zana zile ambazo zimetumika katika baadhi ya maeneo zikichoka wanapeleka Mkoa wa Katavi. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atambue kwamba Mkoa wa Katavi ni sehemu ya Tanzania na wote wanastahili kupata stahili ya mgawanyo wa keki ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mradi wa *Orion* ambao ulikuwa unaunganisha Mkoa wa Katavi baada ya Wilaya ya Biharamulo na Ngara tunahitaji sana ule mradi upelekewe fedha ili uweze kutoa umeme wenye uhakika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni umeme vijijini, eneo hili bado kuna ubaguzi ambao unatolewa katika baadhi ya maeneo. Mkoa wa Katavi ni baadhi ya maeneo ambayo yana vijiji vichache sana ambavyo vimepelekewa umeme, Jimboni kwangu sina hata kijiji kimoja ambacho kimepelekewa umeme vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa *Phase II*. Nilikuwa na kijiji cha Kabungu, Mchakamchaka, Ifukutwa, Igalula na Majalila, bahati mbaya mpaka *Phase II* inakwisha bado huo umeme haujafika. Kwenye eneo la *Phase III*

limetengewa vijiji 49, ninaomba hivyo vijiji vipelekewe umeme ikiunganishwa na vile vijiji ambavyo havikupata awamu ya kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ya msingi ambayo yanahitaji kuboreshwa kupelekewa umeme vijijini, hasa maeneo ya Ukanda wa Ziwa. Eneo la Ukanda wa Ziwa lina vijiji vya Kapalamsenga, Itunya, Karema, Ikola, Kasangantongwe na vijiji ambavyo viko jirani vinahitaji kupata umeme kwa sababu kuna maeneo ya uzalishaji mali. Upo utafiti unaofanywa wa mafuta kwenye maeneo hayo lakini kuna shughuli za uvuvi zinazofanywa na wananchi katika kata hiyo na tarafa ya Karema kwa ujumla naomba vijiji hivi vipewe kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate majibu ya uhakika kwenye vile vijiji ambavyo vilikuwa vimelengwa kwa awamu ya kwanza na muunganisho wa vijiji vya tarafa ya Mishamo ambapo kuna vijiji 16 havina hata kijiji kimoja ambacho kimepata umeme vijijini, naomba vijiji vya Bulamata, Kusi, Kamjela, Ifumbula na vijiji vya eneo la Isubangala, Ilangu, tunahitaji vipewe umeme ambao ni muhimu uwasaidie wananchi katika maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi umeanzishwa ambao ungesaidia eneo zima la Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma, Mradi wa Umeme wa Malagarasi, ungekuwa suluhisho la umeme wa uhakika. Bahati mbaya sana eneo lile la Malagarasi kuna vitu ambavyo vinaelezwa huwa tunashindwa kuwaelewa, kinapozungumzwa unashindwa kuelewa kwamba Serikali ina maana gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kuna vyura, hawa vyura wamekuwa na thamani kubwa kuliko hata mahitaji ambayo yanaweza yakawasaidia wananchi. Umeme ule ambao ungefungwa mradi mkubwa ungesaidia Mkoa wa Kigoma na ungesaidia Mkoa wa Katavi kwa ujumla. Naomba Serikali ije na majibu ya msingi; je, mpaka sasa uwepo wa wale vyura kwenye maeneo yale umetoa tija kwa Taifa hili kwa kiasi gani? Tuambiwe kwamba kuna thamani ya fedha imetolewa kubwa ambayo inazidi kuleta ule mradi ambao ungetusaidia wananchi kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie suala la utafiti wa mafuta kwenye Ziwa Tanganyika. Eneo la Karema ni eneo ambalo limekuwa likifanyiwa utafiti, lakini mpaka sasa hivi hatujajua kinachoendelea kwani baada ya tafiti na wale waliokuwa wanatafiti hawapo kwa sasa. Wananchi bado wanaangalia ni nini ambacho kitafanyika na walikuwa tayari kutoa baadhi ya maeneo kwa ajili ya kupata utafiti ule wa mafuta na gesi katika Ziwa Tanganyika. Sasa mpaka saa hizi hatujui ni kitu gani ambacho kimefanyika na kina tija ipi kwa wananchi wa maeneo yale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la madini. Jimboni kwangu kuna miradi ya madini ya dhahabu kwenye Kata ya Katuma na kwenye Kata ya Kapalamsenga kuna machimbo ya shaba; nilikuwa naomba Serikali inawasaidia vipi hawa wachimbaji wadogo wadogo? Kwani wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa kama yatima ambao hawasaidiwi na Serikali kwa karibu ili waweze kupata manufaa ya machimbo yale ambayo yanafanywa ili yaweze kuwanufaisha wachimbaji. Naiomba Serikali iandae mazingira ya kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kunufaika na machimbo ambayo yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijue kuhusu mradi wa shaba ambao uko Kata ya Kapalamsenga, naiomba Serikali ije na majibu mpaka sasa ule mradi unawanufaisha vipi wananchi? Wawekezaji wamekuja wamewekeza pale lakini hakuna mrahaba wowote unaopatikana kuwapa manufaa wananchi wanaozunguka kwenye maeneo yale na bado hata Halmashauri ya Mpanda hawajapata fedha za kuwanufaisha kutokana na madini yale yanayochimbwa. Niombe sana Serikali ije na majibu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nasisitiza Wizara iangalie umuhimu wa kuweka uwiano ulio sawa kwenye Mikoa iliyosahaulika hasa Mikoa ya pembezoni. Miradi mingi hasa ya umeme vijijini bado imekuwa ikielekezwa kwenye maeneo ambayo wao wana miradi mengine, wanaongezewa mradi juu ya mradi. Tunaomba vijiji vya Wilaya ya Mpanda kwa ujumla vipewe miradi ya umeme ili iweze kuwasaidia na sehemu hizo zifunguke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Zainab Katimba halafu tutahamia upande mwingine.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii adhimu ya kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Nishati na Madini.

Ninapenda kuendelea kupongeza juhudi za Serikali katika kuleta maendeleo kwa Taifa hili, pia ninapenda kupongeza jitihada za Waziri wa Nishati na Madini, Profesa Sosthenes Muhongo kwa kazi kubwa anayoifanya. Vijana wa Tanzania tuna imani kubwa sana na Waziri huyu wa Nishati na Madini kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua kazi kubwa iliyofanywa na Wizara hii ya Nishati na Madini katika kuongeza kiwango cha uzalishaji wa nishati ya umeme kutoka kiwango cha *megawatts* 1226.24 mpaka kufika kiwango cha 1491.69 *megawatts* ndani ya kipindi kifupi cha mwaka mmoja,

kutoka Aprili, 2015 mpaka Aprili, 2016 ambayo ni ongezeko la uzalishaji wa umeme kwa kiwango cha asilimia 19. Sasa kama Wizara hii imeweza kuleta ongezeko la asilimia 19 ndani ya mwaka mmoja tu, basi tuna imani mpaka itakapofika kipindi cha miaka mitano watakuwa wameweza kuongeza uzalishaji wa umeme kwa zaidi ya asilimia 95. Kwa hiyo, ningependa kupongeza jitihada hizi, lakini ningependa Watanzania wote waweze kutambua jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kupongeza jitihada za Wizara hii za kuongeza kiwango cha usambazaji wa umeme yaani *access level* kutoka asilimia 36 mpaka asilimia 40. Hili ni ongezeko ambalo limepatikana ndani ya kipindi kifupi tu Machi, 2014 mpaka Machi, 2015. Kwa hiyo, tuna imani kubwa sana na Wizara hii, tuna imani kubwa sana na Waziri Profesa Sosthenes Muhongo, tuna imani ku...

MWENYEKITI: Siyo Sosthenes, ni Sospeter Muhongo!

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani kubwa sana na Waziri Sospeter Muhongo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana tunashukuru sana kwa jitihada za Serikali, jitihada za Wizara za kupunguza gharama ya umeme. Kumekuwa na punguzo la umeme kwa asilimia 1.4 mpaka asilimia 2.4 ndani ya kipindi kifupi cha uongozi wa Wizara hii katika mwaka mmoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa Serikali kufuta tozo ya *service charge* ambayo ilikuwa ni shilingi 5,250; pia tunashukuru sana kwa Serikali kupunguza tozo la kuwasilisha maombi ya kuunganishwa umeme (*application fee*) ambayo ilikuwa ni shilingi 5,000, tunaomba sana Serikali iweze kuongeza au kupunguza gharama za umeme katika umeme unaotumiwa katika viwanda, kwa sababu imepunguza umeme kwa wateja wa *grade T1* na *D1* ambayo ni matumizi ya nyumbani. Sasa tunaomba Serikali iweke pia mkakati wa kupunguza gharama ya nishati hii kwa matumizi ya viwandani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana kutoa msisitizo kwamba, nishati ya umeme ni nishati ambayo inategemewa sana katika kukuza uchumi wa Taifa hili, kwa sababu ukizungumzia maendeleo ya viwanda unazungumzia upatikanaji wa nishati ya umeme, lakini ukizungumzia mawasiliano unazungumzia upatikanaji wa nishati ya umeme! Ukizungumzia sekta nyingi za uchumi, hata ukizungumzia kilimo cha kisasa (*mechanized agriculture*), unazungumzia upatikanaji muhimu wa nishati hii ya umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi sekta nyingi za uchumi katika Taifa hili zinategemea nishati muhimu ya umeme. Ukizungumzia pia ajira kwa vijana

utazungumzia nishati ya umeme kwa sababu sekta nyingi za uchumi ambazo ndiyo chanzo cha ajira kwa vijana zinategemea nishati ya umeme. Hivyo, tunaiomba sana Serikali iendelee na juhudi kubwa inazozifanya, vijana wa Kitanzania tunatambua jitihada hizi na tunawaunga mkono na tunawaomba wazidi kuziendeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Kigoma tunatumia umeme unaozalishwa na mitambo maalum na mitambo hiyo inatumia nishati ya mafuta. Kusema kweli inagharimu Serikali fedha nyingi sana, tunatambua Serikali kupitia mradi wake wa Malagarasi unatengeneza mfumo au utaratibu wa upatikanaji wa umeme wa *megawatts* 44.8 ambao mradi huo utaweza kuzalisha umeme unaotokana na nguvu ya maji (*hydro electric power*). Kwa hiyo, tunaomba sana mradi huu wa Malagarasi Igamba II uweze kutekelezwa kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Serikali ina mpango kwamba, mpaka itakapofika 2019 mradi huu utakuwa umekamilika. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iweke usimamizi mahiri, ili itakapofika 2019 mradi huu uwe umeweza kukamilika kwa sababu, utawanufaisha vijana wa Kigoma. vijana wa Kigoma wanajishughulisha na biashara, wanajishughulisha na uvuvi, vijana wa Kigoma wanajishughulisha na viwanda vidogo vidogo, pia Kigoma tayari tuko katika utekelezaji wa mpango wa kuanzisha kiwanda cha kuzalisha mafuta kwa kutumia michikichi. Tunafahamu kwamba ili mradi huo na kiwanda hicho kiweze kufanikiwa tunahitaji nishati ya umeme, hivyo tungeomba sana Serikali iweze kutekeleza mpango huu ili uweze kukamilika kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote ningependa sana kuiomba Serikali katika mkakati wake wa kuongeza uzalishaji wa nishati ya umeme basi, jitihada hizo ziende sanjari na usambazaji wa umeme huu kwa sababu kama kukiwa kuna uzalishaji lakini usipowafikia watumiaji basi ina maana jitihada hizi zinakuwa hazina tija. Ninaomba sana Serikali iweze kuzingatia haya yote ili Watanzania waweze kunufaika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema machache hayo napenda kuwapa nguvu sana na kusisitiza kwamba Watanzania, vijana na wanawake wa Tanzania tunatambua mchango wa Wizara hii na tuna imani kwamba itatusaidia kwa sababu, katika kipindi kifupi tumeona mambo makubwa ambayo yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Nawakumbusha Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, kikao kimeanza. Tunaendelea, tuanze upande huu tena, ninao Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, atafuatiwa

na Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi na Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii ya leo. Naamini kabisa kwamba, katika historia ya bajeti ya Nishati na Madini na hususan katika Mafungu ya Maendeleo Wizara hii imevunja rekodi kwa safari hii. Wamepewa fedha za kutosha, japo kuandikwa katika vitabu ni suala moja, sasa tungojee wakati wa kugawa mafungu haya kwa Wizara hii husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri ni kipindi kifupi kilichopita alitembelea Mkoa wetu wa Kagera na sehemu mojawapo alitembelea Manispaa ya *Bukoba Town*, mojawapo ya kazi ambayo tuliifanya baada ya kuongea naye ni suala la kufikiria kuweza kutupa umeme katika vijiji mji vya Mji wa Bukoba ambavyo kimsingi haviko katika programu ya REA. Naamini Mheshimiwa Waziri anatambua kabisa nyaraka husika zimeshafika kwenye ofisi yake kama alivyohitaji, tunaomba vijiji vya Nyanga, Kitendagulo, Ijuganyondo, Buhembe, Kibeta, Kagondo pamoja na visiwa ambavyo kule Bukoba tunaviita Pemba na Unguja ndogo, bila shaka tunaamini Waziri atatimiza ile azma na matumaini aliyowaachia wananchi wa *Bukoba Town* kwamba vijiji mji hivi atavitaifutia fursa ya kuviingiza katika mpango wa REA. Vijiji hivi pamoja na kuwa katika eneo la mji ni vijiji ambavyo kwa kweli maisha yao ya kila siku ni sawasawa na maeneo mengine ya vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni suala la mpango mzima wa nishati na vyanzo vyake. Ukisoma kitabu cha bajeti ya Wizara hii kuna vikolokolo vingi ambavyo vimeandaliwa kwa ajili ya kuwa vyanzo vya umeme. Kwa mtizamo wangu, kama walivyokuwa wametangulia kuzungumza wenzangu, Tanzania ina bahati ya kuwa na vyanzo vingi vya nishati, nashauri ni vema tukafikia mahali kama Taifa tukaamua ni chanzo gani tuingize nguvu zetu zote ili tuweze ku-*utilize* nguvu hiyo kuweza kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaamua kuingia kwenye upande wa umeme unaotokana na makaa ya mawe, basi tuelekeze nguvu na *investment* kubwa ielekezwe huko, lakini hii ya kutawanya tawanya nguvu kwenda kwenye vyanzo vingi pamoja na kwamba tunavyo, tunatawanya *man power*, tunatawanya *a concentration* ya *human resource* tuliyonayo katika Wizara hii japo ni chache, kwa hiyo, unakuta Makamishna wanabaki kuzunguka sehemu nyingi na matokeo yake tija inakuwa ni ndogo. Kwa kweli, tufike mahali ambako *concentration* tunaweza tukaiweka ikawa kubwa kwenye mradi mmoja mkubwa ninajua tunavyo vyanzo ambavyo vinaweza vikatoa umeme wa kutosha kama ni gesi, kama ni makaa ya mawe, kama ni vyanzo vya maji, mimi naamini tuchague badala ya kutawanyatawanya *resources* na matokeo yake tunabaki tunahangaika na hatupati umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa tatu ni ushauri kwa ndugu zangu wa TANESCO. Kama tumefika mahali ambapo makampuni mengi yana-*out source services*, nafikiri TANESCO nao kidogo wangechukua ushauri huu kwamba sidhani kama ni mahesabu ya kiuchumi, kama inapigwa simu kutoka Katoro kilomita 60 kutoka Bukoba Town labda kuna hitilafu ndogo imetokea kwenye nguzo kwenye *transfoma*, hata kwenye nyumba ya mtu, unakuta kikosi cha TANESCO kwa sababu hakijui nini tatizo limetokea wanahama mji mzima na mafundi wake wote wanajazana kwenye gari wanakwenda kilometa 60, kumbe unakuta ni *fuse* ni kitu kidogo tu kimeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya sekta ambayo tuna watu wamebobeza na hawana kazi wana makampuni ambayo yanaweza kujikita katika suala la kuingia katika sekta ya kutoa huduma ya kurekebisha hata shughuli ndogo ndogo basi TANESCO iweze kuwa na *authorized agents* ambao wanaweza kufanya shughuli ndogo ndogo sawa na makampuni yanavyofanya, kwa mfano, Vodacom kwa M-Pesa, unaweza ukatawanyia kwa maajenti wakafanya kazi nzuri tu, tajiri anakaa Afrika ya Kusini au huko Ulaya anakula hela tu, ana-*outsource* hizi *services* kwa watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa nne na ninaamini utakuwa wa mwisho ni kwamba kama nilivyosema Wizara hii imetengewa fedha za kutosha, lakini inanitia wasiwasi binafsi kwamba unapotoa shilingi 1,56,350,669,000 lakini ukatenga OC kwa maana ya ku-*supervise* hizi pesa shilingi 66,220,848,000 kwamba hii asilimia sita iende ku-*supervise* asilimia 98 ya bajeti hapa ni mgogoro. Ni sawa na kutaka kupika kilo 1000 za mchele kwa gunia moja la mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunatoa fursa ya kuendelea kutendeka mambo tuliyoyakuta Njombe, nina-*declare* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati hii bahati nzuri, kwamba mkandarasi yuko kule kwenye Mradi wa REA, anafanya vitu vya ajabu, anafunga matransfoma ambayo ni mabovu yanalipuka kila siku, anafunga transfoma na anawaambia wanakijiji kwamba hawaruhusiwi kufunga mashine ya unga zaidi ya moja, tunamuuliza *supervisor* wa TANESCO na bosi wake wa Mkoa anaanza kutueleza alikuwa hajaenda wala hajui kinachoendelea, alikwenda siku Kamati imekwenda, ndiyo na yeye mara ya kwanza anakwenda kule kukagua mradi. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo maskini yule bwana hawezi kuzungumza ukweli, lakini kwa mafungu ya OC kama hayapo na hii nazungumzia kwa miradi hata mingine ambayo inatengewa mafungu makubwa ya maendeleo, kama fedha za *supervision* kwa misingi ya OC kwamba anahitaji mafuta, anahitaji gari, gari inaharibika, inahitaji vipuri hawa wakandarasi wataoagelea katika kutufanyia mambo ya ajabu kwa fedha hizi chungu mzima mlizozitenga kwa ajili ya maendeleo, hata kama makandarasi

watafanya kazi, hawa *supervisors* wetu kuna uwezekano wa kuwa vibarua wa makandarasi. Wakati wa kwenda kuwasupervised mkandarasi anaweza akamwambia *supervisor* wake ambaye anatokana na TANESCO hata Wizara anampitia na anamlipia nauli kwenda kum-supervise ili asaini *certificate*. Hii biashara ina *convince* rushwa, mazingira haya yana *convince* hawa watu ku-*collaborate* hata kufanya hujuma ya aina yoyote. Kwa hiyo, suala la OC ni vizuri pamoja na kwamba najua kuna watu wameshapewa *yellow card* wakithubutu kuomba OC watapigwa *red card*. Naomba suala la OC lipatiwe tafsiri sahihi. Tunakubali kwamba kuna wakati linakuwa *misused* na ubadhilifu unapitia hapo, lakini katika maana halisi wa ku-*supervise projects* na kusimamia ipasavyo OC ina umaana wake, tusije tukajikuta tumetenga fungu kubwa lisilokuwa na usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nilipata bahati ya kwenda Merereni na sikuishia juu tu peke yake, lakini niliingia chini kabisa kwenye mgodi zaidi ya mita 700 na kitu kushuhudia ili nisisimuliwe.

Waheshimiwa Wabunge, kama ni kuibiwa pale *Tanzanite* sisi tumefungua milango tuibiwe. Mambo yanayofanyika pale, huyu anayejiita mwekezaji ambaye naamini hakuna kitu ambacho ameshawekeza tangu akabidhiwe huo mgodi ni kwamba tutaendelea kuibiwa na kuibiwa na kuibiwa, na hata hawa wawekezaji wazalendo waliowekwa pale inaonekana wale watu ni watu wa *deal* tu. Wale ni *third part* wanategeategea kuchukua mzigo. Mbaya zaidi kama nilivyowaeleza suala la kutokuwa na fedha ya ku- *supervise*, niliwakuta kule chini wale vijana wa TMAA wanaopaswa kufanya kazi ya *auditing* ya madini yanayochimbwa kule, naamini ni njaa ya kutopelekewa hela ya kuishi, wale unawaona moja kwa moja wana njaa na wamechoka kuliko kawaida. Sasa unanza kujuliza.....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, atafuatwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii kuchangia Wizara ya Nishati na Madini. Nitajikita sana upande wa Nyamongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Nyamongo ulianzishwa na wananchi wenyewe pale Nyamongo na Serikali ikaleta wawekezaji kwa makubaliano kwamba watawajengea wananchi wa eneo husika watawawekea hospitali, watawawekea maji, watawajengea barabara yenye lami na pia watawajengea kituo cha afya. Matokeo yake hayo makubaliano mpaka leo hayajafanyika, watu wa eneo lile kwa kweli wanatia huruma na inatia aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haioneshi kwamba wale wananchi wako kwenye nchi yao, ukikaa ukiangalia eneo kwamba linachimbwa madini na kwamba yale makubaliano ya mwaka 2011 walivyoenda Mawaziri yakawa kwamba wao wanachimba ule udongo ili wale wachimbaji wadogo wadogo wawe wanaenda kuchambua ule udongo, matokeo yake wakienda kuuchambua wanapigwa risasi. Je, ni halali kwa mwekezaji kuja kumpiga raia wa Tanzania?

Mheshimiwa Waziri ninakuomba na nina kusihi, hakikisha unaweka mipango ambayo ni mizuri kuhakikisha wale wananchi wa Nyamongo hawapati shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia mkataba wa wale wawekezaji pale Nyamongo uwekwe wazi na mnatakiwa pia muwaulize kama mkataba ulikuwa ni kwamba kuwajengea wananchi kuwawekea lami katika barabara na kuwawekea vituo vya afya, kwa nini hayo makubaliano hayakufanyika?(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita pia upande wa Dangote, nimeenda Mtwara. Dangote amekuja kuwekeza hapa nchini eneo la Mtwara kwa lengo la kutumia gesi yetu ya Mtwara. Lakini matokeo yake Dangote hatumii gesi yetu ya Mtwara anatumia mafuta. Je, yale mafuta wanayoyaagiza, yanalipiwa kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia kuhusu REA. REA ni nzuri na imekuja kwa ajili ya kumkomboa mwananchi ambaye yuko kijijini, lakini mmewasahau wale wananchi ambao wako pembezoni kwenye vile vijiji. REA imepita mjini tu, wale wananchi walioko pembeni ni ile wanakaa tu wanaangalia umeme ule. Jamani tunaomba kama Serikali imeamua kumkwamua mwananchi aliyeko kijijini, tuhakikishe kwamba REA inaenda kwenye kila kijiji na vitongoji vyake kwenye kila eneo, siyo REA ipite upande wengine wapate umeme, wengine wasipate umeme. Ninamuomba Waziri wa Nishati na Madini, kwenye hili suala la REA aliwekee mkazo, kwa kweli inatia aibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwa mfano kule Kangetutya, Kabulabula umeme umepita tu, wale walioko ndani ndani hawana umeme, watafikiwa na umeme lini? Ninakuomba Mheshimiwa Waziri, jikite sana katika maeneo ya ndani msipitishie tu umeme eneo la barabarani, wale walioko vijijini kwa ndani nao wanahitaji umeme. Mwananchi amezaliwa miaka nenda rudi anatumia kibatari, basi angalau hata miaka hiyo iliyobaki jamani angalau na inabidi aende mjini, yeye awashe umeme ajue umeme huu unawakaje na una starehe gani. Siyo hata ku-charge simu inabidi aende mjini kwenye center zinaitwa, watafanya namna hiyo mpaka lini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee tena Mgodini wa Nyamongo. Ninakusihi sana Mheshimiwa Waziri, ninakusihi mno, wale wananchi wa pale kwa kweli wanateseka, watateseka mpaka lini? Wewe ukiwa Waziri tena mwenyeji wa Mkoa wa Mara nina hakika kwamba utaenda kulifanyia kazi kuhakikisha Mkoa wetu wa Mara unainuka, wale wananchi wa eneo la Nyamongo hawatapata shida tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri ukiangalia hata kama wakichimba visima eneo hilo yale maji siyo salama kutokana na ile sumu inayomwagwa kwenye Mto Tigiti, maji inabidi wayafuate mbali sana. Ninamuomba Waziri wa Nishati na Madini atusaidie kwa hilo tujikwamue maana hayo mauaji yanayotokea Nyamongo kwa kweli ni aibu kwa Taifa letu. Wawekezaji wanakuja nchini wanakuwa wao ni bora kuliko Watanzania wenyewe tuliozaliwa katika nchi yetu. Tutaendelea kudharauliwa namna hii mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi, nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako na kwa kulinda muda, sasa twende kwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninakushukuru kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Wizara ambayo iko mbele yetu. Kwa sababu ya muda nichangie moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka zaidi ya 15 sasa tumekuwa tunashuhudia tunajadili hapa Bungeni suala la makaa ya mawe, tangia sijawa Mbunge alikuwepo Profesa alikuwa anaitwa Profesa Mwalyosi ndani ya Bunge hili, kila akisimama ndani ya Bunge nilikuwa nasikia anazungumzia Mchuchuma, Liganga, makaa ya mawe miaka iliyopita, alikuwa ni Profesa wa mimea na mazingira. Leo nimeingia ndani ya Bunge miaka 10 tunazungumza makaa ya mawe, ni kwa nini tunashindwa kutumia makaa ya mawe kwa ajili ya nishati ya matumizi ya nyumbani? Tunaomba Mheshimiwa Waziri akija atueleze kuna tatizo gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inaenda kuwa jangwa, hatuna *means*, kwa sababu umeme haushikiki, hata Mheshimiwa Waziri hawezi kupikia umeme. Mafuta ya taa hayashikiki, gesi haishikiki, tunachemshia vitu vidogovidogo tu, asilimia 80 tunatumia mkaa, nchi inakuwa jangwa. Kama kwa mwezi mmoja Dar es salaam peke yake wanatumia magunia 200,000 kwa takwimu za Waziri *can u imagine* nchi nzima tunatumia gunia ngapi kwa mwezi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoangalia tunaenda kuwa jangwa, lakini tunashangaa tumepewa makaa ya mawe ndani ya nchi yetu, kuna tatizo gani

Mheshimiwa Waziri, tunaomba kesho utujibu hapa, kwa nini hatuoni umuhimu wa kutumia rasilimali hii tuliyopewa ndani ya nchi yetu tutoe nishati kwa ajili ya kuitumia, naomba sana Mheshimwa Waziri atuambie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikwenda Likuyu - Namtumbo mwaka juzi, nilikaa pale Namtumbo karibu siku tatu, jambo la kushangaza niliona malori zaidi ya 100 kila siku yanabeba makaa ya mawe, kwanza napenda kujua yanapelekwa wapi cha kwanza, Mheshimiwa Waziri uniambie, yale makaa ya mawe, yanayotoka Namtumbo, malori 100 kila siku yanapelekwa wapi, kwa sababu kwa takwimu ambazo nilijaribu kuuliza wananchi pale wanasema wanakwenda Uganda nan mengine yanakwenda Kenya. Nikawa nashangaa kama malori 100 yanabeba makaa ya mawe kutoka Namtumbo, rasilimali ya nchi yetu, leo tunaendelea kuteketeza misitu yetu, *are we serious?*

Naomba uje utuambie yanakwenda wapi, na wale wananchi pale wananufaikaje na sisi kama Tanzania tunanufaikaje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Wizara ya Madini na Nishati kutoa leseni za kutafuta madini kwenye maeneo ya hifadhi...

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwa nia njema tu kwamba hafahamu makaa hayo.....

MWENYEKITI: Ngoja basi sijakuruhusu...

Mheshimiwa Mbunge unafahamu mimi huwa sipendi hii, tufuate Kanuni, huwezi ukaanza kuzungumza tu mimi sijakuruhusu. (Makofi)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilindie muda wangu, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na utaratibu ambao kunakosekana *coordination* kati ya Wizara ya Madini na Nishati na Wizara ya Maliasili. Wizara ya Nishati na Madini inatoa leseni za utafutaji wa madini ndani ya maeneo ya hifadhi, kwa hiyo imeleta migogoro mingi sana. Kuna baadhi ya maeneo ya hifadhi ambayo mpaka sasa hivi kuna migogoro mikubwa sana mojawapo ni Hifadhi ya Manyara. Wamepewa leseni ndani ya hifadhi, hakuna *coordination* matokeo yake leo kuna migogoro ambayo haiishi. Kwa hiyo, tungependa wakati Wizara inatoa leseni za kutafuta madini kuwepo na *coordination* kati ya Wizara hizi mbili ili kuondoa migogoro ambayo inatokea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nimeangalia kitabu cha Mheshimiwa Waziri, tuna madini ya *Uranium* ambayo tunachimba maeneo mengi sana ya Tanzania, napenda kujua haya madini ya *Uranium* maeneo gani yameanza kuchimbwa, maeneo gani yanafanya kazi, maeneo gani na tunanufaika na madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nilitembelea Mgodi ule wa *Uranium* kule Likuyu Namtumbo, tuliona jinsi ambapo kuna *Uranium* nyingi iko nje, tulitembea pale wanaita *yellow cake*, iko peupe ni ya kukusanya. Kwanza ningependa kujua ule mgodi umeshaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tunanufaika kama Watanzania na lingine wananchi wa eneo lile wananufaika na ule mgodi kama umeshaanza kufanya kazi. Maana naona kimya, nilikuwa nategemea angalau tuone huku kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri, sioni chochote ambacho kimeandikwa huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la REA, kiukweli kwenye sula la REA kwa kiasi fulani limesaidia sana umeme kusambaa, lakini bado changamoto zake ni kubwa sana. Suala la REA kila Mtanzania anashiriki kwa fedha ya REA, hata bibi wa kule kijijini kabisa akinunua lita moja ya mafuta ya taa tayari kasaidia mchango wa REA kuendelea kuwepo kwa kukatwa shilingi 150. Jambo la kushangaza kwa nini fedha zile hazielekezwi zote maeneo yaliyopangiwa?

Mheshimiwa Waziri hebu kesho utuambie, zile fedha ambazo hazikutumika kwa hii miaka mitatu hazikupelekwa kwenye REA zimeelekezwa wapi na ni kwa sababu gani? Kwa sababu kupanga ni kuamua, kama tumeamua kutengeneza mradi wa kusaidia umeme vijijini, tumeamua kama Watanzania, tunawakata kwenye mafuta, kwanye *diesel*, *petrol*, na kwenye mafuta ya taa. Tuwe na nidhamu basi ya matumizi ya hizi hela. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli kama Wabunge wengine walivyosema, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja kwenye Jimbo langu la Kaliua, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kiukweli alikuta hali ni mbaya. Wakati anakuja katika Jimbo la Kaliua tulikuwa na asilimia moja tu ya usambazaji wa umeme wa REA katika Wilaya nzima mpaka alishtuka.

Nashukuru baada ya kuwepo kwake alisukuma watendaji wake angalau shughuli zimeanza kwenda lakini Mheshimiwa Waziri uliagiza tarehe 30 mwezi wa nne, umeme wa awamu ya kwanza na ya pili uwake, mpaka leo ni kijiji kimoja tu kinawaka umeme, hivyo, bado tunayo changamoto nyingi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, REA inahitaji ufuatiliaji wa hali ya juu, siyo suala kwamba watendaji wa TANESCO wanawaachia wale makandarasi hapana. Nimeona mfano mmoja Kaliua, Mameneja walikuwa wamekaa ofisini hawafanyi kazi, walivyonyanyuka kutoka ofisini kuwafuata makandarasi leo kazi inafanyika.

Kwa hiyo, watu wa TANESCO watoke maofisini waende kwa makandarasi wahakikishe kwamba wanawasimamia, makandarasi wale wanapoachiwa peke yao wanafanya wanavyotaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia nguzo zinazopelekwa kwenye maeneo ya vijiji ni chache sana, wanasambaza barabarani mwa kijiji au makao makuu ya kijiji, vitongoji vyote hakuna umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali na Watanzania ni kila Mtanzania anayetaka kutumia umeme atumie umeme, siyo maeneo ya barabarani, ni lazima pia umeme uende mpaka maeneo ya vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni migodi mikubwa ya dhahabu kutolipa Kodi ya Mapato. Leo nimesikia kauli ya ajabu, eti wanasema watu wa migodi wamekuwa wanapata hasara endelevu. Sijawahi kusikia hasara endelevu. Hakuna mfanyabiashara yeyote duniani, hata kama ni mama ntilie akubali kupata hasara endelevu. Kama wanapata hasara endelevu, kwa nini waendeleo kuwepo? Kama wanapata hasara endelevu, kwa nini waendeleo ku-run? Wanakuwaje na watumishi? Wanakuwaje na kila kitu? Hapa ni wizi mtupu. Tunataka migodi yote ilipe kodi. Tumekuwa tunayabeba sana makampuni. Leo kama Tanzania hatunufaiki sana na migodi yetu ya madini kwa sababu wanabebwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati, wametuambia kwamba kuna makampuni yanayodaiwa shilingi bilioni kadhaa. Makampuni ambayo hayakulipa Kodi ya Zuo yanadaiwa shilingi bilioni 89 lakini kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema *Acacia* wamelipa *almost* karibu shilingi bilioni 13. Sasa hebu tujue, Mheshimiwa Waziri utuambie, kwanza haya makampuni mengine ambayo hayakulipa, umesema kuna makampuni matatu hapa ambayo hayakulipa, wamelipa tu *Acacia* kidogo, yale mengine tunayafanyaje, ikiwepo *Mantra* na hao wengine *Tanzania One*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hawakulipa na ni kwa sababu gani? Kwa nini Mheshimiwa Waziri hajatueleza kwenye kitabu chake kwamba wanafanywaje? Kwa sababu ametuambia tu wamelipa *Acacia* kiasi kidogo. Kwanza *Acacia* hawajamaliza, tunataka walipe kodi yetu yote, lakini yale ambayo hawajalipa, tunawafanyaje? Mheshimiwa Waziri, tuache kuwabeba, wanatunyonya, hii rasilimali ni yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la wachimbaji wadogo wadogo. Kwenye Jimbo langu ninayo machimbo ya madini ya dhahabu kwenye eneo la Ulyankulu, machimbo ya Silambu. Tulikubaliana hapa Bungeni Serikali iwezeshe wachimbaji wadogo wadogo, kuwapatia maeneo lakini pia wapatiwe mitaji, pamoja na vitendea kazi. Bado halitekelezwi kama tulivyokuwa tumekubaliana, bado wana hali ngumu ya utendaji wao wa kazi, bado wanahangaika hapa pale, wamekuwa ni watu wa kufanyia kazi kama za utumwa, wanatumika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaomba sana, Serikali inajua na Mheshimiwa Waziri anajua, anawajua wote wako wapi na vitalu vyao, hebu wekeni utaratibu wa kuwawezesha, waweze kunufaika na ile kazi yao wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ndani ya Wilaya yangu ya Kaliua, Kata ya Igwisi, Kijiji cha Twende Pamoja, kuna machimbo ya madini ya mawe, yanachimbwa na kampuni ya CHICO. Kampuni ya CHICO imechimba pale karibu miaka mitatu wanatengeneza kokoto, hawajawahi kulipa chochote kwenye kata ile wala kwenye kijiji kile, lakini kikubwa kuliko yote, kuna nyumba zaidi ya 25 hazijalipwa, baruti zinapasuliwa usiku na mchana, wananchi wale wengine wanateseka, wengine wanazimia, hawajaweza kuhamishwa, lakini wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofuatilia kwa CHICO anasema, sisi tuna-*deal* na watu wa madini. Sasa Mheshimiwa Waziri utusaidie, pale kampuni inapopewa mlima, pale ni mlima wamesambaratisha mlima wote umekwisha, wananchi wanateseka. Hakuna hata *coin* moja ambayo wamewahi kulipa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri ukija kujibu utuambie, wale kampuni ya CHICO ambao mmewapa mlima wa pale Twende Pamoja, Igwisi, wamechimba miaka mitatu, wanatengeneza kokoto, kwa nini hawalipi ushuru unaotakiwa kwa kijiji husika na kwa Halmashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwa nini mpaka leo hawalipi watu haki zao? Wawaondoe pale. Nilishawahi kukuta mwanamke amezimia pale, mpaka kijiji kwa huruma, wakamhamisha wakampeleka sehemu nyingine. Wananchi wa kawaida, lakini Serikali ipo na sheria iko wazi kwamba pale unapotaka kutumia eneo kwa ajili ya matumizi mengine, lazima watu wapewe haki zao waondoke. Makanisa, mawe yanadondoka mpaka ndani ya kitanda cha mtu. Makanisa... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea, Mheshimiwa Philipo Mulugo, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla.

MHE. PHILIPPO A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana angalau kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mfumo mzima wa miradi ya REA. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alifika Jimboni kwangu, wakati anakuja kusuluhisha mgogoro wa Saza nashukuru sana angalau sasa hivi mgogoro umemalizika, japo yapo mambo madogo madogo ambayo nadhani mimi na wewe tunaendelea kuya-solve pole pole, kwa sababu migogoro ya wachimbaji wadogo wadogo, haiwezi kwisha leo wala kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mfumo wa REA, kwenye Jimbo langu la Songwe, kwanza Awamu ya Kwanza sikupata kijiji hata kimoja. Awamu ya Pili nimekuja kupata vijiji vinne; na sijajua hii Awamu ya Tatu, nitapata vijiji vingapi. Naweza kusema ni kama kuna upendeleo fulani hivi, kwa sababu wakati ule wana-sort kwenye Awamu ya Kwanza, walipokuwa wakiandika tu neno Chunya, basi REA vijiji vingi vilienda upande mmoja kwa Mheshimiwa Mwambalaswa, Mbunge wa Jimbo la Lupa. Jimbo la Songwe sikupata kijiji hata kimoja. Baadaye nikawa nimeenda pale Mkoani Mbeya nikaambiwa basi angalau utapata baadhi ya vijiji kwenye Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Pili mwaka 2012 Mheshimiwa Simbachawene alipokuwa Naibu Waziri wa Wizara hii, alitembelea Jimbo langu tukaja tukaandika vijiji kama 15, lakini mpaka hivi ninavyosema ni vijiji vinne ndiyo angalau kuna nguzo na waya lakini hata matransfoma bado na vijiji havijaanza kuwaka. Kwa hiyo, Jimboni kwangu niseme katika huu mradi, hata kijiji kimoja umeme haujaanza kuwaka; toka Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, leo tunakwenda kwenye Awamu ya Tatu. Jamani ninaposema kwamba kuna upendeleo katika baadhi ya maeneo, huo ni upendeleo wa waziwazi Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba hata kama kesho utakapokuwa unatoa majibu, hebu turidhisheni sisi ambao Awamu ya Kwanza tulikosa na Awamu ya Pili bado vijiji ni vichache. Basi kwenye Awamu ya Tatu mtujazie vijiji vingi tuweze kulingana na wenzetu ambao mliwapa Awamu ya Kwanza na Awamu ya Pili; kwa kweli inasumbua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata yule Mkandarasi ambaye amekaa kule Mbeya, SINOTEC yule Mchina, sijui kama ameshindwa kazi, lakini Mheshimiwa Muhongo kwa namna ninavyokufahamu, Waziri uko makini na unachukua hatua pale pale unapoona mtu anakosa, njoo Mbeya utembelee maeneo yale ya Chunya, utakuta kabisa yule mkandarasi labda ameshindwa kazi. Si afukuzwe tu wapewe watu wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji 12 ni vijiji vinne tu na sijajua maeneo ya kwa mama Mbene kule Ileje kama nako kuna kazi zinafanyika. Wapeni wazawa basi hizi kazi kuliko kuwapa Wachina hizo *tender*. Wapeni wazawa, mbona wanaweza wakafanya kazi vizuri? Hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile niongelee upande wa madini. Nadhani kwa Mkoa wa Mbeya Jimbo langu ndiyo lenye migodi mingi kuliko sehemu nyingine, ama tuseme Mkoa mpya wa Songwe, nina migodi karibu 12. Naomba niongelee kitu fulani kinaitwa 0.03 ambayo inaenda kwenye Halmashauri, tunaita *service levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hii inapokuwa *calculated*, watu wa Halmashauri wanakuwa hawapo, kwa sababu pale panakuwa pana TMAA, panakuwa na watu wa TRA, lakini vile vile panakuwa na mmiliki mwenyewe wa mgodi, kama kule kwangu niseme labda moja kwa moja Shanta. Mtu wa Halmashauri anayewakilisha kwamba sasa yule ndiye mzawa, mwenye mgodi mwenyewe anakuwa hayupo pale ambapo unakuta ndege inakuja, inachukua dhahabu, TRA yupo, TMAA yupo, lakini mtu wa Halmashauri anakuwa hayupo.

Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba turekebishe sheria hiyo, kwa sababu tunaibiwa. Mnatupa asilimia 0.03 lakini hatujui ni ya nini kutoka kwenye nini, kwenye mapato gani? Nadhani hata wenzangu wenye migodi kama mkiliangalia hilo, ni kama vile tunaibiwa. Labda Mheshimiwa Waziri uje utufafanulie vizuri juu ya hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba niishauri Serikali, mtueleweshe vizuri, ile *service levy* mnayotupa kwenye Halmashauri, ile ela imetoka kwenye mapato ya nini? Sasa kwa nini ndege inapokuja pale Saza, inachukua madini, TRA yupo, anawakilisha Serikali Kuu, TMAA yupo, naye anawakilisha Serikali Kuu, lakini mtu wa Halmashauri anakuwa hayupo, kama yupo labda yupo Afisa Madini ambaye naye sio mkazi wa maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka sisi wakazi, maana yake Baraza la Madiwani liteue labda Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango na Fedha wa Halmashauri, awe anakuwepo pale ambapo ndege inakuja inachukua dhahabu na yeye yupo, tuweze kujua kwamba basi kama ni bilioni kadhaa, ndiyo una-*calculate* sifuri nukta sifuri tatu ndiyo imechukuliwa hapa, ndio inakuja kwenye Halmashauri, ningependa sheria hiyo kidogo tuweze kuirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sikuwa hata nimesomwa kwamba nitaweza kuchangia leo, nimesomwa tu huku nimetoka kusalimia huko, nilikuwa

natembea kidogo nimetoka nje, lakini nilikuwa nimejiandaa angalau mambo mawili haya niweze kuchangia Wizara hii. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Norman Sigalla, yupo? Mheshimiwa Desderius Mipata.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Na mimi niungane na wenzangu kuchangia hotuba ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima, lakini vilevile nawashukuru wana Nkasi Kusini kwa namna ambavyo wananipa ushirikiano wakiwepo viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi, Mkurugenzi wangu Kaondo, DC wangu Kimantra na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana mkono na watu wote wanaosema kazi ya Wizara hii ni nzuri na Mheshimiwa Muhongo pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Kalemani wana uwezo wa kutosha na wanafanya kazi vizuri sana. Mimi bahati nzuri niko kwenye Wizara hii, naona uongozi wanaoutoa kwetu sisi ushirikiano kama wana Kamati, lakini pia kwa Wizara nzima. Kwa hiyo, tunawatia moyo na kuwapa *big up*, waendele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la muhimu ni kwamba katika kazi ya kupeleka umeme vijijini, yapo maeneo yamebaki nyuma. Kwa mfano, tunaposema umeme mkubwa Gridi ya Taifa, Mikoa kama ya uzalishaji ya kilimo kama vile Rukwa na Katavi wamechelewa na Kigoma pia hawajapata. Tunaomba Wizara ifanye juhudi kuhakikisha kwamba tunapata umeme mkubwa ili tuweze kulisimua maendeleo katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Mkoa wa Rukwa yako hodari kwa kilimo, namna pekee ya ku-*attract* wawekezaji katika kuongeza thamani ya mazao yetu ya kilimo ni kupatikana kwa nishati ya uhakika. Vilevile katika maeneo ya Namwele, Komolo II pale kwenye Jimbo langu, kuna *deposit* ya kutosha ya makaa ya mawe, muichunguze, ambapo inaweza ikasaidia kuongeza umeme katika Gridi ya Taifa kama inapita sehemu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo tunahitaji kupata umeme ni vijijini kwa kupitia REA. Kusema ukweli utekelezaji wa REA Awamu ya Kwanza na ya Pili kwa Wilaya yangu na Jimbo langu, umetia moyo sana wananchi kwa utekelezaji wa Serikali hii. Kwa hakika ni kitu ambacho tumejivunia hata kurudi hapa Bungeni. Nawapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa tu ninaloliona ni kwa Serikali kutopeleka pesa ya kutosha inayotengwa kwa REA. Hiki kimekuwa kikwazo kikubwa ambacho kinarudisha juhudi kubwa zinazofanya na watendaji wakuu hawa wa Wizara huko vijijini. Umeme unakuwa hauendi kwa wakati. Sasa tunaweza tukajidanganya tena, leo tumetenga hela za kutosha, lakini kama mtindo ni huu wa kutowapa pesa, bado tutarudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya kupeleka umeme vijijini, wenzangu wamesema, ni ya muhimu sana, inatusaidia hata kuokoa suala la mazingira. Umeme utakapofika vijijini kote, tutaokoa tatizo la uharibifu wa mazingira kwa sababu litapeleka nishati, ukiachilia mbali ajira na mambo mengine ambayo yametajwa na wenzangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu, mwaka 2015 tulitarajia kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Jimbo, Kate, kupitia vijiji vya Kalundi, Miula, Komolo II, Katani, Chonga lakini mpaka sasa umeme haujawaka. Bado vijiji ambavyo vimeorodheshwa tena katika awamu hii, naomba na vyenyewe vifikiliwe, navyo viko katika vijiji vya Tuchi, Kitosi, Sintali, Nkana Mkomanchindo, Kasapa na Kata tatu za Mwambao wa Ziwa Tanganyika. Mheshimiwa Waziri kata tatu za mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata tatu za mwambao mwa Ziwa Tanganyika naomba uziwekee umuhimu wa mbele sana, ni maeneo ambayo hayana barabara na kila mara huduma tunawafikishia kwa kuchelewa na wakati mwingine hawapati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ninavyozungumza, Kata hizi hazina mawasiliano ya simu, hazina barabara nzuri, lakini juhudi na uthubutu wa Wizara hii nafikiri mnaweza mkawahi ninyi. Nawaomba kwa heshima niko chini ya miguu yenu, naomba mwapelekee wananchi hawa ili waweze kuonja neema ya nchi yao. Wananchi hawa wa Kata hizi wamekuwa wakizalisha samaki, wanavuna sana samaki, lakini wanazipeleka Zambia kufuata soko, kwa sababu hatuna uwezo wa kuchakata minofu. Utakapopeleka umeme utatusaidia sana kuhakikisha kwamba sasa wanaweza wakapata wawekezaji ambao wanavutiwa na nishati hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *geological survey*. Mkoa wa Rukwa, una miamba na mazingira yanayofanana na sehemu nyingine nchini, lakini hatuna bahati ya kupata aina yoyote ya madini tunayoshughulika nayo kule.

Kwa hiyo, inaonesha kwamba utafutaji wa madini katika maeneo yale, kazi hiyo haijafanywa kwa juhudi ya kutosha; na tunaona mahali ambapo juhudi zimefanywa watu wanapata ajira, mzunguko wa pesa umekuwa mwingi

na wawekezaji wamepatikana katika maeneo ambayo tumeona madini yamepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba kitengo kinachoshughulika na kazi hiyo, kijaribu kutafuta kwa nini Mkoa wa Rukwa tu pasipatikane madini yoyote ambayo tunashughulika nayo kwa sasa? Hebu tujaribu kuona katika nchi yote, ni eneo gani tunaweza tukanufanika? Ni aina gani ya madini yanaweza yapatikana katika maeneo hayo? Zipo *traces* na watu wengi wamekuwa wakija wanazunguka zunguka, siyo maalum sana, lakini wanapata na wanasafiri wanarudi. Kwa hiyo, inaonekana kama juhudi ikifanyika ya kutafuta madini, tunaweza tukapata madini ambayo yanaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamesema hapa jiografia inatueleza kwamba maumbile ya miamba yaliyoko Rukwa na yale ambayo yako kwenye eneo la Ziwa Albert kule Uganda ambako kulipatikana mafuta, yana asili moja. Sasa kama yana asili moja, maana yake, juhudi ikifanyika zaidi tunaweza tukanufaika na jambo hilo la kupata mafuta katika Bonde la Rukwa. Kwa hiyo, tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kama siyo mwaka juzi, Wizara ilitueleza kwamba kuna leseni ya kutafuta mafuta katika maeneo ya Ziwa Tanganyika, hasa katika Jimbo langu au kule juu; na nimeona juhudi ya hawa watu waliokuwa wanatafuta, lakini sijaona kama imeripotiwa humu kwenye hotuba yako na ningependa kupata maelezo hawa watu hoja yao imeishia wapi? Walisema mnataka leseni msizitoe ili watu waweze kuanza kutafuta mafuta katika maeneo hayo. Sasa ni kitu kimekaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikizunguka kwenye ziara yangu, wananchi wananiuliza, nitakosa kupata majibu, kwa sababu wameona ambavyo watu wameenda, wamezunguka sana, lakini sasa nimeona kwenye bajeti hii hakuna kitu kilichotajwa kama hicho.

Mheshimiwa Waziri, naamini udhubutu wako unaweza, tuhakikishe kwamba ziwa lile Tanganyika nalo tukilifanyia kazi vizuri tunaweza tukafanikiwa kupata aina fulani ya madini, kama siyo mafuta na tukanufaika kama hao wengine wenzetu ambao sasa hivi Mtwara wameonesha kabisa matumaini kwamba pamoja na kwamba walikuwa wamebaki nyuma kidogo, sasa hivi wanakuja juu na uchumi wao utapanda kwa haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana, naomba umeme ufike katika Jimbo langu la Nkasi Kusini uwashwe, waya umeshafika lakini bado kuwasha na pengine mnawapa wakandarasi goigoi. Huyu Mchina ambaye anajenga huu umeme kupeleka kwenye Jimbo langu,

hata kwa Mheshimiwa Malocha amezungumza hapa, ni mtu nadhani hana uwezo wa kutosha. Mjaribu ku-recruit watu ambao ni wenyeji wetu. Muwatafute wazawa ambao watakuwa na uchungu pia wa uzalendo. Hawa wenzetu, hata mimi nina wasiwasi na vifaa vyenye haina *specification* ya kutosha, wanakuja vina-bounce, vinakuwa haviwezi kufanya kazi vizuri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea. Mheshimiwa Jamal Kassim Ali atafuatiwa na Mheshimiwa Alex Gashaza.

MHE. JAMAL KASSIM ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuchangia jioni ya leo. Awali ya yote, napenda kuwashukuru Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa kunichagua kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM. Nawaahidi kwamba nitaitumikia nafasi hii kwa maslahi yetu na maslahi ya chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa bajeti nzuri kabisa ambayo imetafsiri ile dhana ya Mheshimiwa Rais ya kwenda kwenye Tanzania ya viwanda, Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo nakupongeza sana. Hao wanaokubeza, naamini kabisa ndani ya nafsi zao wanajua kwamba katika viongozi wenye dira wewe ni miongoni mwao. Naweza kudiriki kusema kwamba wewe sio wa Kitaifa, bali wewe ni wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja, kwenye upande wa umeme. Tumeona jitihada za Mheshimiwa Waziri na wataalam wake katika kuipeleka Tanzania kuondokana na changamoto mbalimbali za umeme ambazo ilikuwa inakabiliwa nazo huko nyuma. Tumeona coverage ya umeme ilivyoongezeka, upungufu wa bei, ongezeko la *install generation capacity*, kwa hiyo, nawapongeza sana. Naamini bado tuna changamoto kubwa katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshauri Waziri na Wizara na sekta husika kwamba kuna maeneo inabidi tuzidi kuyafanyia kazi ili kuhakikisha kwamba ile dhamira ya kuwa na umeme wa uhakika na wenye kutosheleza inafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye mpango wetu wa miaka kumi hadi mwaka 2025 tunatarajia kuwa na umeme usiopungua *megawatts* 10,000 na sasa tupo kwenye *megawatts* 1461. Kwa hiyo, tunatakiwa kwa hesabu za haraka haraka, kwa wastani kila mwaka tuongeze *install generation capacity* isiyopungua *megawatt* 948. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli *Megawatts* hizi ni nyingi sana na kwa kuiachia TANESCO peke yake hawataweza. Ninachokusudia kusema ni kwamba kuna haja ya kufanya *reform* katika sekta yetu ya umeme. Tunajua TANESCO imekabiliwa na changamoto nyingi katika muda mrefu. (Makofi)

Kwanza, shirika letu hili la umeme kwa kipindi cha takriban miaka minne sasa limeshindwa kuzalisha faida, linaendeshwa kahasara, kwa hiyo, halina mtaji wa kwenda kuwekeza kwenye uzalishaji wa umeme wote ule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hata ukiangalia vitabu vyao vya mahesabu, pia wana-*operate* katika *deficit working capital*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba kabisa wakati umefika kwenda kufanya *reform* ya sekta ya umeme nchini mwetu. Serikali ifungue milango, wawekezaji binafsi waingie katika uzalishaji na katika usambazaji wa huduma hii muhimu kwa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatufanya kwanza kupata ongezeko kubwa la umeme kwa sababu tutafungua mwanya kwa wazalishaji wengi kuingia, lakini tutapata nafasi ya mashirika haya ambayo yanafanya usambazaji wa umeme ku-*compete* na kushusha bei ya umeme; na yenyewe yata-*compete* kwasababu yatakuwa katika *business oriented*. Naamini kabisa yataendeshwa kibiashara na yatazalisha faida tofauti na sasa ambavyo TANESCO inavyoenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa *East Africa* wote walikuwa na matatizo kama ya kwetu, wenzetu Wakenya walikuwa na kama ya kwetu au kuzidi ya kwetu; Waganda hali kadhalika, lakini walifanya *reform* kubwa kabisa katika sekta hii muhimu ya umeme, lakini hatimaye leo mashirika yao yanazalisha faida, hayaendi kwa ruzuku na pia wanapata wasaa wa kuchangia pato kwa Serikali kama sehemu ya gawio la Serikali. Kinyume na hapa kwetu ambapo Shirika letu la TANESCO mara zote limekuwa kila mwaka likiendeshwa kwa ruzuku ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kabisa Mheshimiwa Profesa nia hii unayo, dhamira unayo na uwezo unao. Kwa hiyo, ni wakati sasa wa kufanya *reform* kubwa ya kuhakikisha tunaenda katika uzalishaji ambao ile dhamira ya kufikia kwenye Tanzania yenye viwanda tunafikia. Kwa sababu bila kuwa na umeme wa kutosha na uhakika, suala la viwanda litabakia kwenye vitabu vyetu na mipango yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, niende kwenye upande wa EWURA. Nimepitia kitabu cha bajeti, ukurasa wa 80 kuna jedwali lile la bei elekezi za EWURA za umeme. Katika jedwali lile kuna vitu nimebaini niweze kusema ni changamoto ambazo naomba Mheshimiwa Waziri uzifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia upande wa *tariffs* hizi za bei ya mahitaji ya juu (*demand charges*); mteja ambaye yuko katika *T3HV* (*high voltage*) wanachajiwa shilingi 16,550 kama tozo lao la bei ya mahitaji ya juu, wakati *logic* hapa hawa waliokuwa kwenye *transmission line*, *cost* ya kuupeleka umeme kwenye *transmission line* ni ndogo *compared* na *cost* ya kuupeleka umeme kwenye *T3MV* na *T2*, lakini wamebebebwashwa mzigo mkubwa ambao hata najjuliza *EWURA* walipoweka hii bei walikusudia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wateja waliokuwepo hapa ni watatu tu waliokuwepo kwenye *T3HV*. Kuna Shirika la Umeme la Zanzibar, Bulyankhulu na Twiga Cement. Kwa mfano, kwa upande wa Shirika la Umeme la Zanzibar, ni *bulk purchaser* ambao waliingia mikataba na *TANESCO* ya *Purchase Power Agreement* ambayo sasa baada ya kuja *EWURA* ile mikataba imekuwa haina nguvu tena. Huyu ni *bulk purchaser* ambaye mwenyewe anatarajia huu umeme auze kwa wateja wake wa kati na wadogo. Sasa kama tunam-charge katika bei hii tunatarajia yeye auze kwa shilingi ngapi? Kusema ukweli katika kipindi kirefu kumekuwa na mlundikano wa madeni ambayo *ZECO* inadaiwa na *TANESCO*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huenda moja ya sababu ya madeni haya naweza kusema ni *appropriate tariff* ambayo *ZECO* imekuwa ikitozwa kama ambavyo tunavyoona katika mwongozo huu wa bei ambao *EWURA* wameutoa mwezi Aprili. Kwa sababu wao wanachukua umeme katika *transmission level* ambapo gharama za *depreciation*, gharama za *maintenance* katika *level* hiyo ukilinganisha na wanaochukua *T3MV* na *T2* ni ndogo lakini wamepewa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako, tunaendelea.

MHE. JAMAL KASSIM ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alex Gashaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia afya na uzima kuwepo ndani ya jengo hili.

Pili, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi, kwa sababu tangu Mkutano wa Tatu umeanza nilikuwa sijapata nafasi ya kuchangia, nakushukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake na timu nzima kwa hotuba nzuri ambayo wameilata mbele yetu, hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mmoja anatambua umuhimu wa nishati hii ya umeme kwamba ni nyenzo muhimu katika maendeleo na mageuzi ya kiuchumi katika nchi yoyote ile. Kila Idara, kila sekta na kila Wizara inaguswa na Wizara hii, kwa maana hiyo ni *cross-cutting Ministry*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na nishati ya umeme, katika Wilaya yangu ya Ngara Jimbo langu la Ngara, nina kila sababu ya kuipongeza Wizara hii na kumpongeza Mheshimiwa Profesa Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika Jimbo langu la Ngara. Amenitembelea Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo ametembelea Naibu Waziri, ametembelea Waziri Mkuu katika kuzindua Mradi wa *Orion Holland* ambao utazalisha megawatt 2.5 kitu ambacho nina amini kwamba kinafungua fursa kwa wananchi wa Jimbo la Ngara na kwa Taifa kwa ujumla kuleta maendeleo na hasa katika sekta ya uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima niendeleo kukupongeza kwa jitihada zinazoendelea sasa kwamba kufikia mwezi wa nane mwaka huu Wilaya yetu ya Ngara itakuwa imeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa, kwa hiyo, kuendelea kutupa fursa ya kuwa na umeme wa kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi, Wilaya ya Ngara ni Wilaya ambayo mradi mkubwa ambao ninaweza kusema ni mradi ambao upo kwenye zile miradi ya *flagship project* ya umeme wa maporomoko ya Rusumo ambapo umeme huo utazalisha takriban megawatt 80, kati ya hizo megawatt 27 zitakuwa upande wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Profesa Muhongo kwamba wananchi wa Jimbo la Ngara wanafurahi na wanakupongeza kwa jitihada hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kwamba sasa tutakuwa na umeme wa kutosha ndani ya Jimbo la Ngara, kwa kuzingatia kwamba kwa sehemu kubwa tuna vijiji takribani 49 ambavyo mpaka sasa hivi havijafikiwa umeme, lakini kwa uhakika kwamba kufikia mwezi wa nane mwaka huu tutakuwa na umeme wa kutosha, wanataraji kwamba REA III sasa iweze kugusa vijiji vyote na vitongoji vyote takribani 240 ambavyo vimebaki ili kusudi umeme huu uweze kuleta tija. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye upande wa madini. Mheshimiwa Waziri anatambua kwamba Wilaya ya Ngara ni Wilaya ambayo ina madini mengi ambayo yanaweza yakaleta mabadiliko makubwa katika uchumi wa Tanzania. Wilaya ya Ngara ina madini ya *nickel* na ndiyo maana hata katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ile reli ya kati wameelekeza kwenda Keza. Keza iko Ngara ambapo kuna madini ya *nickel*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini haya ni madini ambayo kwa Tanzania yanaifanya Tanzania i-*rank* nafasi ya tatu duniani kwa kuwa na *deposit* kubwa ikitanguliwa na Russia pamoja na Canada. Kumekuwepo na vikwazo ambavyo vimepelekea mgodi huu wa *nickel* usianze, mgodi ambao umeanza utafiti tangu miaka 1973. Nina uhakika wengi wetu humu walikuwa hawajazaliwa, lakini mpaka leo mgodi huo haujaanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu miaka 2002 kumekuwepo na ahadi kwamba mwaka kesho tutafungua, mwaka kesho tutafungua mgodi, lakini mpaka sasa hivi bado mgodi huo haujafunguliwa. Kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano umeeleza vikwazo vitatu ambavyo vilikuwa vinaonesha kwamba mgodi huu ili uweze kufunguliwa ni lazima vikwazo hivyo viwe vimeondolewa. Ni pamoja na kikwazo cha umeme, kikwazo cha miundombinu ya usafiri na kikwazo cha bei kwenye Soko la Dunia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikwazo hivyo viwili naweza kusema kwamba vimeondoka kwa sababu umeme sasa ambao tunategemea kuwa nao katika Wilaya hii ya Ngara ni umeme wa kutosha kuendesha mgodi huo na wananchi vijiji vyote wakapata umeme kwa matumizi ya majumbani na hata kwa matumizi ya viwanda vidogo vidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mawasiliano kulingana na bajeti kwamba reli ya kati sasa kwa *standard gauge* ndani ya miaka mitatu, minne ijayo kwa maana kufikia mwaka 2019 yawezekana tayari reli hii ikawepo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba madini haya muhimu na ambayo yanaweza yakaleta mabadiliko ya uchumi katika nchi yetu, inaonekana kama vile inasahaulika sahaulika kwamba madini hayo yapo na mradi huu upo. Kwa sababu hata kwenye kitabu hiki cha bajeti haikuonesha kwamba mradi huo unafikiriwa. Ndiyo maana hata wawekezaji katika mgodi huo (*Barrick*) leo ukiangalia hakuna shughuli zozote zinazoendelea pale mgodini, pamoja na kuomba *retention* ya miaka mitano kwa maana ya mwaka 2015 kwenda 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgodi haujengwi kwa siku moja, haujengwi kwa miaka miwili au miaka mitatu; tunahitaji kuona kwamba kunakuwepo na msukumo na kampuni hii ambayo inahusika pale iweze kuweka nguvu tuone

jitihada. Sasa hivi wame-*abandon site*, hakuna kinachoendelea. Tunahitaji kuona jitihada zinazofanywa na Wizara hii kwa maana ya Serikali kuhakikisha kwamba wanapeleka miundombinu inayotakiwa, iende sambamba na jitihada zao katika kufanya maandalizi. Tunajua kufanya fidia siyo chini ya miaka miwili, wananchi hawajafidiwa.

Kwa hiyo, naomba Wizara iweze kusukuma kampuni hiyo ianze maandalizi ya ujenzi wa mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pia katika Wilaya ya Ngara kuna madini ya *manganese*. Ipo kampuni ambayo sasa inafanya utafiti na uchimbaji pale. Nilikuwa najaribu kuteta na Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwamba mazingira yalivyo ya shughuli inavyofanyika, inahitaji wakajiridhishe. Tuna mashaka kwamba pengine hawakufuata taratibu na sheria za utafiti na uchimbaji. Barua ambayo mwekezaji huyu ameandikiwa na Wizara ya Nishati na Madini kupitia Kanda Maalum, ni kwamba ni lazima awasiliane na Halmashauri na afuate taratibu na sheria za Halmashauri. Hakuripoti Halmashauri na mpaka sasa hivi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imebidi kumwandikia barua kusitisha ili tuweze kupata ufafanuzi. Ninaamini kwamba hilo wataweza kulifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye gesi. Baada ya kugundua gesi nchini Tanzania, imeonekana kwamba sasa ni tumaini la Watanzania wengi kwamba gesi hii itaweza kuleta mabadiliko ya kiuchumi na gesi hii maeneo mengi ndani ya nchi hii tunaitegemea ili iweze kusaidia kwa kuzalisha nishati ya umeme lakini pia hata kwa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kuishauri Wizara hii ni kwamba tujaribu kuangalia ni namna gani ambavyo tunaweza ku-*establish substations* ambazo zitatumika kwa ajili ya kusambaza gesi hii katika maeneo mbalimbali ikiwezekana kutenga *substations* hizi kikanda ili kusudi wananchi wote waweze kunufaika na gesi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba yapo makampuni kadha wa kadha ambayo yako tayari kuja kuwekeza kwa maana ya kutumia gesi hii na kufanya uzalishaji wa umeme. Kuna kampuni kutoka Uturuki, kuna kampuni kutoka maeneo mbalimbali ambao wanatamani waingie Tanzania kwa ajili ya kutumia gesi hii. Tunapoweza kukaribisha makampuni hayo, nina uhakika kwamba yataweza kutusaidia katika kuzalisha umeme wa kutosha kutokana na gesi na kusambaza kwa wepesi zaidi na kuweza kuleta mabadiliko mazuri ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye madini ambayo ni *unique*, madini ya *Tanzanite*. Kwa muda mrefu tumekuwa tukipiga kelele kwamba inakuwaje

Tanzanite ambayo ni madini yanayozalishwa Tanzania peke yetu tunakuja kujikuta kwenye Soko la Dunia Tanzania tuko nyuma; eti nchi kama Kenya na *South Africa* ndio ambao wanaonekana kuuza na kuteka soko la *Tanzanite!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatutia aibu. Hebu niombe Wizara husika iweze kujikita na kuona ni namna gani ambavyo tunaweza tukawa na umiliki wa *Tanzanite* kama fahari ya Tanzania na madini ambayo yanaweza yakainua uchumi wa Tanzania na kuleta manufaa kwa wataanzania walio wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika hili, hata kama ni kutafuta wataalam wa kufanya utafiti ili kuona ni namna gani ambavyo tunaweza tukarejesha heshima ya madini haya, kama nembo ya Taifa hata kwa jina lenyewe kwamba ni *Tanzanite* kwa maana ya kwamba ni madini yanayopatikana Tanzania tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kwamba Wizara hii imejipanga na ndiyo maana hata katika bajeti yake imeonesha jinsi ambavyo matumizi kuelekea kwenye bajeti ya maendeleo imepewa kipaumbele kikubwa, asilimia 94. Zaidi ni pale ambapo nimefarijika kwamba katika fungu hili la maendeleo takribani asilimia 68 ni bajeti ya ndani ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha kwamba ni rahisi na tutaweza kufanikiwa kutekeleza miradi hii ambayo tumeipanga kwa sababu ya own source kwa maana ya kwamba ni pesa za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimtie moyo Mheshimiwa Profesa Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini; unajua wakati mwingine unapoenda kufanya kitu kizuri wengine hawakubali, ndiyo maana mtu mmoja akasema kwamba *don't focus on barriers or obstacles, always focus on your destiny*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba Wizara hii chini ya Profesa Muhongo, mmeamua kuleta mabadiliko makubwa ndani ya nchi hii kwa sababu viwanda vitapatikana kutokana na nishati ya umeme, huduma bora za afya zitapatikana kutokana na nishati ya umeme kwa maana ya kutumia mitambo, *Ultra Sound* na *CT-Scan*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ubora wa huduma ya afya kwa Mtanzania inatokana na nishati ya umeme. *Just keep on, usibabaike, songa mbele*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, tunakushukuru kwa mchango wako. Tunaendelea na mchangiaji wetu anayefuata, Prof. Norman Sigalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa na Mheshimiwa Ally Seif Ungando ajiandae.

MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii.

Kwanza kabisa napende kumpongeza Mheshimiwa Sospeter Muhongo na msaidizi wake na timu yake nzima kwa kazi kubwa ambayo wanalifanyia Taifa hili kuhakikisha kwamba nishati ya umeme inapatikana. Sambamba na hilo, napongeza kwa sababu ni ukweli ulio bayana kwamba kwa sasa Tanzania ni moja ya nchi ambazo zinafanya vizuri zaidi Afrika, kwa maana ya coverage, yaani kwenda kwa kasi katika kusambaza umeme. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua uwezo wako na weledi wako, lakini nimesikitika sana ulipokuwa unawasilisha bajeti yako, hasa baada ya kuona Mto Lumakali ambao uko Makete ambao *study* yake ya kwanza imekamilika mwaka 1998 ikionesha kwamba tuna uwezo wa kuzalisha umeme *megawatts* 222; ikarudiwa tena mwaka 2002, ikaonesha kwamba tuna uwezo wa kuzalisha *megawatts* 340.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mto pekee ambao *study* kwa miaka 60 inaonesha kwamba maji yake hayapungui. Ninatambua changamoto tuliyonayo kwenye mito mingi iliyoko Tanzania, ni kupungua kwa maji. Ndiyo maana wakati nachangia Mpango wa Serikali nilisema Mheshimiwa Sospeter Muhongo anaonekana ana ugonjwa wa gesi; bila shaka nilimtania, lakini najaribu kusema kwamba upo umuhimu mkubwa wa kupeleka nguvu kubwa kwenye mradi wa maji wa Mto Lumakali unaopatikana Makete, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unajumuisha kuweka kingo za bwawa. TANESCO wameshafika mara nyingi kule, makampuni ya Afrika Kusini, China yamefika kule, yameshawaweka tumbo joto wananchi wangu wa Makete kwamba mpaka hapa tutakuwa na bwawa. Wameendelea kusubiri toka mwaka 1998 bwawa hilo halitokei.

Naomba sana Waziri mhusika aone umuhimu wa kipekee sana kupeleka bwawa hili. Bwawa hili pamoja na uzalishaji wa umeme litakuwa muhimu kwa uchumi wa Nyanda za Juu Kusini na Tanzania kwa ujumla. Utakuwa umepanda zao jipya la samaki kuvunwa katika bwawa hili la Lumakali pamoja na Mto wenyewe wa Lumakali. Kwa hiyo, ni muhimu sana jambo hili likatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena Wizara ione umuhimu wa kupeleka maeneo yaliyosalia umeme wa REA na hasa Kata za Lupila, Mbalache, Ukwama, Mang'oto, Kipagalo, baadhi sehemu za vijiji vya Tarafa ya Magoma, Tarafa ya Ikuo, Tarafa ya Matamba na Tarafa ya Lupalilo. Ni jambo la msingi sana ili wananchi wa Makete wapate kuleta maendeleo kwenye nchi yetu. Kwa bahati nzuri unatambua, wananchi wa Makete kwa asili ni wachapakazi, kwa hiyo, nishati ya umeme kwao ni nguzo pekee ya muhimu itakayowezesha tukimbizane na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kidogo eneo la madini. Sheria ya Madini ni muhimu sana ikafanyiwa marekebisho. Utaratibu uliopo sasa wa kupata leseni Makao Makuu na kupewa eneo Makao Makuu bila ushiriki wa Halmashauri husika, hautendi haki. Ni muhimu sana tutengeneze mahusiano kati ya Mamlaka ya kutoa leseni na Halmashauri mama yenye kumiliki ardhi ambayo inaangukia kwenye eneo hilo ili kuondoa migongano isiyo na sababu lakini pia ili kuwapa faida wananchi ambao maeneo haya kimsingi ni ya kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie EWURA. Wenzangu wallyotangulia walikuwa wanasema kwamba wana *interest* na maeneo hayo; nami kwenye madini pamoja na mafuta nina-*declare interest*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Makete pale mjini ina vituo vinne vya mafuta. Wamekwenda Maafisa wetu wa EWURA kufunga vituo vyote. Makete hakuna *transit*, kwa maana ya malori yanayobeba mafuta kupita Makete. Mafuta haya yanatwaliwa Dar es Salaam kwenye *depot*. Ni muhimu sana Maafisa wetu wa EWURA wajikite kwenye ku-*control quality* Dar es Salaam yanakotoka mafuta. Wajikite kwenye kufanya mahusiano stahiki na mamlaka nyingine zinazohakikisha kwamba mafuta yanayokwenda nchi jirani yanakuwa *monitored* ili kwamba mafuta hayo yasipelekwe mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo sahihi hata kidogo, inaonekana kama ni uonevu hivi kidogo, pale ambapo mafuta yanatoka Dar es Salaam, muuzaji wa mafuta yuko Makete, kilometa 900 kutoka Dar es Salaam, hakuna barabara inayopita kule kwenda nchi jirani, barabara yenyewe ni mbovu, halafu wafanyabiashara hawa wanafungiwa vituo vyao kwa sababu tu ya maafisa wetu wa EWURA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa labda nimwombe Mheshimiwa Waziri, ninaamini sana katika *competence based recruitment*, ninaamini Sheria ya EWURA ni nzuri, kwenye hili, tatizo ni la watu. Tusioneane haya kwenye hili. Tatizo ni la maafisa wetu. Ni muhimu sana, maafisa wetu, sheria hata ingekuwa nzuri, kama *an official* ni *corrupt* ata-*jeopardize the entire system*.

Kwa hiyo, ni muhimu sana maafisa wetu hawa waangaliwe ili wanapofanya maamuzi, basi waone madhara ya uchumi pia. Tukisema hivi, hatumaanishi kwamba sasa watu waendeleo kuvunja sheria, hapana. Tunachotaribu kusema ni kwamba mafuta yanakotoka yanajulikana, ni Bandari ya Dar es Salaam pekee inayoingiza mafuta Tanzania. Kwa hiyo, eneo la *ku-control* linajulikana. Inaumiza sana kuona watu wa Makete nao wanafungiwa vituo vyao kwa sababu tu ya maafisa hawa wanaoshindwa kuzingatia umuhimu wa kuzingatia mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize kusema kwamba Tanzania kwa sasa ninafahamu, tunakoelekea ni kuzuri, tena kuzuri sana na kazi hii kwa vyovyote vile nitakuwa nimekosa nidhamu kutokumsifia Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa maamuzi yake ya kuongeza bajeti ya jumla ya maendeleo kufikia asilimia 40. Leo Waziri mwenye dhamana anatuambia, asilimia 94 ya bajeti yake inakwenda kwenye maendeleo. Mungu aibariki sana Tanzania na Mungu aibariki sana Serikali ya CCM kwa jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, Mungu awabariki sana. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa. Tunaendelea, Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Seif Ungando.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Muhongo na Naibu wake kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya katika kuhakikisha kwamba umeme unasogea na nishati ya umeme na madini zinaweza kusogea katika majimbo yetu na katika nchi yetu ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza tu napenda kugusia maeneo machache sana. Hotuba hii wengi wameshachangia na wameeleza kwa undani zaidi namna gani umeme ulivyokuwa na umuhimu katika majimbo yetu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kujikita katika maeneo ya *research na development*. Nchi yetu ya Tanzania dakika hii kama tutafanya *research* ya kutosha, tutajikuta kwamba maeneo mengi ya nchi yetu yana madini, maeneo mengi ya nchi yetu yana kila aina ya utajiri ambao ungeweza kutusogea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu maeneo mengi ambayo tume-concentrate kama maeneo ya utafiti tumejikita katika eneo moja; eneo la madini tu. Madini hayo tumeangalia katika upande wa madini machache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo katika nchi yetu ambayo yana madini ya kutosha na kuna watu ambao wameshaingia katika maeneo hayo na kuanza kupata faida na kuhakikisha kwamba wanachukua rasilimali zetu zote bila kujali nini wanakiacha katika nchi yetu ya Tanzania. Sababu moja, ni kukosa kufanya utafiti wa kutosha na kuhakikisha kwamba tunapata faida katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Kalenga kuna eneo ambalo tayari watafiti wamefika, wageni wamefika na wameanza kuchimba, lakini bado kama nchi hatujapeleka wataalam kule kuhakikisha kwamba maeneo haya kama Watanzania tunafaidika vipi? Hii inatugharimu sana kwa sababu tumekosa kufanya utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo hilo la utafiti, najikita hasa katika maeneo muhimu sana. *Tanzanite* kama nchi ya Tanzania tumeshindwa kuitumia na tumeshindwa kufaidika kupitia *Tanzanite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1967 *Tanzanite* ilipogunduliwa katika nchi yetu ya Tanzania mpaka leo hii tunaweza tukasema yote lakini bado hatujapata faida. Kama watu ambao tunaichimba na tunaitoa *Tanzanite* katika nchi yetu, bado tunasimama katika nafasi ya nne katika uuzaji, haya ni maajabu ya dunia. Nchi ya Kenya inatutangulia, Afrika Kusini inatutangulia, India inatutangulia, sisi ndio wenye *Tanzanite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utafiti umefanywa na Waingereza, pesa ambayo tunaikosa katika nchi yetu kupitia *Tanzanite* ni kubwa. Kama tutaamua kwa hali na mali kujikita katika eneo hili na kama wachangiaji waliopita walivyoieleza, inasimamisha au inasimama kwa nembo ya nchi yetu, inasimama kwa jina la nchi yetu, tufanye nini zaidi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kusesitiza eneo hili ambalo lingetupa sisi pesa nyingi za kigeni, lingetusaidia sisi kuhakikisha kwamba miradi mbalimbali nayo inaendelea. Jambo moja ambalo naliona kama tatizo kubwa, ni namna gani tunaipoleka *Tanzanite* katika nchi za kigeni ili tuweze kwenda kuiuza? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni kwamba bado tuna miundombinu mibovu, usafirishaji wetu bado haujakaa vizuri. Kama tutapata ndege ambazo zitakuwa zinaweza kusafirisha *Tanzanite* hii kupeleka nchi za nje

kwenda kuuza tuka-compete na nchi kama Kenya ambao wana ndege zaidi ya 45, South Africa wenye ndege zaidi ya 76 wanachukua *Tanzanite* hapa wanakwenda kuuza nchi za nje, wanatangaza nchi zao kwamba zinapatikana katika nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la muhimu sana kuhakikisha kwamba tunaamka na tunafanya jambo moja la muhimu kuhakikisha kwamba pesa zote ambazo tumekuwa tukizikosa tunazirudisha katika nchi yetu kupitia *Tanzanite*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kujikita katika miradi ya REA. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake yote kwa ujumla kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Kalenga, bado tunahitaji nishati ya umeme, lakini tunaipataje nishati ya meme? Leo hii bado ninafahamu kwamba tuko kwenye *Phase Two* ambapo miradi hii na nguzo zinapita kwenye barabara kuu. Ifike wakati sasa wananchi wetu tunajua kwamba wameshaanza kusogea ndani na vijiji vyetu vimeendelea kutanuka, mashamba yameendelea kulimwa na hivyo basi inawafanya wananchi waweze kusogea mbali kidogo na barabara.

Kwa hiyo, tunaomba sasa tutakapoingia kwenye *Phase Three* basi miradi hii ianze kuingia kule kwa wananchi, ifike kwenye vitongoji, ifike kule kwa mwananchi wa mwisho ili tuweze kuhakikisha kwamba watu wa vijijini wanapata faida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu hatuwezi tukasema tunakwenda kwenye *industrialization* kama hatujawafikia wananchi wa ndani. Wananchi wa ndani ambao nao wanafanya kilimo, ambao wanatakiwa wafikishe mjini, kuna viwanda ambavyo vinaanzishwa kule vijijini ndani. Ni jambo la msingi sana kuhakikisha kwamba tunapata umeme kwa wananchi wetu ambao wako ndani. Mimi nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Muhongo na msaidizi wake kwa kazi nzuri ambazo wameendelea kuzifanya kwa kipindi kirefu, na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais aliona ni bora aweze kumrudisha Mheshimiwa Muhongo aweze kuchukua nafasi ile ile ambayo alikuwa nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikigusia masuala mengine, ninaangalia katika masuala ya bajeti kwamba asilimia 94 ya bajeti hii imeelekezwa kwenye maeneo ya maendeleo. Hili ni jambo la ajabu, kwa maana ya nzuri. Bado sijaona kwamba asilimia 94 katika nchi za Afrika kupeleka pesa za maendeleo kwenye nishati ya umeme na madini. Naomba tumpongeze sana Mheshimiwa Muhongo, tuipongeze Serikali yetu kwamba wamefanya jambo moja la maana

sana. Na mimi naamini kwamba kwa utaratibu huu, miaka mitano ijayo tutafika mbali na nchi yetu itaendelea kusonga mbele kwa sababu tutapata viwanda vya kutosha kama tutaamua kuisimamia sera hii na tutaamua kuisimamia bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa kwamba REA kuna pesa ambazo zinafungwa, lakini utaratibu kutoka Wizara ya Fedha kupeleka pesa kwenye mfuko huu au kupeleka pesa kwenye miradi ya umeme inachelewa. Hatuwezi tukasema tutafika asilimia 94 kama pesa hizi hazifiki kwa wakati. Hili ni tatizo kubwa, pesa ambazo zimefungwa zikae pale zisitumike vinginevyo ili tuweze kuhakikisha kwamba miradi hii inasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali itikadi zetu tunahitaji umeme katika majimbo yetu. Tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri na Serikali yetu tuweze kupata umeme na ninaamini ndoto yetu ya kuwa na viwanda, tutaweza kuwa na viwanda na tutasonga mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ningependa kuvitaja baadhi ya vijiji na kata ambazo napenda Mheshimiwa Waziri aweze kuviangalia. Nina kijiji kimoja kinaitwa Kipera, kipo katika Kata ya Nzii. Katika kata hii nina vijiji sita. Kijiji hiki ni kijiji pekee ambacho hakijapata umeme. Napenda sana Mheshimiwa Muhongo ajitahidi kwa kadri ya uwezo wake tuweze kupata umeme katika kijiji hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina Kata nyingine za Ulanda, Luhota, Lyamungwe, Maboga, Wasa, Kihwele na Kata ya Mgama, bado tunahitaji umeme. Ninaamini kwa kupitia jembe letu, Mheshimiwa Muhongo tutapata umeme katika kata hizi na katika vijiji hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda sana kuwashukuru wote ambao wamechangia, na ninaamini tutaismamia Serikali vizuri kama tulivyotumwa na wananchi wetu tuweze kuisimamia Serikali yetu. Bila kujali itikadi, naomba tuunge mkono kwa asilimia mia moja bajeti yetu ya Wizara hii ya Nishati na Madini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Anafuata Mheshimiwa Ally Seif Ungando.

MHE. ALLY S. UGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa salama salimini. Napenda kukushukuru

wewe kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia katika mada hii ya Nishati na Madini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Waziri mwenye dhamana, ndugu yetu Mheshimiwa Muhongo na Naibu wake kwa kufanya kazi kubwa katika Wizara hii. Kweli nia yake ya kuzima kibatari katika nyumba zetu na kwa wananchi kwa ujumla inaonekana. (Makofi)

Pili, napenda kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kunipa umeme katika vijiji vyangu 18, kikiwemo Kibiti, Nyamisati, Mchukwi, Bungu, umeme unawaka. Kwa hiyo, sina budi kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inayoifanya kwa kuwatumikia wananchi wa Jimbo langu la Kibiti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko vijiji kadhaa ambavyo havina umeme katika Jimbo langu la Kibiti lakini uwekaji wa miundombinu unaendelea. Cha ajabu ni kwamba kasi hiyo haiendani na matakwa ya wananchi. Vijiji hivyo ambavyo wakandarasi wako *site* ni kama Nyamatanga, Lungungu, Lwaluke, Kikale, Mtunda na Muyuyu. Naomba sasa Waziri mwenye dhamana afike na kuona kwa nini wakandarasi hawa wanashindwa kukamilisha miradi hii kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni fidia katika mradi wa umeme wa Kinyerezi, watu 400, kwamba cha ajabu kuna baadhi ikiwemo Dar es Salaam fidia hizo wamelipwa lakini wananchi wangu wa Jimbo la Kibiti mpaka leo hawajalipwa. Ukiangalia tathmini imepita muda mrefu, je, sasa Waziri huyu mwenye dhamana akija kuwalipa wananchi fidia hii watalipwa kwa bei ile ile au kwa tathmini nyingine? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti lipo tatizo katika maeneo ya Delta....umeme. Eneo hili la Delta lina kata tano, vijiji 16, vitongoji 27 mpaka leo hakuna hata kitongoji kimoja kilichopata umeme. Naomba Mheshimiwa Profesa Muhongo atumie jitihada zake zote kuhakikisha vitongoji hivi vinapata umeme hata wa nguvu za jua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi anayofanya na sisi Wandengereko wote tuna imani naye katika kuhakikisha kwamba ataleta maendeleo katika wananchi wangu wa Jimbo la Kibiti na kwa nchi nzima kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niseme katika matumizi ya gesi majumbani. Haya matumizi ya gesi majumbani wananchi wapewe elimu fasaha ili kwamba sasa watumie gesi waachane na kukata miti, mkaa na kuni. Umeme ndiyo njia ambayo itachangia kutunza mazingira. Katika nishati hii ya

gesi kwamba watolewe vikwazo ambavyo siyo vya lazima kwamba gesi ipatikane kwe bei nafuu na kila mmoja aweze kuitumia majumbani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Kibiti viko vijiji 40 ambavyo bado havijapata umeme. Naomba katika *Phase III* iangalie vijiji hivyo ikiwemo Inyamatanga, Lwaluke, Matima, Lungungu na Itawatambwe nayo iangaliwe na tuhakikishiwe tunapata umeme katika *Phase III*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Kibiti, na mimi nawaahidi kwamba sitawaangusha, nitawapa ushirikiano katika kuangalia tunaleta maendeleo katika Jimbo langu la Kibiti. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Endelea, bado muda.

MHE. ALLY S. UGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niseme viko vijiji ambavyo mradi huu unaendelea, lakini bado ujenzi wake hauendi kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo lingine niliseme ambalo ni changamoto ya Shirika letu la umeme (TANESCO) katika Wilaya yetu ya Kibiti, ni kwamba yako matatizo mengi ikiwemo usafiri, posho za ziada na maslahi yao ya kazi na elimu za fidia. Tunafahamu kwamba miradi hii ya REA haina fidia na inakuwa vigumu wananchi wanapokosa elimu, wanapokwenda kukatiwa miti yao inaweza ikaleta migongano baina ya wananchi na mtendaji husika katika maeneo yale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia kwamba sasa wananchi wanahitaji maendeleo. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Dakika tatu Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Nitachangia kesho.

MWENYEKITI: Haya! Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wachangiaji wetu kwa jioni ya leo. Tumekwenda vizuri sana, lakini kwa orodha ambayo nilikuwa nayo kwa vyama tumefanya vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka asubuhi uliombwa Mwongozo na Mheshimiwa Bobali kuhusiana na tukio la kusikitisha kidogo lililotokea Mjini Mwanza.

Mwongozo wa Mheshimiwa Spika ilikuwa ni kwamba kwa sababu ni tukio limetokea ambalo hata upande wa Serikali kwa wakati huo haukuwa na taarifa

ya uhakika, basi alielekeza angalau tujipe muda, Serikali iweze kutumia vyombo vyake na ije itoe taarifa ya awali tu. Wamefanya hivyo na ninaomba tu nitumie muda huu, nimwombe Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masauni aweze kutoa taarifa fupi tu ya Serikali kwa sababu haya ni masuala ya uchunguzi hatuwezi kwenda na wala wasifike katika *details* zozote waseme tu kwa ujumla. Karibu Mheshimiwa Naibu Waziri. (Makofi)

KAULI ZA MAWAZIRI

Tukio la Mauaji - Mwanza

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa taarifa fupi kwa niaba ya Serikali kutokana na tukio la kusikitisha ambalo limetokea Mwanza jana siku ya tarehe 18 Mei, 2016. Tukio hilo lilitokea wakati wa saa 2.35 usiku ndani ya Msikiti unaoitwa Masjid Rahman ambao unamilikiwa na BAKWATA ambao upo katika eneo la Mapankini, Mtaa wa Ibanda Relini, Kata ya Mkolani, Mkoani Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tukio hilo, watu watatu waliuawa kwa kukatwa mapanga na mashoka sehemu mbalimbali za miili yao na mmoja kujeruhiwa sehemu ya kichwani baada ya watu wapatao takribani 15 kuvamia msikitini. Watu hao waliuawa wakati walipokuwa wanaswali swala ya *Insha* ndani ya msikiti huo. Walikuja wauaji hao wakavamia msikiti wakiwa wamejificha kwa mavazi ambayo yalikuwa yanaficha sura zao. Walizima taa na kuanza kuwakata kwa mapanga na kumjeruhi mtoto mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliouawa katika tukio hilo ni Ndugu Feruzi Ismail Elias ambaye ana miaka 27 ambaye ndiye aliyekuwa Imamu wa Msikiti huo, mkazi wa Ibanda Relini. Mwingine ni Ndugu Mbwana Rajabu ana miaka 40, yeye ni mfanyabiashara na mkazi wa Ibanda vilevile na mwingine ni ndugu Khamis Mponda miaka 28 ni dereva, pia ni mkazi wa Ibanda, Mkolani. Aliyejeruhiwa ni mtoto ambaye ana miaka 13 anaitwa Ismail Abeid ambaye ni mwanafunzi wa shule iitwayo Jabal.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali, kwanza tunaomba kuchukuwa fursa hii kuwapa pole familia ya Marehemu, ya mtoto aliyejeruhiwa pamoja na Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, Mheshimiwa Stanslaus Mabula pamoja na Watanzania wote kwa ujumla kwa msiba huo mzito, kutokana na tukio la kinyama ambalo limefanywa na watu wasio na chembe ya ubinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii vilevile kuwajulisha kuwa Jeshi la Polisi limeshaanza kufanya upelelezi juu ya tukio hili na kazi hiyo inaendelea vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie wananchi kupitia Bunge lako Tukufu kwamba damu za watu hawa waliouawa kikatili hazitapotea bure. Serikali haitolala mpaka wahusika watiwe mkononi na kuchukuliwa hatua za kisheria. Kwa kupitia Bunge lako hili Tukufu, naliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha linafanya kila linalowezezana mpaka wahusika wote wapatikane. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwisho nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wanafamilia na wananchi wote kwa ujumla kuwa na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu na waendeleo kuwa na imani kwamba Serikali inalishughulikia tatizo hili pamoja na matukio mengine ya aina kama hii ya kinyama kuzuia yasijitokeze tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa taarifa hii ya kusikitisha juu ya tukio hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, ndiyo mwisho wa shughuli zetu na taarifa nyingine sina hapa, lakini nadhani kesho wataikamilisha, kulikuwa na Mwongozo mwingine.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.49 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 20 Mei, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*